

4 FEBRUARI, 2015  
**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA NANE**

**Kikao cha Nane - Tarehe 4 Februari, 2015**

(Mkutano Ulianze Saa tatu Asubuhi)

**D U A**

Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu tuanze.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na :-

**MHE. RIZIKI OMARI JUMA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII):**

Taarifa ya Mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii Katika Kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii Katika Kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015.

4 FEBRUARI, 2015  
**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Maswali yetu kama kawaida yanaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. David Malole, kwa niaba yake Mheshimiwa Hezekiah Chilibunje.

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jina langu ninaitwa Hezekiah Chibulunje.

Na. 83

**Ujenzi wa Barabara za Dodoma Mjini**

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE (K.n.y. MHE. DKT. DAVID M. MALOLE)** aliuliza:-

Serikali imefanya kazi nzuri ya kutengeneza barabara za Dodoma Mjini kupitia fedha za mfuko wa World Bank awamu ya kwanza:-

Je, ni lini fedha za awamu ya Pili za World Bank zitatoka ili kukamilisha ujenzi wa barabara ambazo bado hazijawekewa lami katikati ya Mji wa Dodoma.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mciwa Malole, Mbunge wa Dodoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011 Mkoa wa Dodoma kupitia Mradi wa Uendelezaji wa Miji Tanzania (TSCP) ulitengewa kiasi cha dola za Kimarekani

4 FEBRUARI, 2015  
milioni 32 kutoka Benki ya Dunia na Serikali ya Denmark kwa ajili ya ujenzi wa barabara zenyen urefu wa kilomita zipatazo 42 katika Mji wa Dodoma.

Ujenzi wa mifumo ya maji ya mvua, dampo la kisasa katika Kijiji cha Chidaya nje kidogo ya Mji wa Dodoma, mitambo kwa ajili ya usombaji taka pamoja na kujenga uwezo wa Taasisi za Mamlaka za Ustawishaji Makuu (CDA) na Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zilizojengwa kwa kutumia fedha hizi hadi sasa zinahusisha maboresho za barabara za Mwanza, Kondo, Hospitali, *Independence*, Mwangaza, Siasa, Daima, Mtendeni Market, Tembo, Tabora, Barabara ya Sita hadi ya Kumi na Moja, barabara za Nkuhungu, Chamwino na Chang'ombe zenyen jumla ya kilomita 15.7. Ujenzi huu umekamilika kwa asilimia mia moja.

Aidha, jumla ya kilomita 27.12 za barabara za pemberi ya Mji ambazo hazikuwahi kuwa na lami zilijengwa katika maeneo ya Area 'A' kilomita 5.82, Kikuyu kilomita 5.62, Kisasa kilomita 12.90 na Chang'ombe kilomita 2.75.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Dunia imeahidi kutoa nyongeza ya fedha kiasi cha dola za Kimarekani milioni 7.66 kwa ajili ya kukamilisha mapungufu yaliyojitekeza katika awamu ya kwanza ambayo yatahusika pamoja na mambo mengine ujenzi wa barabara ya lami ya *Independence* kuelekea shule ya Uhuru kilomita 0.4 na barabara ya Mbeya eneo la Uhindini kilomita 0.25.

Baada ya kukamilika hatua hii Benki ya Dunia bado haijatoa ahadi nyingine ya kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara nyingine mpya za lami katika Mji wa Dodoma. (Makofii)

4 FEBRUARI, 2015

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nataka niishukuru sana Serikali kwa jitihada ilizozifanya katika kutengeneza barabara za Mji wa Dodoma. Mji wetu sasa unapendeza na kwa kweli tuishukuru pia Benki ya Dunia kwa msaada iliooutoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Mji wa Dodoma uendelee kupendeza zaidi kwa Miundombinu ya Barabara, zipo barabara za eneo la Area C ambazo zilijengwa na CDA katika miaka ya 1980 ambazo sasa hivi zina hali mbaya sana. Maadam Serikali imepokewa mzigo na Benki ya Dunia.

Je, Serikali haiwezi kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara hizo za Area C ili ziweze kuendelea kupendezesha Mji wa Dodoma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la Pili, Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino inayo barabara ambayo iko karibu sana na Manispaa ya Dodoma, barabara hii inatoka Msanga kwenda Kawawa ambayo kwa muda mefu haijafanyiwa matengenezo.

Je, Serikali itakubali Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino ilete ombi maalum kwa ajili ya matengenezo ya barabara hii ya Kawawa Msanga?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, kwa kuziona juhudzi za Serikali za kuboresha Mji huu wa Dodoma kama Makao Makuu ya Nchi, kwa kujenga barabara nzuri na zinazovutia, ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameomba kufahamu ni kwa kiasi gani Serikali itaendeleza ushirikiano wake na Manispaa ya Dodoma katika kuhakikisha kwamba barabara zilizobakia ikiwemo barabara ya Area C inaweza kutengewa fedha na kufanyiwa ukarabati kwa kuwa ni ya muda mrefu.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu na wananchi wa Dodoma na Tanzania nzima kwamba Serikali bado ina dhamira ya dhati ya kuhakikisha barabara za Mji huu wa Dodoma zinafanyiwa kazi na zinazidi kuwa bora kulingana na hadhi ya Mji huu wa Makao Makuu Dodoma.

Kwa sasa kupitia wakala wa Barabara Tanzania Mkoa wa Dodoma, Serikali imeshatenga fedha ya kufanya ukarabati na ujenzi wa barabara inayoanzia St. Peters Clever, kupitia UDOM mpaka round about ya Kikuyu, barabara hiyo inaelekea kuunganishwa na barabara inayokwenda Iringa.

Hata hivyo, Manispaa yenye we pia imeanza kufanya matengenezo inayoanzia Martin Luther kupitia Royal Village mpaka njia panda ya Wajenzi. Tukishamaliza barabara hizo tutaona zinaingililanaje na maeneo hayo ya Area C na kama maingilio yatakuwa si ya kutosha sana basi Serikali kupitia mipango yake mbalimbali itajitahidi kuona inafanya nini ili barabara za Mji huu wa Dodoma ziweze kuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Mbunge pia ameionba Serikali kuangalia uwezekano wa kuunganisha nguvu kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino kujenga na kukarabati barabara ya Msanga na Kawawa. Namshauri Mheshimiwa Mbunge maombi hayo yapitie katika utaratibu wa kawaida kupitia vikao vya Halmashauri kwenda kwenye wakala wa barabara Mkoa na hivyo basi Serikali kwa kushirikiana katika Wizara mbalimbali itaona kama uwezekano wa kutengeneza barabara hiyo upo basi kazi hiyo itafanyika kwa kuzingatia taratibu na sheria za ujenzi wa barabara nchini. (Makofii)

**MHE. ALLY KEISSY MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana hapa kulikuwa na upinzani mkubwa wa Wabunge wawili walitaka Dodoma isiwe Makao Makuu.

4 FEBRUARI, 2015

Lakini Serikali ikathibitisha kwamba Dodoma itaendelea kupewa kipaumbele na Dodoma ni Makao Makuu, naishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha qjabu Dodoma hii hapa Saba saba sokoni, mimi ndiyo mpitaji mkubwa wa barabara hiyo. Sasa hivi kunaweza kuzuka magonjwa ya kuambukiza, wananchi wanaishi pale kama wanaishi sijui sehemu gani katika nchi hii, hailingani kabisa na hadhi ya Dodoma. Uchafu umelundikana, wananchi wanakaa pale sokoni, hawatendewi haki wanalipa ushuru lakini bidhaa zao zinanyanyaswa, zinakaa chini, yaani siyo soko, siyo chochote na hii ni Makao Makuu ya nchi yetu. Dodoma tunauita ni Makao Makuu! Ni aibu! ni aibu! (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninapita kila siku pale kwa miguu ni aibu, ni aibu!

Je, Serikali inachukua hatua gani kuwasaidia wananchi wa soko lile kuliweka kuwa soko la kisasa. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Waziri majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, kwa swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la usafi katika eneo lolote kwenye nchi yetu ya Tanzania kwanza ni lazima tujue linahusisha wadau mbalimbali ikiwemo watumiaji wa soko na wananchi kwa ujumla.

Kwa kuwa usimamizi wa usafi unazingatia mamlaka zilizopewa majukumu ya kuhakikisha kwamba maeneo katika Miji yetu yanakuwa safi yanaleta usalama wa afya kwa wakazi na watumiaji wa maeneo hayo.

4 FEBRUARI, 2015

Ninamhakikisha Mheshimiwa Mbunge tutalichukua suala hilo na mamlaka zinazohusika zitaarifiwa na kuambiwa kushughulikia tatizo hilo la kuboresha usafi kwenye eneo la soko la Sabasaba haraka iwezenavyo ili kuondoa tatizo hilo la uchafu na kuondoa hatari ya kuweza kulipuka kwa magonjwa mbalimbali ya mlipuko kwa usalama wa wananchi wote waishio hapa Dodoma.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda kuuliza swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, Manispaa ya Dodoma barabara zake zimejengwa kwa fedha za *World Bank* na kwa kuwa Manispaa ya Singida barabara zake ni mbaya sana napenda kujua.

Je, huu mradi wa *World Bank* ni wa kutengeneza barabara za Manispaa zote Tanzania au ni baadhi tu zimeteuliwa? Kama ni baadhi tu!

Je, Manispaa zingine ni lini zitatengewa hela ya kutengeneza barabara ikiwemo Manispaa ya Singida?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mheshimiwa Diana Chilolo kwa swali hilo zuri jingine la nyongeza ambapo anaona kwamba kuna umuhimu wa kuboresha barabara nyingine hapa nchini.

Serikali inapokea maoni hayo itaendelea kufanya majadiliano na Benki ya Dunia ili kama uwezekano huo utakuwepo basi miradi hiyo iweze kusambazwa katika Manispaa nyingine nchini, na hiyo itakubaliana na matakwa ya Benki ya Dunia kama uwezo huo utakuwepo wa kuweza kuendeleza barabara zingine katika Manispaa zilizobakia. (Makofij)

4 FEBRUARI, 2015

Hata hivyo, tunaendelea kuwaomba Wamiliki wa Manipaa na Halmashauri hizo ambazo wanahitaji kuboresha barabara katika Miji yao kuendelea pia kufuata utaratibu wa kutenga fedha katika Bajeti zetu, kuendelea na matengenezo ya barabara hizo wakati tukingojea fedha zingine zinazoweza kupatikana kutoka katika vyanzo vingine.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Deogratius Aloyce Ntukumazima. (Makofi/Kicheko).

Samahani sana ni Mheshimiwa Ntukamazina.

Na. 84

**Kuajiri Watendaji Kata na Vijiji wenye  
Elimu ya Sekondari**

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA** aliuliza:-

Watendaji wengi wa Vijiji na Kata wana uwezo mdogo sana kutokana na elimu duni waliyonayo na hawana fursa ya kuijendeleza kutokana na ufinyu wa Bajeti na hivyo kuwa kikwazo cha maendeleo.

Je, ni lini Serikali itawaondoa Watendaji hao wenye uwezo mdogo na kuajiri Vijana wenye elimu ya Sekondari ambao wengi wao wapo huko Vijijini(Mtaani) baada ya kumaliza shule.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu. Jamani haya majina mengine magumu, kuna Mchezaji wa Simba naye anaitwa hivi hivi tu, ninaomba radhi sana Mheshimiwa Ntukamazina.

4 FEBRUARI, 2015  
**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA  
MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deogratius Aloyce Ntukamazina Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundo ya Utumishi wa Kada za Maafisa Watendaji wa Kata, Mitaa na Vijiji inayotumika sasa iliidhinishwa kwa nyaraka za maendeleo ya Utumishi kwa Serikali za Mitaa Na. 29, Na.30, Na.31 za mwaka 2003 zilizotolewa na Tume ya Utumishi wa Serikali za Mitaa (TUMITAA).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sera za menejimenti na usimamizi wa Watumishi ya mwaka 1999 imeweka masharti ya kujiunga na utumishi wa umma ambapo kiwango cha chini cha kumwezesha mtumishi kuajiriwa kwa masharti ya kudumu katika utumishi wa umma ni kidato cha Nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa waraka wa Maendeleo Utumishi Na. 1 wa Mwaka 2013 kipengele cha 4, baada ya marekebisho ya Miundo ya Utumishi wa Watendaji wa Kata na Vijiji Sifa za kuanzia Kada ya Watendaji wa Vijiji, Mitaa ni Astashahada na kwa Watendaji wa Kata ni Stashahada na Shahada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2004 Serikali iliwataki Watumishi wote wa Serikali wasio na kiwango hicho cha elimu ambacho kinatakiwa kujiendeleza ili kuendelea kupata sifa ya kubakia kwenye Utumishi wa Umma, Watendaji wa Vijiji na Kata kama sehemu ya Watumishi wa Umma pia wanaangukia katika vigezo hivyo.

4 FEBRUARI, 2015

Kwa hiyo, Serikali ilitoa nafasi kwa watumishi waliokuwa hawana elimu ya sekondari kuijendeleza na kupata elimu hiyo kwa muda maalum. Sharti hili ilikuwa ni kwamba Mtumishi atakayeshindwa kujiendeleza atakuwa amejiondoa mwenyewe katika utumishi wa umma na nafasi hiyo kuajiriwa mtumishi mwingine mwenye sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kuwahamisha vijana waliomiliza elimu ya sekondari wenyе sifa ya kujunga na Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo ambacho kinatoa Astashahada na Shahada kwa masuala ya Serikali za Mitaa ili waweze kuajiriwa katika mamlaka za Serikali za Mitaa. (Makofi)

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mwanri kwa majibu mazuri, hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Kama alivyosema mwenyewe ni mwaka 2004 miaka kumi iliyopita Serikali iliwataka Watendaji wa Kata na Vijiji wawe wamejiendeleza kufikia kiwango cha Astashahada na Shahada.

Je, kipindi hicho maalum kilikuwa ni miaka mingapi na kama wapo ambao hawakuweza kuijendeleza katika kipindi hicho mnawafanyaje?

Swali la Pili, wakati tuna tatizo hilo la Watendaji ambao wana uwezo mdogo kielimu inaendelea na wameshindwa kuijendeleza na Halmashauri hazina fedha za kuendesha semina kuwaongeza ujuzi.

Je, inawezekana tutakitumia Chuo cha Hombolo kutoa mobile service yaani kuendesha semina za kuongeza ujuzi kikanda au Kimkoa ili Watendaji wa Kata na Vijiji waweze kufaidika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

4 FEBRUARI, 2015

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anayezungumza hapa ni Mamlaka katika jambo hili kwa sababu amekuwa Utumishi pale kwa muda mrefu. Kwa hiyo, nipo conscious kwamba ninamjibu mtu wa namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi ambacho kulitokea jambo hili linalozungumzwa hapa bahati nzuri Mheshimwia Ngwilizi ambaye yumo humu ndani ndiyo wakati huo yeye alikuwa Waziri mwenye dhamana. Kilichosemwa pale ilikuwa imesemwa miaka minne, baadaye ikapunguzwa ikasemwa miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea ni kwamba wapo watumishi ambao walionekana karibu wanastaafu akienda kusoma miaka mitatu minne anakuwa na miaka 58.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri jibu kwa kifupi tuna tatizo la *time*.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Serikali ikaangalia kwamba huyu mtu anaondoka yaani kesho akimaliza kusoma unabakia mwaka mmoja, Serikali ikasema hivi hawa ambao wamefikia katika hali hiyo tuwaache wamalizie, tulichobana ni huku mwanzo anayeingia yeyote yule hawezi kuingia bila kuwa na sifa hizi tunazozungumza hapa na ndiyo kumekuwa kuna *development* ya kuwa na Hombolo pale na utaratibu mzima wa kuhakikisha kwamba hawaingii tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza wapo watu wenye Digrii sasa wapo kwenye Kata na imeanza kutiririka wanakwenda mpaka kwenye vijiji kule, kwa kifupi ni hilo.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *mobile services*, sisi tumesema utaratibu wetu ni kwamba kama tunaipata hii kada tunipeleka pale Hombolo, kwa sababu tunazungumza *recruitment* sasa jinsi ya kuwapata hawa watu. Tunachofanya ni kwamba tunaendesa semina za aina mbalimbali, kama mnakumbuka tumekwenda kwenye Mikoa tumefungua semina za namna ile ili tuweze kuzipata hizi kada nazo ziweze kujifunza.

Kwa hiyo tunachoweza kusema ni ku-accommodate hii ya *mobile services* kuitia semina na *workshops* na kadhalika. Watu waweze kupata elimu zaidi kuhusu jambo hili tunalolizungumza hapa hasa kwa wale ambao bado wameendelea kubaki hapa. Lakini kundi kubwa lilikwenda likasoma mpaka *Form four* na kwa hiyo wakawa pia wamekidhi hiyo haja inayozungumzwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Pauline Gekul, jiandaye Mheshimiwa Michael Lekule Laizer na Mheshimiwa Joseph Selasini.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kunipa nafasi niulize swalii moja la nyongeza. Kwa utaratibu uliopo sasa Watendaji wa Mitaa, Vijiji na Kata wanafanya kazi chini ya Halmashauri zetu kwa pamoja.

Lakini ajira za Watendaji wa Mitaa na Vijiji imerudishwa kwa Halmashauri, wakati ajira za Watendaji wa Kata bado iko chini ya Sekretarieti ya Ajira Wizara ya Utumishi. Ni lini ajira za Watendaji wa Kata zitarudishwa kwa Halmashauri zetu ili wafanye kazi kwa pamoja?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachosema hapa ni kwamba anazungumzia sasa kada hii ya Mtendaji wa Kata. Mtendaji wa Kata by definition ndiye Msaidizi wa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya husika, ni kama mwajiriwa kidogo pale.

4 FEBRUARI, 2015

Kwa hiyo, hayuko katika kada hii na kwa vile umenitaka. Mimi ninayo orodha pale ambayo ameandika Mheshimiwa Yambesi ambaye ni Katibu Mkuu. Ametoa kada 22 ndizo zimetamkwa pale. *You have the point Member of Parliament*, kama tunafikiri kwamba kuna haja pia na hili kundi likaingizwa ili liajiriwe na Halmashauri kwa maana ya recruitment, this is an idea ambayo sisi tutai-buy.

Lakini kwa sasa kwa sheria na utaratibu na hiyo barua ninayoizungumza hapa kundi hili la Watendaji wa Kata limeendelea bado kubakia Ofisi ya Rais Utumishi. (Makofij)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, jiandaye Mheshimiwa Joseph Selasini.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti ninashukuru kunipa nafasi niulize swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa katika Halmashauri nyingi hawana Watendaji wa Kata kwa sababu ya mfumo huu wa kusubiri Sekretarieti ya Ajira.

Je, Wizara hii haioni kwamba tatizo kubwa la ucheleweshaji wa Miradi ya Maendeleo inasababishwa na hao Watendaji wa Kata ambao hawapo katika Halmashauri zetu na bado mnang'ang'ania Sekretarieti ambayo haiwezi. Imeshindwa kuajiri, kuwaajiri Watendaji wa Kata zote zilizoko hapa nchini, hamwoni ninyi kwa muda wote mliopo madarakani kwamba hiyo Sekretarieti imeshindwa kazi? (Makofij)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii development tunayoizungumza ni development kubwa sana. Hawa wote hawa niliyosema 22 hawa, wote walikuwa wanakwenda Sekretarieti kule Utumishi. Tukakutana katika Association of Local Authorities of Tanzania likawekwa bayana jambo hili. Akaja Makamu wa Rais akasemea jambo hili kwa niaba ya Serikali na tukakubaliwa kwamba kada hizi ziingie sasa ziwe zinaajiriwa moja kwa moja kupitia pale.

4 FEBRUARI, 2015

Sasa labda hapa hatujaelewana kitu kimoja labda sijampata vizuri Mheshimiwa Michael Lekule Laizer. Hawa wote wanakuwa ni waajiriwa walioko katika Halmashauri. Ninachozungumzia hapa ni *process* ya *recruitment* ya kumpata huyu inapitia kule. Hata hao 22 tunaozungumza hapa huwezi kuajiri mpaka upate kibali kutoka Utumishi otherwise the wage bill ya kwetu inaonekana inakuwa kubwa kuliko ile ya development. Kwa hiyo, inakuwa kubwa ni kazi ngumu.

Naiona point yako, kama tunafikiri kwamba kuna haja pia na hili kundi liingie kama alivyosema Mheshimiwa Gekul, sisi tutaendelea kupokea mawazo haya. Haya ni maamuzi ambayo yanafanyika, si mtu mmoja anafanya hayo au Idara moja inafanya.

Sisi wote kwa kushirikiana tukasema jamani hata na hawa Watendaji wa Kata nao hawa tunafikiri kwamba warudishwe katika level hiyo ya Kata na Halmashauri ili waweze kuajiriwa kule kule. Ni jambo ambalo linazungumzika na ambalo tunaweza tukalipeleka mbele kwa ajili ya kumshauri Waziri mwenye dhamana ambaye Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Pamoja na shida hii ya ajira, Watendaji wengi waliopo, baadhi yao hawaitishi vikao, hawakai Ofisini, wengine wanajihusisha na siasa. Hawafungui Ofisi na wengine ni walevi.

Huu ni ushahidi kwamba baadhi ya Watendaji hawana uwezo na wanazui shughuli za maendeleo. Wakati kuna vijana wengi waliomaliza vyuo vikuu na wana uwezo wako vijijini hawana kazi.

Kwa nini Serikali isitoe agizo la moja kwa moja kwamba Watendaji wa namna hii waondolewe mara moja kwenye utendaji ili kuweka vijana ambao wana uwezo wa kuwashudumia watu wetu vizuri?

4 FEBRUARI, 2015

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimeduwa nikisema katika Bunge lako Tukufu kwamba mtumishi pekee katika mamlaka za Serikali za Mitaa ambaye tunaweza kumtolea tamko na kuweza kumchukulia hatua ni Mkurugenzi pekee.

Kwa hiyo, agizo ambalo ninaweza nikalitoa ni kwamba Mabaraza ya Madiwani akiwemo na Mheshimiwa Mbunge aliyezungumzia hilo suala, wawachukulie hatua watumishi hao ambao hawafanyi kazi zao kwa mujibu wa Sheria. Badala ya kusukumiza mzigo au lawama kwa watu wengine.

Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI haiwezi kushughulika na Mtendaji wa Kijiji au wa Kata. Tunaomba Halmashauri, Wakuu wa Idara wote mna uwezo wa kuwachukulia hatua, wachukulieni hatua huko huko. (Makofij)

Na. 85

**Tatizo Sugu la Maji Mchinga**

**MHE. SAID M. MTANDA** aliuliza:-

Je, ni lini tatizo la maji Mvuleni, Mnang'ole, Lihimilo na Kitohavi litapatiwa ufumbuzi na kwa garama gani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, Mbunge wa Mchinga, kama ifuatavyo:-

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, jimbo la Mchinga linakadirwa kuwa na wakazi wapatao 65,466 kati yake asilimia 62.2 ya wakazi wake wanapata huduma ya maji safi na salama toka kwenye visima vifupi na vya kati vyenye pampu za mikono 38, visima vyenye pampu za mikono vitano na miradi mingine ni ya kusukuma kwa mashine nane na miradi ya kuvuna maji ya mvua 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vya Mvuleni, Mnang'ole, Lihimilo na Kitohavi vinakadirwa kuwa na jumla ya wakazi wapatao 5,912 ambaa asilimia 10 ndiyo wanaopata huduma ya maji safi na salama kutoka kwenye visima na tanki la uvunaji maji ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua tatizo hili, Halmashauri ya Wilaya ya Lindi inatekeleza miradi ya maji ya Lihimilo na Kitohavi. Mradi wa maji Lihimilo umetengewa shs.143,926,363/= na Kitohavi ni shs.152,080,832/=. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Halmashauri ya Wilaya ya Lindi ilipokea shilingi milioni 10,131,186/= kwa mradi wa maji Lihimilo na shilingi milioni 10,705,191/= kwa mradi wa maji Kitohavi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 Halmashauri imepanga kutumia shilingi milioni 595,679,000/= kwa miradi ya maji na usafi wa mazingira katika vijiji vya Mvuleni, Makumba, Kiwawa, Kilolambwani, Litingi, Chiuta, Linoha, Navanga, Shuka na Mkanga II.

Hata hivyo mfuko wa Jimbo umetoa shilingi milioni 4 kwa ajili ya utafiti wa maji chini ya ardhi katika kijiji cha Mvuleni kwa mwaka huu wa fedha. Aidha jumla ya shilingi 206,880,953 zimepokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa mwaka huu Halmashauri imetenga shilingi milioni 110 fedha za Ruzuku ya Maendeleo kwa miradi ya maji ya Mnimbila kwa utaratibu ufuatao:-

4 FEBRUARI, 2015

Shilingi milioni 50 Tulieni, shilingi 30 Mtua na Kilimahewa milioni 30. Serikali itaendelea kuboresha huduma ya maji katika vijiji vya Mnong'ole, kwa kadiri rasilimali ya fedha itakavyopatikana. (Makof)

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwanza Naibu Waziri ni mchapa kazi na aliwahi kufika kwenye jimbo langu akashughulikia tatizo la daraja Mnyangala ambalo liliwama kwa miaka 10 na sasa linapitika. Lakini nina maswali mawili tu ya nyongeza.

Kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri atuambie kama Serikali imeahidi kupeleka milioni 143 Lihimilo na shilingi milioni 152 pale Kitohavi na wananchi niliwaeleza juu ya matumaini hayo ya Serikali. Lakini hadi leo imepeleka shilingi milioni 10. Nataka kujua sasa huu utaratibu wa kupeleka milioni kumi, kumi utachukua muda gani ili kufikia kiwango cha shilingi 142 ili mradi huu uweze kukamilika kwa wakati kabla ya mwezi wa tano kama ambavyo tumekubaliana na Serikali?

Lakini swali la pili. Kwa kuwa Waziri aliahidi na wananchi wa maeneo haya walipewa matumaini na mimi Mbunge wao akapata matatizo ya kufiwa na tunampa pole. Safari ile aliahirisha. Je, Waziri wa Maji nazungumzia Naibu Waziri wa Maji.

Je, sasa Waziri mwenyewe mwenye dhamana ya maji au Naibu Waziri wa Maji, yuko tayari sasa kuandaa safari ili twende kwenye maeneo haya akajionee mwenyewe hali halisi na kupambana na maswali ya Wapiga Kura kwenye maeneo haya? (Makof)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Said Mtanda, kama ifuatavyo:-

La kwanza nimhakikishie kwamba Vijiji alivyovitaja hivyo vya Lihimilo na Kitohavi tayari utafiti umeshafanyika

4 FEBRUARI, 2015  
watu wa Board wameshaenda na hizo hela ni za utangulizi  
tu hizo hela ambazo zimetengwa tutazipeleka.

La pili, kama ambavyo aliongea jana na mimi  
mwenyewe niliongea naye. Nataka nimhakikishie niko tayari  
kujibu maswali ya Wapiga Kura wake na kuwapa majibu  
mazuri na tutakwenda kufanya ziara katika maeneo haya.  
(Makofi)

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti,  
nashukuru kunipa nafasi. Tunafahamu tatizo la maji ni kubwa  
karibu nchi nzima. Lakini hivi karibuni Mkoo wa Dar es Salaam  
hasa Jimbo la Kinondoni ambako tunapata maji eneo kubwa  
linapata kutoka Mtambo wa Ruvu Chini limekuwa na shida  
ya maji takribani wiki ya pili hivi sasa. Wananchi  
wanahangaika pamoja na maelezo yenu kwamba maji  
yatapatikana. Ni kitu gani na Serikali inasemaje juu ya tatizo  
hili?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti,  
kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la nyongeza  
la Mheshimiwa Iddi Azzan, Mbunge wa Kinondoni, kama  
ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kulikuwa na tatizo  
la maji karibia wiki moja kwa wakazi wa Dar es Salaam na  
maeneo mengi yaliathirika. Hii ilitokana tu na mtambo  
kuzimwa tarehe 23 Januari, 2015 ili kumruhusu mkandarasi  
*Sino Hydro* ambaye anatengeneza, amepewa kazi hiyo  
kuunganisha bomba jipya na boma la zamani. Kwa tarehe  
23 mtambo ulizimwa lakini kabla ya kuzimwa tarehe 20, 21  
mpaka 22 Dawasco walitoa taarifa kwa vyombo vyaa habari.  
Gari lilipita likitangaza kwamba kutakuwa na tukio hilo.

Lakini pia tarehe 26 Januari, 2015 wakati  
wameshafunga yale maungio yaliachia kwa sababu ya  
pressure ya maji. Kwa hiyo, walianza tena kufunga upya kwa  
sababu bomba jipya ni la chuma na hili la zamani ni la zege.

4 FEBRUARI, 2015

Lakini niseme tu kwamba kuanzia tarehe 1 Februari, 2015 tulifanikiwa kufunga tukafungua pampu moja tarehe 2 Februari, 2015 tukafungua pampu ya pili na sasa maji yamerejea katika hali yake ya kawaida na maeneo mengine yanaendelea kufika maji kwa sababu yanachukua muda mrefu. Kwa hiyo, niwaombe radhi kwamba iliokea hivyo kwa sababu ya kiufundi suala ambalo tulikuwa tunaunganisha bomba la zamani na bomba jipya. (Makofij)

Na. 86

**Ajira za Kijeshi Nchini**

**MHE. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Bunge lilipitisha sheria kwamba ajira zote za majeshi wachukuliwe vijana waliopitia JKT kama vile Jeshi la Magereza, Polisi na kadhalika:-

(a) Je, mpaka sasa hivi ni vijana wangapi wameshanufaika na utaratibu huo?

(b) Je, ni lini wafanyakazi walioko Serikalini ambao hawajapitia JKT na baadhi ya Wabunge ambao hawajaenda JKT wataendelea na utaratibu huo?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Kabati, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana waliohuduria mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ambao wamesha ajiriwa na vyombo vya ulinzi na usalama kuanzia mwaka wa 2011 hadi 2014 ni kama ifuatavyo:-

4 FEBRUARI, 2015

Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania idadi 12,499, Jeshi la Polisi idadi 2,745, Jeshi la Magereza idadi 1,107, Jeshi la Zimamoto idadi 100 na usalama wa Taifa idadi 143. Hivyo jumla ya vijana walionufaika na utaratibu huu jumla ni 16,594.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijaweka utaratibu kisheria wa kuwataka watumishi wake kuitia mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kama ilivyokuwa hapo awali. Sheria iliyopo ni kwa wahitimu wa Kidato cha Sita kuhudhuria mafunzo hayo.

Aidha, Wizara yangu ipo tayari kuendelea kutoa mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa Waheshimiwa Wabunge Vijana kwa kadiri itakavyopokea orodha ya Wabunge hao kutoka Ofisi ya Bunge. (Makof)

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza kabisa, niwapongeze sana wale Wabunge wenzangu waliohudhuria mafunzo haya ya JKT wakiwa Bungeni. Kwa sababu kuna changamoto nyingi sana waliweza kuzibaini tukiwa katika mafunzo hayo. Kwa sababu tatizo hili la ajira Mheshimiwa Waziri ni kubwa sana sana katika makambi yetu.

Sasa naomba nikuulize maswali madogo ya nyongeza. Pamoja na kuwa Serikali ilitekeleza azma yake ya kuajiri vijana hao 16,594 kutoka JKT. Lakini bado haijaanza kuajiri askari hao kutoka bandari, kutoka wanyamapori, Halmashauri zetu pamoja na majiji.

Je, kwa nini Serikali isiajiri askari hao kutoka JKT pia?

Swali la pili, kwa kuwa vijana waliomaliza mafunzo ya JKT hupata mafunzo ya ujasiriamali na stadi zingine za maisha. Tuliona pia katika makambi hayo kuna vyuo vya VETA vimekuwa vikiwafundisha askari hao hizo stadi za maisha.

4 FEBRUARI, 2015

Lakini hao vijana wanapomaliza mafunzo hayo wamekuwa tatizo kubwa hawana vifaa, pamoja na kuwa wameshapata taaluma. Kwa nini sasa isiweze kuajiri bado?

Kwa nini Serikali isiweze kuwapatia vifaa vyta taaluma zao ili waweze kujiajiri mara baada ya kumaliza mafunzo hayo, kwa sababu wengine wamekuwa hawaajiriwi ili waweze kujiajiri?

**MWENYEKITI:** Swali, swali, swali.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Swali langu kwa nini Serikali isiweawezeshe kimitaji na vifaa vyta taaluma zao ili waweze kujiajiri baada ya kumaliza mafunzo yao ya Jeshio la Kujenga Taifa (JKT) na hapo wanaweza wakaajiri na wenzao ili kupunguza wimbi la ajira la vijana mitaani, ili wasiweze kujingiza kwenye vikundi vyta panya road?

**MWENYEKITI:** Ahsante jibu swali, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti swali la kwamba kwa nini vijana hawa wanaomaliza JKT hawapati ajira katika maeneo mengine.

Kwa mfano Bandari, Idara ya Wanyamapor, TANAPA na kadhalika. Jibu ni kwamba pamoja na vyombo vyta Ulinzi na Usalama vijana hawa wamekuwa wakipata ajira katika maeneo mengine ikiwemo hayo aliyoyataja Mheshimiwa Kabati. TANAPA wanaajiri baadhi ya vijana kutoka JKT. Bandari wameanza kuajiri vijana kutoka JKT na kadhalika.

Lakini ni kweli kwamba bado ziko taasisi au niseme asasi nyininge ambazo zinatusaidia sana endapo nao wataanza kuajiri kutoka JKT. Ikiwemo Halmashauri na majiji kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbunge. Vijana wanaojiunga na JKT kwa kujitolea ni wengi sana. Lazima

4 FEBRUARI, 2015

tukiri kwamba Serikali haiwezi ikawaajiri wote. Kwa hivyo kila mwaka watakuwepo baadhi ambao wanarudi majumbani kwa kukosa ajira katika vyombo vyatia ulinzi na usalama.

Kwa hiyo tunaomba asasi mbalimbali ziweze kuwachukua vijana hawa ambao kwa kweli wamefunzwa vyema.

Sasa swali la pili kuhusu ni kwa nini Serikali isiwasakiie vijana hawa kuwawezesha kwa mitaji ili waweze kujajiri. Kwa kweli ni wazo zuri sana na ni kweli kwamba vijana hawa wanapewa stadi za kazi katika baadhi ya kambi zetu ambazo kuna Vyuo vyta VETA na huwa wanatoka pale wakiwa na ujuzi wa aina mbalimbali.

Kwa hiyo, tutalizungumza suala hili na Wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Vijana, Wizara ya Kazi na Ajira pamoja na wadau wengine kwa ujumla wao, ili tuone njia bora ya kuwawezesha vijana hawa kwa vifaa na pengine mitaji ili waweze kujajiri wao na kuweza kuajiri wengine pia, ili kupunguza tatizo la ajira hapa nchini.

**MHE. HAMAD ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, Zanzibar kuna JKU ambayo shughuli zake ni kama JKT kwa huku Tanzania Bara. Kwa kuwa kwa vijana wa Zanzibar inakuwa shida sana kupata nafasi za kujunga na JKT.

Je, ni kwa nini kwa vijana wa Zanzibar kigezo kisiwe ni kwa wale waliopita JKU? Ahsante sana.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

4 FEBRUARI, 2015

Kwanza nimpe taarifa tu kwamba, vijana wanaojinga na JKT kuna mgawo kwa ajili ya Zanzibar. Kwa hiyo, kila mwaka tunapochukua vijana wa kujitolea kwenda JKT kuna idadi maalum inayopelekwa Zanzibar na utaratibu wa kuzigawa nafasi hizo uko sawa na upande wa Tanzania Bara. Kwa maana kwamba, nafasi hizo zinagawiwa Wilayani, nafasi hizo zinagawiwa Mikoani, na kadhalika.

Kwa hivyo, kuna kundi kubwa la vijana wa Zanzibar ambao wako katika makambi ya JKT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyotambua sisi ni kwamba, JKU inaandaa vijana kwa ajili ya ajira katika Idara Maalum za SMZ. Kwa hivyo, wanaomaliza JKU wanapata fursa ya kuingia katika Idara Maalum na wale vijana wa Zanzibar walioko katika Makambi ya JKT wakati wa ajira wanachukuliwa katika vyombo vyaa ulinzi na usalama kwa ujumla bila ubaguzi wowote.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Mara nyingi katika Wilaya zetu wakati wa kuwachagua hawa vijana wa kwenda JKT taarifa inakuwa imetoka na kwenda mijini na wanaokuja kuomba nafasi hizo na kupata mara nyingi wanatoka nje ya Wilaya husika. Isingekuwa vizuri sasa kwa Serikali kutoa maelekezo kwenye Kamati za Ulinzi na Usalama kwamba, angalao  $\frac{3}{4}$  ya vijana wanaochaguliwa watoke katika Wilaya husika?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kwamba, kuna sababu ya kwa nini tunagawa nafasi katika kila Wilaya. Lengo ni kwamba, vyombo vyetu vyaa Ulinzi na Usalama viwe vina uwakilishi kutoka kila Wilaya, kwa maana makabila yote yawemo katika vyombo vyaa ulinzi na usalama.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hili analolisema Mheshimiwa Ole-Nangoro kwamba, Mamlaka kwa maana ya Kamati za Ulinzi na Usalama zipewe maelekezo ya kuchukua vijana kutoka Wilaya hiyo, maelekezo hayo yapo kwao na tunaomba mtusaidie kuyasimamia kwa sababu, sio ¾ wanatakiwa wote watoke katika Wilaya husika. Kila Wilaya ina mgawo wake, hatuoni kwa nini Wilaya moja ikatoe nafasi kwa watu wa kutoka Wilaya nyingine.

Kwa hiyo, tunachosema ni kwamba, ni lazima watoke pale na hili tulisimamie kwa pamoja, ili vijana wa Wilaya husika wawe hao ndio wanaoteuliwa kuingia JKT kutoka kwenye Wilaya hizo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana tunaendelea. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı, Mheshimiwa Roman Selasini?

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, lakini mimi ninaitwa Joseph Roman Selasini. Roman Selasini ni Marehemu baba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo, ninaomba sasa Swalı langu Namba 87, lipatiwe majibu:-

Na. 87

#### **Viwango vya Ufaulu Kidato Kimoja Kwenda Kingine**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI** aliuiliza:-

Shule zisizo za Serikali huweka viwango maalum na tofauti vya ufaulu kutoka kidato kimoja kwenda kingine:-

(a) Je, Serikali, inajua na kuunga mkono utaratibu huu, hasa unapotumika kwa wanafunzi wa kidato cha tatu kwenda cha nne?

(b) Je, kwa nini Serikali haiweki kiwango elekezi kama utaratibu huo unakubalika?

4 FEBRUARI, 2015

(c) Je, shule inapomrejesha au kumkataa mwanafunzi wa kidato cha tatu, huku sio kukwepa majukumu ya malezi, unyanyasaji wa kisaikolojia na kuzingatia biashara zaidi kuliko kutoa elimu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**  
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundı, napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Rombo, lenye Sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwepo kwa utaratibu wa viwango maalum na tofauti vya ufaulu kutoka kidato kimoja kwenda kingine katika shule za Sekondari zisizo za Serikali. Napenda ieeweke kwamba, Serikali haiungi mkono utaratibu huo kwa kuwa, umekiuka Nyaraka za Elimu; Waraka wa Elimu Namba 12 wa Mwaka 2011 na Waraka wa Elimu Namba 4 wa Mwaka 2012. Kulingana na majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundı wakati akijibu Swali Namba 3 la tarehe 27 Januari, 2015 napenda kusisitiza kuwa, yejote atakayekaidi maelekezo haya ya Serikali atachukuliwa hatua kali ya kinidhamu kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Namba 25, Sura ya 353, Kifungu Namba 35.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Waraka wa Elimu Namba 6 wa mwaka 2011 umetoa maelekezo kuhusu wastani wa ufaulu katika mtihani kuwa ni 3% tu na si vinginevyo. Kiwango hiki ni kwa shule za Serikali na zisizo za Serikali.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, utaratibu huu uliowekwa na shule zisizo za Serikali haukulaliki na Serikali.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, kwa muda mrefu wamiliki wa shule hizi wameendelea kukaidi agizo hili la Serikali na hata mwaka

4 FEBRUARI, 2015  
huu shule nyingi zimekaidi. Mfano shule ya Stanley pale Mbagala, watoto waliofikia alama 50 waliondolewa shulenii wote.

Je, Serikali iko tayari kufanya uchunguzi wa shule hizi jeuri na kuwachukulia hatua mara moja, ili kuondoa dhana ya Serikali kudharauliwa na maagizo ya Serikali kutotekelizwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Ni kwa nini basi kama Serikali haiungi mkono jambo hili, isiweke kiwango elekezi kwa shule zote, ili kuondoa utaratibu wa shule kujiveka kiwango chake ambapo baadhi ya shule wameweka kiwango mpaka alama 60 ambazo ni wanafunzi wachache sana wanaweza kufikia?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Selasini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niseme kwamba, kuanzia leo, kuanzia tarehe 27 Januari, 2015 Serikali imefikia mwisho haitatoa Nyaraka tena wala haitatoa Barua kwa shule zisizo za Serikali kuendelea kuwaonya na kuwaelekeza kwamba, wasiendelee kukaidi.

Kuanzia tarehe 27 Januari, 2015 ambapo Mheshimiwa Waziri alitoa tamko hapa Bungeni la kuwa shule zote ambazo zitaendelea kukaidi zitachukuliwa hatua husika, naomba nitamke kwa mara ya pili kumwunga mkono au kusisitiza tamko la Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwamba, tutaanza kufanya uchunguzi kuanzia tarehe 27 Januari, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba, shule zote ambazo zitaendelea kukaidi, pamoja na nyie Waheshimiwa Wabunge amba mna shule kama mtaendelea kukaidi,

4 FEBRUARI, 2015  
tutachukua hatua kikamilifu ambazo zitafika mahali  
kwamba, shule zile zitafungiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swal i la  
Mheshimiwa Selasini, namba ya pili:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia ni Mwalimu.  
Walimu wote wanatakiwa waelewe kwamba, wanafunzi  
hawana uelewa sawa ndani ya darasa; kuna wanafunzi  
ambao wanachelewa kuelewa na kuna wanafunzi ambao  
ni very slow learner.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe wito wa shule  
zote za Serikali pamoja na zile ambazo siyo za Serikali  
kwamba, ni vyema basi ikaeleweka kwamba, Serikali  
imeweka kiwango maalum kwamba, ni alama 30 ndio  
alama ya ufaulu. Kwa wale wanafunzi ambao ni slow learners  
ni vyema Walimu wakaweka programu ambazo ni za  
kuwarekebisha wale wanafunzi, ili wawasadie na isiwe  
kwamba, kuwa na shule zisizo za Serikali ni biashara na siyo  
kutoa taaluma. (Makofi)

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti,  
ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa, Serikali ya Chama  
cha Mapinduzi (CCM) imeamua kufanya elimu ni biashara  
na sio huduma na hivyo kusababisha watu kupeleka watoto  
wao katika shule za binafsi.

Je, Serikali sasa ina mpango gani wa kuhakikisha  
kwamba, inaboresha shule zake za Serikali, ili kuondoa  
mtafaruku uliopo? (Makofi)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swal i la nyongeza  
la Mheshimiwa Susan Lyimo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwashakikishia  
Wabunge wote kwamba, sasa hivi Serikali ina mipango mingi  
sana ya kuboresha elimu hapa nchini. Sasa hivi tarehe 7  
Februari, 2015 Serikali itazindua Mpango Maalum wa KKK

4 FEBRUARI, 2015  
na ninaomba Waheshimiwa Wabunge wote muwepo  
kwenye uzinduzi huu.

Pia naomba niseme kwamba, hapa UDOM  
tumeanzisha Diploma za Juu za kusomesha Walimu wa  
Sayansi pamoja na Walimu wa Hisabati kwa nia ya  
kuboresha elimu nchini Tanzania.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunaendelea, Wizara ya  
Uchukuzi. Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa?

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa  
Mwenyekiti, kabla sijazungumzia swali langu naomba  
nichukue fursa pekee kuwapongeza Wabunge wanawake  
ambao wamekuwa Wenyeviti kama wewe; Mheshimiwa  
Lediane Mng'ong'o na Mama yetu Kidawa, ninawapongeza  
sana. Baada ya kusema hayo, sasa ningeomba swali langu  
Namba 88 lipatiwe majibu.

Na. 88

#### **Uwanja wa Ndege wa Zamani, Mbeya**

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA** aliuliza:-

Kiwanja Kipyta cha Ndege cha Kimataifa cha Songwe,  
kimekamilika na kiko umbali wa kilometra 25 toka Jiji la  
Mbeya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia Kiwanja cha  
Ndege cha Zamani cha Mbeya kwa matumizi chanya, kama  
hoteli kubwa?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa  
Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mary  
Machuche Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum, kama  
ifuatavyo:-

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, Kiwanja Kipyä cha Ndege cha Kimataifa cha Songwe kimeanza kutumika. Kiwanja hiki kipo umbali wa kilometra 25 kutoka katikati ya Jiji la Mbeya na kina uwezo wa kuhudumia ndege nne kubwa kwa wakati mmoja. Baada ya kuanza kutumika kwa kiwanja hicho, Kiwanja cha Ndege cha Zamani cha Mbeya kilifungwa. Hivyo ndege zote zinazoondoka au kufika Mbeya hutumia kiwanja kipyä cha Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Kiwanja cha Zamani cha Mbeya kufungwa kwa ndege zinazotua au kundoka, bado kuna baadhi ya vifaa na mitambo ambayo ipo katika kiwanja hicho. Vifaa na mitambo iliyopo katika Kiwanja cha Zamani ni ile ya kuongozea ndege zinazopita katika anga la juu la nchi (*Non-Directional Beacons*). Na Wizara ya Uchukuzi inafanya kazi matumizi bora ya eneo hilo na kuititia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeajiri Mtaalam ambaye anaandaa Mpango Kamambe wa Matumizi ya eneo hilo (*Land Master Plan*) amba rasimu yake itawasilishwa kwa wadau na uongozi wa Mkoa wa Mbeya kujadiliwa kabla ya kutekelezwa.

**MHE.DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nilikuwa na swali moja dogo sana la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Jiji hili la Mbeya lilishakuwa limeomba kwa muda mrefu sana juu ya matumizi ya uwekezaji mkubwa katika Uwanja huo wa Zamani wa Ndege amba o uko kwenye very strategic area. Sasa nilikuwa ninaomba, ili taswira ya Jiji la Mbeya iweze kuwa pia, ni nzuri yenye mwelekeo, niombe Serikali itueleze nini majibu ya ile barua tuliyokuwa tumeandika, wana-Mbeya waweze kusikia? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, kama ifuatavyo:-

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu, ni kweli, amekuwa analifuatilia hili jambo kwa karibu sana na anafahamu wananchi wa Mbeya pia, wangependa kuona sasa eneo hilo linapata matumizi mengine.

Lakini kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ni kweli, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wamekwishaajiri huyo Mshauri, ili aweze kutengeneza *Master Plan* ambayo uongozi wa Mbeya, akiwamo na yeye Mheshimiwa Mbunge, ndio watakaoipitisha na kama watakuwa na mpango mwingine mbadala, basi kabla ya *draft* ya mwisho ya mpango huo kutolewa wataweka maoni yao, ili iweze kukidhi haja waliyokuanayo. (Makof)

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swalii la nyongeza. Nikubaliane na Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, Uwanja wa Ndege wa Songwe umeanza kutumika, lakini haujakamilika! Ni kilio chetu cha muda mrefu sasa kwamba, ndege zinazotua Mbeya mara zifike pale zishindwe kutua zirudi Dar-es-Salaam na kuleta hofu kwa wananchi na wasafiri kwa ujumla! Tunapenda kujua abiria wanapoteremka kwenye ndege kama mvua inanyesha ni matatizo namna ya kufika kwenye lounge!

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua tangu tatizo la ndege kurudi Dar-es-Salaam...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliza moja tu! Sasa utayajua yote ya!

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua tangu ndege iliporudi kutoka Mbeya kurudi Dar-es-Salaam na abiria, suala ambalo ni la hatari, Serikali imechukua hatua gani za dharura mpaka sasa hivi? Jambo ambalo wananchi wa Mbeya na wasafiri kwa ujumla wanapenda kujua? (Makof)

4 FEBRUARI, 2015

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aliko Kibona, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, kulikuwa na tukio la ndege ya Kampuni ya Fast Jet kushindwa kutua katika Uwanja wa Ndege wa Songwe kwa sababu ya ukungu mkubwa uliokuwapo katika uwanja. Kwa sababu taa za kuongozea ndege hazijafungwa katika uwanja huo kwa hivyo, pilot alilazimika kutotua na kurudi na abiria Dar-es-Salam na huo ni uamuzi ambaeo ni sahihi kabisa na ni practice katika usafiri wa anga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, Serikali inalifahamu hili tatizo na ndio maana tunasema bado haujakamilika kikamilifu. Yako mambo mengi ambayo yanatakiwa kuwekwa katika Uwanja wa Ndege wa Songwe ikiwa ni pamoja na taa za kuongozea ndege na kukamilisha jengo la uongozaji wa ndege na la abiria, ambavyo bado sasa hivi havijakamilika kikamilifu.

Tutakapokuwa tumepeata fedha zote kama zilivyokuwa zimetengwa katika Bajeti haya mambo yote yatafanyiwa kazi. (Makof)

Na. 89

#### **Mauzo ya Tanzanite**

**MHE. KIDAWA H. SALEH** aliuliza:-

Nchi yetu imebarikiwa utajiri mwingi wa madini ya vito vyatya aina mbalimbali ikiwemo Tanzanite, ambayo haipatikani mahali popote duniani isipokuwa Mererani – Arusha:-

4 FEBRUARI, 2015

(a) Je, ni kiasi gani cha mapato yatokanayo na mauzo ya *Tanzanite* katika pato la Taifa kwa miaka 2011/2012, 2012/2013 na 2013/2014?

(b) Je, ni kiasi gani cha pesa kimepotea kutokana na vito vya *Tanzanite* kwa kuuzwa kwa njia isiyo halali katika kipindi cha 2011 – 2014?

(c) Ni nani wanunuzi wakubwa wa *Tanzanite* Duniani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES JOHN PAUL MWIJAGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu Swali Namba 89 la Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2011 hadi 2014 kiasi cha shilingi bilioni 5.92 kililingia katika pato la Taifa kama mrabaha baada ya kuuzwa kwa Madini ya *Tanzanite* kwa mchanganuo ufuatao:

Mwaka 2011 shilingi bilioni 1.24;  
Mwaka 2012 shilingi bilioni 1.53;  
Mwaka 2013 shilingi bilioni 1.69; na  
Mwaka 2014 shilingi bilioni 1.48.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vigumu kutambua kwa uhakika nini kiasi cha fedha ambacho kimepotea kutokana na mauzo ya *Tanzanite* kwa njia zisizokuwa halali, kwani watoroshaji hufanya uhalifu huo kwa siri.

4 FEBRUARI, 2015

Uchunguzi uliofanywa na Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA) umebaini kuwa, mwaka 2013 Tanzania iliuza *Tanzanite* yenyé thamani ya Dola za Kimarekani 37 wakati katika kipindi hicho India iliingiza *Tanzanite* yenyé thamani yenyé thamani ya takribani Dola za ki-Marekani milioni 300 kwenye Soko la Dunia na Kenya ilikadiriwa kusafirisha nje madini hayo kwa jina la Zoisite yenyé thamani ya Dola za ki-Marekani milioni 100.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, wanunuzi wakubwa wa *Tanzanite* Duniani ni Marekani, India, Hong Kong, Jamhuri ya Afrika Kusini, Sri-Lanka na Thailand.

**MHE. KIDAWA H. SALEH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri ametoa Taarifa ya utafiti ambayo inauma sana. Kwamba, Tanzania ni nchi pekee inayotoa vito hivi na mwaka 2013 Tanzania imeuza vito vyenye thamani ya milioni 37 tu za Kimarekani.

Wakati India na Kenya ambazo hazizalishi Madini haya zimeuza kwa zaidi ya Dola Milioni 400 za Kimarekani kutokana na uhalifu aliouzungumzia wa kuuza kwa siri.

Je, Serikali imechukua hatua gani, ili kumaliza uhalifu wa namna hii unaoiumiza nchi?

Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakilalamika hapa kuwa kwenye machimbo ya Mererani kuna wachimbaji wadogo wadogo ambao siyo Watanzania. Wameingiaje humu nchini na nani amewapa kibali cha kwenda kuchimba? Ahsante sana. (Makofij)

4 FEBRUARI, 2015

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES**

**J. P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Kidawa.

Nianze na sehemu ya pili. Mamlaka husika zikiongozwa na Kamishna wa Madini na Uhamiaji, hakikisheni watu wote wanaofanya kazi katika Mgodi wa Mererani ni raia wa nchi hii. Bwana Magayane wewe ni Kamishna pale Mererani, hilo ni jukumu lako, kabla hawajanisulubu mimi, wewe utasulubiwa mwanzo. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza ya swalii la Mheshimiwa Kidawa, anataka kujuua Serikali imefanya nini. Dawati la TMAA limeanzishwa kwenye viwanja vyatundege kujaribu kuwadhibiti wale wanaotorosha *Tanzanite*. Tunalenga ujenzi wa Kituo cha Madini pale AICC kusudi madini yanunuliwe pale na kuchakatwa pale. Tunaanzisha uanzishwaji wa Sheria ya Uongezaji wa Thamani Madini, lengo letu ni kuona madini yakiwa ghafi yanachakatwa hapa kusudi thamani iongezwe hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango wa kutoa motisha ya asilimia tano ya madini yatakayokamatwa kwa mtu atakayetoea taarifa apate hiyo asilimia tano na tuna imani kwamba, hiyo itatusaidia. Tunatengeneza utaratibu ambapo Sheria zitarekebishwa ili Kamishna au Polisi akikukamata una madini, hakuna cha kwenda Mahakamani kuweka Wakili, ukikamatwa yanachukuliwa. Kwa jitihada hiso tunajua kwamba, tutawakomesha watu hawa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mlata, Mheshimiwa Zitto na Mheshimiwa Sanya!

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Ninaomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba; pale Mererani kwa wale wachimbaji wadogo wanaozunguka machimbo ya Mgodi wa *Tanzanite One*, walifungiwa na vyombo vyao vilichukuliwa na haijulikani viko wapi na haijulikani ni nani

4 FEBRUARI, 2015

aliyewatuma wale walioenda kuwasulubu wachimbaji. Ninaomba kujua hatima ya migodi ile kufunguliwa na kurejeshewa vifaa vyao. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongenza la Mheshimiwa Martha Mlata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wachimbaji wadogo ambao wana mtifaruku Mererani, liko mezani mwa bosí wangu, Mheshimiwa Simbachawene na analiangalia kwa makini na atalitolea maamuzi.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, majibu ya Waziri ni utani, anajaribu kufurahisha Wabunge, kwa sababu suala hili la *Tanzanite* limekuwa kwenye mijadala ya Wabunge takribani miaka 20 sasa. Pendeleko lilitokuwepo ni kwamba, eneo la Mererani liwe protected area na wachimbaji wadogo tu ndiyo wachimbe na eneo hili litumike kwa ajili ya kuongeza thamani ya madini haya. Madini yanayotoka pale yawe tayari yameshakatwa kwa ajili ya kuongeza ajira na kuongeza thamani nchini. Tatizo lote la madini na njia za panya hayatakuwepo. Mambo haya tayari yametolewa mapendeleko kwenye Kamati ya Bomani, mambo haya yapo kwenye Sheria.

Serikali itaanza lini kutekeleza Sheria kuhakikisha pale Mererani panakuwa ni protected area, tunapata thamani halisi ya *tanzanite* yetu, vijana wanapata ajira na tunaondokana na hili tatizo la kuongelea Mererani kila mwaka? (Makofii)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mbunge wa Kigoma. Mtani wake na Zitto ni Mwijage siyo Waziri, Mwijage ndiyo mtani wa Zitto.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya majibu ni mapendekezo ya Kamati ya Nishati na Madini kwenye Taarifa yake ambayo mmeipitisha. Mimi nilisimama hapa nikasema nitayatekeleza. Nimeingia ofisini jana utani unatoka wapi! (Makofi)

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nataka kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa kunakuwa na protection katika *World Trade Organization*; na kwa kuwa kuna baadhi ya nchi hutoa bidhaa hata kama ni ndogo lakini zinakuwa na *trade mark* yake; tuchukulie mfano mdogo tu ni chai na mdalasini unaotoka Sri-Lanka, huwezi kusafirisha bila kutumia nembo yao ambayo wao wameikubali na inakubaliwa na Jumuia za Kimataifa. Je, Tanzania tumeshindwaje sisi na ni *unique place* ambayo inatoa *tanzanite* kuweza kuitengenezea *trade mark* ambayo haitachezewa na nchi nyingine yoyote ambayo inachukua bidhaa hiyo kutoka Tanzania na kuuza? (Makofi)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa majibu kwa swali la Mheshimiwa Sanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza kutoka sakafu ya moyo wangu, ushauri anaoutoa Mheshimiwa Sanya, yako kwenye Kamati ya Nishati na Madini. Hili suala la *tanzanite* kwa wale ambao wanalisikia, siyo rahisi kama livilyo. Yapo mazito sina muda wa kuyaeleza. Liko kwenye meza ya Waziri, kuna maamuzi makubwa yatakayofanyika. Ngoja niwaambie, tumefikia hatua, Kamati imependekenza kwamba, Tanzania *tu-control ile supply*, kwa sababu sisi ndiyo *supplier* pekee tuweze ku-determine price. Haya siyo maneno yangu, ni maneno ya kwenye Kamati, kwa hiyo, yanayozungumzwa yamezungumzwa kwenye Kamati. Siwezi kutania ofisi hii, siwezi kutania sehemu hii. (Makofi)

4 FEBRUARI, 2015

Na. 90

**Faida Itokanayo na Uwekezaji - Eneo la TIPPER**

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE (K.n.y. MHE. MARIAM N. KISANGI)** aliuliza:-

Serikali imeingia ubia na Mwekezaji katika eneo la *TIPPER*:

- (a) Je, Serikali imepata faida gani kutokana na uwekezaji huo?
- (b) Je, kwa nini mpaka sasa hakuna uendelezaji mkubwa katika eneo la *TIPPER*?
- (c) Je, ni lini uboreshaji wa mazingira ya *TIPPER* utakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali namba 90 la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kunufaika na uwekezaji wa *TIPPER* kwa kupata hifadhi kubwa ya mafuta kwa ajili ya soko la ndani na nje. Pia imeweza kupata gawio la shilingi bilioni 4.4 kwa kipindi cha miaka mitano (2009 mpaka 2013).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ya *TIPPER* ina uwezo wa kuhifadhi mita za ujazo 141,000 za mafuta yaliyosafishwa. Kampuni ya *TIPPER* inafanya ukarabati wa matanki yenye mita 72,000 za mafuta na kufanya hifadhi hiyo kuwa na jumla ya mita za ujazo 213,000 za mafuta pindi ukarabati huo utakapokamilika. *TIPPER* ina mpango wa kupanua hifadhi hiyo mpaka kufikia uwezo wa mita za ujazo 315,000 za

4 FEBRUARI, 2015

mafuta ifikapo mwisho wa mwaka 2015. Kwa sasa kampuni hiyo iko katika taratibu za kupata fedha kwa ajili ya ukarabati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *TIPPER* inaendelea kuboresha mazingira ya eneo hilo hatua kwa hatua, kwa kuondoa miundombinu iliyochakaa na kurejesha ama kujenga miundombinu mipya pale inapobidi. Shughuli zote za Kampuni ya *TIPPER* zinaendeshwa kwa kuzingatia usalama wa afya na mazingira na usalama wa wafanyakazi.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muuliza swali la msingi amekuja, nitaomba kupata fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza kwa ridhaa yako.

**MWENYKITI:** Unasema?

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Muuliza swali amefika, Mama Kisangi yupo, nitaomba fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza baada ya yeye kuuliza maswali ya nyongeza, kwa ridhaa yako.

**MWENYEKIDI:** Mimi nimekuruhusu wewe Mheshimiwa Ndugulile!

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuniruhusu kuuliza maswali ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Kampuni hii ya *TIPPER* ipo katika Jimbo la Kigamboni na inahusika sana na masuala ya utunzaji wa mafuta. Nilitaka kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri; ni nini *corporate social responsibility* ya Kampuni hii kwa Wilaya ya Temeke pamoja na Jimbo la Kigamboni hususan sasa hivi ambapo tunaelekea kujenga Kituo cha Zimamoto na matanki haya ya mafuta ni moja ya hazard ya masuala ya moto katika Jimbo la Kigamboni?

4 FEBRUARI, 2015

(ii) Kampuni hii ilipoanzishwa lengo lake lilikuwa ni kusafisha mafuta (*refinery*), lakini imegeuzwa majukumu na sasa hivi imekuwa ni sehemu ya kuhifadhi mafuta (*reserve*). Natambua kwamba, Serikali sasa hivi ina mkakati wa kuanzisha tena *refinery*. Je, iko tayari kubadilisha malengo ya Kampuni hii kurudi katika masuala ya *refinery*?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu corporate social responsibility, mahusiano ya jamii na Kampuni; natambua kwamba, Kigamboni kuna makampuni mengi yamejenga hifadhi pale; iko *Lake Oil, Moil, Hass Petroleum, TIPPER* na *World Oil*. Sina takwimu nani amelipa corporate social responsibility. Nawaomba wenye makampuni, mkitaka kulipa corporate social responsibility, mumjulisha Mbunge wa sehemu husika. Ukimjulisha Mbunge, yeye hataniuliza mimi maswali. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kigamboni na mambo ya usalama na moto; nawapongeza Wananchi wa Kigamboni kwa kuamua kujenga Kituo cha Zimamoto. *TIPPER* inamilikiwa asilimia hamsini na Serikali, asilimia hamsini na huyo mwekezaji wa nje. Nawaomba ninyi wabia wawili, lazima mkae na Wananchi wa Kigamboni, mchangie kituo hicho, kwa sababu bidhaa mnayotunza ni hatari kwa wananchi.

Mheshimiwa Mbunge wa Kigamboni, nakuahidi wiki ijayo nitatembelea eneo hilo, kwa sababu mimi nilikuwa Mtaalamu wa Usalama na Mazingira, kwa hiyo, utakuwa umenirudisha kazini. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ngoja, swalii la pili kwanza.

4 FEBRUARI, 2015

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES**

**J. P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina jibu kuhusu mipango ya Serikali kujenga refinery, tusubiri Serikali itatoa maamuzi yenyewe. Nitalifikisha mbele ya safari.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Swali ambalo nilitaka kuuliza Mheshimiwa Waziri ameligusia kidogo, lakini nataka kuweka msisitizo.

Kwa kuwa inavyoonekana bei za mafuta ghafi, / mean raw oil, inazidi kuteremka, isingekuwa sasa wakati mwafaka kwa Serikali kuangalia uwezekano wa kuharakisha uwekezaji katika refinery kuliko kuendelea kununua mafuta ambayo tayari yameshachakachuliwa na unajua yale yaliyosafishwa bei zake hazishuki kwa kasi kama mafuta ambayo hayajawa refined?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES**

**J. P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Cheyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu swali hili, naomba nitoe taarifa mbele ya Bunge kwamba, tofauti na jana, leo bei za mafuta zimebadilika katika Soko la Dar es Salaam, ambako diesel imeshuka kwa shilingi 138 kutoka shilingi 1,846 mpaka shilingi 1,708; mafuta ya petroli yameshuka kutoka shilingi 1,955 mpaka 1,768; mafuta ya taa yameshuka kutoka 1,833 mpaka shilingi 1,657.

Wito wangu, Watanzania mnaotumia mafuta, angalia pump price kabla hujanunua. Vilevile niwaombe watu wa EWURA, wahakikishe watu wa Mikoani wanajua taarifa za pungozo la mafuta kusudi wasipunjwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, nijibu sasa swali la Mheshimiwa Cheyo. Inahitaji busara katika kuamua kujenga refinery. Ziko refinery mbili sasa duniani kwa upande wa kwetu zinazo-supply mafuta ambazo zinatuhangaisha. Refinery moja iko India inamilikiwa na Alliance na nyingine iko Saudia. Pamoja na kuwa tija haitokani na kuwa na refinery,

4 FEBRUARI, 2015

tija ni kutokana na refinery kubwa inayokupa economies of scale. Ukijenga refinery ya kuchuja mapipa 3,000, mwenzako anachuja mapipa 100,000 kwa saa, huwezi kushindana naye. Kwa hiyo, tija siyo hiyo.

Jambo la pili siyo kuchuja mafuta tu, ni kuchuja mafuta na kupata mahali pa kuyauza. Unaweza ukachuja mafuta ukakosa mahali pa kuyauza. Kushuka kwa mafuta siyo nafuu tu, unaweza ukachuja mafuta halafu yakaja yakapanda bei, ikakuletea tatizo ukakuta una mzigo wa bei kubwa. Kuna mambo mengi ya ku-consider, lakini nimesema liko mbele ya safari, Serikali itafanya maamuzi.

Na. 91

#### **Utandawazi na Utamaduni Wetu**

**MHE. AMINA M. MWIDAU** aliuliza:-

Utandawazi unaathiri kwa kiasi kikubwa utamaduni wa kila Taifa kwa sababu watu wengi wanajifunza kuitia mitandao mbalimbali kama kompyuta, smart phones na television:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kulinda utamaduni wetu?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli utandawazi na teknolojia vinaleta mabadiliko na athari kwa kiasi kikubwa katika utamaduni na Mataifa mbalimbali ikiwemo Tanzania. Vipindi vyaa habari, burudani, muziki, filamu, mavazi na chakula kutoka nje, visivyoendana na maadili, mila, desturi

4 FEBRUARI, 2015

na Utamaduni wa Mtanzania, hutazamwa na kuigwa na Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mikakati kadhaa kulinda Utamaduni wa Mtanzania. Kwanza, ni kuhuisha na kuimarisha Sera, Sheria na Kanuni mbalimbali, zitakazoweza kudhibiti matumizi ya teknolojia na athari za utandawazi; mfano, Sera ya Habari, Sera ya Utamaduni, Sera ya Vijana na Sera ya Michezo ili kusisitiza, kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu wajibu wao wa kulinda maadili, mila, desturi na Utamaduni wa Mtanzania na kuweka mbele masilahi ya Taifa letu. Aidha, Serikali itaendelea kuhamasisha jamii kuongeza uzalishaji wa bidhaa na huduma zenye kuimarisha utambulisho wa nchi kuzinunua na kuzitumia.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa utamaduni ni kielelezo kikubwa cha utaifa wa nchi yoyote ile; na kwa kuwa utandawazi unaenda kwa kasi sana na Mheshimiwa Waziri amekubaliana na mimi katika jibu lake la msingi hapa na unaharibu nchi nyingi sana kwa kiasi kikubwa. Je, Serikali imeshafanya tafiti zozote zile zinazoonyesha athari ni kwa kiasi gani utamaduni wetu umeathirika?

(ii) Kwa kuwa kasi ya utandawazi ni kubwa sana na kasi ya Serikali katika kuhuisha na kuimarisha hizo Sera, Sheria na Kanuni ni ndogo sana; mfano mdogo tu, tuliomba hapa Sheria ya Vyombo vya Habari, mpaka leo mwaka wa nne huu kimya. Kundi kubwa sana linaloathirika na kasi hii kubwa ni vijana na vijana ndiyo nguvu kazi ya Taifa. Je, Serikali haioni kuwa kasi hii ndogo mno waliyonayo itaangamiza nguvu kazi ya Taifa na kupoteza tamaduni zetu zote?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Amina Mwidau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

4 FEBRUARI, 2015

Serikali kwa upande wake kwa kuhakikisha kwamba, maadili, utamaduni na mila za Mtanzania zinalindwa na kuhifadhiwa na kuheshimika, tuna vyombo mbalimbali ambavyo vinasimamia jambo hili. Kwanza, tuna Bodi ya Filamu ambayo inasimamia filamu zote zinazotoka nje na zile za ndani ili kuhakikisha filamu zinazoingia kwenye soko na kuonekana kwa Watanzania ni zile ambazo zinafuata maadili ya Mtanzania. Tuna Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), ambalo nalo kazi yake ni ku-regulate lugha. Japo tumekuwa na matatizo sana ya lugha yetu ya Kiswahili, hata hapa ndani ya Bunge ni rahisi tu kusikia mtu amesema mimi kama Serikali au mimi kama Mbunge, kwa Kiswahili siyo sahihi, Profesa Kahigi anaweza kutusaidia. Tuna Kamati ya Maudhui ambayo iko chini ya TCRA, kazi yake ni kusimamia maudhui yanayotoka katika vyombo vyote vya habari na tumekuwa tukiendesha tafiti mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, (b) kama ulivyosema kwamba kasi ya kushughulikia jambo hili ni ndogo, si sahihi sana, ni kwamba; vyombo hivi vinafanya kazi yake, pengine kasi ya kutoa habari kwa wananchi ndiyo ndogo. Kwetu sisi tutasisitiza kwamba, kasi ya kutoa habari kwa wananchi namna gani Serikali inafanya kudhibiti masuala haya, tuweze kuiongeza kidogo na mimi nakushukuru kwa ushauri wako.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa wasanii wetu hapa nchini wanaiga sana mambo ya Magharibi na filamu zao nyingi wanazozionyesha zinakiuka maadili ya Mtanzania. Je, ni hatua gani mmechukua mpaka hivi sasa kuzuia filamu ambazo hazina maadili kwa Watanzania wengi wakiwemo watoto?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, alichosema ni kweli, ziko filamu mbalimbali zinaingia nchini. Kama nilivyosema, vyombo mbalimbali vinasimamia; kwa mfano, Bodi ya Filamu, hakuna filamu inayoingia katika soko kwa sasa bila

4 FEBRUARI, 2015

kutazamwa na kuruhusiwa na Bodi ya Filamu. Ziko filamu nyingi zimezuiwa na tunaendelea kuchukua hatua hiyo. Sisi kwa upande wetu tunahakikisha filamu inayoingia katika soko, haiharibu utamaduni wa Mtanzania. Inawezekana zikapita kwa njia ya panya na zile zinazopita kwa njia ya panya zinaingia katika soko. Vipo vyombo vingine ambavyo tumeviweka kwa ajili ya kuzuia na ikiwezekana kukamata. Zipo filamu mbalimbali zimeteketezwa kwa sababu zinakiuka maadili ya Mtanzania.

Na. 92

**Fidia kwa Wananchi wa Misenyi Kutokana  
na Vita vya Kagera**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA** aliuliza:-

Hadi sasa Serikali imekwishapokea takribani shilingi bilioni 15.5 kutoka Nchi ya Uganda kama fidia kutokana na uvamizi wa nchi hiyo wakati wa Vita ya Kagera ambayo iliyathiri Wakazi wa Mkoa wa Kagera:-

Je, Wilaya ya Misenyi wamefidiwa kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA)**  
aliijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mbunge wa Viti Madalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, tangu Vita ya Kagera imalizike mwaka 1979, Serikali ya Tanzania imepokea takribani Shilingi za Kitanzania shilingi bilioni 15.5 kama fidia itokanayo na athari ya vita kutoka Serikali ya Uganda kulingana na makubaliano yaliyofikiwa. Serikali ya Uganda ilitakiwa kulipa fidia Tanzania kiasi cha Dola za Marekani milioni 18.4, lakini hadi leo imeweza kulipa kiasi cha Dola za Marekani milioni 9.7 tu. Fedha hizo zilipokelewa zikaingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kufidiana kwa hasara zinazotokana na vita, yaani war reparations, zinaongozwa na Sheria Kanuni za Kimataifa na utaratibu wa kutathmini kiwango cha hasara pia una vigezo vinavyotambulika. Licha ya kwamba, vita ilianzia eneo ambalo sasa liko Wilaya ya Misenyi, athari zake ziligusa Taifa zima la Tanzania kwa namna mbalimbali. Hivyo basi, Wilaya ya Misenyi, Mkoa wa Kagera, kama ilivyo maeneo mengine ya nchi yetu, imepokea fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, ambayo imekusudia kusukuma maendeleo ya wananchi wa maeneo hayo, katika kipindi chote hiki kilichofuatia Vita ya Kagera.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninayo maswali mawili ya nyongenza.

(i) Ninakubaliana kwamba kweli vita huchangiwa na kodi za wananchi wote kama ilivyokuwa katika Vita ya Kagera. Vita ni maafa kama maafa mengine, kwa hiyo, wale waathirika wa moja kwa moja wanastahili kuwekewa mkakati wa kuinua uchumi wao. Je, kwa maneno haya ambayo yamesemwa kwamba Kagera imesaidiwa, Serikali haioni kuwa haikutimiza wajibu wake kushindwa kuwasaidia waathirika wa moja kwa moja wa eneo hilo la Misenyi ili waweze kuinua uchumi wao?

(ii) Wananchi wa Misenyi wamekuwa wakiweka juhudzi zao wao wenyewe kuinua uchumi wao na hii vita sasa ni takribani miaka 36. Ukifika katika eneo la Kyaka pale Mji Mdogo, utakuta ni jinsi gani wanawake wanavyohangaika kuchoma ndizi na wale ni waathirika, miaka 36 ni mingi, ambao aidha ni watoto wa wazee waliopoteza maisha, mashamba yao na makazi. Kwa kuwa sasa kuna deni la takribani dola milioni nane point something; kama zitalipwa mtawafikiriaje kuwasaidia hawa akina mama kuinua uchumi wao? (Makofi)

4 FEBRUARI, 2015

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyo sema awali, vigezo vya kulipa fidia ya vita (*war reparations*), vina misingi mingi. Kwa bahati nzuri hili ni somo ambalo limeanza miaka mingi, kuna masuala ya *Treaty of Versailles* baada ya Vita vya Kwanza ya Dunia, *Treaty of San Fransico* iliyobaini namna ya kulipa fidia baada ya Vita ya Pili ya Dunia. Kwa hiyo, wakati wa Serikali ya Awamu ya Tatu, maana fidia hii haikuja baada ya vita, ilijadiliwa na Serikali ya Mheshimiwa Mzee Mkapa, ndiyo waliokuwa wakafikia milioni 18 hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme tu kwamba, kwa Vita ya Kagera na gharama tulioingia Tanzania, bado milioni 18 ilikuwa ni ndogo as US Dollars, lakini tukafikia pale na wao wakalipa milioni tisa. Hasara iliyopatikana Tanzania kwa vita haikuwa ya Misenyi peke yake, ilikuwa ya Taifa zima; na ndiyo maana hata Mwalimu alipotangazia vita nchi hii hakusema Misenyi inakwenda vitani, alisema Tanzania tunakwenda vitani. Maaskari wakatoka Zanzibar, Mtwara na sehemu nyingine. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi yanayojadiliwa kwenye ile fidia ya Serikali. Ninaomba niseme tu kwamba, ukiachia fidia kwa *prisoners of war*, kwa wanajeshi na kadhalika na familia zao, bado baada ya pale Serikali imefanya jithada za makusudi na ndiyo maana hata kwa sisi wote ambao tumekwenda Kyaka, Kyaka ya leo siyo Kyaka ya mwaka 1979. Kwa hiyo, naomba niseme katika hali hiyo, Serikali imetimiza wajibu wake kwa kusimamia na kusukuma maendeleo ya Wananchi wa Wilaya ya Misenyi kama tunavyofanya kwa wilaya nyingine.

Mheshimiwa Mwewayekiti, hili suala la pili naomba niseme tu kwamba, hii dola milioni tisa iliyobaki, tutaendelea kuzungumza na Uganda kuona namna itakavyolipa. Kwenye masuala ya war reparations, Japan wametumia miaka sitini kulipa madeni yaliyotokana na Vita ya Pili vya Dunia na ni Taifa kubwa na lenye uwezo. Kwa hiyo, kutegemea Waganda hata hiki kitu kidogo, tutaendelea kuzungumza nao walipe hili deni.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama pesa zingine zote zinazoingia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, tutatumia pesa hizi kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania wote, ikiwa ni pamoja na Wananchi wa Misenyi.

Na. 93

**Fedha Zilizokaa Muda Mrefu Kwenye Mifuko  
ya Hifadhi ya Kijamii**

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED** aliuliza:-

Taasisi za Fedha na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii hapa nchini, zimekuwa na fedha ambazo zimekaa muda mrefu bila kuchukuliwa na wenyewe kutokana na sababu mbalimbali ambapo Hazina huendelea kupeleka makato yao (*unclaimed assets*):-

Taasisi za Fedha na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii hapa nchini, zimekuwa na fedha ambazo zimekaa muda mrefu bila kuchukuliwa na wenyewe kutokana na sababu mbalimbali ambapo Hazina huendelea kupeleka makato yao (*unclaimed assets*):-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani na fedha hizo?
- (b) Je, ni kiasi gani cha fedha hizo kipo mpaka sasa?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

- (a) Mifuko ya Hifadhi ya Jamii hupokea na kuwekeza michango ya Wanachama katika vitega uchumi mbalimbali kwa madhumuni ya kupata faida ambayo inatumika katika gharama za uendeshaji na malipo ya

4 FEBRUARI, 2015

mafao. Ni kweli kwamba, baadhi ya mafao huchelewa kulipwa na Mifuko hii kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo:-

- (i) Kutokujua taratibu za mafao ya mirathi pindi Mwanachama anapofariki;
- (ii) Migogoro iliyopo ya ugawaji wa mirathi;
- (iii) Kutokuwepo na kumbukumbu thabiti zinazohitajika wakati wa kulipa mafao ya mirathi; na
- (iv) Kutokuwepo na miongozo sahihi na elimu kuhusu mafao kwa Wanachama.

Hivyo basi, kutokana na sababu hizo, fedha hizi hubaki katika Mifuko ya Hifadhi za Jamii hadi taratibu husika za mafao zitakapokamilika na kulipwa kwa Wanachama au mrithi wa mafao mara taratibu zinapokamilika.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vigumu kufahamu takwimu halisi za kiasi cha fedha ambazo hazijachukuliwa na Wanachama au warithi katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Hii ni kutokana na ukweli kuwa, madai ya mafao hufanyika kila siku pindi taratibu za ulipaji zinapokamilika. Hivyo, takwimu sahihi za kiasi kilichopo katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii hubadilika kila mara. Mamlaka ya Uhibiti na Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii, imeweka mtathmini kutoka Shirika la ILO, kuangalia suala hili kwa undani na kushauri hatua za kuchukua.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Rajab Mbarouk!

Waheshimiwa Wabunge, kama kuna mtu amewasha mike yake hebu aizime.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nasikitika kwamba, maswali yangu hayakupata majibu yenyeye kustahiki, kwa sababu Serikali inajua kwamba hizi fedha zipo na ziko nyingi na ziko katika

4 FEBRUARI, 2015

*unclaimed account.* Sasa leo Serikali inapokuja na majibu ya kwamba, fedha hizi hawajui ni kiasi gani, mnasema uongo mchana ninyi Serikali! Hizi fedha ndizo ambazo ninyi CCM mnazichukua na kwenda kuzitumia katika kufanya mambo yenu na nydingine mnazikopa ninyi Mawaziri, kwa sababu ziko katika *unclaimed account*, leo mtaniambia Serikali ninyi mnatoa *financial statement* ya kila mwaka?...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbarouk, tulikubaliana tuwe na mijadala ya kiungwana. Tumekubaliana usitaje majina ya watu au vyombo vya watu au vyama vya watu. Tumekubaliana hilo na tunaendelea hivyo hivyo na siyo chama hicho ulichokitaja, chama chochote haturuhusu kutaja humu ndani bila uthibitisho wowote. Habari ndiyo Bwana Wenje. (Kicheko)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu!

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijauliza swali bado.

**MWENYEKITI:** Haya uliza swali.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naheshimu Kiti chako.

Katika majibu ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba, hizi fedha hawazifahamu na hawajui ni kiasi gani na wameitaka ile ILO sasa kufanya uchunguzi wa fedha hizi. Sisi tuna Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hapa nchini. Je, ni lini Serikali itamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuangalia hizi fedha ni kiasi gani? (Makofij)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Mbarouk, kwa niaba ya Serikali na si kwa niaba ya Vyama, kama ifuatavyo:-

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekit, tumesema hizi fedha zinafanyiwa tathmini na wenzetu wa ILO, lakini kama alivyosema mwenyewe, Ripoti hii na mimi nina uhakika, Mheshimiwa Mbarouk, ametoa taarifa hii kwenye Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Mimi nataka nimhakikishie kwamba, Serikali kila siku inaendelea kutekeleza mapendekezo ya CAG kwenye masuala mbalimbali. Katika hili, CAG ana mapendekezo ambayo tunaendelea kutekeleza na moja ya mapendekezo ni kufanya tathmini ya fedha hizi ambazo ni *unclaimed* ili ziweze kujulikana na kama hazina wenyewe kabisa ziende kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba Mheshimiwa Waziri wa Kazi, naomba kuongeza katika majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza.

Sisi kama Serikali vilevile tumeona kuna haja kubwa ya kuanzisha sheria ya kuweka namna gani hizi *unclaimed assets* zingeweza kutumika. Hii tayari tumeshaanzisha paper, tunatarajia kuanzisha policy as well na baadaye iwe sheria. Kwa sababu hizi *unclaimed assets* haziko kwenye pension funds peke yake, lakini ziko banks na vilevile katika capital markets; ziko sehemu nyingi. Kwa hiyo, tunatarajia tutakuwa na hiyo sheria ya kuonesha jinsi ya kutumia *unclaimed assets*. Ahsante. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa!

Na. 94

#### **Kuyafutia Miliki Mashamba Pori Jimbo la Kibaha Vijijini**

**MHE. HAMOUD A. JUMAA** aliuliza:-

Kuna kero ya mashamba pori katika Jimbo la Kibaha Vijijini, kuna takribani mashamba themanini (80) ya Ngeta, Vikuge, Mpiji, Kikongo, Dutumi, Misufini, Mlandizi, Msongola,

4 FEBRUARI, 2015

Kwala, Mperamumbi, Disunyara, Lupunga, Bokomnemela, Minazi Mikinda, Mkuza Mkwala, Vikuruti na Soga ambayo yametumiwa ilani ya kufutiwa milki (*Notice of Revocation*):-

Je, ni lini Serikali itayafutia milki mashamba hayo na kuirudisha ardhi hiyo kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO  
YA MAKAZI alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijiini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ilipokea mapendelekezo ya ubatilisho wa mashamba pori yaliyopo katika Mkoa wa Pwani kutoka Ofisi ya Mkuu ya Mkoa wa Pwani kuititia barua ya tarehe 12 Julai, 2012 yenye Kumb. Na. Ba.8/158/07/16 ili milki za mashamba hayo ziweze kubatilishwa. Hata hivyo, Wizara yangu haikuweza kushughulikia mapendelekezo hayo kwa kuwa taratibu za awali za kutuma ilani ya kufuta milki kwa wamiliki wa mashamba hayo hazikufanyika kama ambavyo Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 inavyoelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoptana na hali hiyo, Wizara yangu ilizandikia barua Halmashauri zote za Mkoa wa Pwani, iliyoelekeza taratibu sahihi zinazopaswa kufuatwa katika ufutaji wa milki. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha ilipewa maelekezo na Wizara yangu kwa barua ya tarehe 7 Oktoba, 2013, yenye Kumb. Na. LD/285657/31 kuwa wanatakiwa kutuma ilani ya siku 90 kwa wamiliki kwa mujibu wa kifungu cha 48(1) cha Sheria ya Ardhi. Vilevile kwa kutumia Fomu ya Ardhi Namba 11 iliyopo katika Kanuni za Sheria ya Ardhi za Mwaka 2001. Kwa sasa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha iko katika hatua ya kutangaza katika Gazeti la Serikali, mashamba yote yaliyotelekezwa na kukiuka masharti kwa mujibu wa Sheria za Ardhi ili yaweze kubatilishwa. Baada ya hatua hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, itawasilisha mapendelekezo rasmi Wizarani kwangu ili Waziri mwenye

4 FEBRUARI, 2015

dhamana ya ardhi, aweze kuwasilisha kwa Mheshimiwa Rais, mapendekezo ya ubatilisho wa milki za mashamba hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuziagiza Halmashauri zote nchini, ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, kuwasilisha Wizarani mapendekezo ya ubatilisho wa milki za mashamba yote ambayo yamevunja masharti ya milki na yaliyotekelizwa, kwa kuhakikisha mapendekezo hayo yanafuata Sheria, Kanuni na taratibu za ubatilisho, kwa mujibu wa Kifungu cha 48(1) na Kifungu cha 51 cha Sheria ya Ardhi (Na. 4) ya Mwaka 1999.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba Maendeleo na Makazi, lakini nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri anakiri katika maelezo yake kwamba jambo hili limechukua muda mrefu; na kwa kuwa jambo hili limechukua muda mrefu na Wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijiji wanahitaji kuwa na ardhi; na kwa kuwa wawekezaji ambao wamechukua mashamba haya hawayafanyii shughuli za kilimo. Je, ni lini Serikali itayatwaa mashamba haya ili wananchi waweze kuondokana na matatizo ya ardhi waweze kufanya shughuli zao vizuri?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO**  
**YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nimpongeze Mheshimiwa Hamoud Jumaa, kwa namna ambavyo anaafuatilia masuala mazima ya maendeleo ya ardhi nchini. Naomba nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge, kama ambavyo nimejibu katika swali la msingi; kinachosubiliwa hivi sasa ni kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha kukamilisha mchakato wa kutangaza katika Gazeti la Serikali ilani ya utekelezaji kwa mujibu wa kifungu cha 51(2).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa ambazo nimezipata ni kwamba, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha,

4 FEBRUARI, 2015

haijaweza kutenga pesa kwa ajili ya jukumu hili. Ukiangalia mashamba yaliyotelekezwa katika Mkoa wa Pwani ni takribani ekari zaidi ya 83,000, lakini katika Jimbo tu la Kibaha Vijiji ni ekari 40,000. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge na niiagize Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, ekari 40,000 kutelekezwa ni jambo ambalo halipaswi kufanyiwa mzaha hata kidogo. Tunawapa siku saba, Gazeti hilo la Serikali liwe tayari limeshatolewa ili tuweze kuendelea na hatua zingine. (Makof)

Na. 95

### **Historia na Taarifa za Madereva Kujulikana Wazi**

**MHE. SHAFFIN AHMEDALI SUMAR** aliuliza:-

Ajali za barabarani zimekuwa zikiongezeka siku hadi siku na kusababisha madhara mengi ikiwemo ulemavu na vifo:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka wazi taarifa na historia za madereva wote kwa kutumia vyombo kama tovuti ili kuwadhibiti na kutathmini utendaji kazi wao kabla ya kuwaajiri kwani wengine hukimbia baada ya kupata ajali na kuajiriwa sehemu nyingine?

**MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar, Mbunge wa Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kumekuwa na ongezeko la matukio ya ajali za barabarani. Ongezeko hili halijafumbiwa macho bali kumekuwepo na jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika kukubaliana halo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mradi wa Maboresho ya Leseni za Kielektroniki (*Electronic Drivers*

4 FEBRUARI, 2015

License), imekuwa ikiweka wazi taarifa na historia za madereva wote, kwa kutumia tovuti ya kumbukumbu za wamiliki wa leseni za udereva ili kuwadhibiti madereva wazembe. Hatua mbalimbali zimepangwa kuchukuliwa dhidi yao ikiwa ni pamoja na kuwafutia leseni za udereva chini ya Mfumo wa Nukta (*Point System*) na hivyo kutoweza kupata leseni nyingine mahali popote. Aidha, SUMATRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, wameanzisha utaratibu wa kutangaza kwenye vyombo vyahabari, majina ya madereva wote wa mabasi na malori, wanaosababisha ajali kwa uzembe. Picha za madereva wanaofungiwa leseni zao zitatangazwa kuititia vyombo mbalimbali vyahabari na mawasiliano ili kukomesha tabia ya uzembe kwa madereva.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mwisho wa maswali ni saa nne na nusu, sasa hivi bado nina maswali mengine matatu. Mheshimiwa Esther nilitaka nikupe nafasi, lakini sasa nimeshindwa kutockana na hiyo *constrain*, kwa hiyo, unaweza ukateta na Mheshimiwa Waziri baadaye akakujibu.

Mheshimiwa Sumar!

**MHE. SHAFFIN AHMEDALI SUMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili.

(i) Katika majibu ya msingi, Mheshimiwa Waziri ametueleza kwamba, Serikali huwa inaweka wazi taarifa na historia ya madereva wazembe katika tovuti. Naomba atufahamishe hiyo tovuti inaitwaje, lakini pia atujulishe tukio linapotekea mpaka taarifa ianze kupatikana katika tovuti inachukua muda wa siku ngapi?

(ii) Kwa kuwa tayari tuna leseni za ki-electronic na tunaweza kabisa kuhifadhi historia na taarifa ya madereva katika leseni ki-electronic. Kwa nini Serikali haianzishi utaratibu wa kuwa na mfumo ambao hata askari wa usalama wa barabarani waweze kusoma historia na taarifa za madereva kwa kutumia vifaa vinavyohitajika?

4 FEBRUARI, 2015

(iii) Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na matukio mengi ya ujambazi barabarani hasa Barabara ya Msata na Bagamoyo, japokuwa kuna Kituo cha Polisi kinajengwa kwa kusuasua pale Kiwangwa. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuharakisha hicho kituo kijengwe ili ujambazi wa barabarani uweze kudhibitiwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi tu na Polisi wote na IGP wako hapa leo.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mengi ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Tovuti iko chini ya SUMATRA. Taarifa zinapelekwa mara moja katika tovuti hiyo mara tu zinapopatikana. Uwezekano wa Trafiki kusoma kutokana na leseni pale anapomkamata mtu ni wazo zuri, lakini bado hatujafikia hatua hiyo, hatukawa na card readers, lakini ni wazo zuri na mimi nitenda nikalifanyie kazi.

Kuhusu uwezekano wa kujenga Kituo cha Polisi Kiwangwa kwa haraka ili kizue ujambazi, tutajitahidi tujenge Kituo cha Polisi lakini sina hakika kama kitazuia ujambazi. Tutaweka Kituo cha Polisi kwa sababu wananchi wanahitaji Kituo cha Polisi mahala pale.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji; Mheshimiwa Chiligati!

Na. 96

#### **Mradi wa Maji Mbwasa**

**MHE. CAPT. JOHN ZEFANIA CHILIGATI** aliuliza:-

Mradi wa Maji Mbwasa Wilayani Manyoni unaosambaza maji kwenye vijiji 10 vya Bonde la Ufa uko kwenye Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) na umetengewa fedha katika Bajeti ya Mwaka 2014/2015:-

4 FEBRUARI, 2015

(a) Je, ni lini Mradi huu utaanza kutekelezwa na utachukua muda gani kukamilika?

(b) Je, Mradi huo utagharimu kiasi gani cha fedha na hadi sasa Serikali imeshapeleka Manyoni kiasi gani cha fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huo?

**NAIBU WIZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Capt. John Zefania Chiligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Mbwasa umeanza kutekelezwa mwaka huu wa 2014/2015, kwa kufanya kazi ya usanifu na utafiti wa maji chini ya ardhi. Aidha, usanifu na uchimbaji wa majoribio ya awali ulionyesha kuwa maeneo ya Vijiji vya Kintinku na Lusilile, hayana maji ya kutosha. Kwa kuzingatia hali hiyo na ushauri wa Mhandisi Mshauri, ilionekana ni vyema kutumia chanzo cha maji kilichopo katika Kijiji cha Mbwasa, eneo ambalo limeonekana kuwa na maji ya kutosha ambalo liko kandokando ya Mlima wa Saranda. Mradi utakapokamilika, utahudumia vijiji kumi vya Kintinku, Lusilile, Mbwasa, Mtiwe, Chikuyu, Mwimboo, Chilejeho, Maweni, Mvumi na Ngaiti. Usanifu wa Mradi huo tayari umeshakamilika na hatua inayofuata ni kuchimba visima ili kuongeza vyanzo vya maji na baadaye kuanza rasmi kwa ujenzi huo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu unakadirwa kugharimu kiasi cha shilingi bilioni sita. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015, Mradi ultengewa shilingi 857,843,790. Mpaka sasa Wizara imekwishakupeleka kiasi cha shilingi 460,446,352 katika Wilaya ya Manyoni.

**MHE. CAPT. JOHN ZEFANIA CHILIGATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa

4 FEBRUARI, 2015

majibu ya kutia moyo. Pia namshukuru yeye mwenyewe binafsi, alifika katika eneo la Mradi na kuhimiza utekelezaji.

Baada ya shukrani hizo, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa fedha alizozitaja kwenye jibu la msingi kwamba zimefika Manyoni zinaonekana kwenye mtandao lakini hazijaingia kwenye Akaunti ya Halmashauri. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa kufuatilia ili fedha hizo ziingie kwenye Akaunti ya Halmashauri na kazi ianze?

(ii) Katika vijiji kumi vilivyotajwa ambavyo vitanufaika na Mradi, kuna Kijiji cha Makutupora hakimo katika orodha hii. Hiki ni kijiji ambacho kipo jirani na chanzo cha maji, lakini kiko pembedi na ile line kuu. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuwashauri Wataalam waweke mchepuo katika njia kuu ili Kijiji cha Makutupora nacho kiingizwe kwa sababu kina shida kubwa sana ya maji? (Makofii)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu kama ifuatavyo:-

Pamoja na pongezi hizo, niseme tu kwamba, jana Waziri wa Fedha, alitoa maelekezo namna ambavyo Wizara yao itafuatilia jambo hili na kuhakikisha kwamba hela zote ambazo zimeshaidhinishwa, zifike katika Miradi ya Maji, kama ilivyokuwa imekusudiwa. Mimi ninakuahidi nitafuatilia na Waziri wa Fedha naye anasikia.

La pili, ni kweli nilifika huko kukagua huu Mradi. Kwa kuwa Kijiji hiki cha Makutupora hakiko mbali sana, Sera yetu ni kwamba, vijiji vyote ambavyo vinapitiwa au viko jirani au viko kwenye chanzo, vina haki ya kupata maji. Kwa hiyo, katika hili nitaagiza Wataalam wafike eneo husika.

4 FEBRUARI, 2015

Na. 97

**Mradi wa Maji Vijijini na Benki ya Dunia**

**MHE. JOSEPHAT SINKAMBA KANDEGE** aliuliza:-

Upatikanaji wa maji katika Wilaya mpya ya Kalambo umekuwa wa tatizo kubwa sana ikizingatiwa kuwa Mradi wa Kuvipatia Maji Vijiji Kumi kila Halmashauri unaofadhiliwa na Benki ya Dunia umechukua muda mrefu bila mafanikio:-

(a) Je, ni lini Mradi huo utakamilisha ushambazaji wa maji kwenye Vijiji vya Mwazye, Mwimbi, Kisumba na Matai?

(b) Je, ni lini vijiji vingine vyenye adha kubwa ya maji vya Myunga na Kalalasi - Kata ya Mkali; Ulimi na Kalepula - Kata ya Kasanga; Ninga na Kafukula - Kata ya Katazi vitapatiwa maji?

(c) Halmashauri mpya ya Kalambo ilipata vijiji vitano tu badala ya vijiji 10; je, ni lini Serikali itaongeza vijiji vingine vipya?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutekeleza Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi sasa Halmashauri ya Kalambo imeshakamilisha Miradi ya Maji kwenye Vijiji vya Matai na Mwimbi, vyenye uwezo wa kuwapatia huduma ya maji safi wakazi wapatao 19,027. Aidha, Serikali inaendelea kutekeleza Mradi wa Mwazye ambao kwa sasa umetekelizwa kwa asilimia 65 na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni.

4 FEBRUARI, 2015

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kukabiliana na tafizo la upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo mbalimbali vijiji ni hapa nchini na kwa upande wa Kalambo Serikali inakamilisha Mradi wa Maji wa Kijiji cha Ulumi. Kuhusu Kijiji cha Kalalasi, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, Wazara yangu na Halmashauri kwa pamoja, tukipe kipaumbele kijiji hiki kwenye Awamu ya Pili ya Utekelezaji wa Programu.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji 11 vilivyopewa kipaumbele kwenye utekelezaji wa Programu ya Sekta ya Maji na Usafi wa Mazingira kwa Halmashauri ya Kalambo, ambapo utekelezaji umekamilika katika Vijiji vitatu vya Matai, Ulumi na Mwimbi. Aidha, utekelezaji unaendelea katika Vijiji vitano vya Mwazye, Kisumba, Kafukula, Mabwekenya na Kamawe. Miradi mingine miwili ni ya Myunga na Kalepula ambayo utafiti maeneo ya visima umeshafanyika. Kuhusu Mradi wa Kasanga, mkataba wake wa ujenzi umeshakamilika na Mkandarasi ameshaanza kupeleka mabomba kwenye eneo la Mradi.

**MHE. JOSEPHAT SINKAMBA KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, naomba niipongeze Serikali kwa kukamilisha ujenzi wa maji kwa Miji ya Ulumi, Mwazye na Kisumba. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, a-check na chanzo chake cha majibu kwa sababu Kijiji cha Mwimbi ndiko ninakotokea na mpaka leo hii hakuna maji ambayo yanapatikana.

Maswali mawili ya nyongeza ni kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Mkandarasi aliyepata kazi ya kupeleka Mradi wa Maji Kijiji cha Mambwekenya, Kafukula, Kalepula pamoja na Myunga, ameenda kufanya kazi kule na akalazimika kuondoka baada ya kutolipwa hata senti tano. Je, Serikali itakuwa tayari kuhakikisha inapeleka pesa ili mkandarasi yule aweze kurudi site?

4 FEBRUARI, 2015

(ii) Kwa kuwa Vijiji vya Mwambao wa Ziwa Tanganyika, kwa maana ya Kipwa pamoja na Kilawani vina adha kubwa sana ya maji. Je, Serikali itakuwa tayari katika bajeti ya 2015/2016 kuhakikisha vijiji hivi vinaingizwa katika Mpango? (Makofij)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kandege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakubaliana naye kwamba, tutaa ngalia juu ya haya waliyoyasema, ikiwemo taarifa hizo kuzifanya kazi.

La kwanza, kuhusu hela za Mkandarasi, ninamuahidi kwamba, tutafuatilia kuona Miradi ambayo ameanza kuifanya anaitekeleza na fedha isiwe tatizo. Kwa hiyo, tutashirikiana na Wizara ya Fedha kusukuma jambo hilo.

La pili, Waziri wa Maji ana mpango wa kufanya ziara katika Mkoa wa Rukwa, Katavi na Kigoma, kwa hiyo, nafikiri atapata fursa ya kufika katika maeneo hayo na kuviingiza vijiji hivyo katika Mpango wa Bajeti inayokuja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yetu ya leo yamekwisha na muda wetu umekwisha vilevile. Sasa nitatangaza wageni walioko Bungeni asubuhi hii. Wageni walioko Ukumbi wa Spika ni Wakuu wa Idara na Vyombo vya Ulinzi na Usalama kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, wakiangozwa na Ispekte Jenerali wa Polisi, Ndugu Ernest Jumbe Mangu. (Makofij)

Commissioner General wa Magereza, Ndugu John Casmir Minja; Kamishna Mkuu wa Uhamiaji, Ndugu Sylvester Ambokile; Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Wakimbizi, Ndugu Deusdedit Masusu; Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Huduma kwa Jamii, Ndugu Aloyce Musika; Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Mipango, Ndugu Joyce Momburi; Kamishna wa Operesheni Zimamoto, Ndugu Rogatos Kipali; Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, SACP David Misime; Mkuu wa

4 FEBRUARI, 2015

Magereza Mkoa wa Dodoma, SACP Engineer Antonio Kirumbi, karibu Bungeni, wewe uko hapahapa tu. (*Makofi*)

Wapo pia Afisa Uhamiaji Mkoa wa Dodoma, Ndugu DCI Ally Amiri na Kamanda wa Zimamoto Mkoa wa Dodoma, ACP Regina Kaombwe. (*Makofi*)

Wafuatao ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge:-

Wageni wa Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe, Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, ni Mwanafunzi Mlemavu, Ndugu Joseph Ernei, ameongozana na rafiki yake, Ndugu Elias Samweli. Karibuni Dodoma.

Wageni wa Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe, ambaao ni Viongozi wa Chama cha Wafugaji kutoka Serengeti; Ndugu Edward Makaba, Ndugu Mtiro Maunya, Ndugu Thomas Manyeresa na Ndugu Josephat Magambangati.

Mgeni wa Mheshimiwa Ezekia Wenje, ambaye ni Ndugu Joel Sesabo, Katibu wa Baraza la Wazee CHADEMA, Jimbo la Segerea Dar es Salaam.

Wageni wa Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mbunge wa Kisesa, kutoka Jimboni kwake ni Ndugu Shabani Omari, Katibu wa Mbunge; Peter John, kama mpo mkiitwa msimame. Mwakande Geofrey, Sedekia Costa, Max Kaaya toka Chuo Kikuu cha UDOM, Emanuel Mpina, Thomas Mathias, Godfrey Kibona, Wilson William, Zabron Paul, Daniel Mpigasupi na Silas Sylvester.

Katika wageni wa Idara na Vyombo vyta Ulinzi, sikumtaja DG wa NIDA, Ndugu Maimu; karibu sana Dodoma.

Wageni wa Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya kutoka Mji Mdogo wa Mwandiga Kigoma, ni Ndugu Nyembo Mustafa Temba, Ndugu Boaz Chuma Ndaha na Ndugu Neema Shayo.

4 FEBRUARI, 2015

Wageni wa Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge na Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA) Taifa, ambao ni Ndugu Grace Tendega, Katibu Mkuu wa BAWACHA Taifa; Ndugu Hawa Mwaifunga, Makamu Mwenyekiti wa BAWACHA Taifa; Ndugu Kunti Yusuph, Naibu Katibu Mkuu BAWACHA; Ndugu Hamida Abdallah, Makamu Mwenyekiti BAWICHA Taifa Zanzibar. (Makofij)

Wageni wa Mheshimiwa Sylvester Mabumba kutoka Chuo Kikuu cha St. John's Kitengo cha Tehama ambao ni Ndugu Simon Shimmy John na Ndugu John Kennedy Kungula; Karibuni Dodoma. (Makofij)

Mgeni wa Mheshimiwa Pindi Chana, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ambaye ni Ndugu Augustino Oscar Matefu; karibu Dodoma.

Mgeni wa Mheshimiwa Pauline Gekul, ambaye ni Ndugu Suzy Migire, Diwani Mbulu na Katibu BAWACHA Mkoa wa Manyara; karibuni sana.

Wageni wa Mheshimiwa Herbert James Mntangi, ambao ni Ndugu Juma Killo na Ndugu Ramadhani Killo; karibuni sana.

Mgeni wa Mheshimiwa Abia Nyabakari, ambaye ni Ndugu Nchise Chuma kutoka Kigoma.

Wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo Bungeni; wanafunzi 60 na walimu wanane kutoka Shule ya Msingi Zepisa, Dodoma.

Wanafunzi 85 na walimu sita kutoka Shule ya Mtakatifu Monica Arusha. Karibuni sana Dodoma, wakati mwingine mbadilishe uniform kidogo ziwe rangi nyekundu.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo la kazi. Mheshimiwa Magret Sitta, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, anaomba kuwatangazia Wajumbe wa Kamati yake kuwa, leo tarehe 4, saa saba mchana, kutakuwa

4 FEBRUARI, 2015

na Kikao cha Kamati katika Ukumbi Namba 227, Ghorofa ya Pili, Jengo la Utawala.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. KABWE ZUBERI ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) na mwongozo huo ninaulekeza kwenye Kanuni ya 46(1). Waziri anayeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kulijibu swali hilo kwa ukamilifu kama lilivyoulizwa, isipokuwa kwamba kama jibu hilo linalohusika ni refu au lina takwimu nydingi na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Swalii Namba 89 la Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, pamoja na maswali ya nyongeza yaliyofuata, Naibu Waziri wa Nishati na Madini hakujibu kabisa maswali ambayo Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanauliza na alikuwa anapiga kelele tu. (Makofi)

Katika swali la msingi, kwa mfano, swali (a), Waziri alisema, nanukuu: "Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2011 hadi 2014, kiasi cha shilingi bilioni 5.9, kiliingia katika Pato la Taifa kama mrabaha."

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchumi hakuna kitu kama hicho. Kwa sababu mrabaha siyo Pato la Taifa na hapa ni kuchanganya kati ya mapato ya Serikali na Pato la Taifa. Pato la Taifa ni *GDP*, mapato ya Serikali ni *government revenue*. Kwa hiyo, sehemu (a) ya swali la Mheshimiwa Kidawa haikujibiwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na maswali ya nyongeza kuhusiana na Mji wa Mererani kuwa *protected area*, ambayo ni matakwa ya kisheria, pamoja na uchimbaji wa wachimbaji wadogo wadogo wa *tanzanite* pale Mererani na kuongeza thamani ya *tanzanite* pale Mererani, ambayo ni maagizo ya kisera na ni Sera ya Madini ya Mwaka 2009 na Sheria Mpya ya Madini ya Mwaka 2010, Waziri hakujibu haya maswali kabisa.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwamba, Wizara ya Nishati na Madini ikajibu upya swali hili, liletwe Bungeni liweze kuulizwa na wajiandae na majibu ili tuweze kuokoa tanzanite yetu na nchi iweze kufaidika na tanzanite yetu. (Makofij)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kanuni yetu ya 45(3), inatoa mamlaka kwa Kiti kutoa maagizo. Kwa hiyo, mimi namwomba tu Mheshimiwa Waziri, baadaye ulijibu tena kwa maana kukaa naye privately, ujaribu kumjibu na kama bado hajaridhika, tunaweza tukali...

(*Hapa Wabunge fulani walipiga kelele kuonyesha kutokubaliana na mwongozo wa Kiti*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa ngojeni nimalize basi, mbona mnakuwa mna kihelehele hivi.

Ukae naye na utafute mengine ambayo unafikiri ni ya manufaa, na wewe najua ni mchapa kazi mzuri sana, ili tuweze kupata majibu sahihi na pande zote ziweze kuridhika. Kwa hiyo, nakuomba ufanye hilo.

Mheshimiwa Chambiri!

Mheshimiwa Mbatia subiri, naona ya kwako tunaweza kuhangaika na makanuni, kwa hiyo, subiri kwanza.

**MHE. KISYERI W. CHAMBIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa Mujibu wa Kanuni ya 68(7) nikiomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Kanuni ya ngapi?

**MHE. KISYERI W. CHAMBIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Babati Mjini ambapo ni Jimbo langu, sisi tunategemea kilimo, mapato yote yanatokana na kilimo. Toka tukopwe mazao, hatujalipwa

4 FEBRUARI, 2015

fedha hata kidogo, watu wamechukuliwa magunia mawili, manne, watu wa chini kabisa wenyewe maisha magumu, mpaka leo hawajalipwa na Serikali...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chambiri, hiyo unaisoma Kanuni au unasoma nini? Hayo magunia ni Kanuni? (Kicheko)

**MHE. KISYERI W. CHAMBIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwamba, watu maskini namna hiyo, wanaokopwa na Serikali kubwa kama yetu, wameshindwa kupeleka watoto shule, watalipwa lini hizo fedha na watafidhiwa nini badala yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chambiri, Kanuni hiyo uliyoitumia, natoa fursa tu kumwambia Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, baadaye aweze kukupa majibu; kwa sababu Kanuni uliyoitumia wewe ni jambo lililotoka mapema Bungeni na issue kama hiyo haikuwahi kutokea Bungeni mapema. Kwa hiyo, namwagiza Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ukae naye ili akueleze kuhusu hawa watu. Haya maeneo yako mengi sana. Kwa hiyo, akueleze lini na wakati gani na fedha zao hao ambaa unaona wamedhulumiwa na uchaguzi huu unakuja hawawezi kukurudisha ili waweze kulipwa. (Kicheko)

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba kutumia Kanuni ya 47 ya Kanuni za Bunge hili Tukufu, kuhusu jambo lenye masilahi kwa umma. Kanuni inasomeka hivi, kwamba; baada ya muda wa maswali kuisha, Mbunge ye yeyote anayeweza kutoa hoja kuwa shughuli za Bunge kama zilivyoonyeshwa kwenye Orodha ya Shughuli ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma.

(2) inasema; hoja ya namna hiyo itakuwa ni maalumu na inaweza kutolewa wakati wowote, hata kama majadiliano yatakuwa yanaendelea; na (3), hoja itatolewa na Mbunge kwa kusimama mahala pake na kuomba idhini

4 FEBRUARI, 2015

ya Spika kutoa hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge kwa madhumuni ya kujadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma.

(4) inasema; iwapo Spika ataridhika kwamba, jambo hilo ni la dharura, halisi na lina masilahi kwa umma, basi ataruhusu hoja hiyo itolewe kwa muda usiozidi dakika tano na mjadala juu ya hoja hiyo utaendelea kwa muda ambao Spika ataona unafaa kwa kuzingatia mazingira ya suala linalojadiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa kutumia Kanuni ya 47, kuhusu jambo lenye masilahi kwa umma. Jambo hilo ni kuhusu *Biometric Voter Registration (BVR)*, Uandikishaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

**MWENYEKITI:** Nilikuwa sijakuruhusu bado, sasa nakuruhusu.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa ruhusa yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu hapa tulipo leo hii, hatuna Daftari la Wapiga Kura. Tarehe 9 Julai, 2014, Tume ya Uchaguzi ya Taifa ilituita Wadau na ikatuambia kwamba, Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lilitokuwepo limechafuliwa, ni chafu na halifai kutumika tena. Wakatuambia kwamba, wameanzisha utaratibu wa kuandikisha upya wapiga kura wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mfumo watakaotumia siyo ule tuliokuwa tunautumia zamani, utatumika mfumo mpya wa kuandikisha wapiga kura kwa mfumo wa kielektroniki *Biometric Voter Registration System (BVR)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walituhakikishia kwamba, zoezi hilo la kuandikisha wapiga kura wote nchi nzima lingeanza mwaka jana mwezi wa tisa mwanzoni, haikufanikiwa. Wakatuambia baadaye mwezi wa tisa mwishoni, haikufanikiwa. Mwezi wa kumi, kumi na moja, mpaka mwezi wa kumi na mbili, ambapo walifanya

4 FEBRUARI, 2015

majaribio kwenye Majimbo matatu; Dar es Salaam, Kilombero na kule Katavi na ikaja na changamoto nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwezi uliopita, tarehe 8 Januari, 2015, tukiwa na kikao cha Wadau wa Vyama vya Siasa, vilivyopo ndani ya Kituo cha Demokrasia Tanzania, aliyekuwa Mwenyekiti wetu wakati huo, Mheshimiwa John Momose Cheyo, alifanya juhudhi za ziada kualika Tume ya Uchaguzi ya Taifa kwenye kikao hicho. Tume ya Uchaguzi ya Taifa ilituhakikishia kwamba, ina changamoto nyingi za kuendesha zoezi hili.

Pamoja na changamoto nyingi, ni zile *kits* za kuandikishia wapiga kura wote, ambapo tuna vituo zaidi ya 40,000 nchi nzima. Wakatuambia zoezi lenyewe litaanza tarehe 15 Februari, 2015, yaani Jumapili ya wiki ijayo. Wakatuambia kwa kuwa terehe 8 ilikuwa karibu na Sikuu ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, baada ya tarehe 12, Siku ya Jumatatu ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Tume ya Uchaguzi ya Taifa, itakaa na Tume ya upande wa Zanzibar, ZEC, ili wajadili kwa pamoja, waweze kurudi kwetu kama wadau, kutuelimisha namna zoezi litakavyofanyika, ikiwepo na kutumia huo mfumo wa sasa wa kielektroniki, ili tukubaline sote kama wadau kwa kuwa jambo hili lina masilahi kwa Taifa; na kwa kuwa tumebakni na takribani kama miezi minne, mitano tu Bunge liweze kuvunjwa twende kwenye uchaguzi, basi suala hili la uandikishaji wa wapiga kura, ndiyo uhai wa Taifa letu, ndiyo uhai wa Uchaguzi Mkuu ujao na tusipolimanage vizuri, sintofahamu inaweza kutokea na tunaweza kwenda kwenye machafuko.

Na kwa kuwa jana, Tume ya Uchaguzi ya Taifa, ndiyo sababu nimesema la dharura, jana, Tume ya Uchaguzi ya Taifa imekutana, imeanza kufanya utaratibu wa zoezi hili katika Mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma na Njombe, bila wadau wakuu kushirikishwa kama tulivyokubaliana kwenye meza ya mazungumzo ili kuhakikisha jambo hili linafanyika kwa ufanisi, jambo hili linafanyika kwa uadilifu, jambo hili linaaminika pande zote. (*Makofij*)

4 FEBRUARI, 2015

Wadau tuliookaa wote ni vyama vyote vyaa siasa, kikiwemo Chama cha Mapinduzi, kiliwakilishwa na Mzee Philip Japhet Mangula; CHADEMA Dkt. Wilbrod Slaa, CUF Profesa Ibrahim Lipumba; UDP Mheshimiwa John Momose Cheyo; TLP iliwakilishwa na Katibu Mkuu wa Chama hicho; NCCR Mageuzi na vile vyama ambavyo havina uwakilishi viliwakilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hili ni jambo lenye masilahi mapana kwa umma na Tume ilisema mambo mengi na sisi tukawashauri kwa nia njema kabisa, vyama vyote, kwamba; ni bora tukae tuzibe ufa tusije tukajenga ukuta. Tuaminiane, tujenge *trust*, pande zote ziweze kukubaliana kwa pamoja, zoezi hili lifanyike kwa uadilifu wa hali ya juu, kwa ufanisi wa hali ya juu, tushirikiane sote kwa pamoja ili tuhakikishe kwenye Uchaguzi Mkuu malalamiko yanapungua. Tuhakikishe kwenye Uchaguzi Mkuu mambo ambayo yametokea Kenya, yametokea Ghana, Mozambique, Namibia na Malawi, kwenye mfumo huu huu wa kielektroniki, hayatatokea hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwa mujibu wa Kanuni ya 47; kwa kuwa katiba yetu, Ibara ya 63(2), kazi ya Bunge, ndiyo Chombo Kikuu kwa niaba ya Wananchi wa Tanzania, kuvisimamia na kuishauri Serikali. Bunge hili lichukue nafasi yake, kuvisimamia Serikali, kuishauri Serikali, zoezi hili liweze kufanyika kwa uadilifu na uaminifu wa hali ya juu na ufanisi uweze kuwepo. Matatizo yaliyotokea kwa wengine yasije yakatokea hapa kwetu ili tuweze kuaminiana na hakuna jambo jema kama kuaminiana kwenye jambo nyeti kwa masilahi mapana ya Taifa kama hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
(Makofij)

**MWENYEKITI:** Wala haihitaji hoja jamani, kaeni kwanza. Mikwara mbona imekuwa minge hivi!

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mbatia, mwongozo wangu; nakubaliana na wewe ni jambo muhimu. Nakubaliana na wewe, tukae pamoja. Nakubaiana na wewe, Chombo Kikuu cha kuishauri Serikali ni Bunge. Naagiza sasa hivi, Waziri wa Fedha, Serikali na Mheshimiwa Mbatia, Kamati ya Uongozi inakutana sasa hivi; kwa maana hiyo, nafasi yangu sasa atachukua Mwenyekiti mpya, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, aje anipokee Kiti ili sisi Kamati ya Uongozi, Waziri wa Fedha, Serikali na Mheshimiwa Mbatia, tukae kwa pamoja tukazungumze kwenye Kamati ya Uongozi sasa hivi. (Makofi)

Mheshimiwa Mg'ong'o! (Makofi)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Mussa Zungu Azzan)  
Alitoka Ukumbini

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Lediana Mafuru Mng'ong'o)  
Alikalia Kiti

**MWENYEKITI:** Katibu, hatua inayofuata!

#### HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa  
Kimataifa na Taarifa ya Kamati ya Uchumi,  
Viwanda na Biashara**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawaita Wenyeviti kutoa Taarifa, naomba nichukue nafasi hii, kuwashukuruni sana kwa kuniamini na kuniclagua kuwa Mwenyekiti wa Bunge. (Makofi)

Naomba pia niwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi, wakiwemo Wenyeviti wa Kamati na Makamu Wenyeviti, kwa kunipendekeza. Hata hivyo, nitakuwa sina fadhila kama sitaishukuru Kamati yangu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, kwa kuniclagua bila kupingwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo. (Makofi)

4 FEBRUARI, 2015

Naomba niwashukuru Wanawake wa Mkoa wa Iringa na Chama cha Mapinduzi, kwa kunichagua; ahsanteni sana na ninaomba wote tushirikiane. (Makof)

Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama au Mwakilishi wake. Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Chiligati!

**Taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama kuanzia Januari, 2014 hadi Januari, 2015 kama ilivyosomwa Bungeni**

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ULINZI NA USALAMA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama na kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka 2014 ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge yameainishwa katika Fasili ya Tatu, Kifungu cha sita, pamoja na Fasili ya Kwanza ya Kifungu cha saba ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Majukumu hayo ni kusimamia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, pia kupokea Taarifa ya Hali ya Usalama wa Taifa kutoka kwa Waziri wa Nchi, Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015, Kamati ilitekeleza majukumu yake kuhusiana na mambo yafuatayo:-

Moja, kusimamia na kuishauri Serikali kupitia Wizara zinazosimamiwa na Kamati.

Pili, utungaji wa Sheria na kuridhia Mikataba, Itifaki na Makubaliano ya Kimataifa yanayohusu masuala ya ulinzi na usalama.

4 FEBRUARI, 2015

Tatu, ufuatiliaji wa hali ya ulinzi mipakani na pia usalama wa raia na mali zao nchini.

Nne, ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Wizara husika kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015.

Njia zilizotumika kutekeleza shughuli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilitumia njia zifuatazo:-

Moja, kuzitaka Wizara husika ziwasilishe Taarifa za Ulinzi na Usalama kwenye Kamati katika vipindi mwafaka.

Pili, kupitia na kuchambua Taarifa zilizowasilishwa na Wizara husika na Taasisi zilizo chini ya usimamizi wa Kamati.

Tatu, kupitisha bajeti na kutathmini utekelezaji wa kazi zilizofanywa na bajeti iliyoidhinishwa na Wizara husika.

Nne, kufanya ziara katika baadhi ya mikoa ili kuona utendaji kazi wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama na changamoto zinazovikabili ili kuzitafutia majawabu Serikalini.

Tano, Kamati ilitembelea Bunge la India kwa ajili ya kubadilishana mawazo na uzoefu na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zilizofanyika ni kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kamati ilifanya ziara kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Wizara husika.

Miradi na maeneo yaliyotembelewa na Kamati ni kama ifuatavyo:-

4 FEBRUARI, 2015

Kwanza, Makao Makuu ya Ofisi ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, yaani NIDA, ili kukagua maendeleo ya uchapishaji na ugawaji wa Vitambulisho vya Taifa.

Pili, Chuo cha Uhamiaji Moshi, ili kukagua ujenzi wa Chuo na utoaji mafunzo.

Tatu, Ofisi za Vikosi vya Zimamoto na Uokoaji za Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro.

Nne, Chuo cha Mafunzo ya Polisi Moshi.

Tano, Magereza ya Mwanga, Karanga na Rombo.

Sita, Ofisi za Magereza za Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro.

Saba, Ofisi ya Polisi ya Mkoa wa Arusha.

Nane, Chuo cha Maafisa wa Kijeshi Monduli.

Tisa, Kituo cha mpakani cha Namanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukaguzi huo, Kamati ilibaini, pamoja na mambo mengine, kuwa licha ya fedha kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Miradi mbalimbali, fedha hizo huchelewa mno kupelekwa na hazipokelewi zote.

Hali hii inakwamisha utimizaji wa malengo ya kibajeti na kuathiri utekelezaji wa Miradi hiyo. Maelekezo ya kina na maoni ya Kamati kuhusu hali hiyo, yalitolewa katika Mkutano wa 15 wa Bunge wakati wa kujadili Makadirio na Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo ya kina na maoni ya Kamati kuhusu hali hiyo yalitolewa katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge wakati wa kujadili Makadirio na Matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 98 (2) inaielekeza Kamati kufanya vikao vya kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti za Wizara ya Mambo ya ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na JKT kwa kipindi kisichozidi siku tisa. Matokeo ya uchambuzi uliofanywa na Kamati yalidhihirisha dosari mbalimbali kuhusu utekelezaji wa kazi za Wizara hizo. Dosari kubwa ni tatizo la mtiririko wa fedha kutoka hazina kutokuwa wa kuridhisha, kutotengwa kwa fedha za kutosha za miradi ya maendeleo na kutotengwa kabisa kwa fedha za miradi ya maendeleo kwa ajili ya Vikosi vya Zimamoto na Uokoaji. Maelezo ya kina kutohana na uchambuzi wa bajeti yalitolewa wakati wa Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Januari 14 hadi Januari, 2015 Kamati ilichambua Muswada mmoja wa sheria ulioletwa kwenye Kamati kwa mujibu wa kanuni ya 84(1). Muswada huo ni Sheria ya Usimamizi na udhibiti wa silaha na risasi ya mwaka 2014, yaani *The Arms and ammunition Control Act*. Katika kuufanya kazi Muswada huo, Kamati ilizingatia masharti ya kanuni ya 84(2) na ya 117(a) kuhusu kualika wadau ili kupata maoni na ushauri wao kwa ajili ya kuuboresha Muswada huo. Hata hivyo, Kamati haikumaliza kazi hiyo kutohana na wadau kueleza kwamba hawakushirikishwa vya kutosha, hivyo walihitaji muda zaidi. Kwa hiyo, Muswada huo utaletwa hapa Bungeni katika kikao kijacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kuridhia itifaki na mikataba ya Kimataifa, Kamati ilichambua Itifaki ya Ushirikiano wa Masuala ya Ulinzi kwa Nchi za Afrika Mashariki. Katika uchambuzi huo Kamati iliishirikisha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Maoni ya Kamati yalifikishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Sita na Kumi na Saba na Bunge hili liliridhia itifaki hiyo.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wamajukumu yake, Kamati ilipitia na kuchambua taarifa za Ulinzi na Usalama zilizowasilishwa na Wizara husika kila baada ya miezi mitatu. Mapitio ya taarifa hizo yalilenga kutekeleza jukumu la kibunge la kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Kutokana na uchambuzi na utekelezaji uliofanyika, Kamati ilibaini mambo mbalimbali ambayo yanafafanuliwa hapa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mbalimbali yalibainika, yalihusu:-

- (1) Usalama wa Raia na Mali Zao;
- (2) Uhamiaji;
- (3) Utoaji wa Vitambulisho vya Taifa;
- (4) Ulinzi na Usalama wa Mipakani;
- (5) Hali ya Magereza; na
- (6) Huduma za Zimamoto na Uokoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara ya Kamati pamoja na taarifa kutoka kwenye Wizara husika, Kamati iliridhika kwamba kwa ujumla hali ya ulinzi wa nchi na usalama wa raia katika kipindi hiki ilikuwa shwari, japo zipo changamoto chache za uvunijfu wa amani kama vile vitendo vya uporaji mali, ajali za barabarani na pia matukio ya mauaji ya vikongwe na Albino yaliyotokea katika baadhi ya Mikoa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki, tatizo la uhamiaji haramu lilijitokeza katika Mikoa ya mipakani ya Arusha Kagera na Kilimanjaro. Tatizo hili bado ni changamoto kubwa. Wahamiaji haramu wanaingia nchini kwa kutumia njia za miguu, baiskeli, pikipiki na magari, wengi wakitokea Ethiopia, wengine ni kutoka Kenya, Somalia, Pakistan, Uganda

4 FEBRUARI, 2015

na Burundi. Wahamiaji haramu wakikamatwa, inabidi wapelekwe Mahakamani kwa mujibu wa sheria na baadaye kuhifadhiwa Magerezani ambako tayari kuna msongamano mkubwa wa wafungwa na mahabusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki, hali katika mipaka yetu yote imekuwa shwari licha ya kuwepo kwa tatizo la uingiaji wa wahamiaji haramu. Aidha, katika baadhi ya vituo vya mipakani kama Namanga, kuna tatizo la upungufu wa magari, hivyo kufanya kazi ya doria ya mipakani kutofanyika kwa ufanisi. Changamoto nyingine za mipakani ni kama ifuatavyo:-

(a) Wananchi kujenga mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya wananchi wamejenga nyumba au kulima mashamba na kufanya shughuli nyingine kama za biashara katika maeneo ya mipaka hasa kwenye mpaka wetu na Zambia katika eneo la Tunduma. Ukurasa wa 19 wa kitabu chenu imeandikwa "Tunduru." Naomba mfanye masahihisho na Hansard vilevile ifanye masahihisho. Katika eneo hilo, watu wamejenga nyumba kuzunguka, na wengine hata juu ya beacons za mpaka.

(b) Kuharibiwa mawe ya Mpaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawe ya mpaka yameharibiwa na mengine kung'olewa. Kwa mfano, Kamati ilijulishwa kuwa, jiwe la mpaka lililopo Kaskazini Mashariki katika Mji wa Namanga umbali wa kilometra tatu limeangushwa na kusogezwa pemberi kutohaka na shughuli za uchimbaji mawe na changarawe katika eneo hilo. Aidha, Kamati ilijulishwa kwamba kwa kushirikiana na Serikali za Kenya na Burundi, mawe yaliyoharibiwa yameanza kufanyiwa ukarabati katika mipaka na nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Magereza nchini yanakabiliwa na matatizo mbalimbali, kwa mfano msongamano wa wafungwa na mahabusu, upungufu wa

4 FEBRUARI, 2015

magodoro na mablanketi, upungufu wa sare za Askari na Wafungwa na upungufu wa mabweni ya Wafungwa. Kwa mfano, Kamati ilipotembelea Gereza la Rombo ilikuta ujenzi wa bweni la wanawake halijakamilika, hivyo wanawake Wafungwa wanahifadhiwa sehemu ya Gereza lenye mabweni ya wanaume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahabusu katika Magereza yote yaliyotembelewa na Kamati, walilalamika kuhusu kesi zao kuchelewa kusikilizwa kutokana na upelelezi kutokamilika mapema, kubambikiziwa kesi, masharti magumu ya dhamana, watuhumiwa kutofikishwa Mahakama za Mwanzo ili kesi zao zisikilizwe na Mahakama kuahirisha kesi mara kwa mara.

Vilevile Wafungwa katika Magereza yote yaliyotembelewa walilalamikia kitendo cha kutotolewa kwa haraka nakala za hukumu mapema ili kuwawezesha kukata rufaa. Aidha, walilalamikia kupewa chakula cha aina moja, yaani ugali na maharage.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa na kujionea yenye kuwa nyumba za Askari Magereza ni chache na ni chakavu, hivyo kuwafanya baadhi ya Askari kuishi nje ya Kambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea na kukagua shughuli za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa. Madhumuni ya ziara hii ilikuwa kuona maendeleo ya uchapishaji na ugawaji kwa wananchi Vitambulisho vya Kitaifa. Kamati ilikuta kazi ya kuchapisha vitambulisho vya uraia inaendelea sambamba na kazi ya kuandikisha walengwa katika Mkoa wa Dar es Salaam na katika Mikoa yote ya Tanzania Zanzibar.

Hata hivyo, kazi hii haiendi kwa kasi inayotakiwa kutokana na upungufu wa zana za kusajili walengwa, yaani *Mobile Enrollment Units*. Aidha, bajeti ya kununulia zana hizo iliidhinishwa na Bunge, lakini hadi wakati wa ziara ya Kamati, fedha hizo zilikuwa hazijatolewa kutoka Hazina.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Vikosi vya Zimamoto na Uokoaji vya Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro. Vikosi hivi vinaendelea kutekeleza vizuri majukumu yao. Hata hivyo, vyote viwili vinakabiliwa na changamoto mbalimbali za upungufu wa Askari, ukosefu wa magari ya kuzima moto na uhaba wa maeneo ya kujazia maji, yaani *fire hydrants*. Kwa ujumla, vikosi vyote vya Zimamoto nchini vinakabiliwa na tatizo la kukosa zana za uokoaji, yaani *search and rescue equipments*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na shughuli zilizotekelawa na Kamati, yalibainika mambo mbalimbali kama nilivyoyaeleza hapo awali. Kwa kuzingatia mambo yaliyobainika, Kamati inatoa ushauri kwa Serikali na mapendekezo kwa Bunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kuhusu Jeshi la Polisi; katika ziara ya Chuo cha Polisi Moshi, Kamati iliridhika na uendeshaji wa Chuo hicho. Hata hivyo, ili kuongeza ufanisi zaidi, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani, inashauriwa kuzifanya kazi haraka changamoto zilizopo katika Chuo hicho kuhusu:-

- (1) Upungufu wa vyumba vya madarasa na mabweni ya wanafunzi;
- (2) Upungufu wa vifaa vya kufundishia; na
- (3) Majengo mengi ni chakavu na yanahitaji ukarabati mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa pongezi kwa Jeshi la Polisi nchini kwa jitihada za kudhibiti uhalifu pote nchini. Aidha, Kamati ilipotembelea Mkoa wa Arusha iliridhika na hali ya kupungua matukio ya uhalifu na pia ilikuta hali ya utulivu na amani imejerea tena katika Jiji la Arusha.

Pamoja na pongezi hizi, Kamati haikuridhishwa na taarifa za wakati huo kwamba bado upelevaze ulikuwa unaendelea wa kuwasaka waliohusika katika matukio mawili

4 FEBRUARI, 2015

ya ulipuaji mabomu katika Jiji la Arusha. Hata hivyo, Kamati imetiwa moyo na taarifa za hivi karibuni kwamba baadhi ya watumiwa wa matukio hayo ya kigaidi wamekamatwa na wamefunguliwa kesi Mahakamani. Kamati inaishauri kwamba kesi hiyo isikilizwe haraka na kutolewa hukumu ili kukidhi matarajio ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi litafute njia mbadala na za kisasa za kupambana na kudhibiti uingizaji nchini wa madawa ya kulevyo ukiwemo usafirishaji wa bangi kwenda Kenya na mirungi kutoka Kenya, kuingia Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na jamii lioneze jitihada za kubuni mbini mpya za kuwadhibiti wale wote wanaoendesha uhalifu wa uuaji wa watu wenye ulemavu wa ngozi, yaani Albino na vikongwe.

Aidha, Wizara za Ardhi, TAMISEMI, zishirikiane na Jeshi la Polisi kudhibiti mapigano baina ya wakulima na wafugaji yanayotokea katika baadhi ya Mikoa kutoptana na migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti ya chakula cha wafungwa kutoka Sh. 500/= kwa siku mpaka Sh. 1,500/= kwa siku. Hata hivyo, Serikali haikutoa fedha kwa ajili ya chakula cha wafungwa kwa mwezi wote wa Oktoba 2014 na mwezi wa Desemba, 2014 ilioa nusu tu ya kiwango kinachotakiwa kwa ajili ya chakula cha wafungwa.

Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha za zote za chakula kwa wafungwa na kwa wakati kwa kuwa kutotoa fedha zote kunasababisha Wizara kukopa na kuendelea kulimbikiza madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu msongamano Magerezani, Kamati inazidi kuishauri Serikali kwamba; moja, isimamie utekelezaji wa Sheria ya Community Service, ambapo wafungwa wenye makosa madogo madogo wapewe adhabu ya vifungo vya nje, huku wakipewa kazi za

4 FEBRUARI, 2015  
kutumikia jamii. Sheria hii ikitumika vizuri na katika Mikoa yote Tanzania Bara itasaidia kupunguza idadi ya wafungwa Magerezani.

Pili, vile vile Serikali isimamie utekelezaji wa Sheria ya Parole ambapo mfungwa anayeonyesha mwenendo na tabia njema Gerezani, anaweza kutumia nusu ya kifungo Gerezani na nusu iliyobaki akamalizia nyumbani kwake.

Tatu, Kamati za Kusukuma Kesi, yaani Case Flow Management Committees za ngazi za Wilaya na Mikoa, zипитie kesi mara kwa mara ili kuhakikisha mahabusu hawakai Magerezani muda mrefu wakisubiri kesi zao kusikilizwa.

Nne, Serikali iongeze bajeti ya kuhudumia Magereza ili kudumisha haki za msingi za wafungwa na mahabusu hasa kuhusu huduma za chakula, mavazi, matibabu na malazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uhamiaji. Kamati iliridhika na utendaji kazi wa Kituo cha mpakani cha Namanga. Hata hivyo, Serikali inashauriwa izifanyie kazi changamoto zifuatazo zinazovikabili vituo vyote vya mipakani.

Moja, upungufu wa vyombo vya usafiri (magari na pikipiki) kwa ajili ya kuimarisha doria katika mipaka yote.

Pili, kutokuwepo kwa zana za kisasa za upekuzi wa abiria na mizigo na hasa scanners. Vile vile hakuna mbwa wa kunusa na kubaini madawa ya kulevya.

Tatu, Serikali ifanye maandalizi ili vituo vyote vikubwa vya mipakani vitoe huduma kwa saa 24. Hii ni pamoja kuongeza shifts za kazi na pia wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tatizo la wahamiaji haramu wanaokamatwa mipakani, Kamati inashauri kwamba, wakishafikishwa Mahakamani kwa mujibu wa sheria, wasiendelee kupelekwa Magerezani, bali warudishwe makwao kwa njia ya barabara ili wasiongeze msongamano na gharama za kuwatunza Magerezani.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Vikosi vyote vya Zimamoto nchini vinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa zana za kazi, hasa magari ya kuzima moto na vifaa vya uokozi, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kiwango cha bajeti ili kuviwezesha vikosi hivi kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna moja ya kuongeza bajeti ya chombo hiki ni kwa Serikali kuongeza kiwango cha fedha wanazobakishiwa baada ya kuzikusanya (*retention*) kutoka asilimia 49 za sasa hadi asilimia 70 kama ilivyokuwa huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ulinzi na JKT, kwa upande wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Kamati inaishauri ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Jeshi la Wananchi, Kamati iliridhika na uendeshaji wa Chuo cha Maafisa wa Kijeshi, Monduli kinachotoa mafunzo kwa Maafisa wa Jeshi letu na pia Maafisa kutoka Majeshi ya nchi jirani za Kenya, Congo DRC, Uganda, Burundi, Rwanda na Sychelles. Hata hivyo, Wizara izifanyie kazi changamoto zinazokikabili chuo hiki, hasa kwa mambo yafuatayo:-

Moja, uchache wa mabweni, hasa ya wanawake; pili, ukarabati wa majengo hasa nyumba za Maafisa, mabweni ya wanafunzi, ukumbi wa mikutano na uwanja wa kwata; tatu, tatizo la uvamizi wa maeneo ya mafunzo ya medani lipatiwe ufumbuzi wa haraka na wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa nyumba za Askari na Maofisa uliopo katika vikosi vingi vya jeshi letu, Kamati inaishauri Serikali kwamba iongeze kasi ya kukamilisha mradi wa ujenzi wa nyumba 10,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Chuo cha Unadhimu, yaani staff college katika eneo la Duluti, Arusha, upewe msukumo mpya ili Chuo hiki kiwe na majengo yake. Hivi sasa kinaendeshwa kwa kujibana katika majengo ya Chuo cha Kijeshi cha Monduli.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inalipongeza Jeshi la Wananchi kwa kazi kubwa na nzuri ya kulinda mipaka yetu, kwani katika kipindi hiki hali ya mipaka yetu imekuwa shwari.

Vilevile, Kamati inawapongeza wanajeshi wetu wanaolinda amani nchi za nje chini ya usimamizi wa Umoja wa Mataifa katika nchi za Congo DRC, Darfur kule Sudan, Lebanon, Sudan Kusini, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Ivory Coast, kwa kazi nzuri na ya kutukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuusu Jeshi la Kujenga Taifa:-

(a) Kambi ya JKT Oljoro isaidiwe kuongezewa nyumba za Askari na vifaa vya mafunzo;

(b) Muda wa mafunzo ya JKT kwa vijana kutoka vyuoni kwa mujibu wa sheria uongezwe kutoka miezi mitatu ya sasa na uwe angalau miezi sita. Vijana wanaokwepa mafunzo haya bila sababu za msingi, hawa wanavunja sheria, hivyo Serikali iwachukulie hatua za kisheria; na

(c) Kwa kuwa kuna mgongano wa muda wa vijana hao kuripoti kwenye mafunzo ya JKT na hapo hapo kuripoti Vyuo, Kamati inazidi kuishauri Serikali kwamba Wizara ya Ulinzi na Wizara ya Elimu wakae pamoja na kutafuta njia ya kuoanisha mihula hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama taarifa hii ilivyoonyesha, ni kwamba vyombo vyote vya ulinzi na usalama katika kipindi hiki vimefanya kazi nzuri na ndiyo maana nchi yetu imetulia, ina amani na umoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili vyombo hivi vidumishe amani iliyopo, tunaishauri Serikali itimize wajibu wake wa kibajeti kwa kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya Sekta ya Ulinzi. Fedha hizo zipelekwe zote na kwa wakati.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuhitimisha kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii adhimu kuwasilisha Taarifa ya Mwaka 2014 ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama.

Napenda pia kuwashukuru Waziri wa Ulinzi na JKT - Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi - Mheshimiwa Chikawe na Naibu Waziri wake - Mheshimiwa Pereira Silima; pia Waziri wa Nchi, Utawala Bora - Mheshimiwa George Mkuchika kwa ushirikiano wanaoutoa kwa Kamati yetu.

Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umahiri wao katika kuchambua hoja pamoja na kutoa ushauri wa mara kwa mara ambao umekuwa ukizisaidia Wizara husika kufanya maboresho ya utendaji kazi wao. Majina yako katika ukurasa wa tisa, ili kuokoa muda, Waheshimiwa Wabunge mtayasoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah na watumishi wote wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake.

Kipekee, nawashukuru Ndugu Charles Mloka, Ndugu Ruhilabake, Ndugu Athuman Hussein, Ndugu Nesta Kawamala na Ndugu Onesmo Laulau kwa kuratibu vyema kazi za Kamati hadi taarifa hii inapotolewa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, sasa naomba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuikubali Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekii, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

4 FEBRUARI, 2015

**Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama  
kama ilivyowasilishwa Mezani**

**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI  
YA BUNGE YA ULINZI NA USALAMA KATIKA KIPINDI CHA  
MWEZI FEBRUARI, 2014 HADI JANUARI, 2015**

---

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka 2014 ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama.

**Mheshimiwa Spika**, majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge yameainishwa katika fasili ya 3 ya kifungu cha 6 pamoja na Fasili ya 1 ya kifungu cha 7, Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013. Majukumu hayo ni kusimamia Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, pia kupokea taarifa ya hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi, na usalama wa raia na mali zao.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kiliarifu Bunge lako tukufu kuwa, Kamati ilitekeleza majukumu yake yaliyoorodheshwa kwenye Kanuni za Kudumu za Bunge, kama ilivyoelekezwa hapo chini.

**2.0 KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA**

**2.1 Msingi wa shughuli hizo**

**Mheshimiwa Spika**, kulingana na majukumu ya Kamati yaliyoelezwa hapo juu, Kamati ilianda Mpango Kazi wa utekelezaji wa majukumu hayo. Katika kutekeleza, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ikiwemo Kanuni ya 117 inavyoelekeza utaratibu wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge.

4 FEBRUARI, 2015

**Mheshimwa Spika**, katika kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015 Kamati ilitekeleza majukumu yake kuhusiana na:-

- (i) Kusimamia na kuishauri Serikali kupitia Wizara zinazosimamiwa na Kamati;
- (ii) Utungaji wa sheria na uridhiaji wa mikataba, itifaki na makubaliano ya Kimataifa;
- (iii) Ufuatiliaji wa Hali ya Ulinzi mipakani na pia Usalama wa Raia na mali zao nchini;
- (iv) Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Wizara husika kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015;

## **2.2 Njia zilizotumika kutekeleza shughuli hizo**

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilitumia njia zifuatazo:-

- (i) Kuzitaka Wizara husika ziwasilishe Taarifa za Ulinzi na Usalama kwenye Kamati katika vipindi mwafaka;
- (ii) Kupitia na kuchambua Taarifa zilizowasilishwa na Wizara husika na Taasisi zilizo chini ya usimamizi wa Kamati;
- (iii) Kupitisha bajeti na kutathmini utekelezaji wa kazi zilizofanywa na bajeti iliyoidhinishwa kwa Wizara husika;
- (iv) Kufanya ziara katika baadhi ya mikoa ili kuona utendaji kazi wa vyombo vya Ulinzi na Usalama na changamoto zinazovikabili ili kuzitafutia majawabu Serikalini;
- (v) Kamati ilitembelea Bunge la India kwa ajili ya kubadilishana mawazo na uzoefu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge hilo.

4 FEBRUARI, 2015

## 2.3 Shughuli zilizofanyika

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia majukumu yaliyoainishwa kwenye Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Aprili, 2013, Kamati ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

### 2.3.1 Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ziara kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Wizara husika. Miradi na maeneo yaliyotembelewa na Kamati ni kama ifuatavyo:-

- Makao makuu ya ofisi za Mamlaka ya vitambulisho vya Taifa (NIDA) kukagua maendeleo ya uchapishaji na ugawaji wa vitambulisho vya kitaifa.
- Chuo cha Uhamiaji Moshi – kukagua ujenzi wa chuo na utoaji wa mafunzo.
- Ofisi za Vikosi vya Zimamoto na Uokoaji vya Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro.
- Chuo cha mafunzo cha Polisi Moshi
- Magereza ya Mwanga, Karanga na Rombo
- Ofisi za Magereza ya Mkoa Arusha na Kilimanjaro
- Ofisi ya Polisi ya Mkoa wa Arusha
- Chuo cha maafisa wa Jeshi-Monduli (*Tanzani Military Academy*)
- Kituo cha mpakani cha Namanga.

**Mheshimiwa Spika**, katika ukaguzi huo, Kamati ilibaini pamoja na mambo mengine, kuwa licha ya fedha kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi mbalimbali, fedha hizo huchelewa

4 FEBRUARI, 2015

mno kupelekwa na hazipelekwi zote. Hali hii inakwamisha utimizaji wa malengo ya kibajeti na kuathiri utekelezaji wa miradi hiyo. Maelezo ya kina na maoni ya Kamati kuhusu hali hiyo yalitolewa katika mukutano wa 15 wa Bunge, wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

### **2.3.2 Uchambuzi wa Taarifa za Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti**

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 98(2) inaelekeza Kamati kufanya vikao vya kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti za Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kipindi kisichozidi siku Tisa (9).

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi uliofanywa na Kamati yалидhihirisha dosari mbalimbali kuhusu utekelezaji wa kazi za Wizara hizo. Dosari kubwa ni tafizo la mtiririko wa fedha kutoka HAZINA kutokuwa wa kuridhisha, kutotengwa kwa fedha za kutosha za miradi ya maendeleo na kutotengwa kwa fedha kabisa za miradi ya Maendeleo kwa ajili ya vikosi vya Zimamoto na Uokoaji. Maelezo ya kina kutohana na uchambuzi wa Bajeti yalitolewa wakati wa mukutano wa 15 wa Bunge.

### **2.3.3 Uchambuzi wa Miswada ya Sheria**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015 Kamati ilichambua Muswada mmoja wa sheria ulioletwa kwenye Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1). Muswada huo ni Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha na Risasi wa mwaka 2014. Katika kuufanya kazi Muswada huo, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 84(2) na 117(a) kuhusu kualika Wadau ili kupata maoni na ushauri wao kwa ajili ya kuuboresha Muswada huo. Hata hivyo, Kamati haikumaliza kazi hiyo kutohana na wadau kueleza kwamba hawakushirikishwa.

4 FEBRUARI, 2015

#### **2.3.4 Uchambuzi wa Itifaki na Mikataba ya Kimataifa**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa kuridhia Itifaki na Mikataba ya Kimataifa, Kamati ilichambua Itifaki ya Ushirikiano wa Masuala ya Ulinzi kwa nchi za Afrika Mashariki. Katika uchambuzi huo Kamati ilishirikisha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Maoni ya Kamati yaliwasilishwa Bungeni wakati wa mukutano wa 16 na 17 wa Bunge na Bunge liliridhia Itifaki hiyo.

#### **2.3.5 Uchambuzi wa Taarifa za Hali ya Ulinzi na Usalama nchini**

**Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa majukumu yake Kamati ilipitia na kuchambua Taarifa za ulinzi na Usalama zilizowasilishwa na Wizara husika kila baada ya miezi mitatu.

**Mheshimiwa Spika**, mapitio ya Taarifa hizo yalilenga kutekeleza jukumu la Kibunge la kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Kutohana na uchambuzi na utekelezaji uliofanyika, Kamati ilibaini mambo mbalimbali kama yanavyo fafanuliwa hapa chini.

### **3.0 YALIYOBAINIKA**

**Mheshimiwa Spika**, Mambo mbalimbali yaliyobainika yanahusu:-

1. Usalama wa Raia na Mali zao
2. Uhamiaji
3. Utoaji wa Vitambulisho vya Taifa
4. Ulinzi na Usalama wa Mipakani
5. Hali ya Magereza
6. Huduma za Zimamoto na Uokoaji

4 FEBRUARI, 2015

### 3.1 Usalama wa Raia na Mali zao

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara ya Kamati pamoja na taarifa kutoka kwenye Wizara husika, Kamati ilibaini kuwa, kwa ujumla hali ya ulinzi wa nchi na usalama wa raia katika kipindi hiki ilikuwa shwari, japo zipo changamoto chache za uvunjifu wa amani na vitendo vya uporaji mali, na pia matukio ya mauaji ya vikongwe na albino yalitokea katika baadhi ya mikoa.

#### 3.1.2 Uhamaaji

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi hiki tatizo la wahamaaji haramu lilijitokeza katika mikoa ya mipakani ya Arusha, Kagera, na Kilimanjaro. Tatizo hili bado ni changamoto kubwa. Wahamaaji haramu wanaingia nchini kwa kutumia njia za miguu, baiskeli, pipipiki na magari. Wengi wakitokea Ethiopia, wengine ni kutoka Kenya, Somalia, Pakistani, Uganda, Burundi. Wahamaaji haramu wakikamatwa inabidi kuwapeleka Mahakamani kwa mujibu wa sheria na baadaye kuhifadhiwa magerezani wakati tayari yana msongamano mkubwa.

#### 3.1.3 Ulinzi na Usalama wa Mpaka

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki hali katika mpaka yetu yote imekuwa shwari licha ya kuwepo kwa tatizo la uingiaji wa wahamaaji haramu. Aidha katika baadhi ya vituo vya mipakani kama Namanga kuna tatizo la upungufu wa magari hivyo kufanya kazi ya doria za mpakani kutofanyika kwa ufanisi, changamoto nyingine za mpakani ni:-

##### (a) Wananchi kujenga mpakani:

**Mheshimiwa Spika**, Kuna baadhi ya wananchi wamejenga nyumba au kulima mashamba na kufanya shughuli nyngine kama za biashara katika maeneo ya mpaka hasa kwenye mpaka wetu na Zambia (Tunduru) ambapo kuna watu wamejenga nyumba kuzunguka beacons za mpaka.

4 FEBRUARI, 2015

**(b) Kuharibiwa mawe ya mpaka(Beacons):**

**Mheshimiwa Spika,** Mawe ya mpaka yameharibiwa na mengine kung'olewa. Mfano; Kamati ilijulishwa kuwa, jiwe la mpaka lililopo Kaskazini Mashariki mwa mji wa Namanga umbali wa km. 3 limeangushwa na kusogezwa pembedi kutokana na shughuli za uchimbaji mawe na changarawe katika eneo hilo.

Aidha Kamati ilijulishwa kwamba kwa kushirikiana na Serikali za Kenya na Burundi, mawe yaliyoharibiwa yameanza kufanyiwa ukarabati katika mipaka na nchi hizo.

**3.2 Jeshi la Magereza**

**(a) Matatizo ya magereza**

**Mheshimiwa Spika,** Magereza nchini yanakabiliwa na matatizo mbalimbali mfano, msongamano wa wafungwa na mahabusu, Upungufu wa magodoro na mablanketi. Upungufu wa sare za askari na wafungwa na upungufu wa mabweni ya wafungwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipotembelea Gereza la Rombo ilikuta ujenzi wa bweni la wanawake halijakamilika hivyo wanawake wafungwa wanahifadhiwa sehemu ya gereza la mabweni ya wanaume.

**(b) Malalamiko ya wafungwa na mahabusu**

**Mheshimiwa Spika,** Mahabusu katika Magereza yote yaliyotembelewa walilalamika kuhusu kesi zao kuchelewa kusikilizwa kutokana na upelelezi kutokamilika mapema, kubambikiziwa kesi, masharti magumu ya dhamana, watuhumiwa kutofikishwa mahakama za mwanzo ili kesi zao zisikilizwe, na mahakama kuahirisha kesi mara kwa mara.

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile Wafungwa katika magereza yote yaliyotembelewa walilalamikia kitendo cha kutotolewa kwa

4 FEBRUARI, 2015

nakala za hukumu mapema ili kuwawezesha kukata rufaa. Aidha, walilalamikia kupewa chakula cha aina moja, yaani ugali na maharage.

#### **(c) Uhaba wa makazi ya Askari**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa na kujionea kuwa nyumba za askari magereza ni chache na ni chakavu hivyo kuwafanya baadhi ya askari kuishi nje ya kambi.

#### **3.3 Vitambulisho vya Taifa**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua shughuli za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa. Madhumuni ya ziara hii ilikuwa kuona maendeleo ya uchapishaji na ugawaji kwa wananchi Vitambulisho vya Taifa. Kamati ilikuta kazi ya kuchapisha vitambulisho vya uraia inaendelea sambamba na kazi ya kuandikisha walengwa katika mkoa wa Dar es Salaam na Mikoa yote ya Tanzania Zanzibar.

Hata hivyo kazi hii haiendi kwa kasi inayotakiwa kutokana na upungufu wa zana za kusajili walengwa (*Mobile Enrollment Unit*). Aidha bajeti ya kununulia zana hizo iliidhinishwa na Bunge lakini hadi wakati wa ziara ya Kamati, fedha hizo zilikuwa hazijatolewa na Hazina.

#### **3.4 Huduma za Zimamoto na Uokoaji**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kutembelea vikosi vya zimamoto na ukoaji vya Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro. Vikosi hivi vinaendelea kutekeleza vizuri majukumu yao, hata hivyo vyote viwili vinakabiliwa na changamoto mbalimbali za upungufu wa Askari, ukosefu wa magari ya kuzima moto na uhaba wa maeneo ya kujazia maji (*fire hydrants*). Kwa jumla vikosi vyote vya Zimamoto nchini vinakabiliwa na tatizo la kukosa zana za uokoaji (*Rescue equipments*).

4 FEBRUARI, 2015

#### **4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na shughuli zilizotekelezwa na Kamati, yilibainika mambo mbalimbali kama nilivyoyaeleza hapo awali. Kwa kuzingatia mambo yaliyobainika, Kamati inatoa ushauri kwa Serikali na mapendekezo kwa Bunge kama ifuatavyo:-

##### **4.1 Ushauri kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

###### **4.1.1 Kuhusu Jeshi la Polisi:**

a) Katika ziara ya Chuo cha Polisi Moshi, Kamati iliridhika na uendeshaji wa Chuo hicho, hata hivyo ili kuongeza ufanisi zaidi, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani inashuriwa kuzifanyia kazi kwa haraka changamoto zilizopo hasa kuhusu:

- (i) Upungufu wa vyumba vya madarasa na mabweni ya wanafunzi;
- (ii) Upungufu wa vifaa vya kufundishia;
- (iii) Majengo mengi ni chakavu na yanahitaji ukarabati mkubwa.

(b) Kamati inatoa pongezi kwa Jeshi la Polisi nchini kwa jitihada za kudhibiti uhalifu pote nchini, aidha Kamati ilipotembelea Mkoa wa Arusha iliridhika na hali ya kupungua matukio ya uhalifu na pia ilikuta hali ya utulivu na amani imejerea katika jiji la Arusha.

Pamoja na pongezi hizi, Kamati haikuridhishwa na taarifa za wakati huo kwamba bado upelelezi ulikuwa unaendelea wa kuwasaka waliohusika katika matukio mawili ya ulipuaji wa mabomu katika Jiji la Arusha.

Hata hivyo, Kamati imetiwa moyo na taarifa za hivi karibuni kwamba baadhi ya wahusika wa matukio hayo ya kigaidi wamekamatwa na wamefunguliwa kesi mahakamani. Kamati inaishauri kwamba kesi hiyo isikilizwe haraka na kutolewa hukumu ili ikidhi matarajio ya wananchi.

4 FEBRUARI, 2015

(c) Jeshi la Polisi litafute njia mbadala na za kisasa za kupambana na kudhibiti uingizaji nchini wa madawa ya kulevyo ukiwemo usafirishaji wa bangi kwenda Kenya na mirungi kutoka Kenya kuingia Tanzania.

(d) Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na jamii liongeze jitihada na libuni mbinu mpya za kuwadhibiti wale wote wanao endesha uhalifu wa uuaji wa watu wenyewe ulemavu wa ngozi (Albino) na vikongwe. Aidha wizara za Ardhi, TAMISEMI, zishirikiane na jeshi la Polisi kudhibiti mapigano baina ya wakulima na wafugaji yanayotokea katika baadhi ya mikoa kutokana na migogoro ya ardhi.

#### **4.1.2 Magereza:**

(a) Kuhusu chakula cha wafungwa

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti ya chakula cha wafungwa kutoka **Sh. 500/=** kwa siku mpaka **Sh.1,500/=** kwa siku. Hata hivyo, Serikali haikutoa fedha kwa ajili ya chakula cha wafungwa kwa mwezi wa Oktoba 2014 na mwezi wa Disemba 2014 ilioa nusu tu ya kiwango kinachotakiwa kwa ajili ya chakula cha wafungwa.

Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha za chakula cha wafungwa zote na kwa wakati kwa kuwa kutotoa fedha zote kunasababisha Wizara kukopa na kuendelea kulimbikiza madeni.

(b) Kuhusu msongamano magerezani, Kamati inazidi kuishauri Serikali kwamba:-

(i) Isimamie utekelezaji wa sheria ya “community service”, ambapo wafungwa wenyewe makosa madogo madogo wapewe adhabu ya vifungo vya nje, huku wakipewa kazi za kutumikia jamii. Sheria hii ikitumika vizuri na katika mikoa yote Tanzania Bara itasaidia kupunguza idadi ya wafungwa magerezani.

4 FEBRUARI, 2015

(ii) Vile vile Serikali isimamie utekelezaji wa sheria ya "Parole" ambapo mfungwa anayeonyesha mwenendo na tabia njema gerezani anaweza kutumia nusu ya kifungo gerezani, na nusu iliyobaki akamalizia nyumbani kwake.

(iii) Kamati za kusukuma kesi (*case flow management Committees*) za ngazi za wilaya na Mikoa zипитie kesi mara kwa mara ili kuhakikisha mahabusu hawakai magerezani muda mrefu wakisubiri kesi zao kusikilizwa.

(iv) Serikali iongeze bajeti ya kuhudumia magereza ili kudumisha haki za msingi za wafungwa na mahabusu hasa kuhusu huduma za chakula, mavazi (sare), madawa na malazi.

#### **4.1.3 Uhamaaji:**

(a) Kamati iliridhika na utendaji kazi wa kituo cha mpakani cha Namanga, hata hivyo, Serikali inashauriwa izifanyie kazi changamoto zifuatazo, zinazovikabili vituo vyote vya mipakani.

(i) Upungufu wa vyombo vya usafiri (magari/pikipiki) kwa ajili ya kuimarisha doria katika mipaka yote.

(ii) Kutokuwepo kwa zana za kisasa za upekuzi wa abiria na mizigo, na hasa scanner. Vile vile hakuna mbwa wa kunusa na kubaini madawa ya kulevya.

(iii) Serikali ifanye maandalizi ya vituo vyote vikubwa vya mipakani ili vitoe huduma kwa saa 24, hii ni pamoja kuongeza shifti za kazi na pia wafanyakazi.

(b) Kuhusu tatizo la wahamaaji haramu wanaokamatwa mipakani, Kamati inashauri kwamba, wakishafikishwa mahakamani kwa mujibu wa sheria, wasiendelee kupelekwa magerezani, bali warudishwe makwao kwa njia ya barabara ili wasiongeze msongamano na gharama za kuwatunza magerezani.

4 FEBRUARI, 2015

#### **4.1.4 Zimamoto:**

Kwa kuwa vikosi vyote vya zimamoto nchini vinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa zana za kazi, hasa magari ya kuzima moto na vifaa vya uokozi, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kiwango cha bajeti ili kuviwezesha vikosi hivi kufanya kazi zake kwa ufanisi. Namna moja ya kuongeza bajeti kwa chombo hiki ni kwa Serikali kuongeza kiwango cha fedha wanazobakishiwa baada ya kuzikusanya (retention) kutoka 49% ya sasa hadi 70% kama ilivyokuwa huko nyuma.

#### **4.2 Wizara ya Ulinzi na JKT**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Kamati inaishauri ifuatavyo:-

##### **4.2.1 Kuhusu Jeshi la Wananchi:**

(a) Kamati iliridhika na uendeshaji wa Chuo cha Maafisa wa Kijeshi Monduli kinachotoa mafunzo kwa Maafisa wa Jeshi letu pia wa kutoka nchi jirani za Kenya, DRC, Uganda, Burundi, Rwanda na Sycheles. Hata hivyo, Wizara izifanyie kazi changamoto zinazokikabili chuo hiki, hasa:-

(i) Uchache wa mabweni, hasa ya wanawake

(ii) Ukarabati wa majengo hasa nyumba za Maafisa, mabweni ya wanafunzi, ukumbi wa mikutano na uwanja wa kwata.

(iii) Tatizo la uvamizi wa maeneo ya mafunzo ya medani lipatiwe ufumbuzi wa haraka na wa kudumu.

(b) Kuhusu upungufu wa nyumba za Askari na Maofisa uliopo katika vikosi vingi nchini, Kamati inaishauri Serikali iongeze kasi ya ukamilishaji wa mradi wa ujenzi wa nyumba 10,000.

4 FEBRUARI, 2015

(c) Ujenzi wa Chuo cha Unadhimu (*staff college*) katika eneo la Duluti (Arusha) upewe msukumo mpya ili chuo hiki kiwe na majengo yake. Hivi sasa kinaendeshwa kwa kujibana katika majengo ya chuo cha Kijeshi cha Monduli.

(d) Kamati inalipongeza Jeshi la Wananchi kwa kazi kubwa na nzuri ya kulinda mipaka yetu, kwani katika kipindi hiki hali ya mipaka yetu yote imekuwa shwari.

Vilevile Kamati inawapongeza wanajeshi wetu wanaolinda amani nchi za nje chini ya usimamizi wa Umoja wa Mataifa huko Congo DRC, Darfull( Sudan) Lebanon,Sudan Kusini, Jamhuri ya Afrika ya kati (CAR)na Ivory Coast, kwa kazi nzuri na ya kutukuka.

#### **4.2.2 Jeshi la Kujenga Taifa**

a) Kambi ya JKT Oljoro (833 KJ) isaidiwe kuongezewa nyumba za Askari na vifaa vya mafunzo.

(b) Muda wa mafunzo ya JKT kwa vijana kutoka vyuoni kwa mujibu wa sheria uongezwe kutoka miezi 3 ya sasa na iwe walau miezi 6. Vijana wanaokwepa mafunzo hayo bila sababu za msingi wanavunja sheria hivyo Serikali iwachukulie hatua za kisheria.

(c) Kwa kuwa kuna mgongano wa muda wa vijana hao kuripoti kwenye mafunzo ya JKT na hapo hapo kuripoti vyuoni, Kamati inazidi kuishauri Serikali kwamba Wizara ya Ulinzi na ya Elimu wakae pamoja na kutafuta njia ya kuoanisha mihula hii.

#### **5.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, kama taarifa hii ilivyoonyesha ni kwamba vyombo vyote vya ulinzi na usalama katika kipindi hiki vimefanya kazi nzuri na ndiyo maana nchi yetu imetulia, ina amani na umoja. Ili vyombo hivi vidumishe amani iliyopo,

4 FEBRUARI, 2015

tunaishauri Serikali itimize wajibu wake wa kibajeti kwa kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya sekta ya ulinzi, fedha hizo zipelekwe zote kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuhitimisha kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii adhimu kuwasilisha Taarifa ya Mwaka 2014 ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama.

Napenda pia kuwashukuru Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi (Mb) na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Mathias Meinrad Chikawe (Mb) na Naibu Waziri wake Mhe. Pereira Ame Silima (Mb) kwa ushirikiano wanaoutoa kwa Kamati. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umahiri wao katika kuchambua hoja pamoja na kutoa ushauri wa mara kwa mara ambaou umekuwa ukizisaidia Wizara husika kufanya maboresho ya utendaji kazi wao. Naomba kuwataja kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Anna M. Abdallah, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Mohamed Seif Khatib, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Brig.Gen.(Mst)Hassan A. Ngwilizi,Mb - Mjumbe
4. Mhe. Capt.(mst) John Zefania Chiligati,Mb "
5. Mhe. Mariam Mfaki, Mb "
6. Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mb "
7. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb "
8. Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya, Mb "
9. Mhe. Cynthia Hilda Ngoye, Mb "
10. Mhe. Vita Rashid Mfaume Kawawa, Mb "
11. Mhe. Dkt. David Mciwa Mallole, Mb "
12. Mhe. Hamad Ali Hamad, Mb "
13. Mhe. Rachel Mashishanga Robert, Mb "
14. Mhe. Dkt. Augustino Lyatonga Mrema, Mb "
15. Mhe. Vincent Josephat Nyerere, Mb "


**Mheshimiwa Spika**, Napenda pia kuchukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah na watumishi wote wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake.

4 FEBRUARI, 2015

Kipekee, nawashukuru Ndugu Charles Mloka, Ndugu Theonest Ruhilabake, ndugu Athuman Hussein, ndugu Nesta Kawamala na ndugu Onesmo Laulau kwa kuratibu vyema kazi za Kamati hadi taarifa hii ilipoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako tukufu lipokee, lijadili na kuikubali Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa Mwaka 2014.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.



Anna M. Abdallah, (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA ULINZI NA USALAMA**

4 Februari, 2015

**MWENYEKITI:** Naomba sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mwakilishi wake, Mheshimiwa Jafo.

**MHE. SELEMANI S. JAFO (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza awali ya yote napenda kukupongeza wewe sana, kwa sababu nafahamu ni Mwenyekiti wangu katika Kamati ile ya Mambo ya Lishe. Sisi Wazaramo tunasema, "Waonadovudovu songele kutari." Hiyo ni dalili njema sana. Hongera sana! (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hii ni ya mwaka, inawasilishwa kwa kipindi cha pili, tangu kuundwa kwa Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kufuatia marekebisho ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge ya mwezi Apirili, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali majukumu ya Kamati hii, yalikuwa yakekelezswa na Kamati iliyokuwa ikijulikana kama Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, chini ya Kanuni ya 115, ikisomwa pamoja na nyongeza ya nane ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge ya toleo la mwaka 2007. Hata hivyo, uzoefu uliopatikana kabla ya kutumika kwa Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2007, umeendelea kuisaidia Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi tangu ilipoundwa Aprili, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge walioteuliwa katika Kamati hii, kwa mujibu wa Kanuni ya 116 Kanuni ndogo ya (3), ni 14. Naomba kuwataja kwa majina.

Wa kwanza ni Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu na Makamu Mwenyekiti. Wajumbe ni Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mheshimiwa John Magale Shibuda, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Mohamed Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Thuwayba Idrisa Muhamed, Mheshimiwa Susan Jerome Lyimo, Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo, Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mheshimiwa Eng. Hamad Yussuf Masauni na mimi ninayewasilisha taarifa hii, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa

4 FEBRUARI, 2015

Kimataifa, katika fasili ya (4) ya Kifungu cha (6), pamoja na fasili ya (1) ya kifungu cha (7) vya nyongeza ya nane ya Kamati ya Kudumu ya Bunge, toleo la Aprili, 2013. Majukumu hayo ni kusimamia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya kusimamia Wizara hizo, Kamati hii ina majukumu mengine manne, yaliyotajwa kwenye fasili ya pilii (a) ya Kifungu cha (7) cha nyongeza ya nane, ya Kanuni za kudumu za Bunge ya Toleo la 2013. Majukumu hayo ni kuimarisha ushirikiano kati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mabunge ya nchi nyingine.

Pili, kufuatilia mwenendo wa hali ya mtengamano wa Afrika Mashariki; tatu, kushughulikia taarifa za wawakilishi wa Tanzania katika Bugne la Afrika Mashariki, SADC na Bunge la Afrika; Nne, kushughulikia taarifa za vyama mbalimbali vya Kibunge, ambapo Bunge la Jamhuri wa Tanzania ni mwanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 119 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2013, Kamati zote za Buge ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, zimepewa ruhusa ya kuwa na majukumu ya ziada yaliyoainishwa mahsus kwa kila Kamati. Ruhusa hiyo ya majukumu ya nyongeza imeainishwa kwa namna mbili zifuatazo:-

Moja, Kamati imeruhusiwa kupendekeza jukumu lingine lolote; pili, Mheshimiwa Spika kuipa Kamati jambo lingine lolote kadri anavyoona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa majukumu ya Idara na Taasisi za Serikali, Sera Sheria na Miongozo mbalimbali hutumika katika utekelezaji huo. Kutohana na mwelekeo huo, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ilipokuwa ikisimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ilirejea Sera ya Taifa

4 FEBRUARI, 2015  
ya Mambo ya Nje ya mwaka wa 2001. Mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, pamoja na Sheria Kanuni na taratibu mbalimbali za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia dhima ya Kamati na Majukumu yaliyoreshwa katika Kanuni ya Kadumu ya Bunge, Kamati iliandaa mpango kazi wa utekelezaji wa majukumu hayo. Katika utekelezaji wa mpango wake, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge ikiwemo Kanuni ya 117 inayohusu utaratibu katika Kamati ya Kudumu ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015, Kamati ilitekeleza majukumu yake yanayohusiana na Kuisimamia na kuishauri Serikali, utungaji wa Sheria zinazosimamia Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa pamoja na ile ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Uridhiaji wa Mikataba, Itifaki na Makubaliano ya Kimataifa; ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya shughuli hizo, Kamati ilipanga kupokea na kujadili taarifa za uwakilishi wa Watanzania katika Bunge la Afrika Mashariki, SADC, IPU, ACP-EU na Bunge la Afrika. Vilevile Kamati ilipanga kupokea taarifa za Viongozi wa CPA Tawi la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kupokea na kujadili taarifa hizi, ilikuwa ni kutekeleza jukumu la Kamati katika eneo la uhusiano na ushirikiano wa Kibunge na dhana nzima ya Diplomasia ya Kibunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1), Kanuni ya Kudumu ya Bunge Toleo la 2013, Kamati za Bunge za Kisekta zinatakiwa kukagua utekelezaji wa Miradi wa maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi iliyokaguliwa na Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa chini

4 FEBRUARI, 2015

ya Fungu Vote 34 - Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirkiano wa Kimataifa, Fungu 104 - *Policy and Planning, symbol* ya kibajeti, ambayo Bajeti Code ya Mradi huu husika ilikuwa ni 6391, inayojulikana kama *Acquisition Expansion Rehabilitation of Mission's Building* yaani, Ununuzi na Ukarabati wa Majengo ya Balozi za Tanzania Nje ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukaguzi huo, Kamati ilikagua mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Ubalozi iliyoko Maputo, Msumbiji na ukarabati wa jengo la Ofisi ya Ubalozi iliyoko Paris, Ufaransa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ukaguzi huo, Kamati ilibaini pamoja na mambo mengine, ucheleweshaji wa fedha zilizoidhinishwa. Hali hii ilikwamisha ufikishaji wa malengo ya kibajeti na kuathiri tija ya Miradi hiyo. Maelezo ya kina ya maoni ya Kamati kuhusu hali hiyo yalitolewa katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge, wakati wa kujadkili Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirkiano wa Kimataifa kwa mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 98 (2), ikisomwa pamoja nyongeza ya nane ya Kanuni za Bunge, iliitaka Kamati kufanya vikao vya kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirkiano wa Kimataifa na Wizara ya Ushirkiano wa Afrika Mashariki kwa kipindi kisichozidi siku tisa. Lengo la uchambuzi huo ilikuwa ni kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha wa mwaka 2013/2014 na Makadirio yaliyoombwa kuidhinishwa kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi huo, uliofanywa na Kamati yalidhihirisha dosari mbalimbali zilizobainika kuhusu utekelezaji wa Bajeti za Wizara hizo. Baadhi ya dosari hizo ni tatizo kubwa la fedha kutotumwa katika Balozi zetu kwa wakati, kucheleta kwa Wizara ya Mambo ya Nje ya Ushirkiano wa Kimataifa, katika kukamilisha mchakato wa utayarishaji wa Sera ya Taifa ya uhusiano wa mtangamano wa kikanda ukiwemo mtangamano wa Afrika

4 FEBRUARI, 2015

ya Mashariki. Pamoja na ucheleweshaji wa kufanya kazi, baadhi ya mapendekezo yalitolewa Bungeni. Maeleo ya kina kutokana na uchambuzi wa Bajeti, yaliyotolewa wakati wa Mkutano wa Kumi na Tano wa Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015, Kamati ilichambua Muswada mmoja wa Sheria ulioletwa kwenye Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (1). Muswada huo ni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji wa mwaka 2014. Katika kuufanya kazi Muswada huo, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 84 (2) na Kanuni ya 117 (9) kuhusu kualika wadau ili kupata maoni na ushauri wao, kwa ajili ya kuboresha Muswada wa Sheria. Kwa hatua iliyofikiwa katika Muswada huo, wakati wa kuwasilisha Bungeni ukifika, Kamati itaweza kutoa maoni na ushauri wake, kuhusu Muswada huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kuridhia Itifaki na Mikataba ya Kimataifa, Kamati ilialikwa na Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama ili kushiriki uchambuzi wa Itifaki wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuhusu ushirikiano katika masuala ya kiulinzi, yaani *The East Africa Community Protocol on Cooperation in Defense Affairs*. Baada ya uchambuzi huo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama iliwasilisha maoni na mapendekezo wakati wa Mkutano wa Kumi na Sita na Kumi na Saba wa Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilipitia na kuchambua taarifa zifuatazo:-

Moja, Taarifa ya Sektretarieti ya APRM Tanzania, kuhusu shughuli za APRM Tanzania kwa kipindi cha Januari hadi Septemba, 2014; Taarifa ya Hali ya Mtengamano wa Afrika Mashariki; Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli mbalimbali za Balozi za Tanzania, Ulaya, Asia na Africa; Taarifa kuhusu hatua iliyofikiwa kuhusu maandalizi ya Sera ya Taifa ya Mtangamano wa SADC na Afrika Mashariki; Taarifa ya hali ya Ushirikiano wa Majirani wa

4 FEBRUARI, 2015

Tanzania na Taarifa ya Mwenendo wa SADC na namna Serikali inavyosimamia maslahi ya nchi katika kanda za SADC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya taarifa hizo yalilenga utekelezaji wa majukumu ya Kibunge ya ku simamia Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1977. Kutokana na uchambuzi ulionyika, Kamati ilibaini mambo mbalimbali kama yanavyofafanuliwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuititia kujadili taarifa za Wawakilishi wetu kwenye Mabunge ya SADC, Afrika, Afrika na Afrika Mashariki, IPU, ACP-EU, pamoja na watendaji wa Chama cha Wabunge wa Mabunge ya Nchi Wanachama ya Jumuiya ya Madola, unalenga kuliwezesha Bunge kufahamu jinsi vyombo hivyo vinavyofanya kazi na namna Bunge linavowakilishwa katika shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezjai wa shughuli hizo zinazosimamiwa na Kamati hii, changamoto mbalimbali zilibainika. Changamoto hizo zinahusu; moja, Diplomasia ya Kibunge; pili, Ushirikiano wa Kikanda, SADC na Afrika ya Mashariki; tatu, utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa; nne, uwakilishi wa Wawakilishi wa Bunge katika Mabugne ya Afrika Mashariki, Afrika (PAP), SADC-PF na Ushirikiano na Mabunge mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu wa dhana ya Diplomasia ya Kibunge katika kueneza ushirikiano mionganoni mwa nchi mbalimbali, kuboresha na kuchambua Taarifa za Serikali na kuimarisha uhalali wa Kidemokrasia wa Asasi za Kimataifa, Kamati imebaini kuwa maelezo yaliyowahi kutolewa na Frans W. Wesglas, Spika wa kwanza kuchaguliwa na Bunge la Udachi na Gonne de Boer, aliyekuwa Katibu wa Kamati ya Ulinzi ya Bunge la Udachi, yanahusu pia matokeo ya utekelezaji wa dhana ya diplomasia ya Kibunge kwa Wawakilishi wetu.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Spika, wenzetu hawa walisema: "Parliamentary Diplomacy is only in its infancy and needless to say, it still faces numerous problems. Parliaments are relatively weak actors in International arena when compared to Government, NGOs businesses. The organizations in which Parliamentarians work together are often lack finances, resources and power to exert the influence that they could if better equipped. Mandates very greatly among delegations, often leading to problems when formulating conclusions or declarations, which as a result are often terribly vague and noncommittal."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tafsiri isiyo rasmi hii maana yake ni kwamba, Diplomasia ya Kibunge ni dhana changa na kwamba bado inakabiliwa na matatizo mengi. Mabunge bado siyo imara sana katika medani ya Kimataifa yakilinganishwa na mihimili ya Serikali, Asasi zisizokuwa za Serikali na Wafanyabiashara.

Asasi za Kimataifa ambazo kwa kawaida zinakutanisha Mabunge ya nchi mbalimbali katika ushirikiano wa Kibunge, mara nyingi hukosa fedha, rasilimali na nguvu ya kufanya ushawishi jambo ambalo lingeliwezekana kama lingewezeshwa. Mamlaka ya kuamua mionganoni mwa Wawakilishi wa Wabunge wa Mabunge ya nchi mbalimbali, hutofautiana mionganoni mwa Wajumbe katika Asasi hizo, na husababisha tatizo la ugumu katika kufanya maamuzi au kuazimia. Matokeo yake, maazimio haya huwa siyo dhahiri na pia siyo ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa iliyowasilishwa na Wawakilishi wa Bunge letu kwenye Taasisi za Kibunge za Kimataifa, zinadhihirisha usahihi wa kauli hiyo ilyoandikwa kwenye Journal iitwayo "The Hague Journal of Diplomacy 2."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya Kudumu ya Bunge ya toleo la Aprili, 2013, jukumu la kufuatilia hali ya Mtangamano wa Afrika Mashariki limeainishwa chini ya Kamati hii. Katika kufuatia jukumu hilo, Kamati ilizingatia

4 FEBRUARI, 2015

Mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao Ibara ya (2) inaanisha Umoja wa Forodha na Soko la Pamoja kama hatua za mpito kuelekea kwenye Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kujiridhisha na mwenendo wa Mtangamano katika kila hatua, Kamati ilitaka Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki kuwasilisha Taarifa kuhusu maendeleo ya Jumuiya hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijulisha kuwa Wizara ya Ushirikiano ya Afrika ya Mashariki, imeendelea kuratibu kutekeleza na uundwaji wa himaya moja ya Forodha ya Afrika ya Mashariki. Himaya hii ni sehemu ya utekelezaji wa Umoja wa Forodha na hatua iliyochukuliwa na Serikali ni kuunda Kamati ya Kitaifa ya kusimamia utekelezaji wa himaya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua ya Umoja wa Forodha, Mamlaka ya Mapato Tanzania, imetenga Ofisi katika Bandari ya Dar es Salaam, kwa ajili ya Maofisa wa Forodha kutoka nchi Wanachama ambapo nchi za Burundi na Rwanda zimeanza kutumia Ofisi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni ya Kamati kuwa upo umuhimu wa Serikali kutathmini manufaa ya kiuchumi yanayopatikana na utekelezaji wa hatua ya himaya moja ya forodha. Aidha, mambo mbalimbali yaliyojiteze yakichukuliwa kama ni mazingatio katika hatua zinazofuata kwa madhumuni ya kuwa na Jumuiya yenye tija kwa Wantanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine muhimu katika Mtangamano wa Afrika Mashariki ni Soko la Pamoja. Katika hatua hii, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wanalazimika kuwa na Sera ya Biashara ya Nje kutopteka na utekelezaji wa hatua ya Soko la Pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kushirikiana na wadau mbalimbali,

4 FEBRUARI, 2015

imeendelea na zoezi la ukamilishaji wa mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Soko la pamoja. Katika jambo hili, Kamati imebaini kuwa kasi ya kuzifanyia marekebisho sheria za Tanzania ili ziendane na matakwa ya Itifaki ya Soko la pamoja ni ndogo na inahitaji kuongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 5 Julai, 2014, Bunge Iako Tukufu iliridhia Itifaki ya Umoja wa Fedha. Kwa ridhaa hiyo, Kamati ilijulishwa kuwa Tanzania imewasilisha hati ya uridhiwaji (*Instrument of Ratification*) yaani itifaki hiyo kwa Katibu Mkuu wa Jumuia ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja la kuzingatia kuhusu hali ya hatua ya Mtangamano wa Afrika ya Mashariki, ni kuwa nchi mbili tu kati ya nchi tano wanachama ndizo zilizoridhia Itifaki hii. Nchi hizo ni Tanzania na Rwanda tu. Wakati tarehe ya mwisho ya kuwasilisha Hati ya Uridhiwaji ilikuwa ni mwezi Julai, mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inayo maoni kuwa asilimia 60 ya wanachama kutokamilisha maelekezo kwa siku iliyopangwa, siyo jambo la kupuuzwa. Ni vyema Tanzania ijifunze na kujua ukweli kuhusu kuchelewa kwa nchi tatu wanachama kuridhia Itifaki ya Umoja huo wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo manne yalijitokeza wakati Kamati ilivyofuatilia hali ya mtangamano. Mambo hayo ni kama ifuatavyo:-

Moja, ni ufinyu wa Bajeti. Kwa mujibu wa Mkataba wa uanzishwaji wa Jumuia ya Afrika ya Mashariki, Ibara ya 8 (3), kila nchi mwanachama anawajibika kuwa na Wizara Maalum inayohusika na utekelezaji wa Mkataba huu, Waraka wa Serikali. Waraka Na. 432 wa mwaka 2010, unaainisha Wizara hiyo kuwa ni Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuratibu vyema shughuli za Jumuia ya Afrika Mashariki, Wizara husika inahitaji Bajeti inayowezesha kutekeleza jukumu hilo.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati, Wizara hiyo inakabiliwa na madeni kwa kiasi cha Sh. 792,696,598/= tangu mwaka wa fedha 2013/2014. Aidha, mtiririko wa fedha kutoka Hazina hauko vizuri. Hali hii inaathiri uratibu wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mwenendo huu, Kamati inayo maoni kuwa hali hii isiporekebishwa na kufanyiwa kazi ipasavyo, itakuwa ni vigumu kwa Tanzania kujipanga vyema, ili kunufaika na hatua mbalimbali za Mtangamano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati, nchi ya Kenya, Uganda na Rwanda, zinaendelea kuwa na Mikutano ya Utatu, yaani *Coalition of the Willings (Summit of Heads of State of the Northern Corridor Projects)*.

Katika Mkutano wao wa Sita uliofanyika Kigali Rwanda tarehe 1 - 3 Julai, 2014, ziliendlea kujadili masuala ambayo mengine yanendelea kujadiliwa katika Jumuiya au yalishafungwa au yanaendelea kutekelezwa.

Kwa mfano, nchi hizo ziliendelea kujadili ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Kenya hadi Uganda na Sudan Kusini. Ujenzi wa kiwanda cha kusafishia mafuta nchini Uganda, kuwa na utaratibu wa kutumia vitambulisho vya Taifa kama hati ya kusafiria katika nchi hizo, kuharakisha uanzishwaji wa shirikisho la kisiasa la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni ya Kamati yangu, hali hii siyo njema kwa hatma ya maendeleo ya mtangamano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki inaingia hatua ya tatu ya mtangamano baada ya kusainiwa kwa itifaki ya Umoja wa Fedha mwezi Novemba, 2013 na Wakuu wa Nchi Wanachama. Aidha, majadiliano ya kuunda Shirikisho la

4 FEBRUARI, 2015

Kisiasa la Afrika Mashariki yanaendelea. Hali hii inahitaji kujipanga zaidi kwa kila nchi ili hatua za mtangamano ziwe na tija kwa Mataifa husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni ya Kamati kuwa, iwapo hakuna juhudzi za ziada za kujipanga na kama wadau mbalimbali hawashirikishwi na kushiriki kikamilifu katika majadiliano, siyo rahisi kwa shirikisho hilo kuwa na manufaa yoyote kwa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, timu ya wataalamu iliyopewa kazi Oktoba, 2011 ya Jumuia ya Afrika Mashariki ilibaini kuwa many citizens are unaware what the political federation will look like, concerning was raised that there is no clarity on model of Federation East Africa want to adopt.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi umeonyesha kuwa ingawa Shirikisho la Kisiasa ndiyo lengo kuu la Jumuia kwa mujibu wa Ibara ya 5(2), lakini mkataba hauelezi namna ya shirikisho hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni ya Kamati yangu ni kwamba mkataba hauna maelekezo ya kutosha kuongoza mchakato wa kufikia mchakato wa kisiasa. Ni vema suala hili likachunguzwa na kufanyiwa tathmini ya kina kwa kuainisha model inayoweza kuwa na tija kwa nchi wanachama kabla ya kufikia shirikisho hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la kuimarishe uhusiano na ushirikiano wa Kimataifa limewekwa chini ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Wizara hii kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge hufanyiwa usimamizi wa kibunge, yaani *Parliamentary Oversight* na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Naomba kulijulisha Bunge lako hili kuwa Kamati ilifuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii na kubaini changamoto zifuatazo:-

Moja, majengo ya Balozi zetu nje ya nchi. Hali ya majengo ya Balozi zetu nje ya nchi kwa ujumla siyo nzuri.

4 FEBRUARI, 2015

Majengo hayo kwa ajili ya Ofisi na makazi siyo ya kuridhisha na mwonekano wake unahitaji kurekenishwa. Kamati ina maoni kuwa hali hiyo inaathiri heshima, hadhi na ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kidiplomasia kwa Balozi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya Serikali katika ushirikiano wa uhusiano wa Kimataifa hutegemea pamoja na mambo mengine, utendaji wa watumishi wake kwenye Balozi zetu. Vilevile, mafanikio ya utendaji wa watumishi hao yanategemea mazingira ya kazi, ari na namna watumishi hao wanavyowezeshwa. Kamati imebaini kuwa licha ya watumishi walio wengi katika Balozi zetu nje ya nchi, wanajituma katika utendaji, mazingira ya kazi na maslahi yao bado yanahitaji kuboreshwa ili yalingane na kazi wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ina maoni kuwa kwa kuboresha mazingira ya maslahi ya watumishi wa Serikali katika Utumishi wa Ubalanzi, yaani *Foreign Services* itailetea nchi yetu heshima na hadhi zaidi katika diplomasia hususan ile ya kiuchumi.

Vilevile, Kamati imebaini kuwa upangaji wa watumishi katika Balozi zetu ni jambo linalohitaji kufanyiwa kazi kwa umakini. Kwa mfano, kila Ofisi yetu ya Ubalanzi duniani iliyofunguliwa kwa madhumuni ya jumla, yaani *General Objective* na madhumuni mahsus, yaani *specific purpose*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ina maoni kuwa upangaji wa watumishi katika Balozi zetu uzingatia madhumuni mahsus ya kufunguliwa kwa Balozi za nchi husika. Zipo baadhi ya Balozi zinahitaji kuwa na watumishi wenye weledi mkubwa katika diplomasia ya uchumi ya kijeshi na aina nyingine kulinganishwa na Balozi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Diplomasia ya Kibunge hapa Tanzania inatekeleza kwa namna mbalimbali ikiwemo uwakilishi katika vyombo vya Kibunge, Vyama vya Kibunge, ziara na uhusiano kati ya Bunge letu na Mabunge ya nchi moja moja duniani, yaani *Bilateral Parliamentary Relation* na

4 FEBRUARI, 2015

Urafiki wa Kibunge, yaani *Parliamentary Friendships Groups*. Aidha, Bunge letu pia huwakilishwa pia kwenye Mabunge mawili, yaani Kikanda pamoja na Bunge la Afrika. Mabunge hayo ni Bunge la SADC na Bunge la Afrika Mashariki.

Kutokana na shughuli zinazotekelezwa na Kamati, zilibainika changamoto na mambo mbalimbali kama ilivyoelezwa hapo awali. Hivyo sasa naomba kutoa ushauri kwa Serikali na mapendekezo kwa Bunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri kwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa; kwa kuzingatia sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2004 Dira ya Taifa ya mwaka 2025, llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010/2015 pamoja na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa 2011/2012 mpaka 2015/2016, malengo ya Millenium 2015 na tangazo la Serikali, Kamati inashauri yafuatayo:-

(1) Serikali iongeze kasi ya kushughulikia tatizo la hali mbaya ya majengo ya Balozi zetu nje ya nchi.

(2) Ikama ya utumishi Ubalozini, maslahi ya watumishi hao ni pamoja na makazi, usafiri na mazingira ya kazi yaboreshwe ipasavyo.

(3) Serikali ihakikishe kuwa fursa muhimu kwa manufaa ya kutumia dhana ya Diplomasia ya Uchumi zinatumika vyema. Aidha, upangaji wa watumishi katika Balozi hizo uzingatie umuhimu mkubwa wa kujipanga vema katika Diplomasia ya Uchumi, yaani *economic diplomacy*.

(4) Hatua ya kidiplomasia ya usalama katika kushughulikia suala la mgogoro wa mpaka wa Tanzania na Malawi hususan katika Ziwa Nyasa, zichukuliwe kwa umakini mkubwa ili kulinda ipasavyo maslahi ya nchi.

(5) Ofisi zetu za Ubalozini duniani kote ziboreshe huduma zake ili kuwawezesha Watanzania wanaoishi ughaibuni kushiriki vema na kuchangia ipasavyo katika shughuli za kiuchumi na kijamii hapa nchini.

4 FEBRUARI, 2015

(6) Takwimu sahihi na za kina kuhusu Watanzania wanaoishi katika nchi mbalimbali duniani ziboreshe na kufafanua shughuli za Watanzania hao huko waliko.

(7) Serikali iboreshe utaratibu wa kupertia mikataba, itifaki na makubaliano mbalimbali yaliyosainiwa na nchi yetu ili kuongeza ufanisi, tija na kuiletea heshima nchi yetu.

(8) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ihakikishe kuwa inafanya mikutano na Mabalozi wote Tanzania ili kufanikisha azma ya kuongeza tija katika huduma ya ki-council na manufaa makubwa yatokanayo na utaratibu bora kama diplomasia ya uchumi.

(9) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa iongeze kazi ya kushughulikia tatizo la mawasiliano hafifu baina ya Ofisi ya Balozi zetu za nje na Makao Makuu ya Wizara.

(10) Kasi ya kuimarisha sera na mtangamano wa kikanda iongezwe ili kuondokana na tatizo kubwa la wanachama wa Jumuiya bila kuwa na mwongozo rasmi wa kisera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kamati inashauri yafuatayo:-

Moja, mitaala ya elimu Tanzania iboreshe ili kuingiza program mbalimbali zinazoweza kuwawezesha Watanzania kushiriki na kunufaika na hatua mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kisiasa za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Pili, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki isimamie ipasavyo maslahi ya Tanzania dhidi ya athari ya mikutano ya utatu wa nchi za Kenya, Uganda na Rwanda kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Tatu, Serikali ya Tanzania isimamie na kuhimiza utekelezaji wa mapendekezo la timu ya Wataalamu

4 FEBRUARI, 2015

iliyoundwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa ni suala la namna ya model litakalokuwa shirikisho la kisasa, lifanyiwe uchunguzi wa kina sanjari na kuainisha aina ya shirikisho hilo.

Nne, bajeti ya uratibu wa masuala ya Mtangamano wa Afrika mashariki iwezeshe kumudu mahitaji na uendeshaji ili kuweka nchi yetu katika nafasi nzuri yenyе tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa dhana ya diplomasia ya Kibunge inaihitaji Bunge kujipanga vema kiuratibu pamoja na kukupongeza kwa kusimamia utaratibu huo vizuri, Kamati inapendekeza yafuatayo:-

Moja, safari za kikazi nje ya nchi kwa Waheshimiwa Wabunge zitolewe taarifa inayoainisha pamoja na mambo mengine madhumuni ya ziara na mambo yanayohitaji kutekelezwa na kufuatiwa na Serikali.

Pili, Wawakilishi wa Bunge lako Tukufu kwenye Jumuiya ambazo Bunge la Tanzania ni wanachama, walazimike kuwasilisha taarifa zao Ofisi ya Spika ili kwa kadri itakavyowezekana inafaa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge ziweze kupelekwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Tatu, vyama vyote vya urafiki wa kibunge viorodheshwe na kubainishiwa utaratibu wake ili Waheshimiwa Wabunge wote wajulishwe kwa utaratibu utakaoelekezwa na Ofisi ya Spika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru kwa dharti...

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SELEMANI S. JAFO (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa hii na hatimaye kuyakubali maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje

4 FEBRUARI, 2015  
na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kipindi cha Januari, 2014/  
2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti,  
naafiki!

**Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na  
Ushirikiano wa Kimataifa kama  
ilivyowasilishwa Mezani**

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMATI YA  
KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA  
KIMATAIFA KWA KIPINDI CHA JANUARI, 2014  
HADI JANUARI, 2015**

#### **1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii ya mwaka inawasilishwa kwa kipindi cha pili tangu kuundwa kwa Kamati ya Mambo ya Nje na Uhirikiano wa Kimataifa kufuatia marekebisho ya Kanuni za Kudumu za Bunge mwezi Aprili, 2013. Awali, majukumu ya Kamati hii yalikuwa yakitekelezwa na Kamati iliyojulikana kama Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Kanuni ya 115 ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2007. Hata hivyo, uzoefu uliopatikana kabla ya kutumika kwa kanuni za Bunge Toleo la 2007, umeendelea kuisaidia Kamati katika utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi tangu ilipoundwa mwezi Aprili, 2013.

4 FEBRUARI, 2015

## 1.1 Wajumbe wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Wabunge uliowateua kuwa wajumbe wa Kamati hii kwa mujibu wa Kanuni ya 116(3) ni kumi na nne. Naomba kuwataja kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Edward Ngoyai Lowassa, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Mussa Zungu Azzan, Mb -M/Mwenyekiti
3. Mhe. Anastazia James Wambura, Mb- Mjumbe
4. Mhe. John Magale Shibuda, Mb “
5. Mhe. Khalifa Suleiman Khalifa, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Muhammad Ibrahim Sanya, Mb “
7. Mhe. Leticia Mageni Nyerere, Mb “
8. Mhe. Thuwayba Idrisa Muhamed, Mb “
9. Mhe. Susan Anselm Jerome Lyimo, Mb “
10. Mhe. Faith Mohamed Mitambo, Mb “
11. Mhe. Betty Eliezer Machangu, Mb “
12. Mhe. Selemani Sidi Jafo, Mb “
13. Mhe. Eng. Yussuf Hamad Masauni, Mb “

## 1.2 Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa yameainishwa katika fasili ya 4 ya kifungu cha 6 pamoja na Fasili ya 1 ya kifungu cha 7 vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013. Majukumu hayo ni kuzisimamia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**, zaidi ya kusimamia Wizara hizo, Kamati ina majukumu mengine Manne (4) yaliyotajwa kwenye Fasili ya 2(a) ya Kifungu cha 7 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013.

Majukumu hayo ni:-

- (i) Kuimarisha ushirikiano kati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mabunge ya nchi nyingine;

4 FEBRUARI, 2015

(ii) Kufuatilia mwenendo na hali ya mtangamano wa Afrika Mashariki;

(iii) Kushughulikia taarifa za wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki, SADC na Bunge la Afrika; na

(iv) Kushughulikia Taarifa za Vyama mbalimbali vya Kibunge ambapo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 119 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013 Kamati zote za Bunge ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa zimepewa ruhusa ya kuwa na majukumu ya ziada yaliyoainishwa mahsus kwa kila Kamati. Ruhusa hiyo ya majukumu ya nyongeza imeainishwa kwa namna mbili zifuatazo:-

(i) Kamati imeruhusiwa kupendekeza ipewe jukumu lingine lolote;

(ii) Mheshimiwa Spika kuipa Kamati jambo lingine lolote kadri atakavyoona inafaa.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kiliarifu Bunge lako tukufu kuwa, Kamati ilijielekeza kutekeleza majukumu yake yaliyoorodheshwa kwenye Kanuni za Kudumu za Bunge. Aidha, kwa mwaka 2014 Kamati haikupewa kazi ya ziada ya zile zilizoinishwa kwenye Kanuni za Kudumu za Bunge.

### 1.3 Sera zilizozingatiwa

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekelezaji majukumu ya Wizara, Idara na taasisi za Serikali; Sera, Sheria na Miongozo mbalimbali hutumika katika utekelezaji huo. Kutokana na mwelekeo huo naomba kutoa taarifa kuwa, Kamati ilipokuwa ikisimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara za Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ilirejea Sera ya Taifa ya Mambo ya Nje

4 FEBRUARI, 2015  
ya mwaka 2001, Mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na sheria, kanuni na taratibu mbalimbali za nchi.

## **2.0 KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA**

### **2.1 Msingi wa kazi**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia dhima ya Kamati na majukumu yaliyoorodheshwa katika Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la Aprili 2013, Kamati ilianda Mpango Kazi wa utekelezaji wa majukumu hayo. Katika kutekeleza Mpango kazi wake, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ikiwemo Kanuni ya 117 inayohusu utaratibu katika Kamati za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015, Kamati ilitekeleza majukumu yake yanayohusiana na:-

- (i) Kuisimamia na kuishauri Serikali;
- (ii) Utungaji wa sheria zinazotokana na inazosizimamia za Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa pamoja na ile ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki;
- (iii) Uridhiaji wa mikataba, itifaki na makubaliano ya Kimataifa;
- (iv) Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015;

**Mheshimiwa Spika**, Mbali ya shughuli hizo, Kamati ilipanga kupokea na kujadili Taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki, SADC, IPU, ACP-EU, na Bunge la Afrika. Vilevile Kamati ilipanga kupokea Taarifa za viongozi wa CPA Tawi la Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, Lengo kupokea na kujadili taarifa hizi lilikuwa ni kutekeleza jukumu la Kamati katika eneo la uhusiano na Ushirikiano wa Kibunge na dhana nzima ya Diplomasia ya Kibunge.

4 FEBRUARI, 2015

## 2.2 Njia zilizotumika kutekeleza shughuli hizo

**Mheshimiwa Spika**, ili kufanikisha maudhui ya shughuli hizo na kuwezesha upatikanaji wa tija kwa Bunge na Taifa kwa ujumla, Kamati ilitumia njia zilizoendana na masharti ya Kanuni ya 117(3) na (5) kuhusu kukutana na kuzingatia bajeti ya Kamati iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Njia hizo ni:-

- (i) Kuzitaka Wizara ziwasilishe Taarifa kwenye Kamati;
- (ii) Kuwataka Mawaziri wafafanue na kutoa maelezo kuhusu mambo mbali mbali yaliyohitaji ufanuzi;
- (iii) Kufanya uchambuzi wa Sera ya Taifa ya Mambo ya Nje na Mkataba wa Afrika Mashariki ili kuoanisha malengo yake na hali halisi katika utekelezaji;
- (iv) Kupitia na kuchambua Taarifa za utekelezaji zilizowasilishwa na Wizara na Taasisi zilizo chini ya usimamizi wa Kamati;
- (v) Kutathmini mwenendo wa matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa pamoja na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki;
- (vi) Kufanya vikao vya pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa yale mambo yanayogusa Kamati hizi kwa pamoja;
- (vii) Kuwasilisha kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti hoja mahususi zilizotokana na Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati za Mwaka wa Fedha wa 2014/2015; na
- (viii) Kuwaalika wadau mbalimbali na kusikiliza maoni yao kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (2) pamoja na Kanuni ya 117 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2014 wakati wa kujadili Miswada ya Sheria.

4 FEBRUARI, 2015

## 2.3 Shughuli zilizofanyika

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia majukumu yaliyoainishwa kwenye Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Aprili, 2013, Kamati ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

### 2.3.1 Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013 Kamati za Bunge za Kisekta, zinatakiwa kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**Mheshimiwa Spika**, Miradi iliyokaguliwa na Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ipo chini ya Fungu (Vote) 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Kifungu (Sub vote) 1004 – *Policy and Planning*. Simbo ya kibajeti (*Budget Code*) ya mradi husika ni 6391, unaojulikana kama “*Acquisition, Expansion and Rehabilitation of Mission's Buildingts*” yaani ununuzi na Ukarabati wa majengo ya Balozi za Tanzania nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, katika ukaguzi huo Kamati ilikagua Mradi wa Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Ubalozi lilioko Maputo – Msumbiji na Ununuzi na Ukarabati wa jengo la Ofisi ya Ubalozi liliopo Paris – Ufaransa.

**Mheshimiwa Spika**, katika ukaguzi huo, Kamati ilibaini pamoja na mambo mengine, ucheleweshaji wa fedha zilizoidhinishwa. Hali hii ilikwamisha ufikiaji wa malengo ya kibajeti na kuathiri tija ya miradi hiyo. Maeleo ya kina na maoni ya Kamati kuhusu hali hiyo yalitolewa katika mukutano wa kumi na tano wa Bunge, wakati wa kujadili makadirio ya mpato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

4 FEBRUARI, 2015

### **2.3.2 Uchambuzi wa Taarifa za Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti**

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 98(2) ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, iliitaka Kamati kufanya vikao vya kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti za Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kipindi kisichozidi siku Tisa (9). Lengo la uchambuzi huo lilikuwa ni kufanya ulinganisho kuhusu makadirio ya matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na makadirio yaliyoombwa kuidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi uliofanywa na Kamati yalidhihirisha dosari mbalimbali zilizobainika kuhusu utekelezaji wa Bajeti za Wizara hizo. Baadhi ya dosari hizo ni tatizo kubwa la fedha kutotumwa katika Balozi zetu kwa wakati, kuchelewa kwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa katika kukamilisha mchakato wa utayarishaji wa Sera ya taifa kuhusiana na Mtangamano wa kikanda ikiwemo Mtangamano wa Afrika Mashariki, pamoja na kuchelewa kufanya kazi baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa Bungeni. Maeleo ya kina kutokana na uchambuzi wa Bajeti yalitolewa wakati wa mukutano wa Kumi na Tano wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na dosari hizo, Kamati iliiomba Serikali kupitia Bunge lako tukufu kutafuta ufumbuzi wa mambo mawili makubwa ambayo ni:-

- (i) Kuandaa mukutano wa Mabalozi wote wanaoiwakilisha Tanzania nje ya Nchi hapa nyumbani ili kuzungumzia Diplomasia ya Kiuchumi pamoja na changamoto wanazozikabili.
- (ii) Wizara ya Fedha kupitia Hazina kupeleka michango ya Jumuiya ya Afrika Mashariki moja kwa moja kwa Jumuiya hiyo bila kupitishia kwenye Fungu la Wizara.

4 FEBRUARI, 2015

### **2.3.3 Uchambuzi wa Miswada ya Sheria na itifaki za Kimataifa**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015 Kamati ilichambua Mswada mmoja wa sheria ulioletwa kwenye Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1). Muswada huo ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji wa mwaka 2014. Katika kuufanyia kazi Muswada huo, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 84(2) na 117(9) kuhusu kualika Wadau ili kupata maoni na ushauri wao kwa ajili ya kuuboresha Muswada wa Sheria. Kwa hatua iiliyofikiwa katika Muswada huo, wakati wa kuwasilisha Bungeni ukifika, Kamati itaweza kutoa maoni na ushauri wake kuhusu Muswada husika.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa kuridhia Itifaki na Mikataba ya Kimataifa, Kamati ilialikwa na Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama ili kushiriki uchambuzi wa Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu ushirikiano katika Masuala ya Kiulinzi. Yaani (*The East African Community Protocol on Cooperation in Defence Affairs*). Baada ya uchambuzi huo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama iliwasilisha maoni na mapendelekezo wakati wa mkutano wa Kumi na Sita na Kumi na Saba wa Bunge hili.

### **2.3.4 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji**

**Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa majukumu yake Kamati ilipitia na kuchambua Taarifa zifuatazo:-

- (i) Taarifa ya Sekretarieti ya APRM Tanzania kuhusu shughuli za APRM Tanzania kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, 2014;
- (ii) Taarifa ya Hali ya Mtangamano wa Afrika Mashariki;
- (iii) Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki;

4 FEBRUARI, 2015

- (iv) Taarifa ya Utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Balozi za Tanzania, Ulaya, Amerika, Asia na Afrika;
- (v) Taarifa kuhusu Hatua iliyofikiwa katika Maandalizi ya Sera ya Taifa ya Mtangamano wa SADC na Afrika Mashariki,
- (vi) Taarifa ya hali ya ushirikiano na majirani wa Tanzania; na
- (vii) Taarifa ya mwenendo wa SADC na namna Serikali inavyosimamia maslahi ya nchi katika Kanda ya SADC.

**Mheshimiwa Spika**, mapitio ya Taarifa hizo yalilenga utekelezaji wa jukumu la Kibunge la kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Kutokana na uchambuzi uliofanyika, Kamati ilibaini mambo mbalimbali kama yanavyofafanuliwa katika taarifa hii.

### **2.3.5 Mapitio ya Taarifa za Wawakilishi wa Bunge katika SADC – PF, PAP, IPU, CPA, EALA na ACP – EU**

**Mheshimiwa Spika**, utaratibu wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kupitia na kujadili Taarifa za Wawakilishi wetu kwenye Mabunge ya SADC, Afrika na Afrika Mashariki, IPU, ACP- EU pamoja na watendaaji wa Chama cha Wabunge wa Mabunge ya nchi wananchama wa Jumuiya ya Madola, unalenga kuliwezesha Bunge kufahamu jinsi vyombo hivyo vinavyofanya kazi na namna Bunge linavyowakilishwa katika shughuli mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, Fasili ya (2) (a) ya Kifungu cha 7 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013 imeweka sharti la Wawakilishi wa Bunge katika Mabunge ya SADC, Bunge la Afrika na Bunge la Afrika

4 FEBRUARI, 2015

Mashariki kuwasilisha Taarifa zao kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Aidha, jukumu la kuimariswa ushirikiano baina ya Bunge letu na Mabunge mengine limeainishwa katika Fasili ya (2) ya Kifungu cha 7.

**Mheshimiwa Spika**, ili utaratibu huu uweze kuleta tija iliyokusudiwa kwa Bunge letu mambo mawili muhimu yanayohitajika. Mambo hayo ni:-

(i) Wawakilishi wa vyombo hivyo wawasilishe Taarifa zao za Utekelezaji wa majukumu yao kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa; na

ii) Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ipate fursa ya kuchambua, kutoa maoni na kulijulisha Bunge kuhusu shughuli za Wawakilishi hao.

**Mheshimiwa Spika**, Jukumu hili linaweza kutekelezeka kwa utaratibu uliowekwa na Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013 au kwa Kamati kuomba kuwasilisha Taarifa Mahususi kuhusu shughulil za Wawakilishi wa vyombo hivyo.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa, katika Taarifa hii zimeambatishwa nakala za Taarifa za Wawakilishi hao kwa Taarifa ya Bunge. Nakala hizo ni:-

- (i) Taarifa ya wawakilishi wa CPA (Kiambatisho Na. 01).
- (ii) Taarifa ya wabunge wa Bunge la Afrika – PAP (Kiambatisho Na. 02).
- (iii) Taarifa ya wawakilishi wa IPU (Kiambatisho Na. 03).

4 FEBRUARI, 2015

- (iv) Taarifa ya wawakilishi wa Bunge katika ACP-EU(Kiambatisho Na. 04).
- (v) Taarifa ya wawakilishi wa Bunge katika SADC – PF (Kiambatisho Na. 05).

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hizo zimeeleza kwa kirefu shughuli za wawakilishi hao katika kipindi kinachotolewa taarifa cha mwaka 2014.

### **3.0 CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA PAMOJA NA MAONI YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa shughuli hizo zinazosimamiwa na Kamati hii, changamoto mbali mbali zilibainika. Changamoto hizo zinahusu:-

- (i) Diplomasia ya kibunge.
- (ii) Ushirikiano wa kikanda: SADC na Afrika Mashariki.
- (iii) Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.
- (iv) Uwakilishi wa Wawakilishi wa Bunge katika Mabunge ya: Afrika Mashariki, (EALA), Afrika (PAP) na SADC (SADC-PF).
- (v) Ushirikiano na Mabunge mengine.

#### **3.1 Diplomasia ya Kibunge**

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na umuhimu wa dhana ya Diplomasia ya Kibunge katika kuongeza ushirikiano mionganii mwa nchi mbalimbali, kuboresha uchambuzi wa taarifa za Serikali na kuimarisha uhalali wa kidemokrasia wa asasi za kimatiifa, Kamati imebaini kuwa maelezo yaliyowahi kutolewa na Frans W. Weisglas Spika wa kwanza kuchaguliwa wa Bunge la Udachi na Gonne de Boer aliyekuwa Katibu

4 FEBRUARI, 2015  
wa Kamati ya Ulinzi ya Bunge la Udachi yanahusu pia  
matokeo ya utekelezaji wa dhana ya diplomasia ya Kibunge  
kwa wawakilishi wetu. Wenzetu hawa, walisema:-

**Nukuu:** “Parliamentary diplomacy is only in its infancy and, needless to say, it still faces numerous problems. Parliaments are relatively weak actors in the international arena when compared to governments, NGOs and businesses. The organizations in which parliamentarians work together often lack finances, resources and power to exert the influence that they could if better equipped. Mandates vary greatly among delegations, often leading to problems when formulating conclusions or declarations, which as a result are often terribly vague and noncommittal.

**Mheshimiwa Spika**, kwa tafsiri isiyo rasmi hii maana  
yake ni:-

“Diplomasia ya Kibunge ni dhana changa na kwamba bado inakabiliwa na matatizo mengi. Mabunge bado si imara sana katika medani za Kimataifa ikilinganishwa na muhimili wa Serikali, Asasasi Zisizo za KiSerikali (AZISE) na wafanya biashara.

Asasai za Kimataifa ambazo kwa kawaida zinakutanisha Mabunge ya nchi mbalimbali katika ushirikiano wa kibunge mara nyingi mara nyingi hukosa fedha, rasillimali na nguvu ya kufanya ushawishi jambo ambalo lingewezekana kama zingewezeshwa. Mamlaka ya kuamua mionganini mwa wawakilishi wa mabunge ya nchi mbalimbali hutofautiana mionganini mwa Wajumbe katika asasai hizo na kusababisha tatizo na ugumu katika kufanya uamuzi au kuazimia, matokeo yake maazimio hayo huwa si dhahiri na pia si ya uhakika.”

**Mheshimiwa Spika**, taarifa zilizowasilishwa na wawakilishi wa letu kwenye taasisi za kibunge za Kimataifa zinadhahirisha usahihi wa kauli hiyo iliyoadikwa kwenye Journal iitwayo “**The Hague Journal of Diplomacy 2 (2007) 93-99**”.

4 FEBRUARI, 2015

### **3.2 Maendeleo ya Mtangamano wa Afrika Mashariki**

#### **3.2.1 Msingi wa Mtangamano wa Afrika Mashariki**

**Mheshimiwa Spika**, Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unaongozwa na Mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, uliosainiwa na Wakuu wa nchi Wanachama waanzilishi. Nchi hizo ni Kenya, Uganda na Tanzania zilizosaini Mkataba tarehe 30 Novemba, 1999 jijini Arusha. Mkataba huo ulianza kutumika rasmi tarehe 07 Julai, 2000 baada ya kuridhiwa na nchi zote tatu. Mwaka 2007 nchi za Rwanda na Burundi zilizunga na Jumuiya hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa nchi Wanachama zilikubaliana kwamba Mtangamano wa Afrika Mashariki uendelezwe hatua kwa hatua kuanzia Umoja wa Forodha ikifuatiwa na Soko la pamoja, hatimaye Shirikisho la kisiasa.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, nchi Wanachama zinashirikiana katika maeneo mbalimbali yakiwemo ya Viwanda; Siasa; Ulinzi, amani na usalama, Sheria na Mahakama, Maendeleo ya Rasilimali watu; elimu na mafunzo pamoja na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

#### **3.2.2 Hatua za Mtangamano**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, jukumu la kufuatilia hali ya Mtangamano wa Afrika Mashariki limeainishwa chini ya Kamati hii. Katika kufuatilia jukumu hilo Kamati ilizingatia Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao Ibara ya 2 inaanisha Umoja wa Forodha na Soko la pamoja kama hatua za mpito kuelekea kwenye Shirikisho la kisiasa la Afrika Mashariki.

4 FEBRUARI, 2015

### a) Umoja wa Forodha

**Mheshimiwa Spika**, ili kujiridhisha na mwenendo wa Mtangamano katika kila hatua, Kamati iliitaka Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuwasilisha Taarifa kuhusu maendeleo ya Jumuiya hii.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Taarifa hiyo, Kamati ilijulishwa kuwa, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeendelea kuratibu utekelezaji wa uundwaji wa Himaya Moja ya Forodha ya Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**, Himaya hii ni sehemu ya utekelezaji wa Umoja wa Forodha na hatua iliyochukuliwa na Serikali ni kuunda Kamati ya kitaifa ya kusimamia utekelezaji wa Himaya hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, katika hatua ya Umoja wa Forodha, Mamlaka ya Mapato Tanzania imetenga Ofisi katika Bandari ya Dar es Salaam kwa ajili ya Maofisa wa Forodha kutoka nchi Wanachama ambapo nchi za Burundi na Rwanda zimeanza kutumia Ofisi hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Ni maoni ya Kamati kuwa upo umuhimu wa Serikali kutathmini manufaa ya kiuchumi yanayopatikana kwa utekelezaji wa hatua ya Himaya Moja ya Forodha. Aidha, mambo mbalimbali yanayojitokeza yachukuliwe kama mazingatio katika hatua zinazofuata kwa madhumuni ya kuwa na Jumuiya yenyewe tija kwa Watanzania.

### b) Soko la Pamoja

**Mheshimiwa Spika**, hatua nyingine muhimu katika Mtangamano wa Afrika Mashariki ni Soko la Pamoja. Katika hatua hii, nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wanalahimika kuwa na Sera ya Biashara ya nje kutohakana na kutekeleza hatua ya Soko la Pamoja.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kushirikiana na wadau mbali mbali imeendelea

4 FEBRUARI, 2015  
na zoezi la ukamilishaji wa mkakati wa kitaifa wa utekelezaji  
wa Soko la Pamoja.

**Mheshimiwa Spika**, Katika jambo hili, Kamati imebaini kuwa kasi ya kufazinya marekebisho Sheria za Tanzania ili ziendane na matakwa ya itifaki ya Soko la Pamoja ni ndogo na inahitaji kuongezwa.

### c) Umoja wa Fedha

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 5 Julai, 2014, Bunge lako tukufu liliridhia itifaki ya Umoja wa Fedha. Kwa ridha hiyo, Kamati ilijulishwa kuwa Tanzania imewasilisha Hati ya Uridhiwaji (instrument of ratification) ya itifaki hiyo kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**, Jambo moja la kuzingatia kuhusu hali ya Hatua za Mtangamano wa Afrika Mashariki ni kuwa nchi mbili tu kati ya nchi tano Wanachama, ndizo zilizoridhia itifaki hiyo. Nchi hizo ni Tanzania na Rwanda tu wakati tarehe ya mwisho (deadline) ya kuwasilisha Hati ya uridhiwaji ilikuwa ni mwezi Julai, 2014.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inayo maoni kuwa asilimia 60 ya Wanachama kutokamilisha maelekezo kwa siku iliyopangwa si jambo la kupuuzwa. Ni vema Tanzania ijifunze na kujua ukweli kuhusu kuchelewa kwa nchi tatu Wanachama kuridhia itifaki ya Umoja wa huo wa Fedha.

### 3.2.3 Yaliyojitokeza

**Mheshimiwa Spika**, mambo manne yalijitokeza wakati Kamati ilivyofuatilia hali ya Mtangamano. Mambo hayo ni:-

#### a) Ufinyu wa bajeti

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (Ibara ya 8 (3)) kila nchi Mwanachama inawajibika kuwa na Wizara maalum inayohusika na utekelezaji wa Mkataba huu. Waraka wa

4 FEBRUARI, 2015

Serikali, Waraka Na. 432 wa mwaka 2010 unaainisha Wizara hiyo kuwa ni Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuratibu vema shughuli za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wizara husika inahitaji Bajeti inayoiwezesha kutekeleza jukumu hilo. Kutoptana na taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati, Wizara hiyo inakabiliwa na madeni kiasi cha ShT.792,696598/= tangu mwaka wa fedha 2013/2014. Aidha, mtiririko wa fedha kutoka Hazina hauko vizuri, hali inayoathiri uratibu wa shughuli za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**, kutoptana na mwenendo huu Kamati inayo maoni kuwa hali hii isiporekebishwa na kufanyiwa kazi ipasavyo itakuwa vigumu kwa Tanzania kujipanga vema ili kunufaika na hatua mbalimbali za Mtangamano wa Afrika Mashariki.

**b) Mikutano ya utatu ya nchi za Kenya, Uganda na Rwanda.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati, nchi za Kenya, Uganda na Rwanda zinaendelea na Mikutano yao ya utatu. (*Coalition of the Willing/Summit of Heads of State of the Northern Corridor Projects*). Katika Mkutano wao wa sita uliofanyika Kigali, Rwanda tarehe 1 – 3, Julai, 2014 ziliendelea kujadili masuala ambayo mengine yanaendelea kujadiliwa katika Jumuiya au yalishafungwa au yanaendelea kutekelezwa.

Kwa mfano, nchi hizo zinaendelea kujadili ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Kenya hadi Uganda na Sudani Kusini; ujenzi wa Kiwanda cha kusafisha mafuta nchini Uganda; kuwa na utaratibu wa kutumia vitambulisho vyta Taifa kama hati ya kusafiria katika nchi hizo, kuharakisha uanzishwaji wa Shirikisho la kisiasa la Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa maoni ya Kamati yangu hali hii si njema kwa hatma na maendeleo ya mtangamano wa Afrika Mashariki.

4 FEBRUARI, 2015

### c) Maandalizi ya kufikia Shirikisho la Kisiasa

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki inaingia hatua ya tatu ya Mtangamano baada ya kusainiwa kwa itifaki ya umoja wa fedha mwezi Novemba, 2013 na Wakuu wan chi Wanachama. Aidha, majadiliano ya kuunda Shirikisho la kisiasa la Afrika Mashariki yanaendelea. Hali hii inahitaji kujipanga zaidi kwa kila nchi ili hatua za mtangamano ziwe na tija kwa mataifa husika.

**Mheshimiwa Spika**, Ni maoni ya Kamati kuwa iwapo hakuna juhudzi za ziada za kujipanga na kama wadau mbalimbali hawashirikishwi na kushiriki kikamilifu katika majadiliano, si rahisi kwa Shirikisho hilo kuwa na manufaa yoyote kwa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, Timu ya Wataalamu iliyopewa kazi Oktoba, 2011 na Jumuiya ya Afrika Mashariki ilibainisha kuwa:

*“Nukuu; Many citizens are unaware what the political federation will look like. Concern was raised that there is no clarity on model of federation East Africa wants to adopt.”*

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi umeonesha kuwa ingawa Shirikisho la kisiasa ndio lengo kuu la Jumuiya kwa mujibu wa Ibara ya 5 (2), lakini Mkataba hauelezi namna ya Shirikisho hilo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa maoni ya Kamati yangu ni kuwa Mkataba hauna maelezo ya kutosha kuongoza mchakato wa kufikia Shirikisho la kisiasa. Ni vema suala hili likachunguzwa na kufanyiwa tathmini ya kina kwa kuanisha modeli (model) inayoweza kuwa na tija kwa nchi wanachama kabla ya kufikia shirikisho hilo.

### 3.3 Ushirikiano wa kimataifa na Diplomasia ya Uchumi

**Mheshimiwa Spika**, jukumu la kuimarishe uhusiano na ushirikiano wa kimataifa limewekwa chini ya Wizara ya

4 FEBRUARI, 2015

Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Wizara hii kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, hufanyiwa usimamizi wa kibunge (Parliamentary Oversight) na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya nje na Ushirikiano wa kimataifa. Naomba kulijulisha Bunge hili kuwa Kamati ilifuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii na kubaini changamoto zifuatazo:-

### **3.3.1 Majengo ya Balozi zetu nje ya nchi**

**Mheshimiwa Spika**, hali ya majengo ya Balozi zetu nje ya nchi kwa ujumla si nzuri. Majengo hayo kwa ajili ya Ofisi na Makazi si ya kuridhisha na muonekano wake unahitaji kuborehswa. Kamati ina maoni kuwa hali hiyo inaathiri heshima, hadhi na ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kidiplomasia ya Balozi zetu.

### **3.3.2 Utumishi na Maslahi ya Watumishi katika Balozi zetu**

**Mheshimiwa Spika**, mafanikio ya Serikali katika ushirikiano na uhusiano wa kimataifa hutegemea pamoja na mambo mengine utendaji wa watumishi wake kwenye Balozi zetu. Vile vile, mafanikio ya utendaji wa watumishi hao yanategemea mazingira ya kazi, ari na namna Watumishi wanavyowezeshwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa licha ya watumishi waliowengi katika Balozi zetu nje ya nchi kujituma katika utendaji, mazingira ya kazi na maslahi yao bado yanahitaji kuboreshwa ili yalingane na kazi wanazozifanya.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inayo maoni kuwa kwa kuboresha mazingira na maslahi ya watumishi wa Serikali katika utumishi ubalozini (*Foreign Services*) kutailetea nchi yetu heshima na hadhi zaidi katika diplomasia hususan ile ya kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika**, vile vile, Kamati imebaini kuwa upangaji wa Watumishi katika balozi zetu ni jambo linalohitaji kufanyiwa kazi kwa umakini. Kwa mfano, kila Ofisi yetu ya

4 FEBRUARI, 2015

Balozi duniani ilifunguliwa kwa madhumuni ya jumla (*general objective*) na sababu mahususi (*specific purpose*).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina maoni kuwa upangaji wa watumishi katika balozi zetu uzingatie madhumuni mahususi ya kufunguliwa kwa Balozi za Nchi husika. Zipo baadhi ya Balozi zinahitaji kuwa na watumishi wenyewe weledi mkubwa katika diplomasia ya uchumi, ya kijeshi na aina nyingine ikilingamishwa na Balozi nyinginezo.

### 3.4 Diplomasia ya Kibunge

**Mheshimiwa Spika**, Diplomasia ya kibunge hapa Tanzania inatekelezwa kwa namna mbalimbali ikiwemo uwakilishi katika vyama vya kibunge, ziara na uhusiano kati ya Bunge letu na Mabunge ya nchi moja moja duniani (*Bilateral Parliamentary relation*) na urafiki wa kibunge (*Parliamentary friendship group*). Aidha, Bunge letu pia huwakilishwa kwenye Mabunge mawili ya kikanda pamoja na Bunge la Afrika. Mabunge hayo ni: Bunge la SADC na Bunge la Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**, katika eneo hili Kamati imebaini yafuatayo:-

#### 3.4.1 Manufaa ya Diplomasia ya Kibunge kwa Bunge letu

**Mheshimiwa Spika**, utaratibu wa Diplomasia ya kibunge umewezesha Bunge lako Tukufu kutumia diplomasia ya kitaasisi (*Institutional Diplomacy*) kuwezesha Waheshimiwa Wabunge kuchochea kasi ya kuridhia mikataba ya kimataifa iliyosainiwa na Tanzania. Pale ambapo mikataba hiyo inayo tija ya kiuchumi, kisiasa na kijamii hapa nchini, Bunge limetoa msukumo mkubwa wa utekelezaji wa mikataba hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Ni maoni ya Kamati yangu kuwa utaratibu huu wa Diplomasia ya kibunge ukiboreshwa zaidi utachangia kuongezeka kwa tija ya uanachama wa

4 FEBRUARI, 2015  
Tanzania utokanao na kusainiwa kwa mikataba, itifaki au makubaliano ya kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, utaratibu wa uhusiano na ushirikiano wa kibunge chini ya dhana ya diplomasia ya kibunge unalionezea Bunge lako Tukufu uwezo wa ushawishi wa kibunge katika Afrika, Kanda ya SADC na Afrika Mashariki. Kutokana na uwezo huo, Bunge la Tanzania limepata heshima kubwa duniani.

**Mheshimiwa Spika**, umahiri wa kiongozi wa Bunge hili la Kumi katika Diplomasia ya kibunge umeliwezesha Bunge la Tanzania kupata sifa na heshima kubwa katika ukanda wa kusini mwa Afrika. Katika Historia ya nchi yetu tangu Bunge la Tanzania liwe Mwanachama wa Jukwaa la kibunge katika Ukanda wa Kusini mwa Afrika, (SADC) halijawahi kushika nafasi ya juu kabisa kabla ya mwaka huu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa umahiri, weledi na uzoefu wako wa masuala ya kibunge, katika Mkutano wa 36 wa Jukwaa la Mabunge ya nchi wanachama wa SADC PF uliomalizika tarehe 03 Novemba, 2014, kwa mara ya kwanza, Tanzania ilichaguliwa kuongoza Bunge hilo kwa kumchagua Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, (Mb), Spika wa Bunge la Tanzania kuwa, Rais wa Jukwaa hilo kwa kipindi cha miaka miwili. Kamati iliwasilisha Azimio la kumpongeza Mheshimiwa Spika na kuitishwa na Bunge tarehe 7 Novemba, 2014.

**Mheshimiwa spika**, Kamati vile vile inampongeza Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, (Mb), kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jumuiya ya Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Madola (CPA) Kanda ya Afrika kwa kipindi cha Julai 2013 mpaka Julai, 2014.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati yangu inathamini sana umahiri na uhodari wa Mheshimiwa Anne Makinda, (Mb) wa kuliongoza Bunge hili tukufu na kufikia kuaminiwa kuongoza taasisi hizo za kimataifa, kwa hakika ameipeperusha vyema bendera yetu ya Tanzania nje ya nchi.

4 FEBRUARI, 2015

#### **4.0 MAPENDEKEZO NA USHAURI WA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, kutohana na shughuli zilizotekelezwa na Kamati, zilibainika changamoto na mambo mbalimbali kama nilivyoyaeleza hapo awali, hivyo sasa naomba kutoa ushauri kwa Serikali na mapendekezo kwa Bunge kama ifuatavyo:-

##### **4.1 Ushauri kwa Wizara ya Mambo ya Nje na ushirikiano wa kimataifa**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2004, Dira ya Taifa ya mwaka 2025, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 – 2015, Mpango wa Taifa wa Maendeleo 2011/2012 – 2015/2016, Malengo ya Milenia 2015 na Tangazo la Serikali, Kamati inatoa ushauri ufuataao:-

(i) Serikali iongeze kasi ya kushughulikia tatizo la hali mbaya ya majengo ya Balozi zetu nje ya nchi.

(ii) Ikama ya utumishi balozini, maslahi ya Watumishi hao ikiwa ni pamoja na makazi, usafiri na mazingira ya kazi viboreshwe ipasavyo;

(iii) Serikali ihakikishe kuwa fursa muhimu kwa manufaa ya taifa kwa kutumia dhana ya Diplomasia ya uchumi zinatumika vema. Aidha, upangaji wa Watumishi katika Balozi hizo uzingatie umuhimu mkubwa wa kujipanga vema katika diplomasia ya uchumi (*Economic Diplomacy*).

(iv) Hatua za kidiplomasia na kiusalama katika kushughulikia suala la mgogoro wa mpaka wa Tanzania na Malawi hususan katika ziwa Nyasa zichukuliwe kwa umakini mkubwa ili kulinda ipasavyo maslahi ya nchi.

(v) Ofisi zetu za ubalozi duniani kote ziboreshe huduma zake ili kuwawezesha watanzania wanaoishi ughaibuni (Diaspora) kushiriki vema na kuchangia ipasavyo katika shughuli za kiuchumi na kijamii hapa nchini.

4 FEBRUARI, 2015

(vi) Takwimu sahihi na za kina kuhusu Watanzania wanaoishi katika nchi mbalimbali duniani ziboreshwani na kufafanua shughuli za Watanzania hao huko waliko.

(vii) Serikali iboreshe utaratibu wa kupitia Mikataba, itifaki na makubaliano mbalimbali yaliyosainiwa na nchi yetu ili kuongeza ufanisi, tija na heshima ya nchi yetu.

(viii) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ihakikishe kuwa inafanya mikutano ya Mabalozi wote wa Tanzania ili kufanikisha azima ya kuongeza tija katika huduma za kikonseli, na manufaa makubwa yatokanayo na utaratibu bora katika diplomasia ya uchumi.

(ix) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa iongeze kasi ya kushughulikia tatizo la mawasiliano hafifu baina ya Ofisi za Balozi zetu nje ya nchi na Makao Makuu ya Wizara.

(x) Kasi ya kukamilisha Sera ya Utangamano wa Kikanda iongezwe ili kuondokana na tatizo la kuwa Wanachama wa Jumuiya bila kuwa na Mwongozo rasmi wa kisera.

#### **4.2 Ushauri kwa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kamati inashauri ifuatavyo:-

(i) Mitaala ya Elimu Tanzania iboreshwani ili kuingiza program mbalimbali zinazoweza kuwawezesha Watanzania kushiriki na kunufaika na hatua mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kisiasa za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(ii) Wizara ya ushirikiano wa Afrika Mashariki isimamie ipasavyo maslahi ya Tanzania dhidi ya athari za mikutano ya utatu ya nchi za Kenya, Uganda na Rwanda kwa kuzingatia masharti ya Mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

4 FEBRUARI, 2015

(iii) Serikali ya Tanzania isimamie na kuhimiza utekelezaji wa pendekezo la Timu ya Wataalamu iliyoundwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa suala la namna (model) litakavyokuwa Shirikisho la kisasa, lifanyiwe uchunguzi wa kina sanjari na kuainisha modeli ya Shirikisho hilo.

(iv) Bajeti ya uratibu wa masuala ya Mtangamano wa Afrika Mashariki iwezeshwe kumudu mahitaji ya uendeshaji ili kuiweka nchi yetu katika nafasi nzuri yenye tija.

#### 4.3 Mapendekezo kwa Bunge

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa dhana ya Diplomasia ya kibunge inahitaji Bunge kujipanga vema ki-utaratibu, pamoja na kukupongeza kwa kusimamia utaratibu huo vizuri, Kamati inapendekeza kama ifuatavyo:-

(i) Safari za kikazi nje ya nchi za Wabunge zitolewe taarifa inayoainisha pamoja na mambo mengine, madhumuni ya ziara na mambo yanahitaji kutekelezwa na kufuutiliwa na Serikali.

(ii) Wawakilishi wa Bunge lako tukufu kwenye Jumuiya ambazo Bunge la Tanzania ni Mwanachama walazimike kuwasilisha taarifa zao Ofisi ya Spika ili kwa kadri itakavyoonekana inafaa na kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge ziweze kupelekwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

(iii) Vyama vyote vya urafiki wa kibunge viorodheshwe na kubainishwa utaratibu wake, ili Waheshimiwa Wabunge wote wajulishwe kwa utaratibu utakaoelekezwa na Ofisi ya Spika.

4 FEBRUARI, 2015

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu yake hadi kufikia Mwezi Januari, 2015. Tunaamini kuwa fursa hii inayotokana na masharti ya Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, itasaidia kuliwezesha Bunge lako tukufu kutekeleza wajibu wake wa Kikatiba wa kuishauri na kuisimamia Serikali ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia kuchukua nafasi hii kuitambua kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya awamu ya Nne chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Mkuu wa Nchi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, kwa jinsi inavyosimamia heshima na hadhi ya Tanzania katika masuala ya uhusiano na ushirikiano wa Kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru kwa dhati Mheshimiwa Benald C. Membe (Mb), Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Mheshimiwa Samuel J. Sitta (Mb) aliyekuwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Manaibu Mawaziri wao ambao ni Mheshimiwa Mahadhi J. Maalim (Mb) na Mheshimiwa Juma A. Sadalla (Mb), Makatibu Wakuu na Manaibu wao pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara hizo kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati yangu wakati ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, Mwisho, lakini si kwa umuhimu nawashukuru Ndugu Athuman Hussein na Ndugu Ramadhan Abdallah, Makatibu wa Kamati hii kwa kuratibu vema shughuli za Kamati kwa kipindi chote na kufanikisha taarifa hii kuwasilishwa kwa wakati. Nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake.

4 FEBRUARI, 2015

**Mheshimiwa Spiaka**, baada ya kusema hayo sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili taarifa hii na hatimaye kuyakubali maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kipindi cha Januari 2014 hadi Januari 2015.

**Mheshimiwa Spiaka**, naomba kutoa hoja.



.....  
Edward N. Lowassa, Mb

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO  
YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA**

JANUARI, 2015

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Viwanda, Biashara.

**MHE. LUHAGA J. MPINA (MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nichukue nafasi hii kukupongeza sana kwa kuchaguliwa na Bunge kushika nafasi hiyo.

Kwa utangulizi, hii ni taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara katika kipindi cha kuanzia Machi, 2014 hadi Januari, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya utangulizi kwa mujibu wa kanuni ya 117 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge

4 FEBRUARI, 2015  
toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara kwa kipindi cha kuanzia Machi, 2014 hadi Februari, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi nasoma taarifa hii hajigawiwa, kwa hiyo, naomba Wajumbe wagawiwe na kwamba taarifa yangu iingie kama ilivyo kwenye Hansard kwa sababu ni ndefu sana, sitawezza kuisoma yote na kumaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sehemu kuu tano; sehemu ya kwanza ni utangulizi, sehemu ya pili ni mambo yahusuyo fedha na uchumi; tatu, ni mambo yahusuyo viwanda na biashara; na nne ni mapendekezo na tano, ni hitimisho. Waheshimiwa Wabunge, naomba mnisikilize vizuri na muisome vizuri *report* hiyo, ina mambo mazito sana ya kumalizia Bunge hili miaka yake mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yahusuyo fedha na uchumi; mwenendo wa uchumi. Kuna uhusiano hafifu uliopo kati ya mafanikio katika ukuaji wa uchumi na punguzo la umasikini kunakosababisha ongezeko la kukosekana kwa usawa katika jamii. Hali hii inasababishwa na usimamizi mbaya wa chumi (*Poor Economic Management*).

Kamati imeona kuwa kuna usimamizi dhaifu sana wa uchumi hapa nchini, baadhi ya viashiria vya uchumi havileti matumaini ya kujenga uchumi wenye manufaa kwa wananchi wote. Sasa kuna suala la *inflation* na *exchange rate* halikupata nafasi hapa ya kusemwa lakini mtasoma, mtaona.

Naomba nizungumzie suala la riba katika mabenki na taasisi za fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha riba katika mabenki na taasisi za fedha nchini kipo juu sana hivi sasa kwani ni kati ya 15% mpaka 21% wakati riba ya wenye kuweka ipo kati ya 2% tu na 5% wakati huo huo *inflation* iko juu ya 5% sasa. Tatizo la riba kuwa juu linachangiwa na mambo mengi

4 FEBRUARI, 2015

sana, lakini kikubwa mabenki yasilaumiwe sana, Serikali yenyewe ndiyo ambayo inachangia kusababisha viwango hivi vikubwa vya riba kuwepo.

Sababu ya kwanza ni Serikali kuendelea kukopa katika masoko ya ndani kwa hiyo, inakopa kwenye Benki za Biashara na inakopa kwenye mifuko ya jamii na inakopa kwa wananchi, huwezi kupata *interest rate* katika mazingira hayo.

Vilevile Serikali inaendelea kutoza riba za juu sana katika dhamana zake, zile *treasury bills* inazozitoa ambazo sasa hivi ni 13% mpaka 14% sasa katika mazingira hayo unategemea ni Benki gani ya biashara ambayo itatoa riba chini ya hapo kama Serikali yenyewe ina *interest* ya 14% *almost* 15, sasa hakuna benki nyingine inayoweza kutoa riba chini ya hapo.

Serikali kutolipa madeni ya Wazabuni na Wakandarasi. Inakopelekea *NPL (Non Preforming Loan)* kuwa juu na sasa hivi zimefikia 8.5% kwa hiyo, huwezi kutegemea riba ikapungua katika mazingira hayo. Kiwango cha 10% mpaka 40% kwa Amana za Serikali (*Government Deposits*) kiwango hiki ni kikubwa sana cha lazima ambacho tunasema *Statutory Minimum Reserve* kwenye sekta binafsi 10% na Serikalini 40%. Kwa hiyo, viwango hivi vya *SMR* ni vikubwa sana kiasi kwamba vinaathiri uwezo wa utoaji mikopo katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kujenga uchumi imara, ni vema Serikali ikaandaa mkakati kwa lengo la kushusha viwango hivi vya riba hatua ambayo itawawezesha wengi kupata mikopo kwa gharama nafuu na kushiriki katika shughuli mbalimbali za uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu inayofuata ni madeni ya Serikali ambayo ni deni la mifuko ya jamii, madeni

4 FEBRUARI, 2015

ya Wakandarasi na Wazabuni na Watumishi wa Serikali. Deni la mifuko ya jamii ambalo lilielezwa na PAC lenyewe, sitaki kulizungumza sana, lakini nisemee madeni ya Wakandarasi na Wazabuni na watumishi wa Serikali.

Kwa mujibu wa taarifa ya kuishia Juni, 2014 deni la Wakandarasi, Wazabuni na Watumishi wa Serikali liliifikia trilioni 1.3 na hadi kufikia Septemba, 2014, deni hili lilikuwa limelipwa Shilingi bilioni 259 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya wakulima kama yanavyoelezwa, deni la Serikali kwa wakulima hivi sasa kwa wakulima wa mahindi ni Shilingi bilioni 89, ambazo zimelipwa ni Shilingi bilioni 15 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kujenga uchumi wakati wananchi, hasa wazalishaji unawanyang'anya nguvu ya kifedha, halafu unategemea. Deni hili sasa limefikia trilioni 3.9, hili ni nje ya deni ya Taifa. Shilingi trilioni 3.6 halipo kwenye deni la Taifa, ni madeni tu ya Wazabuni, Wakandarasi pamoja na mifuko ya jamii, Shilingi trilioni 3.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la hatai za kimila. Sheria ya Ardhi ya Viji ya mwaka 1999, sambamba na ile ya Ardhi; Sheria ya Viji inagusa maeneo mengi kama vile umiliki na uendelezaji wa ardhi. Lakini 78% ya ardhi ya Tanzania ni viji na kati ya hiyo, ni chini ya 1% ndio iliopimwa na kutolewa hati za kimila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imanzisha dirisha la kilimo na Benki ya Kilimo wakati hakuna utaratibu uliofanywa kutambua hati za kimila. Dhamana kubwa ya wananchi ni ardhi yao ambayo ipo vijiji na ina sifa za kupata hati za kimila.

4 FEBRUARI, 2015

Kamati inaamini kwamba kama hakutafanyika mabadiliko ya kisera itakayowezesha hati ya kimila kutumika kama dhamana ya kupata mikopo katika mabenki na taasisi za fedha, uanzishwaji wa Benki hizo za Kilimo hautazaa matunda na hautaleta manufaa yoyote kwa wananchi kwa sababu wao dhamana yao ndiyo ardhi hiyo iliyopo vijiji.

Kutokana na muda mfupi sana, kuna hizi hati za kawaida. Ardhi ya Tanzania iliyosajiliwa na kupewa hatimiliki za kawaida ni 10% ya ardhi yote. Kwa hiyo, uchache huu unasababishwa na gharama za upimaji na utoaji wa hati hizo kuwa juu na kufanya wananchi wengi kushindwa kumudu kukopa.

Cha kuchangaza zaidi ambacho Kamati imekiona ni kwamba Serikali imeongeza kodi ya ada katika upimaji wa viwanja. Mfano, gharama ya kulipia kiwanja cha mkaazi chenye ukubwa wa mita za mraba 2,998 imepanda kutoka Sh. 298,750/= hadi Sh. 8,320,510/>. Sasa ni mwananchi gani awezaye manage gharama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la changamoto zilizopo katika ukusanyaji wa mapato. Changamoto zilizopo katika ukusanyaji wa mapato nimezialinsha nyingi sana, lakini nisome moja tu ya makampuni ya simu za mkononi.

Mtambo wa *Telecommunication Traffic Monitoring System (TTMS)* ultarajiwani kudhibiti mawasiliano ya ndani na nje. Cha kushangaza ni kwamba mtambo huu hivi sasa unadhibiti mawasiliano ya simu ya nje pekee.

Kamati inaitaka Serikali kulieleza Bunge sababu za msingi zilizosababisha mtambo huu ushindwe kudhibiti mawasiliano ya ndani kama ilivyokusudiwa hapo awali.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba mtambo wa *Telecommunication Traffic Monitorig system (TTMS)* kwa simu za nje umeweza kuongeza mapato ya Serikali kwani kila mwezi sasa hivi tunapata shilingi billioni 1.7 kutokana na mtambo huu, mapato ambayo hayakuwepo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu imeweza kupata taarifa za kuvunjika kwa mkataba katika SHIVACOM na Vodacom Tanzania Limited (*Contract for the Production of electronic recharge vouchers*). Kamati inazo taarifa kwamba moja ya sababu ya mkataba wa SHIVACOM na Vodacom Tanzania Limited kuvunjika ni kutokana na SHIVACOM kuiibbia Vodacom Tanzania Limited na wateja wake kwa kuzalisha vocha za kielektroniki na kuzisambaza moja kwa moja kwa wateja kwa kutumia namba za siri zilizotolewa na Vodacom Tanzania Limited na baada Ye kuwasilisha vocha ile ile kwa Vodacom Tanzania Limited ambazo hazina thamani na hivyo wateja wengine kununua vocha ambazo zimekwishatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imemwagiza Waziri wa Fedha kuiagiza Mamlaka ya Mapato (TRA) na Waziri wa Mawasiriano Sayansi na Teknolojia, kuiagiza Mamlaka ya Udhhibiti Mawasiliano Tanzania (TCRA) kufanya uchunguzi dhidi ya madai hayo ili kubaini kiasi cha mapato ya Serikali yaliyopotea kutokana na mkanganyiko wa mkataba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba ya misaada na mikopo kutoka nje imekuwa ikiingiwa na Serikali bila Bunge kuelezwu vigezo na masharti ya mikopo hiyo. Kinacholetwa Bungeni kwenye hotuba ya Bajeti ni kiasi cha fedha kinachotarajiwa kukopwa pasipo Bunge kuelezwu vigezo na masharti kama riba na muda wa mkopo. Ni dhahiri kuwa usiri huu unalifanya Bunge kutotimiza wajibu wake wa kuishauri na kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukomo wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (CHC). Katika Azimio la Bunge

4 FEBRUARI, 2015

namba 5 la mwaka 2011, la kuridhia muda wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma yaani "The Consolidated Holding Corporation" Bunge liliazimia kuwa nanukuu:

"Kwa hiyo basi, kwa madhumuni haya maalum, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Mkutano wa Nne kwa mujibu wa kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Benki, linaazimia kuongeza muda wa uhai wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe 1 Julai, 2011 hadi tarehe 30 Juni, 2014 ili kutoa fursa kwa Shirika hilo Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma kukamilisha taratibu za kiutendaji na kisheria. Ndani ya muda huo Serikali itafanya tathmini ya kazi za Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (*Consolidated Holding Corporation*) ili kubaini kama lionezewa tena muda au kufanyiwa uamuzi mwingine." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeshangazwa na Wizara kushindwa kutekeleza Azimio la Bunge kwa miaka mitatu na kutangaza kumpata mzabuni mwezi wa Mei, 2014 ambapo ilikuwa ni mwezi mmoja kabla ya Shirika hili kufikia ukomo. Hata hivyo, Kamati iliiagiza Wizara kuleta taarifa ya tathmini mbele ya Kamati tarehe 2 Juni, 2014; agizo hilo halikutekelezwa na Wizara. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, amri hii ya Serikali (*Government Order*) imetolewa na Waziri wa Fedha wakati uhai Sirika hili ukiwa mikononi mwa Bunge lako Tukufu. Azimio hilo la Bunge lako Tukufu liliitaka Serikali kufanya tathmini ya kazi za Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma ili kubaini kama lionezewa tena muda au kufanyiwa uamuzi mwingine. Hivyo, si sahihi kwa Waziri wa Fedha kusitisha shughuli za Shirika bila kuwasilisha tathmini Bungeni kama Azimio (Na.5 la 2011) lilivyomtaka kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala yahusuyo Viwanda na Biashara. Kamati imebaini kuwa ufanisi wa viwanda vya ndani pamoja na mambo mengine huchangiwa kwa viwanda hivi kutosimamiwa vizuri na Wizara ya Viwanda na Biashara, ingawa Tamko la Serikali Na.494 la tarehe 17

4 FEBRUARI, 2015

Desemba 2010 linaelekeza kwamba Wizara itakuwa na majukumu ya kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera, Kanuni na taratibu za uendeshaji wa Viwanda, Biashara, Masoko, Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuandaa mfumo mzuri wa usimamizi wa viwanda nchini ambapo viwanda vyote vitakuwa chini ya Wizara moja inayosimamia sekta ya viwanda kuliko ilivyo sasa ambapo viwanda vya kilimo kama viwanda vya Sukari vinasimamiwa na Wizara ya Kilimo na Viwanda vya Samaki vinasimamiwa na Wizara ya Mifugo. Kwa hiyo, Kamati hii inaishauri Serikali kuandaa mfumo mzuri wa usimamizi wa viwanda nchini ambapo viwanda vyote vitakuwa chini ya Wizara moja ili kuhusu maendeleo ya viwanda tupate mtu wa kumhoji na kumuuliza vinaposhindwa kuwa na ufanisi kuliko vilivyon tapakaa katika kila Wizara hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda vya Nguo nchini (*Textile Industry*). Tanzania ni mionganini mwa nchi zinazozalisha pamba kwa wingi katika Bara la Afrika. Zaidi ya hekta 412,000 huzalishwa katika mikoa 13 ya Tanzania Bara. Kila mwaka Tanzania imekuwa ikizalisha wastani wa tani 300,000 za pamba. Kutokana na kiasi kikubwa cha pamba kinachozalishwa nchini, Kamati ilifanya ziara katika Kiwanda cha Nguo cha 21<sup>st</sup> Century Limited kilichopo Mkoani Morogoro kujionea fursa na changamoto zilizopo katika sekta ya nguo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara hiyo, Kamati ilibaini kuwa ni takribani asilimia 20 ya pamba inayozalishwa nchini hutumika kwa viwanda vya ndani na asilimia 80 inayobaki huuzwa nje ya nchi ikiwa ghafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Tanzania ni wazalishaji wakubwa wa pamba, Serikali imekuwa ikifanya manunuzi ya nguo zinazotengenezwa kwa pamba kutoka nje ya nchi wakati kuna viwanda vya ndani vyenye uwezo wa kutengeneza nguo za aina mbalimbali zinazofaa kwa matumizi ya maofisini na matumizi mengine.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna faida nyingi zitokanazo na kufanya manunuzi kwenye viwanda nya ndani. Faida hizo ni hizi zifuatazo:-

Kama Serikali itaweka nguvu kununua bidhaa zinazozalishwa na viwanda nya hapa ndani ni kwamba, itawezesha viwanda nya ndani kukua na kuongeza ajira kwa vijana; kuongeza thamani ya zao la pamba kutaongeza matumizi ya pamba nchini, hivyo kuwa na soko la uhakika na bei nzuri ya pamba hapa nchini badala ya kutegemea soko la dunia ambalo limekuwa halitabiriki na kuwezesha kwa kuvipa kazi viwanda nya ndani kutaongeza mitaji, uzalishaji na hivyo kuvifanya kuwekeza zaidi na mapato ya Serikali vile vile yataongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Serikali kuandaa mazingira wezeshi ambayo yatavifanya viwanda hivi kukua kuliko kuendelea kuuza nje pamba yetu ghafi. Wale watu wanunuua kwa bei ndogo, halafu sisi tunakuwa wateja tena mpaka Serikali yenyewe kununua bidhaa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro baina ya Tanga Fresh Limited na Tume ya Ushindani (FCC). Kamati yangu ilipokea malalamiko kutoka Chama cha Ushirika cha Wafugaji wa Mkoa wa Tanga (*Tanga Dairies Cooperative Union-TDCU*) kuhusu mgogoro baina ya Tume ya Ushindani (FCC) dhidi ya kampuni wanayoimiliki ya *Tanga fresh Limited*.

Mheshimiwa mwenyekiti, Kampuni ya *Tanga Fresh Limited* ni kampuni ya usindikaji wa maziwa yanayotoka kwa wafugaji wa Mkoa wa Tanga na mikoa jirani. Baada ya Kamati kuwasikiliza washirika (*TDCU*) na uongozi wa *Tanga Fresh Limited* na Tume ya Ushindani kusikiliza pande zote mbili zenyne mgogoro na kupata ukweli, Kamati ilibaini kwamba kiini cha mgogoro kilianza mnamo mwaka 2009 ambapo Kampuni ya *Tanga Fresh Limited* iliununua majengo na baadhi ya mitambo kutoka kampuni mbili tofauti ambazo ziliikuwa zimefunga biashara ya ununuzi na usindikaji wa maziwa kwa muda wa zaidi ya miaka miwili. Kampuni hizo ni *Morani Dairies*

4 FEBRUARI, 2015

*Limited na International Food Processors Limited*, zote za mkoani Tanga. Kampuni hizi zilikuwa zimekwishafunga viwanda vyao kwa zaidi ya miaka miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati haioni sababu ya Tume ya Ushindani (FCC) kuendelea na msimamo wake wa kuitoza faini kampuni ya *Tanga Fresh Limited* kiasi cha Tsh. Milioni 406.9 kwa makosa ambayo hayana madhara yoyote katika ushindani. Katika kikao hicho maridhiano yalifanyika na Kamati, Tume ya Ushindani (FCC) walikubali kuondoa faini yake lakini baada ya kikao waliendelea na msimamo wao. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaamini kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara ndiyo mtetezi namba moja wa ustawi wa viwanda nchini, lakini imekuwa kinyume chake. Kamati imeshauri mara kwa mara kufutwa kwa faini hiyo lakini ushauri wa Kamati umekuwa hauzingatiwi. Hivyo basi, Kamati inashauri kuwa Tume ya Ushindani (FCC) iondoe ankara yake ya faini ya shilingi milioni 406.9 na kwamba, Tume iwe na ushirikiano na viwanda badala ya kuvikomoa na kusababisha vishindwe kuzalisha, kuwekeza na kushindana na viwanda jirani kama vya Kenya, ambapo sasa hivi nchi yetu inakunywa maziwa mengi kutoka Kenya na sisi tuna ng'ombe wengi kuliko nchi zote za Afrika Mashariki. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Viwango Tanzania (TBS). Katika mkataba uliomalizika, kampuni ya INTERTEK imekuwa ikiripotiwa kukagua bidhaa na kuweka Certificate of Conformity (COC), lakini bidhaa zinapofika nchini zinakuwa hazikidhi viwango vya ubora, licha ya mkataba kusema wazi kuwa Wakala atakae toa cheti Certificate of Conformity (COC) kwa bidhaa hafifu atapewa adhabu kali ikiwa pamoja na kufutiwa mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilishangazwa ni kwa nini Shirika la Viwango nchini halichukui hatua yoyote kwa kampuni hiyo? Kufuatia uzembe huo Kamati inaamini

4 FEBRUARI, 2015

kwamba kuna kutowajibika ipasavyo kwa baadhi ya Watumishi wa Shirika la Viwango nchini katika kusimamia mikataba na viwango nchini. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanikiwa ku-summarize ripoti yangu na sasa niingie kwenye mapendekezo ya Kamati ya Bunge.

- (1) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala la riba kubwa katika benki na taasisi za fedha limekuwa ni la muda mrefu na linaathiri sana uchumi kwa ujumla, hivyo basi, Kamati inapendekeza kwamba, Serikali iandae na kuwasilisha Bungeni mkakati mahususi wa kupunguza na kudhibiti viwango vikubwa vyta riba vinavyotozwa na mabenki na taasisi za fedha nchini kabla ya Bunge la bajeti la mwaka 2015/2016.
- (2) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa jitihada za kuwawezesha wananchi kiuchumi ni pamoja na kuwa na uwezo wa kukopa fedha kutoka mabenki na taasisi za fedha na kwa kuwa, wananchi wengi waishio vijiji ni hutegemea mashamba yao kuweka dhamana ambayo mengi yana hati za kimila ambazo hazikubaliki katika mabenki, pia mashamba na maeneo mengi hayajapimwa hivyo kukosa sifa za kuwa dhamana na hivyo kukosa mkopo benki; hivyo basi Kamati inapendekeza kwamba Serikali ichukue hatua mahususi za kupima ardhi yote na kwamba Sheria ya Ardhi ya Vijiji (*The village Land Act, 1999*) sambamba na Sheria ya Ardhi (*The Land Act,*) zifanyiwe marekebisho mapema iwezekanavyo ili kuziwezesha Hati za Kimila zikubalike katika benki na taasisi za fedha sawa na hati za kawaida na kwamba Wizara yenye dhamana ya Ardhi ipitie upya ongezeko la ada kwa lengo la kuzipunguza ili wananchi waweze kumudu gharama za upimaji. (Makof)
- (3) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa uingizaji wa bidhaa kwa njia zisizo rasmi umeshamiri sana hapa nchini na kupelekea kukosekana ushindani wenye

4 FEBRUARI, 2015

usawa, kuingia kwa bidhaa hafifu, bandia na dawa za kulevyia na kulipelekea Taifa kukosa mapato, viwanda vya ndani kushindwa kushindana na tishio la uhai wa viwanda vyetu hapa nchini na kwa kuwa katika Ukanda wa Bahari ya Hindi wenye takribani kilomita 1,424 kuna bandari bubu zaidi ya 26 ambazo hutumika kuingiza bidhaa kiholela. Hivyo basi, Kamati inapendekeza kwamba Bunge lako Tukufu liazimie kwamba vyombo vya udhibiti TBS, FCC na TFDA vipewe nguvu zaidi ya kupambana ikiwa ni pamoja na kushirikisha Jeshi la Wananchi (JWTZ) katika mapambano na kudhibiti ukanda huu ambaa unaliingizia Taifa hasara kubwa.

- (4) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Viwanda vya Nguo hapa nchini vimekuwa havinufaiki na manunuzi ya nguo yanayofanywa na Serikali, badala yake Serikali imekuwa ikinunua nguo za majeshi na shuka za mahospitali toka nje ya nchi huku viwanda vya ndani vikiathirika kwa kukosa soko na kwa kuwa bei ya pamba ghafi imekuwa ya kusuasua katika soko la dunia, uongezaji thamani pamba hapa nchini utasababisha kupatikana kwa soko la uhakika na bei nzuri ya pamba, mitaji na uwekezaji kuongezeka na hivyo kusababisha ajira kwa vijana na mapato ya Serikali kuongezeka, hivyo basi, Kamati inapendekeza Bunge lako Tukufu liazimie kwamba, Serikali na taasisi zake zishindanishe zabuni za manunuzi ya sare za majeshi, shule na mashuka ya hospitali pamoja na nguo zingine zinazotumia pamba kwa viwanda vya nguo vya hapa nchini. (*Makofii*)
- (5) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa misaada na mikopo imekuwa ikiingiwa na Serikali bila Bunge kuelezwu vigezo na masharti ya mikopo hiyo na kwa kuwa Bunge limekuwa halishirikishwi ipasavyo katika masuala yanayohusu misaada na mikopo na hivyo kushindwa kutimiza wajibu wake wa kuisimamia na kuishauri Serikalini katika eneo hili, hivyo basi, Kamati inapendekeza kwamba katika kila Mwaka wa Fedha,

4 FEBRUARI, 2015

Serikali iwasirishe mchanganuo wa kina wa misaada na mikopo ambayo Serikali inatarajia kukopa. Taarifa hiyo iainishe wahisani, kiasi cha mkopo na vigezo na masharti kama riba, muda na masharti mengineyo. (Makofij)

- (6) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, kitendo cha Waziri kutoa amri ya kusitisha kazi za CHC huku akijua kuna Azimio la Bunge ni kuingilia Uhuru na mamlaka ya Bunge lako Tukufu na kwa kuwa, Serikali ilitoa notisi kuhamisha mali zote na mashauri yote ya CHC zihamishiwe kwa Msajili wa Hazina, hivyo basi, Serikali itekeleze tamko lake kuhakikisha kwamba Watumishi wote waliokuwa CHC wahamishiwe kwa Msajili wa Hazina kama Tamko hilo lilivyozungumza, badala ya kuwafukuza kinyemela.
- (7) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa uendelezaji wa viwanda nchini unategemea mfumo mzuri wa usimamizi wa viwanda na kwa kuwa kuna baadhi ya viwanda hapa nchini vinasimamiwa na wizara mbalimbali kama Kilimo na Chakula, Mifugo na Uvuvi, Maliasili na Utalii, Nishati na Madini na Viwanda na Biashara, kitendo kinachopelekea kukosekana kwa ufanisi na ni kinyume cha sheria, sera na kanuni za viwanda, hivyo basi, Kamati inapendekeza kuwa Bunge lako Tukufu liazimie kwamba, viwanda vyote nchini viwe chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. (Makofij)
- (8) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Kamati imekuwa haipewi majibu ya kutosha kwa nyakati tofauti ilipoomba maelezo ya matumizi ya dola milioni 27 zilizokopwa toka Serikali ya China kwa ajili ya uendelezaji wa kiwanda cha Urafiki na kwa kuwa, muda wote Kamati imekuwa hairidhiki na majibu yanayotolewa kwamba dola za kimarekani milioni 12 zilibaki China kwa ajili ya kununua bidhaa kwa ajili ya kiwanda bila kuainisha bidhaa zilizonunuliwa na kuletwta nchini, matumizi ya dola 15 milioni zilizobaki

4 FEBRUARI, 2015

zilitumika kukarabati mitambo ya kiwanda bila kuainisha mitambo iliyokarabatiwa; hivyo basi, Kamati inapendekeza kwamba Bunge lako Tukufu liridhie kuundwa kwa Tume huru ya Bunge kuchunguza suala hili kwa undani ili kuhakiki uhalali wa matumizi ya takribani shilingi bilioni 48 na hatima ya kiwanda hiki cha Urafiki.

- (9) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, uteketezaji wa bidhaa bandia una gharama kubwa, kuharibu mitaji na uwekezaji na uchumi kwa ujumla, hivyo basi, Kamati inashauri kwamba *TBS* na *FCC* wafanye kazi pamoja hasa katika utaratibu wa *PVoC* ili kuwezesha ukaguzi wa ubora na bidhaa bandia kufanyika kwa pamoja huko huko nje ya nchi kabla bidhaa hazijaingizwa nchini na kwamba Sheria ya *TBS*, *WMA* na *FCC* zifanyiwe marekebisho ili kukidhi changamoto zilizopo sasa.
- (10) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, maelezo ya kupungua kwa eneo la *TIRDO* kutoka hekta 40 mwaka 1979 na kufikia hekta 21.3 mwaka 2013 yamekuwa si ya kuridhisha licha ya Kamati kufuatilia mara kwa mara; hivyo basi, Kamati inapendekeza kwamba Bunge lilidhie kuundwa kwa Kamati Ndogo kufuatilia uhalali wa eneo la Shirika hili.
- (11) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, madeni ya Wazabuni, Wakandarasi, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Wakulima wa mahindi yamekuwa yakilipwa kwa kusua sua na Serikali na kupelekea kufilisika na Mifuko kushindwa kujientesha na kulipa mafao kwa wanachama wao; hivyo basi, Serikali ianze kulipa madeni haya haraka yaliyofikia shilingi trilioni 3.6 na kuleta mpango mkakati utakaonesha jinsi madeni hayo yatakavyolipwa kabla ya Bunge la Bajeti la Mwaka wa Fedha 2015/2016.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Spika, okay, unaweza kuwa Spika siku zijazo. Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kuwashukuru Mawaziri wangu wote ambao ni Waziri wa Fedha na Uchumi, Waziri wa Viwanda na Biashara, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwezeshaji na Uwekezaji), Mama Nagu umehama, Kamati inaku-miss sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwashukuru sana naomba kuwashukuru Ofisi ya Katibu wa Bunge, Makatibu wangu wa Kamati Ndugu Angela Shekifu, Rachel Nyega pamoja na msaidizi wao Paulina Mavunde kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati, hadi taarifa hii imekamilika, lakini pia niwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Kisesa wanavyoendelea kunipa ushirikiano na mimi naendelea kufanya kazi njie ya Bunge na kuahidi kwamba niko imara kabisa na mapambanao yanaendelea. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Toa hoja.

**MHE. LUHAGA J. MPINA- MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja sasa kwamba Bunge lako lipokee, lijadili na likubali mapendekezo ya Kamati kama ambavyo tumeyaleta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MHE. AMINA A. MWIDAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Luhaga Mpina Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara.

4 FEBRUARI, 2015  
**TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU  
YA BUNGE YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA KWA  
KIPINDI CHA KUANZIA MACHI, 2014 - JANUARI, 2015  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la April 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara kwa kipindi cha kuanzia Machi 2014 hadi Februari 2015.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Kamati ninayoiwasilisha imegawanyika katika sehemu kuu tano ambazo ni:-

- Utangulizi;
- Mambo yahusuyo fedha na uchumi;
- Uwekezaji, Viwanda na Biashara;
- Mapendekezo ya Kamati na
- Shukrani na hitimisho.

**1.1 MAJUKUMU YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge Nyongeza ya Nane, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara ni Kamati ya kisekta yenye jukumu la kusimamia :-

- Wizara ya Fedha;
- Wizara ya Viwanda na Biashara; na
- Ofisi ya Waziri Mkuu Uwezeshaji na Uwekezaji.

**1.2 KAZI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati katika utekelezaji wa majukumu yake, imefanya kazi mbalimbali zifuatavyo:-

4 FEBRUARI, 2015

- Kuchambua Bajeti ya Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Biashara na Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji na Uwezeshaji).
- Kujadili miswaada na Maazimio ya Serikali.
- Kukagua utekelezaji wa miradi ya Serikali
- Kushiriki Semina mbalimbali.
- Ziara ya mafunzo nje ya nchi.
- Kufanya ukaguzi kwenye viwanda mbalimbali pamoja na kupokea taarifa za utendaji kazi wa viwanda hivyo.
- Kutembelea Taasisi mbalimbali zinazosimamiwa na Kamati.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 MAMBO YAHUSUYO FEDHA NA UCHUMI

#### 2.1 Mwenendo wa Uchumi nchini

**Mheshimiwa Spika**, taarifa za Benki ya Dunia zinaonyesha kuwa uchumi wa nchi umeendelea kuimarika huku ukuaji halisi wa Pato la Taifa ukiongezeka kwa kasi ya 7.1% katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2014.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kiasi kikubwa ukuaji wa Pato la Taifa umechangiwa na shughuli mbalimbali, shughuli hizo ni pamoja na mawasiliano na uchukuzi (23.3%), kilimo (11.5%) pamoja na uzalishaji viwandani (10%).

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na taarifa hizi za kuimarika kwa uchumi, ni ukweli usiopingika kwamba ukuaji huu wa uchumi hauna uhusiano wa moja kwa moja na maendeleo ya wananchi. Takwimu zinaonyesha uchumi unakua, ingawa kiasi cha wananchi wanaoishi chini ya mstari wa kipimo cha umaskini wa chakula bado ni kikubwa.

4 FEBRUARI, 2015

**Mheshimiwa Spika**, uhusiano hafifu uliopo kati ya mafanikio katika ukuaji wa uchumi na punguzo la umaskini kunasababisha ongezeko la kukosekana kwa usawa katika jamii.

**Mheshimiwa Spika**, hali hii inasababishwa na Usimamizi mbaya wa Uchumi (*Poor Economic Management*) Kamati imeona kuwa kuna usimamizi dhaifu sana wa uchumi hapa nchini, baadhi ya viashiria vya uchumi havileti matumaini ya kujenga uchumi wenyewe manufaa kwa wananchi wote.

#### 2.2.1      **Mfumuko wa bei**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na takwimu kuonyesha kuwa mfumuko wa bei ulishuka kutoka 6.4% mwezi Juni 2014 hadi 4.8% mwezi Desemba 2014, Kamati inapongeza jitihada hizo, hata hivyo kushuka kwa mfumuko wa bei hakujasaidia kushuka kwa bei ya bidhaa za sokoni na viwandani.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini kwamba mfumuko wa bei hapa nchini uko zaidi kwenye tarakimu badala ya kwenye maisha halisi ya wananchi. Mfano, Serikali imekuwa ikijivunia kuwepo kwa bei ndogo kwenye baadhi ya vyakula huku wakulima wazalishaji mazao yao yamekuwa yakioza kwa kukosa soko na mengine kununuliwa kwa bei ndogo.

#### 2.2.2      **Riba katika Benki na Taasisi za Fedha (Interest Rates)**

**Mheshimiwa Spika**, kiwango cha riba katika benki na taasisi za fedha nchini kiko juu sana hivi sasa kwani ni kati ya 15%-21% kwa wakopaji (*lending rates*) kwa upande mwingine riba ndogo kwa mwenye kuweka akiba (*commercial deposit rates*) ni kati ya 2% hadi 5% tu wakati mfumuko wa bei ni zaidi ya 5%.

4 FEBRUARI, 2015

**Mheshimiwa Spika**, tatizo la riba za benki kuwa juu inalalamikiwa na wananchi wengi na hakuna hatua za makusudi zinazochukuliwa na Serikali kuhakikisha kuwa riba hizi zinapungua. Kamati inaona kwamba Serikali kuendelea kuridhia wananchi kutozwa riba hizi ni kuongeza ugumu wa maisha kwani mikopo hiyo husababisha kafilisiwa mali zao pale wanaposhindwa kurejesha.

**Mheshimiwa Spika**, tatizo la riba kuwa kubwa linachangiwa na mambo yafuatayo:-

- Serikali kuendelea kukopa kutoka katika masoko ya ndani ya Benki za Biashara na Mifuko ya Hifadhi za Jamii *Commercial Banks* na *Pension Funds* na kusababisha wakopaji kutopata mikopo kwa wakati na kwa riba kubwa.
- Serikali kuendelea kutoa riba za juu kwa dhamana za Serikali (*Treasury Bills*), ambapo hivi sasa zimefikia wastani wa 13.8% hadi 14.8%. Kama Serikali inatoa riba ya takribani 15% hakuna Benki ya Biashara itakayoweza kukopesha wateja wa kawaida chini ya asilimia hiyo.
- Serikali kutolipa kwa wakati madeni ya wazabuni na wakandarasi na hivyo kusababisha mikopo chechefu (*Non Performing Loans*) kuongezeka ambapo hivi sasa imefikia 8.5%.
- Kiwango cha asilimia 10% na 40% kwa amana za Serikali (*Government deposits*). Kiwango hiki ni kikubwa na cha lazima kwa amana (*Statutory minimum reserve-SMR*) kwenye sekta binafsi (*private sector deposits*). Ukubwa wa viwango hivi unaathiri uwezo wa utoaji mikopo kwa sekta binafsi.

**Mheshimiwa Spika**, takwimu zinaonyesha kuwa kumekuwepo na ongezeko la mabenki kutoka benki 5 mwaka 1992 mpaka 57 Novemba 2014 pamoja na

4 FEBRUARI, 2015

ongezeko hili ni takribani aslimia 14 (14%) tu ya Watanzania ndio wanapata huduma za kibenki. Kamati imebaini kuwa hali hii husababishwa na gharama kubwa za huduma za kibenki pamoja na riba kubwa zinazotozwa na benki hizo.

**Mheshimiwa Spika**, ili kujenga uchumi imara ni vyema Serikali ikaanda mkakati kwa lengo la kushusha viwango vya riba hatua ambayo itawawezesha wananchi wengi kupata mikopo kwa gharama nafuu na kushiriki kwenye shughuli mbalimbali za uchumi.

### 2.2.3 Ubudilishaji Fedha za Kigeni (*Exchange Rates*)

**Mheshimiwa Spika**, hivi sasa shilingi ya Tanzania inaendelea kuporomoka dhidi ya dola ya kimarekani ambapo kwa sasa dola 1 ni sawa na shilingi 1773.

**Mheshimiwa Spika**, kuendelea kushuka kwa shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya kimarekani kunasababishwa na sababu mbalimbali zikiwemo shilingi ya Tanzania kutumika sambamba na dola ya kimarekani (*unofficial dollarization*) na wananchi na kampuni za ndani kupendelea kunukuu bei na kudai malipo kwa fedha za kigeni (*Transaction dollarization*).

**Mheshimiwa Spika**, hivi sasa shilingi ya Tanzania inaenelea kuporomoka dhidi ya dola ya kimarekani ambapo imefikia shilingi 1773 kwa dolla 1. Kamati hairidhishwi na usimamizi wa matumizi ya fedha za kigeni nchini (*Dollarization*) ambapo katika siku za karibuni Tanzania shilingi imekuwa ikitumika sambamba na dola ya kimarekani (*unofficial dollarization*) pia wananchi na makampuni ya ndani kupendelea kunukuu bei na kudai malipo kwa fedha za kigeni (*Transaction dollarization*).

**Mheshimiwa Spika**, Benki Kuu inaweza je kudhibiti kuporomoka kwa shilingi wakati wahitaji wakubwa wa fedha za kigeni hapa nchini kama **MSD, TANROAD**,

4 FEBRUARI, 2015

**TANESCO**, Waagizaji wa Mafuta ambao mapato yao yapo kwenye Shilingi ya Kitanzania, hivyo hulazimika kununua fedha za kigeni toka kwenye benki za biashara kwa rate ya juu ili kulipia ankara zao, Huku mabenki hayo yakinunua dola kutoka Benki Kuu kwa rate za chini? Kwanini hao waagizaji yasinunue dola moja kwa moja kutoka Benki Kuu ili kuongeza udhibiti?

**Mheshimiwa Spika**, Benki Kuu inawezaje kudhibiti ramli (*speculation*) katika soko la fedha za kigeni wakati miamala mingi ya fedha za kigeni inafanywa kiholela na kupelekea shinikizo la kuporomoka kwa shilingi ya Tanzania?

**Mheshimiwa Spika**, Tunawezaje kuongeza mauzo nje wakati mazao ya chakula na biashara hayana soko na yanauzwa bila kuongeza thamani, Serikali kukopa wakulima, wakandarasi na wazabuni? Kushuka kwa bei za mafuta na kupungua kwa mfumuko wa bei zimeshindwa kuiokoa shilingi ya Tanzania kuporomoka.

### 2.3 Madeni ya Serikali kwa Taasisi za Umma

#### 2.3.1 Deni la Mifuko ya Hifadhi za Jamii

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Septemba 2014 madeni yaliyoiva yamefikia **shilingi trilioni 1.875** ambayo Serikali inadaiwa na Mifuko ya Hifadhi za Jamii. Pamoja na nia njema ya Serikali kukopa kwa lengo la kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo, Serikali imekuwa hailipi madeni hayo kwa wakati na kupelekea mifuko hii kushindwa kujidesha na kulipa mafao ya wastaifu.

#### 2.3.2 Madeni ya Wakandarasi, Wazabuni, na Watumishi wa Serikali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa za kuishia mwezi Juni, 2014 deni la Wakandarasi, Wazabuni

4 FEBRUARI, 2015

na Watumishi wa Serikali lilifika shilingi trillioni 1.3 na hadi kufikia Septemba, 2014 madeni yaliyokuwa yamelipwa yalikuwa ni shilingi **bilioni 259.2** tu kwa mchanganuo ufuatao: walimu wa shule za msingi na sekondari shilingi bilioni 5.4, wakaguzi wa elimu, wakufunzi na wahadhiri shilingi **bilioni 9.2**, Parastatal Service Pension Fund(**PSPF**) shilingi **bilioni 50.0**, mahakama shilingi **bilioni 64.2** na wakandarasi na wazabuni shilingi **bilioni 130.4**.

### 2.3.3 Madeni ya Wakulima wa Mahindi na Mpunga

**Mheshimiwa Spika**, deni la Serikali kwa wakulima wa mahindi na mpunga limekuwa na kufikia shilingi **bilioni 89** ambapo hadi sasa kiasi kilichopo zilizolipwa ni shilingi **bilioni 15** tu.

**Mheshimiwa Spika**, deni la Mifuko ya Hifadhi za Jamii, Madeni ya Wakandarasi, Wazabuni, na Watumishi Wa Serikali na madeni ya Wakulima wa Mahindi na Mpunga ni baadhi tu ya madeni ambayo Serikali inadaiwa na madeni haya hayajajumuishwa kwenvye Deni la Taifa na yana jumla ya shilingi **trillioni 3.6**.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali yenye lengo la kuleta mapinduzi ya kiuchumi kwa wananchi wake haiwezi kukopa fedha za umma na kushindwa kurejesha kwa wakati. Kitendo cha Serikali kushindwa kurejesha mikopo hii kwa wakati kunapelekea wananchi kushindwa kugharamia mahitaji muhimu k a m a kilimo, elimu, afya. Aidha, kwa upande wa wakandarasi na wazabuni wamekua wakifirisika, kuondoka katika uzalishaji na wengine wamediriki hata kukatisha maisha yao na kujiuu.

**Mheshimiwa Spika**, hali hii imapelekea kupungua kwa uzalishaji, uwekezaji na biashara kufungwa na hivyo kusababisha athari za kiuchumi ikiwa ni pamoja na kupungua kwa ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

4 FEBRUARI, 2015

## 2.4 Upatikanaji Wa Mikopo (**Access of Finance**)

**Mheshimiwa Spika**, licha ya benki kuongezeka kufikia 57 mwaka 2014 kutoka benki 5 mwaka 1992 lakini bado Watanzania wanaonufaika na mikopo kutoka katika benki hizo ni takribani 14% tu. Aidha katika benki hizo ni benki 10 kati ya 57 ndiyo zinamiliiki nguvu ya kifedha na soko (Banking Market Share) kwa 80%. Hata hivyo, ongezeko hili la utitiri wa      b    e    n    k    i    haujaweza kuwasaidia wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, mionganoni mwa changamoto za upatikanaji wa mikopo ni pamoja na :-

- Umbali wa benki zilipo ambapo mabenki mengi yako mijini;
- Vigezo na masharti ya benki wakati wa ukopaji; mfano dhamana za hati miliki (*Title Deeds*) ambapo ardhi ya Tanzania iliyopimwa ni chini ya 10% ya ardhi yote na
- Riba itokanayo na mikopo ni ya kiwango cha juu ambapo riba inayotozwa iko kati ya asilimia      15 – 20 (15%-21%).

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa zaidi ya 65% watanzania wanajishughulisha na kilimo, Kamati inashauri ni vyema mikopo ya kilimo ikapunguzwa riba kutoka riba ya sasa ambayo ni chini ya 10% ya mikopo yote inayotolewa na mabenki. Hatua hii itasaidia wananchi wengi kushiriki kwenye shughuli za kilimo na kuchangia pato la Taifa.

### 2.4.1      **Micro Finance Act**

**Mheshimiwa Spika**, uchumi wa nchi yetu kwa kiasi kikubwa unategemea shughuli zinazofanywa kupitia sekta isiyo rasmi. Licha ya ukweli huu, Tanzania haina mfumo rasmi wa      usimamizi wa sekta ndogo za fedha (*Microfinance Regulatory Regime*) kama

4 FEBRUARI, 2015

**SACCOS** na **VICOBA**. Hali hii imepelekea shughuli zinazotekelawa na **VICOBA** na **SACCOS** kufanya kazi kwa ufanisi mdogo kutokana na kukosekana kwa sheria mahsusimamia sekta hii.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua hilo, Serikali iliahidi kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya Micro Finance wa mwaka 2012/2013. Hadi ninapowasilisha taarifa hii hakuna taarifa yoyote iliyotolewa na Serikali kuhusu kuwasilishwa kwa Muswada huo au hatua iliyofikiwa. Kutokana na kusua sua huko kwa Serikali pamoja na changamoto zitokanazo na kukosekana kwa Sheria ya Micro Finance Kamati imekamilisha kuandaa Muswada binafsi wa Sheria (*Micro Finance Bill*, 2015) na inategemea kuwasilishwa Muswada huo wakati wowote itakapopangiwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kutungwa na kuanza kutumika kwa sheria hii kutawezesha kuwafikia wananchi wengi ambao hawapati mikopo kwa sasa (*Financial exclusion*), wananchi hawa wengi wapo kwenye sekta zisizo rasmi na wengi wao wako vijijini. Hatua hii pia itaongeza ushindani wa mabenki na kusaidia kupunguza urasimu uliopo (*monopoly*).

#### 2.4.2      **Hati za kimila**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Ardhi ya Vijiji (*The village Land Act*), ilianza kutumika mwaka 1999 sambamba na Sheria ya Ardhi, *The Land Act*. Sheria ya vijiji inagusa maeneo mengi kama vile umiliki na uendelezaji wake. Hata hivyo mashamba au ardhi ya vijijini huwa yanamiliwi kwa njia ya kimila au kupewa na Kamati ya kijiji husika. Aidha, uuzwaji wa ardhi hizi unaweza kufanyika kwa idhini

4 FEBRUARI, 2015

ya Kamati hizo. Wanakijji huweza pia kumiliki hizi ardhi kwa kurithishwa, kupewa kama zawadi, pamoja na kukodishwa kwa muda.

**Mheshimiwa Spika**, asilimia 78 ya ardhi ya Tanzania ni ya vijiji na kati ya hizo ni chini ya 1% ya ardhi ndiyo imepimwa na kutolewa hati za kimila. Pamoja na ukweli huo, hati za kimila hazikubaliki katika mabenki na taasisi za fedha zilizo nyingi kutumika kama dhamana katika mikopo.

**Mheshimiwa Spika**, ni jambo la kushangaza kuwa hata benki za Serikali haziitambui hati hizi, mfano Benki ya Uwekezaji Tanzania (*Tanzania Investment Bank*) haikubali hati za kimila kutumika kama dhamana ya kupatia mikopopamoja na kwamba benki hii ndiyo yenye dirisha la kilimo.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeanzisha dirisha la kilimo na benki ya kilimo wakati hakuna utaratibu uliofanywa wa kutambua hati za kimila, dhamana k u b w a ya wananchi ni ardhi yao ambayo ipo vijijini na ina sifa ya kupata hati za kimila. Kamati inaamini kuwa kama hakutafanyika mabadiliko ya kisera yatakayowezesha hati za kimila kutumika kama dhamana ya kupatia mikopo katika mabenki na taasisi za fedha, uanzishaji wa benki hizo za kilimo hautakuwa na manufaa kwa wananchi maskini ambaeo ndio walengwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua umuhimu wa hati za kimila kutumika kama dhamana katika benki na kuwawezesha wananchi kupata mikopo, Kamati ilifanya kikao cha pamoja na Benki Kuu (**BOT**), Wizara

4 FEBRUARI, 2015

ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na baadhi ya wawakilishi kutoka benki za **TIB, TPB, NBC** na **NMB** na kupendekeza yafutayo:-

- i. Kuhamasisha na kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi (*Land use*) ili kuwa na matumizi bora ya ardhi za vijiji.
- ii. Kuhamasisha na kuwezesha upimaji wa uwekaji wa mipaka ya ardhi za vijiji (*land survey and demarcation*). Na kwa urahisi wa utambuzi wa umiliki, hati za ardhi za vijiji (*certificates*) zuhuishwe ili ziwe hati za kimila zakumiliki ardhi (*Customary Rights Occupancy*);
- iii. Miundo mbinu ya kuzifika hizi ardhi iendelezwe.
- iv. Serikali iharakishe kutengeneza mfumo wa kisheria wa kuweza kushughulikia hati za kimila na matatizo yaliyoorodheshwa hapo juu ikiwepo kuanzisha Masjala Kuu itakayo kuwa inashughulikia uandikishaji wa hati za kimila na pia kuandikisha/kusajili dhamana zitokanazo na hati za kimila (*Central Registry*) kama ilivyo katika hati za kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mapendekezo hayo, Kamati inaitaka serikali kukamilisha upesi iwezekanavyo na kuwasirisha Bungeni Sheria ya Stakabadhi Ghalani (*Warehouse Receipt Act*) na Sheria ya Soko la kubadilidha bidhaa (*Commodity Exchange Act*) ambazo zitasaidia kuwezesha wananchi kupata mikopo.

#### 2.4.3 Hati ya kawaida

**Mheshimiwa Spika**, ardhi ya Tanzania iliyosajiriwa na kupewa hati miliki za kawaida ni chini ya 10% ya ardhi yote, huchache huu husababishwa na gherama za

4 FEBRUARI, 2015  
 upimaji na utoaji wa hati hizo kuwa juu na kufanya  
 wananchi wengi kushindwa kumudu gharama hizo.

**Mheshimiwa Spika**, cha kushangaza zaidi Serikali  
 imeongeza kodi na ada katika upimaji wa viwanja,  
 mfano gharama za kulipia kiwanja cha makaazi  
 chenye ukubwa wa mita za mraba 2998 imepanda  
 toka shilingi **298,750/=** hadi **8,320,510/=** kama  
 zilivyoainishwa katika kanuni na miongozo ya ardhi  
 (Rules and Regulations for Land Amendments 2012).

#### **Angalia jedwali namba 6.**

Jedwali na 6. Ongezeko la ushuru katika upimaji viwanja

	Shughuli	Gharama za zamani	Gharama za sasa	Tofauti
1	Uandaaji hati	1000	160,000	159,000`
2	Ada ya usajili	22,490	67,000	44,510
3	Ada ya upimaji	104,930	7,195,200	7,090,270
4	Ushuru wa stempu	2,440	6,940	4500
5	Deed plan	6,000	6,000	0
6	Kodi ya Ardhi July-June	41,970	134,910	92,940
7	Premium	116,920	750,000	633,080
	<b>Jumla</b>	<b>298,750</b>	<b>8,320,510</b>	<b>8,021,760</b>

**Mheshimiwa Spika**, ongezeko hili kubwa litawafanya  
 wananchi washindwe kupima viwanja vyao na hivyo  
 kukosa haki yao ya kumiliki ardhi, dhamana katika  
 mabenki na serikali kukosa mapato. Kamati inashauri  
 kwamba wizara yenye dhamana ya Ardhi ipitie upya  
 ongezeko la viwango hivi vyaa ada na kuvipunguza ili  
 wananchi waweze kumudu gharama za upimaji.

4 FEBRUARI, 2015

## 2.5 Changamoto ya Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali

### 2.5.1 Sekta ndogo ya Madini

**Mheshimiwa Spika**, taarifa za Walaka wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (**TMAA**) na Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative (**TEITI**) zimekuwa zikiripoti upotevu mkubwa wa mapato katika biashara ya madini. Makampuni makubwa ya madini (*Mult-National Companies*) yamekuwa yakikwepa kodi kwa kuongeza na kupunguza gharama za bidhaa na huduma. Kwa upande mwingine madini mengi yamekuwa yakitoroshwa kuitia njia rasmi na zisizo rasmi.

**Mheshimiwa Spika**, tathmini ya uzalishaji iliyofanywa na Walaka wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (**TMAA**) kwenye maeneo mbalimbali ya uchimbaji dhahabu nchini imeonesha kuwa wachimbaji wadogo wanazalisha wastani wa tani 20 za dhahabu kwa mwaka. Hata hivyo, dhahabu inayopitia kwenye mkondo halali kwa mwaka ni wastani wa tani 2 tu. Hii ina maana kwamba 90% ya dhahabu iliyozalishwa katika kipindi hicho ilitoroshwa kwenda nje ya nchi bila kulipa mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa madini ya Tanzanite, Tanzania iliua Tanzanite yenye thamani ya dola za Marekani **milioni 37** mwaka 2013. Katika kipindi hicho, nchi ya India iliingiza Tanzanite yenye thamani ya takribani dola za Marekani **milioni 300**, huku nchi jirani ya Kenya ikikadirwa kusafirisha nje madini ya Tanzanite kwa jina la zoisite yenye thamani ya dola za Marekani **milioni 100**.

**Mheshimiwa Spika**, madawati ya Ukaguzi wa Madini kwenye viwanja vya ndege vya kimataifa hapa nchini yamewezesha kukamata watu 32 waliokuwa wanatorosha madini kwenda nje ya nchi yenye thamani ya takriban Shilingi **bilioni 15**.

4 FEBRUARI, 2015

**Mheshimiwa Spika**, takwimu hizo zinaonesha wazi kuwa kiwango cha utoroshaji wa madini ya dhahabu na Tanzanite yanayozalishwa na wachimbaji wadogo nchini ni cha kiwango cha juu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashangazwa kuona kwamba, nchi yenye vyombo vyaa usalama viliwyotapakaa kila mahala inakuwaje rasilimali zitoroshwe kwa kiwango hicho?

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba Serikali haina mfumo mdhubuti wa kudhibiti utoroshwaji wa madini na pia hakuna mfumo wa kiintelijensia wa kuwezesha upatikanaji wa taarifa za uchimbaji na uzalishaji wa madini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia inapendekeza Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 ifanyiwe marekebisho ili kumuwezesha Kamishna wa Madini kutaifisha madini yanayopatikana kinyume cha Sheria na kukusanya mapato yatokanayo na utaifishaji wa madini hayo kama ilivyo kwa Wizara ya Maliasili kwa mazao ya misitu kama magogo na mkaa na pia Mamlaka ya Mapato Tanzania (**TRA**) kwa bidhaa zinazoingizwa nchini bila kulipiwa ushuru wa forodha.

#### 2.5.2        **Ukwepaji wa Kodi katika Bandari**

**Mheshimiwa Spika**, baadhi ya wafanya biashara wanaotumia bandari ya nchini aidha kwa makusudi au kwa kushirikiana na Watumishi wa Serikali hufanya udanganyifu kwa kutokuonyesha thamani halisi ya bidhaa (*Under Invoice*), kuonyesha idadi ndogo ya bidhaa wanazoingiza nchini (*Under Declaration*), na mara nyingine kutosema ukweli kuhusu bidhaa zilizomo katika makontena kuwa ni zile zenye misamaha ya kodi kama vyandarua wakati bidhaa hizo zinaweza kuwa vitenge, nguo, khanga

4 FEBRUARI, 2015

na bidhaa za elektroniki n.k na hivyo kukwepa kulipa kodi, hali ambayo imesababisha Serikali kupoteza kiasi kikubwa cha mapato.

#### **2.5.3      Uingizaji wa Bidhaa Kupitia Njia Zisizo Rasm**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na kuwa na ukanda mpana katika bahari ya hindi suala la bandari buba limekuwa likijitokeza mara kwa mara. Katika ukanda wote wa pwani zipo bandari buba takribani 26, mwambao wa bahari ya Hindi unaokaribia Km 1424 na maziwa makuu ambayo ni Victoria na Tanganyika.

**Mheshimiwa Spika**, ni vyema ikumbukwe kwamba licha ya kupoteza mapato mengi kutokana na bidhaa nyingi kupita njia zisizo rasmi, vilevile njia hizi zimekuwa zikiingiza nchini bidhaa zilizo chini ya viwango na ambazo havina ubora, bidhaa bandia, madawa ya kulevyta na n.k.

#### **2.5.4      Mfumo wa Kodi kwa Bidhaa Katika Viwanda vya Ndani**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kutekeleza majukumu yake, Kamati ilikutana na Shirikisho la Wenye Viwanda Nchini (**CTI**). Katika kikao hicho, Kamati ilielezwa kuwa changamoto kubwa kwa wenye viwanda ni pamoja na ongezeko la ushuru wa bidhaa kila mwaka katika bidhaa za sigara, bia, mvinyo, vinywaji vikali na vinywaji baridi.

**Mheshimiwa Spika**, ongezeko hili la ushuru usiozingatia uwezo wa wananchi na ukuaji wa viwanda unasababisha kushuka kwa uzalishaji, viwanda vya ndani kushindwa kushindana na viwanda vya nje na kupungua kwa mapato ya Serikali yanayotokana na bidhaa hizo.

**Mheshimiwa Spika**, katika kila Mwaka wa Fedha ushuru wa bidhaa hizi umekuwa ukiongezeka kwa zaidi ya asilimia 10(10%) na kwamba bidhaa hizi kwa

4 FEBRUARI, 2015  
sasa uzalishaji wa viwanda hivyo umepungua  
kutokana na kodi kubwa zinazotozwa na hivyo  
kuikoseshaa serikali mapato.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 hali ya wenye Viwanda nchini ilikuwa ngumu zaidi kufuatia tamko la Waziri wa Fedha Bungeni kuhusu ongezeko la kodi kwa asilimia 10% (*Budget Speech*) wakati Muswada wa Sheria ya Fedha (*Finance Bill*) ilitaka ongezeko la kodi kuwa asilimia 20%.

**Mheshimiwa Spika**, ongezeko hili halikwenda sambamba na mfumko wa bei ambao ulikuwa 6.5% tu. Aidha, mabadiliko haya hayakuweleweka vizuri kwa wenye viwanda na hayakuwemo kwenye makisio ya bei na hivyo kusababisha usumbufo mkubwa katika ulipaji wa kodi halali kwa mujibu wa Sheria ya Fedha.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine mzigo wa ushuru na ada zinazotozwa na Mamlaka za Udhhibitii (*Regulatory Bodies*) ni mkubwa mmo na unaosababisha kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na kufanya viwanda vya ndani kushindwa kushindana kimataifa. Mfano, ada na ushuru zinazotozwa na **SUMATRA, EWURA, WMA, REA, TBS, Fire and Rescue, TFDA, Water Basins**, na FCC.

**Mheshimiwa Spika**, ili kusaidia viwanda vya ndani kukua na kuongeza ajira kwa vijana, Kamati inashauri kwamba katika Mwaka ujao wa Fedha (2015/2016) Serikali ipitie upya viwango vya kodi zinavyotozwa na kupunguza kodi hizo kwa manufaa ya viwanda vya hivi.

## 2.6 Makampuni ya Simu za Mkononi

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na watumiaji wa simu za mkononi kuongezeka bado sekta ya mawasiliano

4 FEBRUARI, 2015

haijachangia kikamilifu katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Mfano, mwaka wa fedha 2013/2014 mapato ya kodi yatokanayo na mawasiliano yalikuwa shilingi bilioni 576.46 tu.

**Mheshimiwa Spika**, mtambo wa Telecommunication Traffic Monitorig system (**TTMS**) ulitarajiwa kudhibiti mawasiliano ya ndani na nje, cha kushangaza mtambo huo hivi sasa una dhibiti mawasiliano ya simu za nje pekee. Kamati inaitaka Serikali kulieleza Bunge sababu za msingi zinazosababisha mtambo huu usidhibiti mawasiliano ya ndani kama ilivyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Mapato Tanzania (**TRA**) haijawa na uwezo wa kujua na kudhibiti mawasiliano ya simu (*airtime traffic*) yanayofanywa ndani ya nchi na hivyo ukokotoaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (**VAT**) na ushuru wa bidhaa (*Excise duty*) hutegemea takwimu na hesabu zinazotolewa na kampuni za simu husika. Mtambo wa **TTMS** (Telecommunication Traffic Monitorig system) ulitarajiwa kudhibiti mawasiliano ya ndani na nje lakini chakushangaza mtambo huo hivi sasa una dhibiti mawasiliano ya simu za nje pekee. Kamati haikupata sababu za msingi za kwanini mtambo huu usidhibiti mawasiliano ya ndani.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kwamba mtambo wa Telecommunication Traffic Monitorig system (**TTMS**) kwa simu za nje umeweza kuongeza mapato ya Serikali ambapo Serikali inapata mgao wa mapato hayo kwa wastani wa shilingi bilioni 1.7 kwa mwezi. Mapato ambayo hayakuwepo kabla ya kusimikwa kwa mtambo huo.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na mikataba yenyе utata baina ya makampuni ya simu ambapo kukosekana kwa usimamizi thabiti kunapelekeea upotevu mkubwa wa mapato ya serikali na kuingiza hasara watumiaji wa simu. Mfano, kuvunjika kwa

4 FEBRUARI, 2015  
mkataba kati ya SHIVACOM na Vodacom Tanzania Limited (*Contract for the Production of electronic recharge vouchers*).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inazo taarifa kwamba moja ya sababu ya mkataba wa SHIVACOM na Vodacom Tanzania Limited kuvunjika ni kutokana na SHIVACOM kuiibia Vodacom Tanzania Limited na wateja wake kwa kuzalisha vocha za kielektroniki na kuzisambaza moja kwa moja kwa wateja kwa kutumia namba za siri zilizotolewa na Vodacom Tanzania Limited na baadae kuwasilisha vocha ileile kwa Vodacom Tanzania Limited ambazo hazina thamani (no value and usage by customers).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imemuagiza Waziri wa Fedha kuiagiza Mamlaka ya Mapato (**TRA**) na Waziri wa Mawasiriano Sayansi na Teknolojia kuiagiza Mamlaka ya Udhibiti Mawasiliano Tanzania (**TCRA**) kufanya uchunguzi dhidi ya madai haya ili kubaini kiasi cha mapato ya Serikali yaliyopotea kutokana na mkanganyiko huo.

**Mheshimiwa Spika**, endapo itathibitika kuwa madai haya ni ya kweli basi Taifa litakuwa limepoteza mabilioni ya fedha kama kodi, wateja kukosa huduma na kuibiwa kwa kipindi chote cha kuanzia Julai, 2007 hadi Julai, 2012.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto nyingine inayokwamisha mapato ya Serikali kwenye sekta ya mawasiliano ni uwepo wa sheria mbili tofauti za Kodi ya Ongezeko la Thamani (**VAT**) kwa upande wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kunakosababisha usumbuwa wa ukusanyaji wa kodi ya ongezeko la thamani. Kampuni za simu za Tanzania Bara yanayosababisha ankaru katika kampuni za simu za Zanzibar (**ZANTEL**) malipo hufanywa bila Kodi ya Ongezeko la Thamani (**VAT**) kwa madai kuwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar imekwisha kata kodi

4 FEBRUARI, 2015

hiyo, na kwa upande wa Zanzibar wanapoleta ankara zao Tanzania Bara inakuwa hivyo hivyo. Kamati inashauri Serikali ikutane na Mamlaka zote mbili ili kushughulikia tatizo hili la utata huu wa kodi.

## 2.7 Manunuzi ya Umma Yasaidie Wazawa Kupata Kazi

**Mhesimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba manunuzi ya umma hayawasaidii sana wazawa kwani zabuni nyingi zimekuwa zikitolewa kwa wageni, pia bila kuzingatia viwanda vya ndani vinavyoongeza thamani aidha kamati imeona kuwa hata kazi ambazo zinaweza kufanywa na wazawa zinafanywa na wageni. Halii imeleta athali kubwa sana katika uchumi na maendeleo ya nchi kama:

- (i) Makampuni na viwanda vya ndani kushindwa kuimalika kimtaji na kiutaalam;
- (ii) Kusafirisha ajira nje ya nchi na huku vijana wengi wa kitanzania wakiwa na matatizo ya kukosa ajira; Manunuzi ya vifaa kuendelea kufanyika nje ya nchi na faida yote hubaki huko;
- (iii) Serikali kushindwa kujenga msingi bora wa kodi (*Tax Base*) kwa kuwa wananchi wake hawajengwi kimtaji kufanya biashara na kuwekeza zaidi.
- (iv) Aidha, Kamati imebaini kuwa nchi imeshindwa kuongeza thamani ya mazao na rasilimali za taifa kwa kuwa hata bidhaa zinazoweza kuzalishwa na viwanda vya ndani huagizwa kutoka nje ya nchi huku viwanda vya ndani vikiachwa bila soko, mfano sare za majeshi na shuka za hospitali.
- (v) Kukopa kwa ajili ya kujenga miundombinu ya kiuchumi pekee bila kuangalia faida pana (*multiplier effects*) hakuwezi kuimarishe uchumi wa nchi. Mfano kukopa fedha za kujenga barabara kutoka Dodoma kwenda Iringa haitakuwa na maslahi kama wananchi

4 FEBRUARI, 2015

wake hawana ajira, hawana mitaji ya kufanya biashara, mazao hayana soko mfano huko Sumbawanga kuna barabara ya rami hivi sasa lakini bado wananchi wanateseka kwa kukosa masoko na mahindi yao yanaoza.

- (vi) Kamati imebaini kuwa mikopo mingi ya kutoka nje ya nchi ina masharti ya mzabuni au mkandarasi kutoka nchi zao pamoja na kwamba mikopo hii ni ya kibiashara na nchi inalipa riba.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali hii, Kamati imemuagiza Waziri wa Fedha kuiagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi *Public Procurement Regulatory Authority (PPRA)* kufanya ukaguzi katika manunuzi ya Serikali ya sare za majeshi na shuka za hospitali pamoja na kazi zinazotolewa na **TANROAD** kuona ni kwa jinsi gani wazawa wamepewa kazi katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2010/2011 hadi sasa.

## 2.8 Mikataba ya Misaada na Mikopo Kutoka Nje

**Mheshimiwa Spika**, mikataba ya misaada na mikopo kutoka nje imekuwa ikiingiwa na Serikali bila Bunge kuelezwu vigezo na masharti ya mikopo hiyo, kinacholetwa Bungeni kwenye hotuba ya Bajeti ni kiasi cha fedha kinachotarajiwa kukopwa pasipo Bunge kuelezwu vigezo na masharti kama riba, muda wa mkopo n.k.

**Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kuwa usiri huu unalifanya Bunge kutotimiza wajibu wake wa kuishauri na kuisimamia serikali katika eneo hili.

**Mheshimiwa Spika**, imefika wakati Waziri wa Fedha anapaswa awasilishe vigezo na masharti ya mikopo wakati wa Bajeti ili Bunge liweze kupitia na kuridhia, kukubali mkopo huo au la! kuliko utaratibu uliopo sasa ambapo Bunge halielewi chochote kuhusu vigezo na masharti (Riba, muda wa mkopo na masharti mengineyo).

4 FEBRUARI, 2015

## **2.9 Ukomo wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika Ya Umma (CHC).**

**Mheshimiwa Spika**, Azimio namba 5/2011, azimio la Bunge la kuridhia muda wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma yaani "The Consolidated Holding Corporation" Bunge lilazimia kuwa nanukuu "kwa hiyo basi, kwa madhumuni haya maalum, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika mkuutano wa nne kwa mujibu wa kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Benki linaazimia kuongeza muda wa uhai wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe 1 Julai, 2011 hadi tarehe 30 Juni, 2014 ili kutoa fursa kwa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika kukamilisha taratibu za kiutendaji na kisheria. Ndani ya Muda huo Serikali itafanya tathmini ya kazi za Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (Consolidated Holding Corporation) ili kubaini kama liongezewe tena muda au kufanyiwa uamuzi mwingine" mwisho wa kunukuu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati katika kufuatilia utekelezaji wa azimio hili la Bunge katika kikao chake cha mwezi mei, 2014 ilialifiwa na Waziri wa Fedha kuwa, kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma, Wizara ilitangaza kwenye vyombo vya habari ili kumpata mshauri mwelekezi wa kufanya tathmini ya utendaji wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (Consolidated Holding Corporation) mwezi Septemba, 2013. Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kimepata zabuni hiyo baada ya taratibu zote kukamilika. Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) ilipewa muda wa hadi tarehe 30, Mei 2014 kuwasilisha taarifa hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashangazwa na Wizara kushindwa kutekeleza Azimio la Bunge kwa miaka 3 na kutangaza kumpata mzabuni katika mwezi wa Mei, 2014 ambapo ilikuwa ni mwezi mmoja kabla ya shirika hili kufikia ukomo. Hata hivyo, Kamati iliagiza

4 FEBRUARI, 2015

Wizara kuleta taarifa ya tathmini mbele ya Kamati tarehe 2 Juni, 2014 agizo hilo halikutekelezwa na Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, cha kushangaza mnamo tarehe 27 Juni, 2014 Serikali ilitoa Amri (Government order No.203) ya kusitisha shughuli za Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (*Consolidated Holding Corporation*). Amri hiyo ya Serikali ni kwa mujibu wa kifungu Na.5 (1) na (2) kinachompa mamlaka Waziri wa Fedha kusitisha shughuli za Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (*Consolidated Holding Corporation*). Aidha, amri hiyo ilisitisiza kuwa ifikapo tarehe 30 Juni, 2014 Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (*Consolidated Holding Corporation*) itakoma. Na kwamba:

1. Kuanzia tarehe 30 Juni, 2014 Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (*Consolidated Holding Corporation*) na Watumishi wake hawatakuwa na mamlaka yoyote waliyopewa na benki ya Taifa ya Biashara (**NBC**) (*Reorganization and vesting of Assets and Liabilities*) Act, Cap.404.
2. Kuanzia tarehe 1 Julai, 2014, shughuli, mali na madeni vitahamishiwa katika Ofisi ya Msajili wa Hazina.
3. Kuanzia tarehe tajwa, mtu yoyote aliyekuwa muajiliwa wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (*Consolidated Holding Corporation*) atakuwa mwajiliwa wa Ofisi ya Msajili Hazina.

**Mheshimwa Spika**, amri hii ya Serikali (Government Order) imetolewa na Waziri wa Fedha wakati uhai Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (*Consolidated Holding Corporation*) ukiwa mikonomi mwa Bunge lako tukufu, kwani Bunge lilikuwa likiongeza uhai wa shirika mara kwa mara linapoona inafaa, mfano shirika liliongezewa muda wa miaka mitano kuanzia 2002-2007 kupitia Azimio la Bunge Na.20/2002;

4 FEBRUARI, 2015

marekebisho ya sheria ya Na.10 ya mwaka 2007 na Sheria Na.26 ya mwaka 2007 zililiongezea shirika muda wa miaka 4 kuanzia 2007-2011; na kwa Mujibu wa Azimio namba 5/2011 Bunge liliongeza uhai wa Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (*Consolidated Holding Corporation*) kwa muda wa miaka 3 kuanzia 1 Julai, 2011 hadi 30 Juni, 2014.

**Mheshmiwa Spika**, Azimio hilo la Bunge lako tukufu liliitaka Serikali kufanya tathmini ya kazi za shirika hodhi la mali za mashirika ya Umma (*Consolidated Holding Corporation*) ili kubaini kama liongezewe tena muda au kufanyiwa uamuzi mwingine. Hivyo si sahihi kwa Waziri kusitisha shughuli za shirika bila kuwasilisha tathmini Bungeni kama Azimio (Na.5/2011) liliyo elekeza. Msingi wa uamuzi wa aidha Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (*Consolidated Holding Corporation*) iendelee au ikome ilitegemea matokeo ya tathmini.

**Mheshimiwa Spika**, shughuli za Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (*Consolidated Holding Corporation*) hivi sasa zimeshitwa bila Bunge lako tukufu kupewa taarifa na bila kujua ni nini kimo katika tathmini hiyo. Awali Kamati yangu ilisisitiza kuwa taarifa hiyo ya tathmini iwasilishwe mbele ya Kamati na kisha Bungeni ili kukidhi matakwa ya Azimio Na.5/2011.

**Mheshimiwa Spika**, kwa wakati mwingine Kamati ilikwisha onyesha hofu yake kubwa ya shughuli za Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (*Consolidated Holding Corporation*) kulithiwa na Ofisi ya Msajiri wa Hazina ambayo kimsingi haijaandalishiwa kuweza kukabiliana na majukumu yaliyosalia.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na amri hiyo ya Serikali kuamuru kwamba Watumishi waliokuwa katika Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (*Consolidated Holding Corporation*) watahamishiwa katika Ofisi ya

4 FEBRUARI, 2015

Msajili wa Hazina, lakinii kati ya Watumishi 48, Watumishi 22 walifukuzwa kazi bila kupewa maelezo na sababu za kufukuzwa huko wakati agizo limeelekeza kuwa Watumishi wote waliokuwa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (*Consolidated Holding Corporation*) watahamishiwa katika Ofisi ya Msajiri wa Hazina. Huku ni kutokutenda haki kwa Watumishi hawa na kwamba Serikali inaweza ikafikishwa mahakamani wakati wowote na kuliingiza taifa katika gharama zisizokuwa za lazima.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MASUALA YAHUSUYO UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA

#### 3.1 Umuhimu wa Viwanda Vyote Nchini Kuwa Chini ya Wizara Moja

**Mheshimiwa Spika**, ukuaji wa uchumi wa nchi yoyote ile unategemea sana maendeleo ya viwanda. Mara nyingi maendeleo haya huanza na Kilimo ambacho ni chanzo kikubwa cha malighafi za viwandani. Hivyo, nchi nyingi zilizoendelea duniani zilifanya mageuzi kutoka katika uchumi wa kilimo, au uchimbaji au ufgugaji kwenda kwenye uchumi wa viwanda na hatimaye uchumi wa viwanda na huduma na Teknolojia.

**Mheshimiwa Spika**, viwanda vinahitajika kwa ajili ya kuzalisha na kutengeneza mahitaji ya sekta zote za kiuchumi na kijamii. Hakutakuwa na mafanikio ya sekta ya miundombinu, nishati, ujenzi, elimu, utalii, afya na uchukuzi bila kuwepo kwa viwanda. Kwa maana hiyo viwanda ni chachu ya kuvuta sekta nyingine za uchumi na huduma na kichocheo kikubwa cha kukua kwa uchumi.

**Mheshimiwa Spika**, viwanda vya Tanzania vimeduwa havikui kulingana na mahitaji halisi ya wananchi na ya kiuchumi kwa kuwa viwanda vingi vilivyopo husimamiwa na sekta husika. Kwa mfano viwanda

4 FEBRUARI, 2015

vinavyozalisha mazao yatokanayo na mbao husimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii, mazao yatokanayo na mifugo na uvuvi husimamiwa na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na mazao yatokanayo na sukari husimamiwa na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa ufanisi mdogo wa viwanda vyta ndani pamoja na mambo mengine huchangiwa kwa viwanda hivi kutosimamiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara, ingawa **Tamko la Serikali Na.494 la tarehe 17 Desemba 2010** linaelekeza kwamba Wizara itakuwa na majukumu ya kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera, Kanuni na taratibu za uendeshaji wa Viwanda, Biashara, Masoko, Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuandaa mfumo mzuri wa usimamizi wa viwanda nchini ambapo viwanda vyote vitakuwa chini ya Wizara inayosimamia sekta ya viwanda.

### 3.2 Viwanda Vya Nguo Nchini (Textile Industry)

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania ni mionganini mwa nchi zinazozalisha pamba kwa wingi katika Bara la Afrika, zaidi ya hekta 412,000 huzalishwa katika mikoa 13 ya Tanzania Bara. Kila mwaka Tanzania imekuwa ikizalisha wastani wa tani 300,000 za pamba.

**Mheshimiwa Spika**, kutohakana na kiasi kikubwa cha pamba kinachoalishwa nchini, Kamati ilifanya ziara katika kiwanda cha nguo cha **21<sup>st</sup> Century Ltd** kilichopo mkoani Morogoro kujionea fursa na changamoto zilizopo katika sekta ya nguo.

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara hiyo, Kamati ilibaini kuwa ni takribani asilimia 20 (20%) ya pamba

4 FEBRUARI, 2015  
inayozalishwa nchini hutumiwa na viwanda vya ndani na asilimia 80 (80%) inayobaki huuzwa nje ya nchi ikiwa ghafi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kwamba Tanzania ni wazalishaji wakubwa wa pamba, Serikali imekuwa ikifanya manunuzi ya nguo zinazotengenezwa kwa pamba kutoka nje ya nchi wakati kuna viwanda vya ndani vyenye uwezo wa kutengeneza nguo za aina mbalimbali zinazofaa kwa matumizi ya maofisini

**Mheshimiwa Spika**, kuna faida nydingi zitokanazo na kufanya manunuzi kwenye viwanda vya ndani. Faida hizo ni pamoja na:-

- (i) Kuwezesha viwanda vya ndani kukua na kuongeza ajira kwa vijana;
- (ii) Kuongeza thamani ya zao la pamba kutaongeza matumizi ya pamba nchini, hivyo kuwa na sokola uhakika na bei nzuri ya pamba hapa nchini badala ya kutegemea soko la dunia ambalo limekuwa halitabiriki.
- (iii) Kuwezesha kwa kuvipa kazi viwanda vya ndani kutaongeza mitaji, uzalishaji na hivyo kuvifanya kuwekeza zaidi na mapato ya serikali kuongezeka.

**Mheshimiwa Spika**, uuza ji wa nguo zinazotengenezwa ndani na nje ya nchi (*Textile Apparel*) umekuwa mdogo sana ikilinganishwa na nchi jirani za Kenya, Madagascar na Lesotho, mfano katika soko la Marekani mwaka 2009 ambapo Tanzania iliuza Dola za kimarekani milioni 1.2 tu huku Kenya ikiuza Dola za kimarekani milioni 195.4. Wakati huo huo Tanzania inazalisha pamba kwa wingi kuliko nchi ya Kenya.

**Mheshimiwa spika**, Kamati inaitaka Serikali kuandaa mazingira wezeshi ikiwa ni pamoja na kusimamia

4 FEBRUARI, 2015

viwanda vya ndani ili viweze kukua na kushindana  
kwenye ulimwengu wa ushindani.

### **3.3 Kiwanda cha Nguo cha Urafiki (Friendship Textile Company).**

**Mheshimiwa Spika**, kiwanda cha nguo cha Urafiki kinamilikiwa na Serikali ya Tanzania kwa hisa za asilimia 49 (49%) na Serikali ya China inamiliki hisa za asilimia 51 (51%). Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilifanya ziara ya kutembelea kiwanda cha nguo cha Urafiki.

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara hiyo Kamati ilibaini uharibifu mkubwa wa mashine za kiwanda ambapo baadhi ya mashine zimeng'olewa, sehemu ya kiwanda imegeuzwa ghalna sehemu ya maonyesho ya magari yanayouzwa (showroom), baadhi ya ofisi na nyumba ambazo ni mali ya kiwanda zinakodishwa bila kufuata utaratibu. Aidha, kwa nyakati tofauti Kamati imekuwa ikihitaji maelezo ya matumizi ya dola za Kimarekani **milioni 27** zilizokopwa toka Serikali ya China kwa ajili ya uendelezaji wa kiwanda.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haikuridhishwa na maelezo yaliyohusu matumizi ya fedha hizo, Kamati ilielezwa kwamba kati ya fedha hizo, dola za kimarekani **milioni 12** zilibaki China kwa ajili ya kununua bidhaa. Hata hivyo maelezo hayo, hayaainishi bidhaa zilizonunuliwa na kuletwa kiwandani. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa matumizi ya dola za kimarekani **milioni 15** zilizobaki zilitumika kukarabati mitambo ya kiwanda bila kuainisha mitambo iliyokarabatiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapendekeza kwamba, Tume huru ya Bunge iundwe kuchunguza suala hili kwa undani ili kuhakiki uhalali wa matumizi haya na hatima ya kiwanda hiki.

4 FEBRUARI, 2015

### **3.4 Changamoto ya Umeme Katika Viwanda Vilivyopo Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, licha ya sekta ya viwanda nchini kutumia na kulipia zaidi ya 50% ya umeme unaosambazwa na Shirika la Umeme Tanzania (**TANESCO**), upatikanaji na ubora wa umeme huo umekuwa ni changamoto kubwa inayoathiri maendeleo ya sekta ya viwanda nchini.

**Mheshimiwa Spika**, hali hii imepelekea wenye viwanda kutumia nishati mbadala kama jenereta yanayozalisha umeme mkubwa ambayo yana ghamama kubwa na kusababisha kuongezekwa kwa ghamama ya uzalishaji na bei ya bidhaa kupanda. Changamoto wanazopata wenye viwanda kutokana na matatizo ya umeme ni pamoja na:-

- (a) Kukatika kwa umeme mara kwa mara na wakati mwingine pasipo taarifa rasmi kutoka Shirika la Umeme Tanzania;
- (b) Shirika la Umeme Tanzania kutokuwa na kipaumbele kwa ajili ya wazalishaji wakubwa;na
- (c) Shirika la Umeme Tanzania kutolipa fidia na bila kujali umeme unapopungua na kuzidi ghafla (*Eratic Power Supply*) na hivyo kuharibu vifaa na mitambo na kuingiza hasara kubwa.

**Mheshimiwa Spika**, mfano wa baadhi ya viwanda vilivyoathirika kwa kiasi kikubwa na changamoto zilizoelezwa hapo juu ni pamoja na:

- (i) **Kiwanda cha Nguo cha 21<sup>st</sup> Century Ltd**  
Kukosekana kwa umeme mara kwa mara au kupata umeme usio na ubora kumeinginzia kiwanda hasara ya Shilingi bilioni 2.
- (ii) **Kiwanda cha Nguo cha Mwatex**:- Tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara au umeme

4 FEBRUARI, 2015

kuongezeka nguvu ghafla kumeiingizia hasara ya zaidi ya jumla ya shilingi bilioni 2 kwa kipindi cha miezi 30 ambayo tatizo la umeme limekuwepo kiwandani hapo.

**(iii) Kiwanda cha Saruji cha Wazo:** Kwa mwaka 2014 umeme ulikatika kwa masaa 84 kwa njia ya umeme wa KV 132 na masaa 172 kwa njia ya umeme wa KV 33 na kulisababisha hasara ya Dola za Kimarekani 895,000.

**(iv) Viwanda vya Lake Cement na Rhino Cement:** Viwanda hivi ni vipyta na vimeanza uzalishaji mwaka 2014. Moja ya changamoto kubwa inayokabili viwanda hivi ni pamoja na kutopata umeme wa kutosha na umeme kukatika mara kwa katika bila taarifa yoyote.

**(v) Kiwanda cha Kutengeneza karatasi Mufindi Paper Mills Ltd (MPM)**

Kuanzia tarehe 16 Januari, 2015 Kiwanda cha kutengeneza karatasi Mufindi (**MPM**) kilikosa umeme na hasara iliyopatikana hadi tarehe 26 Januari, 2015 ni ya jumla ya Dola za kimarekani 300,000 kwa 264 sawa na siku 11.

**(vi) Kiwanda kama Jambo Spinning Mill cha Arusha:-** Kimefungwa kutokana na kukosekana kwa umeme wa uhakika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaona kwamba, kukosekana kwa umeme wa uhakika kuna dhoofisha uzalishaji viwandani na kuleta hasara kubwa kiasi kwamba viwanda vya ndani kushindwa kuijendesha na kushindana na viwanda vingine vya nchi jirani na kwingineko duniani.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na juhudi zinazofanywa na Serikali za ujenzi wa miradi mikubwa ya umeme itakayo wezesha kupata megawatts (MW) za kutosha

4 FEBRUARI, 2015

kutokana na gesi, makaa ya mawe na upepo, Serikali itafute mikakati ya muda mfupi na wa kati kutatua matatizo haya ikiwa ni pamoja na Shirika la Umeme Tanzania (**TANESCO**) kuhakikisha kuwa inatoa taarifa za kukatika kwa umeme kwa wateja wake na kuangalia namna ya kufidia hasara zinazojitokeza.

### **3.5 Mgogoro Bainya ya Tanga Fresh Ltd Na Tume ya Ushindani (FCC)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati yangu ilipokea malalamiko kutoka chama cha ushirika cha Wafugaji wa Mkoa wa Tanga (*Tanga Dairies cooperative Union-TDCU*) kuhusu mgogoro bainya ya Tume ya Ushindani (**FCC**) dhidi ya kampuni wanayoimiliki ya *Tanga fresh Ltd*.

**Mheshimiwa Spika**, kampuni ya *Tanga Fresh Ltd* ni kampuni ya usindikaji wa maziwa yanayotoka kwa wafugaji wa Mkoa wa Tanga na Mikoa jirani.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kuwasikiliza washirika (**TDCU**) na uongozi wa *Tanga Fresh Ltd* na Tume ya Ushindani ili kusikiliza pande zote mbili zenye mgogoro na kupata ukweli. Kamati ilibaini kwamba kiini cha mgogoro kilanza mnamo mwaka 2009 ambapo kampuni ya *Tanga Fresh Ltd* ilinunua majengo na baadhi ya mitambo kutoka kampuni mbili tofauti ambazo zilikuwa zimefunga biashara ya ununuzi na usindikaji wa maziwa kwa muda wa zaidi ya miaka miwili. Kampuni hizo ni *Morani Dairies Ltd* na *International Food Processors Ltd* zote za mkoani Tanga.

**Mheshimiwa Spika**, mgogoro huu ulisababishwa na ununuzi wa majengo na baadhi ya mitambo na majengo kwa kampuni hizo hali iliyopelekea Tume ya Ushindani kuingilia kati ambapo Tume ya Ushindani iliituhumu kampuni ya *Tanga Fresh Ltd* kwa kukiuka Sheria ya Ushindani ya Mwaka 2003 na iliitaka kampuni ya *Tanga Fresh Ltd* kulipa faini ya asilimia 8(8%) ya

4 FEBRUARI, 2015

mauzo gafhi ya Mwaka 2012 ambayo ni sawa na shilingi bilioni 2.8. Faini hiyo ilipunguzwa hadi kufikia shilingi milioni 406.9.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haioni umuhimu wa Tume ya Ushindani (**FCC**) kuendelea na msimamo wake wa kuitoza faini kampuni ya *Tanga Fresh Ltd* kiasi cha Tsh. Milioni 406.9 kwa makosa ambayo hayana madhara yoyote katika ushindani, Katika kikao cha maridhiano Tume ya Ushindani (**FCC**) ilikubali kuondoa faini yake lakini baada ya kikao iliendelea na msimamo huo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaanini kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara ndio mtetezi namba moja wa ustawi wa viwanda nchini lakini imekuwa kinyume chake. Kamatiimeshauri mara kwa mara kufutwa kwa faini hiyo lakini ushauri wa Kamati umekuwa hauzingatiwi.

**Mheshimiwa Spika**, hivyo basi Kamati inashauri kuwa Tume Ya Ushindani (**FCC**) iondoe ankara yake ya faini ya shilingi **milioni 406.9** na kwamba Tume iwe na ushirikiano na viwanda badala ya kuvikomoa na kusababisha vishindwe kuzalisha, kuwekeza na kushindana na viwanda jirani kama vyta Kenya na nchi zingine.

### 3.6 Tume ya Ushindani (**FCC**)

**Mheshimiwa Spika**, biashara ya bidhaa bandia ni kosa la jinai na inahusisha mitandao ya wafanyabiashara makubwa duniani na hivyo kufanya udhibiti wake kuwa suala la kimataifa, hali hiyo imeleta ugumu katika vita dhidi ya bidhaa bandia kwa kuwa inahusisha uingizaji bidhaa nchini kupitia mwambao bahari ya Hindi wa Tanzania unaokaribia Kilomita 1424. Ulinzi wa mwambao huo dhidi ya wahalifu wa bidhaa bandia ni changamoto kubwa kwa Tume ya Ushindani (**FCC**) na taifa kwa ujumla. Jambo hili

4 FEBRUARI, 2015

lilithibitishwa na kamati baada ya kutembelea viwanda mbalimbali nchini ambavyo vililalamika uwepo wa bidhaa bandia kila mahali kutoka ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliarifiwa kwamba katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 Tume ilifanya ukaguzi wa maghara 101 na kukamata makontena 270 yaliyokuwa yamekiuka Sheria ya alama ya bidhaa. Pia katika kipindi hicho Tume ya Ushindani (**FCC**) ilifanikiwa kuteketeza bidhaa bandia zenyenye thamani ya shilingi **milioni 162.5**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kwamba kitendo cha kuteketeza bidhaa bandia ambazo zinakidhi viwango ni hasara kwa mfanya biashara na Taifa kwa ujumla. Bidhaa bandia kutoka nje hununuliwa kwa fedha za kigeni kutoka nchini na kwamba mfanya biashara aliyeingiza bidhaa hiyo aidha kwa kujua au kutokujua hufirisika kwa sababu mtaji wake umeteketezwa na hivyo kupelekea kuathili ajira, mapato ya Serikali na uchumi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, kuteketeza bidhaa bandia zinazoingizwa nchini bila kudhibiti viwanda vinavyo tengeneza bidhaa hizo siyo suluhisho, dunia ni lazima ijielekeze kudhibiti viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo kwa kutumia nyaraka za wafanya biashara kama ushahidi tu. Kwa kushirikiana na *World Trade Organization (WTO)*, watumie nyaraka kufuatilia kiwanda kilichohusika kutengeneza bidhaa bandia. Kamati inaona kwamba sheria ya kuteketeza bidhaa bandia haitendi haki licha ya kuwa inazingatia matakwa ya kimataifa na masharti ya *World Trade Organization (WTO)*.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia inashauri kuwa badala ya kuteketeza bidhaa, mfanya biashara atozwe faini kubwa, na mwenye kiwanda stock ya bidhaa zake iteketezwe sambamba na kufutiwa leseni.

4 FEBRUARI, 2015

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kwamba, kwa kuwa ni hasara, ghamama na sababu zingine za kimazingira kuteketeza bidhaa bandia au hafifu, hivyo Shirika la Viwango Tanzania (**TBS**) na Tume ya Ushindani (**FCC**) wafanye kazi pamoja hasa katika utaratibu wa **PVoC** ili kuwezesha ukaguzi wa ubora na bidhaa bandia kufanyika kwa pamoja hukohuko nje ya nchi kabla bidhaa hazijaingizwa nchini. Na kwamba sheria ya Shirika la Viwango Tanzania (**TBS**) na Tume ya Ushindani (**FCC**) zifanyiwe marekebisho ili kuwezesha

### 3.7 Shirika la Viwango Tanzania (**TBS**)

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilianzisha utaratibu kukagua ubora wa bidhaa huko zinakotoka na ndio msingi wa mfumo ujulikanao kama “*Pre-shipment verification of Conformity to standards (PVoC)*” utaratibu huu umelenga kuhakiki ubora wa bidhaa ili kubaini iwapo bidhaa hizo zinakidhi matakwa ya viwango husika. Pamoja na “*Pre-shipment verification of Conformity to standards (PVoC)*” bado kumekuwa na wimbi wa uingizwaji wa bidhaa hafifu nchini. Makampuni yaliyokuwa yanafanya ukaguzi nje ya nchi ni **SGS**, **INTERTEK** na **BUREAU VERITAS** ambayo mikataba yao ilishia mwishoni mwa Januari, 2015.

**Mheshimiwa Spika**, katika mkataba uliomalizika, kampuni ya **INTERTEK** imekuwa ikiripotiwa kukagua bidhaa na kuweka *Certificate of Confirmity (COC)*, lakini bidhaa zinapofika nchini zinakuwa hazikidhi viwango vya ubora, licha ya mkataba kusema wazi kuwa wakala atakae toa cheti *Certificate of Confirmity(COC)* kwa bidhaa hafifu atapewa adhabu kali ikiwa pamoja na kufutiwa mkataba.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilishangazwa ni kwa nini Shirika la Viwango nchini (**TBS**) halikuchukua hatua

4 FEBRUARI, 2015

yoyote kwa kampuni hiyo? kufuatia uzembe huo Kamati inaamini kwamba kuna kutowajibika ipasavyo kwa baadhi ya Watumishi wa Shirika la Viwango nchini (**TBS**) katika kusimamia mikataba na viwango nchini.

**Mheshimiwa Spika**, kampuni ya **INTERTEK** pekee iliripotiwa zaidi ya mara sita kuruhusu bidhaa zisizo na ubora kuingia nchini. Kamati inahoji ni kwa nini Shirika la Viwango (**TBS**) haikuchukua hatua dhidi ya kampuni hiyo licha ya masharti ya mkataba kuwa wazi?

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo Kamati imejiridhisha kwamba ukosefu wa vifaa na maabara za kisasa pamoja na ufinyu wa rasilimali watu kunachangia uingizaji wa bidhaa zisizo na ubora nchini, hivyo Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 kwa ajili ya ujenzi wa maabara.

### 3.8 Wakala wa Vipimo (WMA)

**Mheshimiwa Spika**, lengo kuu la kuanzishwa kwa Wakala wa Vipimo (**WMA**) nchini ni kumlinda mlaji na umma kwa ujumla kuititia matumizi sahihi ya vipimo vitumikavyo katika biashara na huduma nyingine, kuhakikisha biashara zote zinafanyika kwa haki na usawa baina ya pande mbili zinazohusika yaani muuzaji na mnunuzi kuititia vipimo.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na malalamiko mengi kutohana na matumizi ya vipimo mfano, petro pumpu, luku, mizani, *flow-meters*, n.k. Sheria inayosimamia vipimo imepitwa na wakati, mfano mtu anaetumia mizani mbovu faini yake ni shilingi **10,000** tu, vilevile wakala amekuwa akilalamikiwa kwa usimamizi dhaifu wa matumizi ya vipimo nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Mtambo wa Telecommunication Traffic Monitoring System (**TTMS**) iliyonunuliwa na kuwekwa Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano

4 FEBRUARI, 2015

(**TCRA**), Wakala wa Vipimo (**WMA**) haikushirikishwa wala haujui kama kuna mtambo wa namna hiyo. Wakati Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano (**TCRA**) wanasema waliwashirikisha Wakala wa Vipimo (**WMA**) katika kipindi cha ununuzi wa kifaa hicho. Udhifu huu unaweza kusababishwa na udhaifu wa Sheria, au usimamizi duni wa wakala na mshirikiano dhaifu baina ya taasisi za Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, mfano mwagine ni flow-meter iliyokuwa uimefungwa bandarini na Mamlaka ya Bandari (**TPA**) kwa ajili ya kupima mafuta baada ya kufanya kazi muda mfupi ikafungiwa na Wakala wa Vipimo (**WMA**) kwa madai kuwa ilikuwa inapunja wafanya biashara. Swali la kujuliza ni kwanini Wakala wa Vipimo (**WMA**) isikatae ununuzi wa flow-meter hizo kabla hazijanunuliwa? Mamlaka ya Bandari (**TPA**) inadai kuwa iliwashirikisha Wakala wa Vipimo (**WMA**) wakati wa ununuzi huku WMA ikitana na kudai kuwa ilishirikishwa wakati wa uzinduzi tu.

**Mheshimiwa Spika**, ni lazima ufuatiliaji ufanyike ili kujua ni nani hasa aliyesababisha matumizi haya mabaya ya fedha? Kwa utaratibu sahihi na kwa mujibu wa Sheria ya vipimo ni vyema serikali au taasisi zake zinapotaka kununua vipimo lazima vipate kibali cha kuidhinisha ubora kabla ya manunuzi.

### **3.9 Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO).**

**Mheshimiwa Spika, TIRDO** ni Shirika la Utafiti wa Maendeleo ya Viwanda nchini. Shirika hili linashindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na ukosefu wa fedha. Hatua hii imesababisha shirika hili kushindwa kutekeleza jukumu lake la msingi ambalo ni kufanya kazi utafiti na kutoa ushauri kwa viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, licha ya changamoto ya ukosefu wa rasilimali fedha, **TIRDO** inakabiliwa na

4 FEBRUARI, 2015  
changamoto ya kuendelea kupungua kwa eneo la **TIRDO** kutoka **hecta 40** mwaka 1979 na kufikia hekta **21.3** mwaka 2013 zilizopo katika viwanja namba 1771-1776;1409,1409/3 eneo la Msasani Penisula .

**Mheshimiwa Spika**, kila Kamati inapohoji kuendelea kupungua kwa eneo la **TIRDO** imekuwa haipati maelezo ya kuridhisha kutoka kwa taasisi pamoja na Wizara, mfano ni uhalali wa **hecta 7.57** kukabidhiwa **CCBRT** kwa ahadi ya kulipa fidia ya shilingi **milioni 167** tu ambayo nayo haijatekelezwa toka mwaka 2004, eneo la **hecta 1.4** kuuzwa kinyemela na watumishi wa **TIRDO** kwa shirika la **PPF** kwa shilingi **bilion 6** ambapo hadi sasa hakuna hatua iliyochukuliwa.

**Mheshimiwa Spika**, kutohana na mkanganyiko huu Kamati inapendekeza kuundwa kwa Kamati ndogo itakayofuatalia uporaji wa eneo la shirika la **TIRDO**.

### 3.10 Uzalishaji wa LABSA Nchini

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Wizara kuhusu mahitaji na matumizi ya **LABSA** nchini yanaonyesha kuwa kuna viwanda viwili tu vinavyozalisha **LABSA** nchini ambavyo ni Murzah soap & Detergent Ltd na Royal Soap and Detergent Industries Ltd, ambavyo kwa pamoja vinazalisha tani 29,648 za **LABSA** kwa mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, kiasi kikubwa cha **LABSA** hiyo hutumiwa na viwanda hivyo viwili na ziada huuzwa kwa watumiaji wengine. Mahitaji ya **LABSA** kwa mwaka ni wastani wa tani **61,045.6** ambapo tani **33,397.6** huagizwa kutoka nje ya nchi. Kamati inashauri kuwa kwa kuwa viwanda hivi havina uwezo wa kuzalisha **LABSA** ya kutosha kuweza kukidhi mahitaji ya viwanda visivyozalisha **LABSA** nchini ni vyema ushuru wa asilimia 0% uendelee kubaki kama ulivyo hadi hapo uzalishaji **LABSA** utakapo ongezekwa nchini.

4 FEBRUARI, 2015  
**SEHEMU YA NNE**

#### **4.0 MAPENDEKEZO YA KAMATI NA MAAZIMIO YA BUNGE**

**4.1 Kwa kuwa** suala la riba kubwa katika benki na taasisi za Fedha limekuwa ni la muda mrefu na linaathiri sana uchumi kwa ujumla,

**Hivyo basi** Kamati inapendekeza kwamba Serikali iandae na kuwasilisha Bungeni mkakati mahususi wa kupunguza na kudhibiti viwango vikubwa vya riba vinavyotozwa na mabenki na taasisi za fedha nchini kabla ya bajeti ya Mwaka 2015/2016.

**4.2 Kwa kuwa** jitihada za kuwawezesha wananchi kiuchumi ni pamoja na kuwa na uwezo wa kukopa fedha kutoka mabenki na taasisi za fedha

**Na kwa kuwa** wananchi wengi waishio vijiji ni hutegemea mashamba yao kuweka dhamana ambayo mengi yana hati za kimila ambazo hazikubaliki katika mabenki, pia mashamba na maeneo mengi hayajapimwa hivyo kukosa sifa za kuwa dhamana na hivyo kukosa mkopo,

**Hivyo basi** kamati inapendekeza kwamba Serikali ichukue hatua mahususi za kupima ardhi yote na kwamba Sheria ya Ardhi ya vijiji (*The village Land Act, 1999*) sambamba na Sheria ya Ardhi (*The Land Act,*) zifanyiwe marekebisho mapema iwezekanavyo ili kuziwezesha Hati za kimila ikubalike katika mabenki na taasisi za fedha sawa na hati za kawaida na kwamba Wizara yenye dhamana ya Ardhi ipitie upya ongezeko la ada kwa lengo la kupunguza ili wananchi waweze kumudu gherama za upimaji.

**4.3 Kwa kuwa** utoroshaji wa madini umeshika kasi hapa nchini na kuifanya Serikali kukosa mapato;

**kwa kuwa** Serikali haina mfumo madhubuti wa kudhibiti utoroshaji wa madini wa kupata taarifa za

4 FEBRUARI, 2015  
uchimbaji na uzalishaji wa madini ili kuhakikisha wahusika wanalipa mrabaha na kodi stahiki kabla ya madini hayo hayajasafirishwa nje ya nchi;

**Na kwa kuwa** Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 haimpi mamlaka kamishna wa Madini kutaifisha madini yanayopatikana kinyume cha Sheria na kukusanya mapato yatokanayo na utaifishaji wa madini hayo;

**Hivyo basi** Kamati inapendekeza kwamba Bunge lako tukufu liazimie kuitaka Serikali kuwa na mfumo wa kiintelijensia wa kupata taarifa na kwamba Sheria ya madini ya mwaka 2010 ifanyiwe marekebisho ili kumuwezesha kamishna wa madini kutaifisha madini yaliyopatikana kinyume cha Sheria na kukusanya mapato yatokanayo na utaifishaji wa madini hayo.

**4.4 Kwa kuwa** uingizaji wa bidhaa kwa njia zisizo rasmi umeshamiri sana hapa nchini na kupelekea kukosekana ushindani wenyewe usawa, kuingia kwa bidhaa hafifu, bandia na madawa ya kulevyta na kulipelekea taifa kukosa mapato, viwanda vya ndani kushindwa kushindana na tishio la uhai wa viwanda vyetu hapa nchini,

**Na kwa kuwa** katika ukanda wa bahari ya hindi wenyewe takribani kilomita 1424 kuna bandari buba zipatazo 26 ambazo hutumika kuingiza bidhaa kiholela.

**Hivyo basi**, Kamati inapendekeza kwamba Bunge lako tukufu liazimie kwamba vyombo vya udhibiti **TBS**, **FCC** na **TFDA** vipewe nguvu zaidi ya kupambana ikiwa ni pamoja na kushirikisha Jeshi la Wananchi (**JWTZ**) katika mapambano na kudhibiti ukanda huu ambaou unaliingizia Taifa hasara kubwa.

**4.5 Kwa kuwa**, viwanda vya nguo vya ndani vimeduwa havinufaiki na manunuzi ya nguo yanayofanywa na Serikali, badala yake serikali imeduwa ikinunua nguo

4 FEBRUARI, 2015

za majeshi na shuka za mahospitali toka nje ya nchi  
huku viwanda vya ndani vikiathirika kwa kukosa soko,

**Na kwa kuwa** bei ya pamba ghafi imekuwa ya  
kususua katika soko la dunia, uongezaji thamani  
pamba hapa nchini utasababisha kupatikana kwa  
soko la uhakika na bei nzuri ya pamba, mitaji na  
uwekezaji kuongezeka, na hivyo kusababisha ajira  
kwa vijana na mapato ya Serikali kuongezeka pia,

**Hivyo basi**, Kamati inapendekeza Bunge lako tukufu  
liazimie kwamba Serikali na taasisi zake zishindanishe  
zabuni za manunuzi ya sare za majeshi, shule na  
mashuka ya hospitali pamoja na nguo zingine  
zinazotumia pamba kwa viwanda vya nguo vya hapa  
nchini.

**4.6 Kwa kuwa** misaada na mikopo imekuwa ikiingiwa na  
Serikali bila Bunge kuelezwu vigezo na masharti ya  
mikopo hiyo,

**Na kwa kuwa** Bunge limekuwa halishirikishwi ipasavyo  
katika maswala yanayohusu misaada na mikopo na  
hivyo kushindwa kutimiza wajibu wake wa kuisimamia  
na kuishauri Serikalini katika eneo hili,

**Hivyo basi**, Kamati inapendekeza kwamba katika kila  
Mwaka wa Fedha Serikali iwasirishe mchanganuo wa  
kina wa misaada na mikopo ambayo Serikali  
inatarajia kukopa, taarifa hiyo iainishe nchi wahisani,  
kiasi cha mkopo pamoja na vigezo na masharti kama  
riba, muda na masharti mengineyo.

**4.7 Kwa kuwa**, kitendo cha Waziri kutoa amri ya kusitisha  
kazi za **CHC** huku akijua kuna azimio la Bunge ni  
kuingilia Uhuru na mamlaka ya Bunge lako tukufu.

**Na kwa kuwa** Serikali ulitoa notisi kuhamisha mali zote  
na mashauri yote ya **CHC** zihamishiwe kwa Msajili wa  
Hazina.

4 FEBRUARI, 2015

**Hivyo basi**, Serikali itekeleze tamko lake kuhakikisha kwamba Watumishi wote waliokuwa **CHC** wahamishiwe kwa Msajili wa Hazina .

**4.8 Kwa kuwa** uendelezaji wa viwanda nchini unategemea mfumo mzuri wa usimaizi wa viwanda,

**Na kwa kuwa** kuna baadhi ya viwanda hapa nchini vinasimamiwa na wizara mbalimbali kama kilimo na chakula, mifugo na uvuvi, maliasili na utalii,nishati na madini na viwanda na biashara, kitendo kinachopelekea kukosekana kwa ufanisi na ni kinyume cha sheria, sera na kanuni za viwanda.

**Hivyo basi**, Kamati inapendekeza kuwa Bunge lako tukufu liazimie kwamba viwanda vyote nchini viwe chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

**4.9 Kwa kuwa**, Kamati imekuwa haipewi majibu ya kutosha kwa nyakati tofauti ilipo omba maelezo ya matumizi ya dola **milioni 27** zilizokopwa toka Serikali ya China kwa ajili ya uendelezaji wa kiwanda cha Urafiki.

**Na kwa kuwa**, muda wote Kamati imekuwa hailidhiki na majibu yanayotolewa kwamba dola za kimarekani **milioni 12** zilibaki china kwa ajili ya kununua bidhaa kwa ajili ya kiwanda bila kuainisha bidhaa zilizonunuliwa na kuletwa kiwandani, matumizi ya dola **15 milioni** zilizobaki zilitumika kukarabati mitambo ya kiwanda bila kuainisha mitambo iliyokarabatiwa.

**Hivyo basi**, Kamati inapendekeza kwamba Bunge lako tukufu liridhie kuudwa kwa Tume huru ya Bunge ili kuchunguza suala hili kwa undani na kuhakiki uhalali wa matumizi ya takribani shilingi bilioni 48 na hatima ya kiwanda hiki.

**4.10Kwa kuwa** uteketezaji wa bidhaa una gharama kubwa, kuharibu mitaji na uwekezaji na uchumi kwa ujumla,

4 FEBRUARI, 2015

**Hivyo basi** kamati inashauri kwamba **TBS** na **FCC** wafanye kazi pamoja hasa katika utaratibu wa **PVoC** ili kuwezesha ukaguzi wa ubora na bidhaa bandia kufanyika kwa pamoja hukohuko nje ya nchi kabla bidhaa hazijaingizwa nchini na kwamba Sheria ya **TBS**, **WMA** na **FCC** zifanyiwe marekebisho ili kukidhi changamoto zilizopo.

**4.11Kwa kuwa** maelezo ya kupungua kwa eneo la **TIRDO** kutoka hekta 40 mwaka 1979 na kufikia hekta 21.3 mwaka 2013 yamekuwa si ya kuridhisha licha ya Kamati kufuatilia mara kwa mara,

**Hivyo basi** Kamati inapendekeza kwamba Bunge lilidhie kuundwa kwa Kamati ndogo kufuatilia uhalali wa eneo la shirika hilo.

**4.12Kwa kuwa** madeni ya wazabuni, wakandarasi, mifuko ya jamii, wakulima wa mahindi yamekuwa yakilipwa kwa kusua sua na Serikali na kupelekea kafilisika na mifuko kushindwa kuijendesha na kulipa mafao kwa wakati,

**Hivyo basi** Serikali ianze kulipa madeni haya haraka yaliyofikia shilingi **trillioni 3.6** na kuleta Mpango Mkakati utakaonyesha jinsi madeni haya yatakavyolipwa kabla ya Bunge la Bajeti la Mwaka wa Fedha 2015/2016.

#### SEHEMU YA TANO

##### 5.0 SHUKRANI NA HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapenda kuwashukuru mawaziri wote ambao wizara zao zinasimamiwa na Kamati yangu Waziri wa Fedha na Uchumi, Waziri wa Viwanda na Biashara, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwezeshaji na Uwekezaji), Naibu Mawaziri wote katika Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Biashara. Makatibu Wakuu wa Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Biashara na Ofisi ya Waziri Mkuu.

4 FEBRUARI, 2015

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda pia kuwashukuru wataalamu wa Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Biashara na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuwa tayari kutoa ufanuzi na kupokea maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati yangu wakati wote wa mjadala ya Kamati Ni matarajio ya Kamati kuwa ushirikiano huu utaendelea katika mwaka huu wa 2015.

**Mheshimiwa Spika**, shukrani za pekee ziende kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Kisesa kwa jinsi wanavyonyiunga mkono na mimi naendelea kuwaahidi kuwa sita pumzika hadi maendeleo ya kweli yapatikane Jimbo la Kisesa. Kwani ni heri Punda aumie lakini mzigo wa tajiri ufike.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara na mimi mwenyekiti wenu najivunia sana kuwa na Wajumbe walio mahiri waliobobea katika masuala ya uchumi biashara na fedha. Michango na ushauri wao utalisaidia taifa na nina washukuru sana.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Luhaga Joelson Mpina, Mb, Mwenyekiti
2. Mhe. Dunstun Luka Kitandula, Mb, M/Mwenyekiti
3. Mhe. Margareth Agness Mkanga, Mb, Mjumbe
4. Mhe. Aieshi Khalfan Hilary, Mb, Mjumbe
5. Mhe. Ester Lukago Minza Midimu, Mb, Mjumbe
6. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb, Mjumbe
7. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb, Mjumbe
8. Mhe. Joyce John Mukya, Mb, Mjumbe
9. Mhe. David Zakaria Kafulila, Mb, Mjumbe
10. Mhe. Shawana Bukhet Hassan, Mb, Mjumbe
11. Mhe. Said Mussa Zubeir, Mb, Mjumbe
12. Mhe. Vicky Pascal Kamata, Mb, Mjumbe
13. Mhe. Naomi Ami Mwakyoma Kaihula, Mb, Mjumbe

4 FEBRUARI, 2015

14. Mhe. Khatibu Said Haji, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Josephine Jonson Genzabuke, Mb	Mjumbe
17. Mhe. Eng. Habib Juma Mnyaa, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Mohamed Hamis Misanga , Mb	Mjumbe
19. Mhe. Dkt Terezya Luoga Huvisa, Mb	Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, naomba nikushukuru pia wewe binafsi, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kutupatia maelekezo na ushauri mbalimbali katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Ushauri na maelekezo yenu yameisaidia Kamati kufanikisha shughuli zake kwa ufanisi mkubwa. Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah kwa jinsi anavyoliwezesha Bunge na Kamati zake kutekeleza majukumu yake ya kikatiba.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini si kwa umuhimu napenda kuwashukuru Makatibu wa Kamati, Ndg. Angela Shekifu na Ndg. Rachel Nyega pamoja na msaidizi wao Ndg. Pauline Mavunde kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kujadili taarifa hii na hatimaye kuyakubali maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Luhaga Joelson Mpina (Mb).**

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UCHUMI,  
VIWANDA NA BIASHARA.**

4 Februari, 2015

4 FEBRUARI, 2015

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge nimepokea vikaratasi vingi vikiomba kuchangia asubuhi hii, wengine wako kwenye orodha na wengine wanataka kuchangia mapema, naomba kuwaarifu kwamba nimeikuta orodha mezani na kwa sababu ya muda wachangiaji asubuhi ya leo watakuwa wawili tu kwa sababu muda mwingi tumeitumia kwenye miongozo iliyokuwepo asubuhi. Kwa hiyo, mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Idd Mohammed Azzan, dakika kumi kumi.

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, lakini pia nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Wenyeviti ambao wamewasilisha Taarifa zao za Kamati wameziwasilisha vizuri sana na kwa umakini mkubwa. Nitachangia kidogo kwenye suala la Usalama wa Raia; kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP pamoja na watendaji wa Jeshi hilo, ninawapongeza lakini wakati huo niwape pole sana kwa yale ambayo yanatokea hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri itafikia mahali sasa tutafute Jeshi lingine la kulilinda Jeshi la Polisi kwa sababu utekaji unaoendelea wa Vituo vyta Polisi, uporaji wa silaha kwa kweli unasikitisha, lakini pia ni tishio kwa sababu hatujui dhamira ya hawa wanaochukua silaha, maana kama ingekuwa silaha zile labda ni mahindi tungesema wanakwenda kusonga ugali wale, lakini silaha zile kutumika kwake ni kuja kuua. Sasa sijui wanaozichukua wana lengo gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye taarifa ya Kamati wameeleza hali ya usalama wa nchi yetu, hali ya usalama wa raia na mali zao mimi niseme tu kuwa wamesema ni nzuri, lakini kwa mtazamo wangu ni kwamba hali ya usalama wa raia na mali zao kwa sasa siyo nzuri, ni hali ambayo inatisha na inahitajika kazi ya ziada sana kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanaendelea kuishi salama wao na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Vituo Vidogo vyta Polisi mitaani na vilijengwa makusudi kwa ajili ya kupambana na

4 FEBRUARI, 2015

uhalifu mdogo mdogo ambao unatokea mtaani, lakini hivi sasa ninapoongea vituo hivyo vimefungwa katika Jimbo langu na nafikiri katika Jiji la Dar es Salaam, lakini kwa hali inayojitokeza ya vituo kuvamiwa na majambazi na kuporwa silaha sioni qjabu vituo hivyo kufungwa, lakini hivi tunawaweka wapi wale wananchi sasa ambao walikuwa wanatarajia kuwa kuwepo kwa vituo vile kungesaidia usalama wao. Sasa vile vituo vimefungwa na askari hawapo, kwa hiyo, uhalifu umezidi kiasi kwamba hata askari wanaogopa wahalifu, sasa wanaamua kuondoka na kurudi kwenye maeneo ambayo watakuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wananchi tunawaachaje huko mtaani, magenge ya kihuni ambayo yamejitokeza, wizi na uhalifu ambao unaendelea, vinatisha sana. Juzi tulitishiwa kidogo tu hapa Panya Road lakini miliona Mji ulivyoharibika na askari wamefanya kazi yao, wamekamatwa watu zaidi ya 1,000, sijui wanajua wao lakini niseme hali ile siyo nzuri. Kuwa na makundi ya namna hii ambayo yanaendelea kushamiri siku lilikuja tishio likaukumba Mkoa mzima wa Dar es Salaam, lakini tishio la Panya Road liko mtaani, kila siku wanafanya hizo kazi, lakini askari ama kwa uchache wao, ama kwa kukosa vitendea kazi wanashindwa kudhibiti hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa moto unaoteketeza unaanza na cheche sasa ili kuzuai moto usiteketeze unazima ile cheche sasa kwa hali ambayo imejitokeza hivi sasa ni kwamba tunakoelekea siyo kuzuri na ndiyo maana nasema hali ya usalama kwa wananchi na mali zao viko hatarini. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, wizi wa kutumia pikipiki ni kawaida siku hizi Dar es Salaam, watu kuporwa mtaani ni kawaida na watu sasa wameshazoea kuwa huku kuporwa labda ni kitu cha kawaida kwa hiyo, mtu unaona taabu kwenda kuripoti Polisi kwa sababu hata ukienda Polisi sasa hupati msaada wowote. Kwa hiyo, imekuwa mtaani huku ni mazoea. Nayasema haya kwa bahati nzuri naishi mtaani, nyie wenzangu mnaishi maeneo ambayo mna ulinzi na mambo

4 FEBRUARI, 2015

mengine, lakini hku mtaani hali siyo shwari. Kwa hiyo, tuombe Jeshi la Polisi sijui mnajipangaje, lakini niliwahi kusema na narudia kusema tena, kama hatuwezi kuajiri askari wa kutosha katika Jeshi la Polisi, tukawapa vitendea kazi Polisi, wakatengenezewa mazingira bora ikiwa ni pamoja na nyumba zao za kuishi vituoni pale, ulinzi au usalama kwa raia wetu utakuwa ni hatari sana huko tunakokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ilivyo hivi sasa kwa sababu na Polisi wenyewe nao wameshakuwa wanaogopa kwa sababu na wao wanaporwa, niliwahi kusema na narudia tena tuyaodbe Majeshi mengine ya Ulinzi ya nchi yetu yalisaidie Jeshi la Polisi. Kama tuliweza kutumia Majeshi, tukatumia vyombo vyao Ulinzi na Usalama mwaka jana kama sikosei kupambana na majangiri, vilungana vyote vikafanya hiyo kazi, leo tunashindwa nini kutumia vyombo hivyo kupambana na wahalifu hawa ambao wamekithiri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo dhambi kuwatumia Wanajeshi wa Jeshi la Wananchi, au kuwatumia askari wa JKT washirikiane na Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba tunawalinda wananchi wetu. Inatia kichefuchefu sana eti wanajeshi wetu wako nchi za nje wanalinda amani ya huko, wanalinda usalama wa raia wa huko na tunasifiwa sana kwa kazi hiyo, lakini ndani ya nchi yetu wananchi wetu wanaumia, wananchi wetu wanaporwa, wanapigwa, wanaauawa kila kukicha utasikia mahali fulani mtu kachinjwa, mtu kanyongwa, mtu kaibiwa, magari yanasmamishwa yanaporwa, ni vitu ambavyo hatukuvizoea huko nyuma, lakini hivi sasa vimekithiri na kwa kweli kunahitajika kazi ya ziada ili kuweza kuvikomesha mapema kabisa kabla hayajatokea maafa makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za jirani tunaona ni jinsi gani zinasumbuliwa na haya makundi ya kihuni yaani Al-Shabab, sijui Boko Haram na mambo mengine kama hayo. Tanzania siyo Kisiwa hayo yanayofanyika huko yanaweza kuja kwetu, Mungu apishie mbali, hizi silaha zinazoibowiwa katika Vituo vyetu vyao Polisi zinaashiria kwamba tunakokwenda siko.

4 FEBRUARI, 2015

Kwa hiyo, kama hatukuchukua hatua za haraka hivi sasa kwa kweli tunakwenda mahali ambapo siyo salama, nimezungumza sana suala la kuboresha maslahi ya askari pamoja na nyumba zao na vitendea kazi. Hivi juzi watu wameporwa barabara hii ya Morogoro - Dodoma gari zimesimamishwa usiku na zimeporwa, lakini askari yuko Dumila au Gairo je anakujaje pale katikati? Kituoni gari hakuna na kama lipo hilo gari basi ni bovu na kama siyo bovu basi halina mafuta, hivi kweli tutakabiliana na majambazi kweli kwa uhalifu unaoendelea namna hii? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusidanaganyane humu ndani kuwa hali huko nje ni shwari, hali siyo shwari, ni lazima tuweke mikakati ya ziada kuhakikisha kwamba usalama wa raia wetu unaimarika, mali zao zinalindwa ili tuweze kuendelea kuishi kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majeshi haya hasa JKT wapo vijana wengii wako kambini kule, wakitoka kwenye kilimo ni wachache lakini walio wengi wapo, ni kwa nini tuisiwtumie, tunaona shida gani kuwatumia hao? Waziri wa Ulinzi upo, Mheshimiwa Chikawe upo, waombe Ulinzi wakusaidie, siyo suala la kukaa na kusema Jeshi Kimataifa haliruhusiwi kulinda, haya yako wapi? Mbona tunaona askari nchi nyingine wamevaa magwanda ya Kijeshi na wanalinda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kabisa kama kweli tunahitaji kudumisha amani ya nchi yetu tuendelee kuhakikisha kwamba usalama wa raia unaendelea kupatikana, makunai haya yanayojitokeza hivi sasa tuweze kuyadhibiti mapema kabisa kwa sababu kuyaachia ni kuendelea kuyalea ili baadaye yawe makubwa, kama ukishindwa kuyazuia yanapoanza huwezi kuyazuia yatakapokuwa yamekomaa .

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningegusia labda ni hotuba ya Mwenyekiti wa Viwanda na Biashara. Amezungumzia masuala ya riba kwenye Mabenki, nami naomba niliseme hili watu wetu ama mahali popote pale wanachi ili waendelee ni lazima wakope, lakini kwetu

4 FEBRUARI, 2015

sisi kwenda kukopa unakopa kwa sababu huna budi riba ni za ajabu mno. Niliwahi kusema hapa siku moja kuwa ni kwa nini kusiwe na uelekezi kutoka Hazina kuwa labda riba ziwe na ukomo mahali fulani kuliko kuwaachia wafanye wanavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenyewe mabenki wanajisifia kila baada ya mwaka, wanatoa hesabu zao na takwimu zao za mabilioni ya faida waliyoyapata kutokana na kuwanyonya wengine. Kwa hiyo, tungeweka bei elekezi au riba elekezi kwamba jamani riba hizi zisizidi 20% au 18%, lakini hivi sasa utakuta kuna benki zinatoza riba mpaka ya 25%. Sasa kwa sababu una shida na huna budi kujiingiza hapo na mwisho wa siku unaweza kushindwa kulipa au ukashindwa kuendelea na hiyo biashara unayoifanya kutokana na hiyo riba kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. (Makofij)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Azzan. Mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Rosweeter Kasikila na mchana tukirudi tutaanza na Mheshimiwa Khatib Said Haji.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nitakwenda kuchangia kuhusu Kamati ya Viwanda na Biashara. Katika Kamati yetu, Kamati ya TAMISEMI tukizunguka huko tumekuta kuna maeneo ambayo mazao yanazalishwa kwa wingi, mazao ya samaki, mahindi na mazao mengine kama ufuta na alizeti, lakini sisi tukaona kwamba, wananchi wanapokuwa wanalima mazao kama haya, ingekuwa ni vizuri kama wangekiwa na viwanda vya kuweza kusindika. Mfano mdogo tu, Mkoa wa Rukwa wanalima sana mahindi, wanalima sana alizeti, wanalima ngano lakini kwasababu hawajapatiwa viwanda basi unakuta mazao kama hayo yanajiozea bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua tatizo ni kwa sababu gani viwanda havijengwi, ni kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti na upungufu wa pesa. Kwa hiyo, natoa wito wangu kwa

4 FEBRUARI, 2015

Serikali, hebu wafanye utafiti juu ya vyanzo vya mapato, vyanzo vipyta lakini na vyanzo vya zamani ili Halmashauri zetu ziweze kukusanya pesa ambazo zinaweza kusaidia hasa watakapokuwa wamewasilisha Hazina ili Hazina iweze kutoa hizo fedha na viwanda vikajengwa hata kama ni viwanda vidogo vidogo kuliko wananchi kuwa wamebaki na mazao ambayo yanajiozea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zimekuwa na kilio kikubwa sana kwamba pesa zinazokusanywa hawapati wanapokuwa wameomba na hata wakiomba zinapelekwa kwa uchache mno, lakini ukiangalia pesa hazipelekwi, kwa sababu Hazina nao wanasema kuwa hawawasilishiwi pesa za kutosha. Kwa hiyo, natoa rai kwa Serikali hasa Wizara ya fedha kwamba wangefanya mpango wa kutuma hata Tume kwenda kuzisaidia Halmashauri ni namna gani ya kuangalia vyanzo vya mapato vile vya zamani vikaboreshwa ili vikaweza kutoa fedha za kutosha, lakini kuwepo na vyanzo vipyta ili pesa ziweze kupatikana, ziweze kuwasilishwa Hazina, lakini pia ziweze kurudishwa Halmashauri kwa muda ambao wanakuwa wameuomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika usanyaji wa mapato imeonekana kwamba ukusanyaji na uwasilishwaji haufanyiki kwa nidhamu. Kwa hiyo, natoa rai kuwa makusanyo ya mapato yafanyike kwa nidhamu, lakini yaweze kuwasilishwa Hazina pia kwa nidhamu na siyo kuwasilishwa tu, lakini hata katika matumizi tuweze kufanya matumizi ya fedha zetu kwa nidhamu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya kwa nidhamu zaidi, tutaweza kujenga viwanda ambavyo vinaweza kuwasaidia wananchi kuliko kuangalia tu wawe wanalima mazao ya ufuta, mafuta wanatengeneza kwa kusuasua hivyo hivyo lakini pengine hayatengenezwi hata katika ubora unaotakiwa. Wapo wafugaji ambaao wanafuga ng'ombe na wanazalisha maziwa lakini utakuta hawana mahali pa kupeleka maziwa yanaharibika kwa sababu hatuna viwanda vya kuweza kusindika maziwa badala yake tunategemea maziwa kutoka Afrika ya Kusini na nchi jirani.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai yangu kwamba, Serikali jjitahidi ili fedha ziweze kupatikana na fedha hizi ziweze kutumika kadri inavyotakiwa. Tumekuwa tukishuhudia Wabunge wakitoa sifa sana kwamba tulitembelea Malyasia, Singapore, China, wapi na tumekuta hivi na hivi ni kwa sababu wenzetu wale wanafanya makusanyo yao na matumizi ya fedha kwa nidhamu, kunakuwa na uadilifu wa hali ya juu, kila mtu anajiona kwamba ana wajibu, yuko *responsible* na *committed* kujenga nchi. Haiwezekani tukawaachia watu wachache wakawa ndiyo wamejikita katika kuleta maendeleo ya nchi na maendeleo ya nchi hayaletwi na mtu mmoja, kila mmoja ni lazima awajibike kwa nafasi aliopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia tu kwamba tunapokuwa tumeponga mipango yetu kwamba tutajenga viwanda basi zile fedha zinazotengwa kwa ajili ya kujenga viwanda zijengewe viwanda bila ya kufanya *reallocation* ambazo mara nyingine zinakuwa ziyo za maana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *reallocation* zinakuwa ni nyingi mno na matokeo yake sasa inakuwa hazi-reflect na mipango tunayopanga kwa sababu ninavyojuu mipango inapokuwa imepangwa ni kwa sababu vipaumbele vinakuwa vimeshachaguliwa na kuwekwa. Sasa kama vipaumbele vimetambuliwa vikawekwa na kuwekewa bajeti basi ile pesa ambayo inayokuwa *released* iwe ni own source au ni ya wafadhili, inabidi pesa hizo zitekeleze kazi ambayo ilikuwa imetengewa, kuliko kuhamisha mafungu, fungu hili linahamishiwa sehemu nyingine ambayo tulikuwa hatujapangia inakuwa kama vile hatuna uhakika na mipango yetu, hatuna uhakika na kazi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa ufupi tu nataka pesa zinapokuwa *released* zifanye kazi ile ambayo imepangiwa, lakini na viporo vyta miradi navyo vinakuwa ni vingi mno. Kwa hiyo, natoa rai kwamba kabla hatujabuni miradi mipy, inabidi tuangalie sana miradi ya zamani ili tuweze kuimalizia na ndipo tuanze kushughulikia miradi mipy.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa Viwanda na Biashara, nakumbushia tu kwamba Wizara husika na Serikali kwa ujumla, waangalie nchi yetu ina mapato mengi ambayo yangeweza kufanyiwa kazi na nchi yetu ikawa imeendelea; tusindike vyakula, tuweze kula wenywewe, lakini na vingine tuweze kuuza nchi za nje ili kuinua kipato chetu kipato ambacho kitatusaidia katika maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Rosweeter. Sasa nitataja majina matatu ili wajiandae kuchangia mchana, nilitaja Mheshimiwa Khatib Said Haji, wa pili atakuwa ni Mheshimiwa Naomi Kaihula, wa tatu atakuwa ni Mhandisi Hamad Masauni. Kwa hiyo, hao wajiandae kuchangia mchana na orodha itaendelea.

Waheshimiwa Wabunge sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(Saa 6.55 Mchana Bunge *lilisitishwa hadi saa 11.00 Jioni*)

(Saa 11.00 Jioni Bunge *lilirudia*)

Hapa Mwenyekiti (*Mhe. Mussa Zungu Azzan*) Alikalia Kiti

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea! Naona kuna majina ambayo yameandikwa kuanza mchana. Mheshimiwa Khatib Said Haji!

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na leo nikaweza kuwa mchangiaji hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nikushukuru wewe binafsi, kwa jinsi unavyoliendesha Bunge letu hili vizuri, hakika busara zako zinatawala na tunajisikia raha.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema, kwanza kabisa nieleze masikitiko yangu sana kutohana na majibu ya wiki iliyopita ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, wakati nilipouliza suala juu ya kujengwa Kiwanda cha Machungwa Tanga na jibu alilolitoa hapa Bungeni, ambalo ni jibu liliwakatisha tamaa sana watu wetu wa Tanga wa kulima machangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliuliza swali kwa kujuu kwamba kuna ahadi ya Waziri Mkuu juu ya watu wa Tanga kupatiwa kiwanda cha kukamulia machungwa. Kuna ahadi ya Rais pia, bahati nzuri sana, Wabunge wa Mkoa wa Tanga wote kwa muda tofauti wamekuwa wakilizungumzia suala hili, lakini juzi kwa bahati mbaya sana, Mheshimiwa Naibu Waziri katika kujibu swali lile, alisema wazi kama machungwa ya Tanga hayana ubora. Jambo hili limewasikitisha sana watu wa Tanga, wakulima wa Mkoa wa Tanga ambao wengi sana wanategemea machungwa yale kuendeshea maisha yao. Limewafanya wamekuwa na mawazo tofauti tofauti kwa kujuu kauli ile imetolewa na Waziri wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitegemea sana Mheshimiwa Waziri kwa kutambua umuhimu wake, jambo hili baada ya kusema machungwa ya Tanga hayana ubora kwa sababu yana mbegu nyingi, yeye ni Wizara husika wa Mambo ya Viwanda ilikuwa atueleze njia mbadala ya nini wananchi wale wafanye? Mbegu gani bora Serikali imewaletea watu wale? Badala yake ilikuwa ni jibu la mkato tu kwamba machungwa ya Tanga hayana ubora, maana yake hayafai kwa juisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kitu kimewasikitisha sana watu wa Tanga, na ninavyokwambia watu wa Tanga wanasi kiliza, wanangojea busara za Waziri, ambaye ni Waziri namwamini. Hebu leo naomba tafadhalii liweke sawa jambo hili. Wakulima wale wa Tanga, wajue mustakabali wa kilimo kile cha machungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge wa Muheza, Mheshimiwa Herbert Mntangi, alifuatilia masuala haya,

4 FEBRUARI, 2015

amefika Ujerumani na Wajerumani kwa kujuu suala la matatizo kidogo, uhatifu wa machungwa yale pengine, wakamshauri kupanda mbegu ambazo ni pungufu wa zile mbegu nydingi, lakini matokeo yake, jitihada zile zimekuwa zikifanywa na Mbunge yule na ninapokwambia, tayari Tanga yamelimwa machungwa mengi sana, mbegu ile ya vallesia kutoka Ujerumani, lakini jitihada za Wizara kuhakikisha wananchi wale wa Tanga wanaendeleza vipi kilimo cha machungwa na Serikali inawasaidiaje, inakuwa ni jambo ambalo Waziri anajibu kwa mkato tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la kusikitisha zaidi, machungwa haya ya Tanga, Waziri anayosema kwamba hayana ubora, ndiyo machungwa ambayo Wakikuyu kila siku wanasafirisha kwa maroli, wanapeleka Kenya, wanasindika juisi ile na kuipeleka nje kuongeza ajira huko, sisi tumekaa hapa Waziri anakuja anajibu tu suala la mkato, machungwa hayana ubora, inasikitisha sana kuwa na Waziri wa namna hii.

Mheshimiwa Waziri, Ndugu yangu Dkt. Kigoda tafadhali wewe ni Mkulima mionganii mwao watu wa Tanga. hebu tafadhali leo nyoosha maneno hapa, angalau wakulima wetu wapate moyo na waondokane na majibu ambayo ameyatoa Mheshimiwa Waziri Janeth Mende, lakini sishangai sana. Kwa majibu ya namna ile, kwa baadhi ya Mawaziri imekuwa ni mazoea sana. Wala sishangai, kwamba Waziri huyu aligombea nafasi ya Uenyekiti wa Kitongoji, ama Kijiji akakosa, lakini kwa Serikali yeye ni Waziri. Kwa hivyo, sishangai na yanayotokea, naujua uwezo wake. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba uweke sawa mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, nataka kuzungumzia suala la Kiwanda cha Tanga *Fresh* na mgogoro ambao Kabati umeueleza humu. Mheshimiwa tumekuwa tukifuatilia suala hili la kuona kwamba ni namna gani hii Taasisi ya ushindani wa kibashara jinsi ilivyoliendesha jambo hili. Tunajua ushindani mkubwa wa biashara hii ya maziwa, majirani zetu Kenya, hawapendi kuona maziwa ya Tanga *Fresh* yanajaa katika ma-super market na ma-mall.

4 FEBRUARI, 2015

Kwa hivyo, ushindani unaweza kusababisha watu hapa wakajipenyeza kiujanja, wakazitumia Taasisi zetu ili kuhakikisha kiwanda kile ambacho kinategemea na wafugaji zaidi ya elfu nane katika Mkoa wa Tanga, watu wanafanya jitihada za makusudi kuona kiwanda kile hakiendelei. Haiwezekani Kamati imeona na imejiridhisha kwamba, kiwanda ambacho wanaambiwa Tanga Fresh walinunua, ni kiwanda ambacho kilikuwa kimefungwa zaidi ya miaka mitatu, ama minne mbele, lakini FCC wanakuja kusema wameua ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushindani na marehemu ni ushindani gani? Ushindani na Kiwanda ambacho kimekuwa? Leo mnakuja kusema tumejiridhisha? Taasisi inasema kwamba tulipokea taarifa. Hatuwezi kwenda kwa taarifa za kupokea. Tunataka mfanye usahihi, na Mheshimiwa Waziri bado imani na wewe tunayo, chukua maamuzi sahihi kunusuru wakulima wale ambao ni kiwanda pekee cha Tanga kwa sasa ndiyo wanakitegemea.

Mheshimiwa Waziri Tanga, hivi ndiyo ulikuwa Mji wa historia wa viwanda, lakini leo vyote vimekuwa. Kulikuwa kuna Kiwanda cha Mbuni, kulikuwa na Kiwanda cha Mbolea, kulikuwa kuna Kiwanda cha Foma, kulikuwa na Kiwanda cha Blanketi, kulikuwa na Kiwanda cha Mboni *plastic!* Hivi vyote vilikuwa ni viwanda. Mji wa Tanga, ulikuwa ni Mji wa viwanda. Leo cha ajabu hapa tunakuja kuambiwa kiwanda cha juisi Tanga hakitajengwa kwa sababu bora Msoga, kwa sababu kule machungwa ni kidogo. Msoga hata mlimao hakuna, lakini unaambiwa kiwanda kile kihame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila kizuri Tanga hakifai. Bandari Tanga haijengwi, ingawa ahadi ya Serikali ipo. Sababu nini bandari ya Bagamoyo. Kiwanda hicho kinahama kinakuja Msoga, Tanga hakuna machungwa yenye viwango. Kila kizuri cha Tanga, barabara ile ya kutoka Tanga, Pangani mpaka Bagamoyo nayo pia imekuwa ni ahadi hewa. Yote hayo hayafanyiki, lakini ukiuliza inakwenda! Neema, keki ya Taifa lazima tupate wote. Tuangalie Tanga ilivyokuwa Mji wa Viwanda, lakini sasa jinsi Mji ule unavyozidi kufukarika.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Waziri wangu, tafadhalii sana, ingilia kati suala hili bado wananchi wa Tanga wana imani, hata mimi mwenyewe nina imani na wewe, tunakupa mashauri yetu yasikilize! Yafanyie kazi, kwa maendeleo ya Tanga ambapo na wewe ni mwenyeji wa Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja na suala la tatu, suala la usalama wa uraia. Nimesoma ripoti jinsi Kamati ilivyoelezea namna ya usalama wa uraia ulivyo. Tunaweza tukazungumza kwenye makaratasijuu ya usalama wa uraia. Lakini Polisi wetu, Wanajeshi hawa wa Jeshi la Polisi, jinsi sasa hivi wanavyochukulia maamuzi mazito juu ya raia wetu. Wanavyotumia nguvu kupita kiasi, katika masuala ambayo hawakupaswa kufanya hivyo, inasikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tukio lilitokea, nampa pole sana Mwenyekiti wangu wa Chama kwa yaliyomfika, lakini namwomba asife moyo. Kila tone moja la damu la mwana CUF linalomwagika, ni hatua moja mbele ya ukombozi wa nchi hii na naamini tutashinda. Naamini Mungu anaiona haki iko wapi, naamini ipo siku tutashinda. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kama Jeshi la Polisi na weledi unaofundishwa, wanamchukua mtuhumiwa kutoka kwenye gari. Mtuhumiwa anapofika kwenye gari, amejifungia, maana yake huyo mtuhumiwa tayari amesalim amri. Unamtoa kwenye gari kwa kipigo, unamwingiza kwenye gari na kumsindikiza kwa kipigo na mpaka tayari mtuhumiwa yupo ndani ya gari, bado unaendelea na kipigo. Hivi ni amri nani? Mwendawazimu gani mtuhumiwa wameshamkamata, wamemweka kwenye gari wanaendelea kumpiga kwa silaha yoyote? Wengine spana wanapiga, kile walichonacho! Lakini mimi sishangai, kauli ya piga ina asili yake na ilitokea hapa Bungeni.

Kwa hivyo, *inshallah* ipo siku! Mwenyezi Mungu atashusha hukumu, kwa yule atakayetoo amri kwa watu wapigwe pasipo na hatia. Naamini Mwenyezi Mungu ni mkubwa na anaiona dhuluma inayotendeka ndani ya nchi

4 FEBRUARI, 2015

hii. Tutaendelea kuwa dhaifu, kwa sababu leo hii, vyama vya upinzani tunapotoa ratiba tunafanya maandamano inakuwa hilo ni nongwa! Ni nongwa kabisa!

Tarehe 27, Januari mimi naiambia Serikali hii, kwamba tutaendelea kufanya kumbukumbu kwa sababu waliouawa kule Zanzibar ni watu wala sio paka! Kwa hiyo, vyombo vya Intelijensia yenu, mnasema intelijensia inatuambia wakifanya maandamano kutakuwa na uvunjifu wa amani. Intelijensia yenu inashindwa kujua vituo vya Polisi lini vitavamia na silaha zitachukuliwa. Inteligensia gani hiyo? Intelijensia ya kuwaonea watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Kinana anaweza kwenda nchi hii, akipita barabarani kwa bahati mbaya akamkuta mwendawazimu kavaa shati la kijani na yeye akajua yule ni mwana CCM, basi anaweza kumwita, akamfukuzia na maandamano ya CCM yakaanza hapo. Wala hawaaulizwi! Huyo huyo, basi hayo ni maandamano ya CCM na watatembea wanavyotaka. Tunasema mlileta sheria ya Vyama vya Siasa, mfumo wa Vyama Vingi kuwa haki itendeke kwa vyama vyote. Mlichokifanya ni kitendo ambacho kimetusikitisha sana na Mheshimiwa Waziri wangu nakuheshimu sana, lakini kauli uliyotoa hapa, Watanzania imewasikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na jana Mheshimiwa Rais ameendelea kupigilia msumari wa mwisho. Gazeti hapa nimelisoma, anasema Kikwete anakichua siri ya kipigo cha Lipumba. Siri ni kwamba anasema, hawafuati sheria! Sheria gani inayofuatwa upande mmoja? Sheria gani? Kama mnafuata sheria! Leo Tanga intelijensia imeshindwa kujua. Madiwani wa Tanga wanashindwa kukutana, kwa sababu tu Diwani mmoja wa CUF ametoka kwa hiari yake amekwenda CCM, analazimisha kuingia vikao vya Halmashauri, hali ya kuwa yeye alijitoa kwa hashuo lake mwenyewe. Kama aliahidiwa kulipwa na hakulipwa, hayo ni yake.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Diwani yule suala limefika hapa Bungeni kwa Waziri Mkuu, imeshindikana kuchukuliwa hatua. Diwani yule amefanya Halmashauri mpaka sasa, huyu hapa ni Diwani wa Tanga, Halmashauri haijapitisha bajeti, hakuna kinachoendelea Tanga. Hawapati akidi kwa sababu Wabunge wa CUF hawaingii mle. Kosa ni mtu ambaye amejitoa kwa hiari yake kwenye Chama cha Wananchi CUF, amekwenda CCM lakini mnalazimisha awe Diwani. Nawaambia na nawaambia Madiwani wa Tanga, Mheshimiwa Amina, yule bwana fuateni falsafa ya Waziri Mkuu. Kama yeye ni mkaidi analazimisha kuingia mle ndani, apigwe tu! Mpigeni tu! Ndiyo fuateni falsafa. (Makofij)

Analazimisha, yeye amejiagua na amejiengua mwenyewe. Ametoka kwenye chama kwa hiari yake, yeye analazimisha kuingia kwenye vikao. Serikali ipo, intelijensia ipo, kila kitu kinawezekana, lakini analazimisha kuingia mle. Amesimamisha maendeleo, Halmashauri ya Tanga haifanyi chochote! Diwani huyu hapa hakuna kikao kinaendelea kwa sababu ya yule mpuunzi mmoja yule, analazimisha kuingia kwenye vikao hali ya kujua ameacha Chama kwa hiari yake mwenyewe. Kwa hivyo, nasema apigwe na atapigwa tu kwa sababu anakitafuata kusudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusema kwamba, yote yanayotokana na matukio haya ni kwamba, sheria ya nchi hii inaelemea upande mmoja. Sheria hii inaelemea kwa upande wa Vyama vya Siasa vya Upinzani, lakini nyinyi mnahaki ya kufanya chochote mnachokitaka. Leo suala dogo kama hilo la Tanga, mabomu pale yameshawahi kupigwa Halmashauri, kwa suala la Diwani huyu. Taarifa hizi zimefika hapa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Magdalena Sakaya alimuuliza, lakini bado mnashindwa kuchukua hatua. Intelijensia imelala, imelala! Lakini hapo Lipumba atoke kwenye gari mbili intelijensia itafanya kazi na atakwenda kupata kichapo. Nawaambia hivi, siku yenu ipo bwanagutu, itawafikia, utakuja kugeuka upepo, mtakuja lia! Ahsanteni sana. (Makofij)

4 FEBRUARI, 2015

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Naomi.

**MHE. NAOMI A. M. KAIHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia katika Bunge letu hili Tukufu. Kwanza kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunipa afya njema mpaka wakati huu karibu Bunge linakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizungumze mambo mawili hasa, lakini kubwa napenda nizungumze kwamba, kwa kweli napenda niwapongeze Ndugu zangu wa Upinzani na hasa Chama changu cha CHADEMA, kwa kufanya kazi nzuri sana. Kwa kufanya kazi ambayo walitumwa na wananchi kuja kuifanya, kwamba, hata ile kauli yangu ya mwanzo niliyosema kuna mapepo, kwa kweli nafikiri mapepo yamepungua. Yamepungua kwa sababu unakuta kwamba sasa hivi kumekuwa na kuelewa kwamba, wanaoisimamia Serikali wakitaka Serikali iende sawasawa, inakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona Mawaziri wetu walivyongatuka. Kwa kweli wamefanya kazi nzuri na niwaambie kabisa tunamshukuru Mungu kwa kuinua Chama kama CHADEMA, kwa sababu kutokana na mambo haya, hatujui kama mpaka sasa uchumi wetu ungekuwa wapi? Sijui nchi ingekuwa imeuzwa yote, lakini Mungu akainua Vyama vya Upinzani na sasa mpaka ikawa UKAWA na vinafanya kazi nzuri. Nasema hivi kwa sababu kukaa kwangu katika Kamati hii ya Uchumi, Viwanda na Biashara, nimeona mambo ya ajabu kabisa ambayo, hata mtoto mdogo hawezi kuelewa yaani nchi hii inafanyaje kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Serikali yetu ambayo tunaisimamia, ambayo inapaswa kutekeleza mambo ambayo yamepangwa humu humu Bungeni. Inavyofanya mambo sivyo! Niwape mfano mdogo tu, unakuta kwamba hii Wizara ya Viwanda, Biashara na Uchumi, ni nyeti pengine hata kilimo, kwa sababu gani? Kwa sababu hii inatoa majawabu ya matatizo makubwa mengi ambayo

4 FEBRUARI, 2015

yanaikabili nchi yetu. Kwa mfano, tatizo hili kubwa la vijana kukosa kazi mpaka wakatokea panya road na wengineo. Kama viwanda na biashara, vingekuwa vinatendewa haki na kupewa kipaumbele, kwa kweli mambo haya yasingetokea; kwa sababu, kule kuna uwekezaji, biashara na kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda sijui viwango ni huko huko, lakini unakuta kwamba, viwango wanalalamika hawakupewa watu wa kutosha wa kufanya kazi. Kwa hiyo, mipaka inaingiliwa, kila kitu kinaingiliwa, kwa hiyo, Watanzania wanalishwa vitu *substandard*, lakini Serikali hii ninayoisema ikisimamiwa na CCM zaidi, haioni kama hiki kitu ni cha kipaumbele kiweze kuruhusu wale waweze kutoa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hivyo tu, lakini ukija pia kwenye viwanda vyenyewe. Viwanda vyote vilivyokufa, mpaka sasa sijui kiwanda kimoja ama viwili ndiyo vimefufuka. Sasa unashangaa! Hivi tunashindwa nini kufufua hivyo viwanda ili viweze kutoa ajira ya kutosha ya kuridhisha vijana wetu, lakini tunakwenda kwenye mambo ya kuiweka Polisi, Majeshi na nini! Ndiyo tunawapa vitu vingi kusudi wawapige Wapinzani, hii ni haki kweli? Unakuta kwamba ooh wameleta mawashawasha, sijui kwa kutayarisha kwa ajili ya Uchaguzi ujao!

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani hivyo sio vipaumbele! Hayo mabilioni mnayopeleka kwenye magari ya kupiga Wapinzani, tungepeleka huko kwenye viwanda ambako vingeweza vingefufuliwa. Halafu kitu kingine ninachowaambia, nafikiri ni Mungu tu. CCM mnachimba shimo lenu, kubwa lefu hawesi kutoka, kwa sababu gani? Kadri mnavyofanya vitu ambavyo sivyo ambavyo wananchi vinawafaidia, mnachimba shimo refu la kujizika wenyewe. Niwaambie! Kwa mfano, kuna Kiwanda hiki cha Urafiki, Urafiki ni kiwanda mama! Kiwanda hiki kweli Wachina ni marafiki zetu, lakini nafikiri, kufikia hapa tulipofikia, tunapaswa pia tuangalie upya, urafiki wetu na tunapofanya Mikataba na watu ambaa tunafikiri ni rafiki zetu.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wamechukua dola milioni 27! Zimetumika bila sababu, lakini kila tunapotaka kuchunguza, Serikali inapata kigugumizi. Hili suala tumeleta mpaka humu Bungeni, kwamba hawa jamaa watueleze matumizi ya dola 27, ambazo zipo equivalent to almost 48 billion za Kitanzania, lakini hakuna kitu kinachotendeka. Kwa kweli leo tunaomba hiki kitu kifanyike. Lundwe Tume ya kuchunguza ieleze na hapa hapa nimekumbuka tena jambo lingine, ambalo nawaambia CCM mnajichimbia shimo refu sana la kufa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunafurahi! Kufa kufaana! Wewe ukifanya vibaya sisi tunaendelea! Kwa sababu kama mngekuwa mna-solve mambo kama hayo, nchi hii isingekuwa hivyo! Si hilo tu, kuna mambo mengine ambayo yanatendeka ambayo ni kinyume kabisa cha sheria. Kwa mfano, kiwanda cha Urafiki ni kiwanda mama, ambacho kingekuwa kina promote pia uzalishaji wa pamba. Kwa sababu, kama kungekuwa na hicho kiwanda yale madhumuni yake ilikuwa ni kutengeneza nyuzi! Ingekuwa inafanya vitu vingi ambavyo vingekuwa vina-absorb pamba za wananchi, kwa hiyo kungekuwa na soko la wakulima, hivyo, tusingekuwa tunababaishana hapa, sijui nini na nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa angalia matokeo yake, ni kwamba kwa sababu tumeua viwanda vyetu vya ndani, MUTEX, MWATEX vyote! Tunapaswa tuagize nguo kutoka nje, hata uniform za Majeshi inabidi tuziagize zote, vitu hivi vilikuwa vinatengenezwa hapa na Marehemu Baba wa Taifa alifanya vizuri sana. Niwaambie ndugu zangu wa CCM hata vile vitu ambavyo ni misingi ambayo iliwekwa na ninyi wenyewe na Baba wa Taifa na yenyewe mmeua kuna mambo mabaya sana mengi ambayo yanaendelea, lakini nimependa nizungumzie hilo, naomba myachukue na myafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kuna mwenzangu Mheshimiwa Kafulila nimempa dakika tano. (Makof)

4 FEBRUARI, 2015

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kwanza kabisa niwapongeze hawa ambao wameteuliwa kushika nafasi za wale waliotoka, na Watanzania huu ni ujumbe kwamba hakuna Serikali duniani ambayo inashindana na Bunge. Bunge likiamua, haipo Serikali ambayo inaweza ikakabiliana na nguvu ya Bunge. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, nina mambo machache kabisa ambayo ningependa kuyazungumza. Jambo la kwanza, kazi ya Bunge ni kutunga sheria. Mwaka 2010 Bunge hili lilitunga Sheria ya Madini na Sheria ya Mawasiliano ya mwaka 2010. Zote kimsingi zilikuwa zikielekeza kampuni za simu na migodi iorodheshwe kwenye masoko ya mitaji ya Tanzania kwa lengo la kuhakikisha kwamba hesabu zao zitakuwa wazi ili kusudi mapato na matumizi yafahamike, ili kusudi Serikali itoze kodi sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu kwamba tangu mwaka 2010 Bunge lilipotunga sheria hiyo, kampuni za simu na migodi ya madini Tanzania imegoma, imeikatalia Serikali isitunge kanuni za kuhakikisha kwamba sheria hiyo inatekelezwa. Hii ni aibu kabisa! Na Mawaziri wake wako humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka mitano Wizara ya Nishati na Madini imeshindwa kutengeneza Kanuni za kuhakikisha migodi inaorodheshwa kwenye soko la mitaji ili kusudi tupate kodi sahihi. Miaka mitano, Wizara ya Mawasiliano imeshindwa kutengeneza kanuni za kuhakikisha kampuni za simu ambazo zinavuna mabilioni ya shilingi ziorodheshwe kwenye soko la mitaji ili kusudi hesabu zake ziwe wazi na Serikali ipate kodi sahihi. Tumeshindwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni za simu leo, kwa mfano, Vodacom na Shivaicom, Mheshimiwa Silinde alizungumza juzi hapa, wana mgogoro wa kutengeneza vocha fake zenyet thamani ya takribani dola milioni 350, zaidi ya shilingi bilioni 500. Serikali inaulizwa juzi hapa Bungeni, inasema kwamba huo ni mgogoro wa wafanyabiashara wawili tu yenye haihusiki kitu.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *factor* ya kodi, kuna kodi, lakini pili zile vocha zilikuwa za shilingi mia tano na elfu moja moja ambazo nyingi zinatumwiwa na maskini, vocha nyingi fake zilikuwa za mia tano na elfu moja moja. Bilioni 500 ni pesa nyingi. Sasa Serikali hii dhaifu inashindwa kudhibiti kodi hiyo, inabaki kila siku kukusanya kodi kwa wafanyakazi, Serikali hii inabaki kutegemea kodi ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasoma ripoti ya mwaka jana ya *Global Tax Comparison* (Ulinganisho wa Kodi Duniani), Tanzania ni nchi ambayo wafanyakazi wanatozwa kodi kubwa kuliko nchi zote za Afrika Mashariki, wastani ni asilimia 18 na wakati Rwanda ni asilimia 6.8, Burundi ni asilimia 10.3, Uganda ni asilimia 11, Rwanda ni asilia 5.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania asilimia 18 kuna kodi kubwa sana ambayo wafanyakazi wanatozwa. Lakini hii ni kwa sababu migodi, kampuni kubwa hamzitozi kodi, mnaleta bajeti za njaa, njaa hapa kwa sababu nyie ni dhaifu wa kukusanya kodi kwa wenyefedha. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mfano mwepesi tu hapa juzi, kampuni za *Cement Tanzania* zimekuwa zikilalamika kwamba kuna uingizaji haramu wa *cement* kutoka nje, wakaongea mpaka na Waziri wa Viwanda na Biashara, lakini nashangaa kwamba Waziri hakuchukua hatua yoyote. Viwanda vya *cement* vinataka kufa kwa sababu kuna *cement* nyingi inaagizwa kutoka nje bila utaratibu.

(Hapa kengele ililia kuashiria muda kuisha)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kafulila dakika zako tano zimekwisha. Sasa namuita Mheshimiwa Opulukwa.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia, lakini nitajikita zaidi kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, amani ya taifa hili ni amani inayoweza kuletwa na Watanzania wote. Watanzania wote tukiwemo sisi wanasiasa tulimo humu ndani na waliopo nje. Kwa hiyo, kazi ya ulinzi na usalama wa taifa ni kazi ya Watanzania wote walio ndani ya mipaka ikiwezekana na nje ya mipaka ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza vijana wote wa CHADEMA Mkoa wa Shinyanga, Wilaya ya Solwa, vijana zaidi ya 4,600 waliohitimu mafunzo ya FTP 200 (*Fast Track Program*), ni mafunzo ambayo yanawasaidia vijana wetu kuweza kujifunza jinsi ya kulinda mali za chama, lakini wakaongeza na *component* nyingine ambayo ilikuwa ni masuala ya Ulinzi Shirikishi na Polisi Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana, alialikwa RPC wa Shinyanga kwa ajili ya kwenda kutoa mada ya Ulinzi Shirikishi na Polisi Jamii, hakuweza kwenda na sijui kwa nini hakwenda, lakini ilikuwa ni kwa nia njema.

Nilikuwa napenda kuwashauri hawa askari wetu wasipende kwenda tu kwenye wito wa Chama Cha Mapinduzi, wajaribu kwenda hata maeneo ambayo ni Wapinzani kwa ajili ya nia njema ya ulinzi wa taifa hili ambalo wote tunalitakia nia njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee sasa masuala ya Meatu. Mnamo tarehe 4 Mwezi uliopita kulikuwa na uchaguzi mdogo kwenye Jimbo la Meatu katika Kijiji kinaitwa Mwambiti. Katika uchaguzi huu yalitokea mambo mengi ya kihuni yakifanywa na wafuasi wa Chama Cha Mapinduzi ambao walijulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ya tarehe 4 kuna mwananchi mmoja anaitwa Lucas Ntinga alipigwa kichwani kwa rungu pamoja na nondo. Kijana huyu baada ya kuwa ameishafanyiwa kitendo hiki alipoteza fahamu, akapelekwa hospitali akalazwa, lakini baada ya kupata nafuu alikwenda kufungua charge Polisi ya kushitaki kwamba ametendewa unyama na mtu ambaye anamfahamu.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tarehe hiyo hiyo kuna Ndugu Nchola Ng'ocha yeye alitekwa na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi ndani ya gari ya Chama Cha Mapinduzi, wakamuingiza mle ndani, wakampiga sana, wakamkung'uta sana na baadaye wakaenda wakamtelekeza kwenye Kituo cha Polisi. Kijana huyu baada ya kuwa na hali mbaya alikwenda hospitali, amelazwa kwa muda wa siku kama nne alipotoka akafungua malalamiko Polisi akawatajaa walioshughulika na mambo haya lakini kwa bahati mbaya hawa watu mpaka tunavyoongea hivi hawajawahi kupelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna dada anaitwa Biria Justina, alipigwa sana siku ya uchaguzi na wana-CCM na akavuliwa nguo, alikuwa amevaa blouse upande wa juu akavuliwa nguo zote barabarani kila mtu anaona asubuhi ya saa moja. Kitendo hiki kiliwasikitisha watu wengi na hakuna aliyefurahishwa na kitendo kama hiki, na mama huyu baadaye alikwenda kutoa taarifa Polisi pale Meatu, lakini kwa bahati mbaya OC CID ameshindwa kupeleka kesi Mahakamani wakati mama ana ushahidi wa kutosha pamoja na kwamba ameishatoa taarifa pale Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kijana mmoja alikatwa mkono anaitwa Nchora Gambago, kijana huyu alipigwa na vijana anaowafahamu wamempiga wakamvunja mkono, baada ya kuvunjwa mkono akapelekwa hospitali ya Wilaya, amefika amelazwa kama zaidi ya wiki nzima, ule mkono baada ya kuonekana kwamba hauna mafanikio mazuri, OC CID akishirikiana na Mkurugenzi wameenda wamemfukuza yule mgonjwa, akatoka kwenye hospitali ile, amekwenda kutibiwa kwenye hospitali ya private ya Kolandoto eti kwa sababu akiendelea kukaa pale hospitali wale watu watakosa dhamana wataendelea kushikiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo kama tusipoweza kuyadhibiti yanaweza kulipeleka taifa mahali ambapo ni pabaya sana. Haya ninayoyazungumza yapo katika karatasi hizi ambazo nimeziandaa, naomba kuziweka mezani, watu wote waliofanyiwa unyama huu, naomba

4 FEBRUARI, 2015

Jeshi la Polisi, bahati nzuri niliongea na RPC, nimeongea na IGP, nimeongea na Waziri, naomba watu hawa wanasubiri kusikia kauli sasa ya Waziri leo hapa Bungeni ili kuweza kujuu hatma ya watu waliofanya haya mambo, wanashughulikiwa kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hii, kuna kijana mmoja alitishiwa kupigwa na mwingine alitishiwa kuuwawa kwa maneno, wamekwenda kutoa taarifa Polisi, lakini OC CID amekwenda Polisi baada ya ile kesi kuwa imeishakwenda Mahakamani ameenda ku-withdraw ile kesi bila kushirikisha watu ambao walikuwa ni walalamikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi ile imeondolewa, kwa taarifa niliyonayo hapa ya *proceedings* za Mahakama, imeondolewa kwa maelezo ya kwamba kama kesi itaendelea kuwepo Mahakamani kwa sababu aliyefanya kitendo hiki cha kutishia kuua pamoja na kuponda gari la mwananchi anaitwa Zakaria Magembe, eti atadhalilisha Chama, kwa hiyo, ni bora kesi iondolewe kuliko Chama Cha Mapinduzi kushitakiwa na kudhalilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo kama haya yakiendelea kufanyika, wananchi watachoka, wataamua sasa kuanza kuchukua sheria mikononi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 26 Desemba, kuna mwananchi mmoja ambaye ni Mtaturu aliuawa. Aliuwawa mnamo tarehe 26 Desemba saa saba mchana na maaskari wa Game ya Mwiba, huyu mwananchi baada ya kuuwawa akachukuliwa akapelekwa hospitali. Baada ya kufanyika *postmortem* ikaonekana kwamba yule mwananchi alipigwa risasi akiwa anakimbia, lakini maelezo yalivyobadilishwa na OC CID kwamba eti alipigwa risasi kwa sababu alionekana alikuwa ankwenda kumshambulia huyu mtu aliyekuwa na silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba, Waziri angalau kuweza kulifuatilia hili kwa sababu watu wanauwawa, watu wanaonewa, hakuna kinachofanya kazi

4 FEBRUARI, 2015

ili angalau watu hawa waweze kuishi kwa amani katika nchi yao. Tukiachia mambo haya yakaendelea, watu wakazidi kuumia kila siku, itafikia pahala sasa watu wakichoka watakuwa wanachukua sheria mikononi wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sina zaidi, naomba Waziri nimeishampa taarifa basi angalau aweze kulichukulia hili suala serious ili watu waweze kupata haki yao na wasiendelee kuonewa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Masauni.

**MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu ama taarifa hii ya Kamati yetu ya Mambo ya Nje ukiangalia ukurasa wa sita inazungumzia kazi ambazo zilipangwa kutekelezwa na Kamati, na mimi nikiwa ni mionganini mwa Wajumbe wa Kamati hii, moja kati ya kazi ambazo tulizifanya kwa umakini mkubwa sana ni ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo kuhakikisha kwamba michakato ya ununuzi wa majengo ya ofisi za Balozi nje ya nchi inafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichukue fursa hii kwanza kabisa kuipongeza sana Kamati yetu kwa kazi nzuri sana ambayo tumeifanya kuhakikisha kwamba tunafuatilia utekelezaji wa sera ya Mambo ya Nje hususani katika hili suala la kuhakikisha kwamba ofisi zetu za Balozi zilizopo nje zinakuwa na majengo yake, hasa hili tukio ambalo limetokea hivi karibuni katika wiki iliyopita ambapo Mheshimiwa Rais alizindua jengo lile la ofisi ya Balozi kule Paris, Ufaransa. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera hii ya ununuzi wa majengo ya ofisi ya Balozi ina tija kubwa sana. Ukichukulia mfano hili jengo la Balozi lililopo Ufaransa, mbali ya kwamba

4 FEBRUARI, 2015

nchi yetu imepata heshima kubwa sana kuwa na jengo lake wenyewe la aina kama ile katika moja ya mataifa makubwa duniani, lakini pia imeweza kuongeza thamani na idadi ya mali zisizohamishika za nchi yetu nje ya nchi. Lakini kubwa zaidi ni kwamba sasa hivi ule mzigo wa kodi ambao Taifa lilikuwa linabeba kulipia kodi kwenye Balozi hii, sasa hautakuwepo tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewahi kunong'ona na Naibu Waziri juzi nikamwuliza kwamba, hizi *Euro* takribani milioni 22 zilizotumika kwa ajili ya ununuzi wa jengo lile pengine inaweza ikawa *equivalent* na kodi ya miaka mingapi, akaniambia pengine inaweza ikawa miaka kumi mpaka kumi na tano. Sasa tafsiri yake ni kwamba baada ya miaka kumi au kumi na tano ni kwamba sasa ule mzigo wa kodi ambazo wananchi walikuwa wanaubeba kulipia Balozi hii sasa hivi fedha zile zitatumika kwa shughuli nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna changamoto mbalimbali zimejitokeza katika kutekeleza kazi nzuri; moja ni ucheleweshaji wa fedha ambazo zimeishaidhinishwa. Changamoto hii na nyinginezo pamoja na faida zake ambazo nimezungumza na nyingine sijazungumza zipo nyingi sana, zote hizi zinahitaji kuangalia uwezekano wa kujipanga vizuri zaidi ili kuhakikisha kwamba kasi hii inaongezeka mara mbili zaidi kama sio mara tatu au mara nne au mara mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja ambalo mimi nilikuwa nashauri sana na kulisisitiza ni Serikali ihakikishe kwamba inawasilisha kwenye Kamati ili tuupitie upya ule mpango kazi wa miaka 15 ambapo unaainisha vipaumbele na programu ya utekelezaji wa shughuli hii kwa maeneo yote yaliyobakia.

Najua kuna kazi imeshaanza kufanyika, Washington, New York, sasa hivi kuna uendelezaji wa viwanja pale Nairobi. Lakini ni vizuri ule mpango tukaupitia kwa sababu baada ya kuupitia ule mpango tutaweza kuuchangia pamoja vipaumbele na programu ya utekelezaji wake, lakini pia vyanzo vya fedha. Kulikuwa kuna utaratibu ambao ulibuniwa

4 FEBRUARI, 2015

sijui umeishia wapi wa kutumia hizi taasisi za mifuko yetu ya hifadhi za jamii ikiwemo NSSF. Sasa naomba maelezo ya kina kuhusiana na ni kipi kilichokwamisha mchakato huu usiendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya majengo ya ofisi zetu za Balozi zilizopo nje ya nchi ni mbaya sana na zinasikitisha na kwa maana hiyo kazi nzuri na kubwa hii ambayo imefanyika ya kununua majengo mapya, baada ya miaka siyo mingi sana mejengo yetu yatakuwa yamechakaa na itakuwa kuna kazi kubwa sana ya kuyafanya matengenezo, hii inatokana na sababu kubwa mbili, kwanza, utamaduni na mipango bado haijawa mizuri ya kuhakikisha kwamba tunafanya matengenezo ya majengo yetu yaliyopo nje.

Kwa hiyo, nataka nitoe wito kwa Serikali kuhakikisha kwamba inakuja na mkakati kabambe wa kuanzisha kitengo maalum Wizarani, kutafuta watalaam waliobobea katika fani hii ambaao watashughulikia masuala haya ili kuepusha athari zaidi huko baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuchangia leo hii ni suala la changamoto zilizobainika kwenye Kamati katika utekelezaji wa dhana ya diplomasia ya Kibunge hasa kwa Wawakilishi wa Bunge letu hili katika maeneo matatu makubwa. Eneo la kwanza ni Uwakilishi wa Bunge la Afrika Mashariki, SADC PF pia, lakini tatu ni Bunge la Afrika.

Mimi naomba njikite kidogo katika hili Bunge la Afrika na hapa na-declare interest kwamba mimi ni mmoja katika ya Wabunge ambaao tunawakilisha nchi yetu kwenye Bunge la Afrika, lakini kuna jambo moja linatuhuzunisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vision na madhumuni ya kuanzisha Bunge la Afrika tokea wakati huo tangia ile Abuja Treaty mwaka 1991 ambapo ilianzishwa ile African Community ilikuwa ni kuhakikisha kwamba inaunganisha wananchi wa Bara la Afrika kupitia wawakilishi wao waliowachagua wenywewe na siyo kuunganisha Bara la Afrika

4 FEBRUARI, 2015

kupitia viongozi labda Marais, Mawaziri ama nchi, lakini ni kuwaunganisha kupitia wananchi wao. Dhana hii naona sasa viongozi wetu hawa kwa kweli wanatuvunja moyo sana, wanatusononesha sana, sioni kabisa kwamba wana dhamira hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sana kumekuwa kuna changamoto mbalimbali ambazo zilikuwa zimejitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya Bunge la Afrika kufikia azma hiyo, lakini ni juzi tu kupitia ile wanaita itifaki ambayo inaitwa *Constitutive Act of African Union Led to Pan African Parliament*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itifaki imezungumzia kwa kina mambo mengi ya msingi ambayo kama yamenganyiwa kazi na kama ingeridhiwa itifaki hii, basi leo changamoto katika Bunge la Afrika zingekuwa zimepunguzwa kwa kiwango kikubwa sana, ikiwemo namna ya kupata ushiriki na utaratibu wa kupata Wabunge, namna ya kuongeza idadi ya wanawake katika Bunge hili, namna ya kuweza kuandaa bajeti ya PAP, lakini kubwa zaidi ni kulipa meno Bunge la Afrika lisiwe ni Bunge tu la kushauri, lakini kulipa ile *legislative power*. Lakini kwa mazingira inavyoonekana haionekani dhamira hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba leo hii Serikali itueleze kwamba Je, Tanzania maana kama Tanzania haina dhamira hiyo tujue na wengine vilevile na wao wachukue jitihada gani kuwashawishi kama wao wanao dhamira hiyo. Mbona Bunge la Europe limeweza, leo mchango mkubwa mbao unatolewa katika maendeleo ya Umoja wa Ulaya yanatokana na mchango mkubwa wa Bunge la Ulaya na kwa sababu wao walifanikiwa kuli-transform Bunge la Ulaya kutoka kuwa ni chombo cha kushauri tu kuweza kukipa nguvu za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka nichangie ni suala la Itifaki ya Umoja wa Fedha ambayo tuliridhia hapa siku ya tarehe 5 Julai, 2014. Tumesikia vilevile kama ambavyo ripoti ya Kamati inaeleza kwamba

4 FEBRUARI, 2015

*Instrument of Ratification* imeishawasilishwa, lakini kitu ambacho kinatushangaza sana, ni kwamba leo hii tunaambiwa Rwanda na Tanzania ndyo nchi pekee ambazo zimeridhia, hasa tunaambiwa hapa kipindi cha nyuma kwamba kuna ile mikutano ya viongozi wanajiita *Coalition of the Willing* na moja katika sababu zake ni kwamba sisi tunaenda kidogo kidogo. Sasa leo hii sisi tumeharakisha, wengine wanachelewa. Nasikia pia *road map* na *task force* imeishaanzishwa.

Sasa, nataka tu nipate maelezo ni kwa nini. Je, kuna mahusiano gani katika uhaulishwaji wa hili jambo kwa nchi hizi nyingine na huo muungano wao usiyo rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho kutokana na muda, nilitaka kulizungumzia kwa haraka haraka ni suala la mkataba wa kuanzishwa mtengamano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakavyokumbuka kwamba takribani miezi miwili au chini ya hapo ijayo tunatarajia kuipitisha kwa kishindo sana Katiba yetu Iliyopendekezwa whether UKAWA watakubali au hawakubali, lakini tunachotarajia kwamba itapita kwa kishindo na itakuwa na tija sana kwa mustakabali wa nchi yetu. (*Makofii*)

Moja kati ya mambo ambayo katika Katiba hii nzuri Iliyopendekezwa imeyazungumza ni kuweza kuliondosha suala la Ushirikiano wa Kimataifa kwamba Zanzibar sasa iweze kufanya hiyo shughuli yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni ipi, ni kwamba tukitumia fursa nzuri ya mabadiliko ya Katiba hii Iliyopendekezwa kuna faida kubwa sana kama Taifa tunaweza tukazipata; moja, kama tutaweza kuona kwamba huu mkataba wa kuanzishwa mtengamano utaipa fursa ya Zanzibar kuingia kama nchi, inaipa Tanzania nguvu ya kisiasa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. (*Makofii*)

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nataka nijue tu kwamba je, kwa hali ilivyo sasa hivi mkataba huu unatoa fursa hiyo, na

4 FEBRUARI, 2015

kama haupo ni nini ambacho kinaweza kufanyika kwa haraka sana ku-review huu mkataba ili kuweza kutoa fursa kwa Zanzibar iingie kwa kuwa Zanzibar ina mamlaka ya baadhi ya mambo katika kuendesha yenyewe iweze kuingia kama nchi kwa faida ya mustakabali wa Jamhuri ya Muungano nzima kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu yalikuwa ni hayo, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Ahsante sana kwa kunisikiliza. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsant. Sasa namuita Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed!

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Kwanza, nilitaka tu Kiti chako na wenzangu Wabunge tusaidiane, nivyofahamu Bunge huwa linapitisha sheria, mapato na matumizi na vile vile huwa linapitisha maazimio na huridhia mikataba na kadhalika. Lakini, katika process tunayoendelea nayo sasa hivi na Kamati hizi, naona Bunge sasa litakuwa lina kama kushauri tu. Sasa, sina hakika kama Kanuni nilizozikuta za Mabunge mengi na hapa kama kuna mabadiliko haya ningependa tupate ufanuzi. Kwa sababu nafahamu Kamati zinapoleta mapendekezo, ni wajibu Wabunge sasa kutoa azimio kwa mapendekezo ambayo yameletwa na Kamati.

Sasa, nitataka ufanuzi wa hilo baadaye mtusaidie Kiti chenu kama ni sahihi hili tunalolifanya kutohana na tradition ambayo tumeizoea kwamba Kamati inaleta mapendekezo na Bunge ndiyo linatoa maazimio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nishukuru sana Kamati zote ambazo zimefanya kazi nzuri na wananchi wa Tanzania wamefaidika sana kuona Kamati zetu zinafanya kazi vizuri na hasa ukiangalia kwa Mabunge ambayo tunayozoea kwenda mara nyingi ni Kamati za PAC ndizo zinazofanya kazi vizuri, lakini Kamati zetu zote za Bunge ziko very active

4 FEBRUARI, 2015

na zimefanya kazi nzuri sana. Naomba kuwapongeza Wajumbe wote wa Kamati mbalimbali na hasa kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ambazo wamefanya kazi kwa kina sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, niishukuru sana Kamati ya Fedha na Uchumi kwa kuja na kitu kinachoitwa *Microfinance Act*. Mimi ni Mjumbe wa Bunge la IPU na niko kwenye Kamati ya Maendeleo, Fedha na Biashara. Moja ambalo tulilizungumza sana ni namna gani hawa wajasiriamali wapya wanaweza kupata mitaji. Tukawa na Wajumbe toka *World Bank* na mabenki makubwa yote duniani, wakieleza kwamba mabenki kwa kweli hayawez  
ku-take risk kwa wafanyabiashara wapya, huo ndiyo utaratibu upo popote duniani. Serikali nyingi ambazo zingetaka kuwakomboa watu wake wamepitia katika hizi *Microfinance Projects*.

Kwa hiyo, ningeomba Serikali pamoja na kwamba imeshindwa mpaka sasa kuleta, basi tuihimize Kamati yetu ilete hii *Microfinance Act* ili iwasaidie wajasiriamali wetu waweze kuingia katika mkondo huu wa kibiashara na waweze kuendelea na biashara zao. Bila ya kufanya hivyo hatuwezi kupambana na umaskini hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili sambamba na hilo ni suala zima la ulinzi wa viwanda vyetu. Kwa bahati mbaya Tanzania toka mwaka 2003 tulipopitisha ile Sera ya Viwanda hatujakaa kitako kuifanya *review* tena mpaka leo. Ulinzi wa viwanda vyetu umekuwa hafifu sana. Viwanda vingi sasa hivi vina uwezo mkubwa wa kuzalisha, lakini kutokana na ushindani usio sahihi, usio halali wa watu wanaoleta bidhaa mbalimbali hasa hizi bidhaa *fake (dumping goods)* imekuwa ni tatizo kwa viwanda vingi kuzalisha. Hivi sasa sina hakika kama Serikali ina habari, kuna Wachina kama 20 wako Mikocheni, wanaleta bidhaa kubwa kubwa nyingi, hawalipi kodi hata senti tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya *products* wanazoleta ni *trailers* hizi ambazo zinazalishwa Tanzania na

4 FEBRUARI, 2015

tuna uwezo wa kuzizalisha na zikatosheleza, wanakuja wanaleta hapa halafu wanaunganisha, wanaauza kwa watu whole sale, wanaondoka, hawalipi kodi hata senti tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasema hakuna sera ya kulinda viwanda vyetu! Tatizo hili litaendelea na kila likiendelea ajira katika nchi itakuwa inapotea kila siku. Kwa hiyo, la kwanza naiomba sana Serikali ni lazima tuwe na sera ya kulinda viwanda vyetu. Tunatumia kodi wakati mwingine, lakini kodi na usimamizi ndiyo peke yake itasaidia kulinda viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda China kuwekeza hivi sasa, kama huna dola laki moja kwanza ukai-deposit kwa muda wa miezi sita bila ya kuigusa, huruhusuwi kufanya biashara. Wachina wamefika hapa mpaka wanachoma mahindi. Yale mahindi tunayochoma barabarani na wao wanachoma mahindi! Sasa nasema hakuna mwekezaji wa aina hiyo ambaye atasaidia uchumi wa nchi ukakua. Ningombaa sana Serikali hili ilisimamie, ionekane kwamba kwa kweli tunavilinda viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo viwanda kama wanaotengeneza trailers wako karibu sasa hivi watafunga viwanda na ajira sio chini ya watu 500/600 watakosa kazi. Sasa kama viwanda hatuvilindi ajira haiongezeki, tatizo la ajira litaendelea kuwepo katika nchi yetu. Hili lilikuwa ni jambo moja ambalo nilitaka niliseme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu katika hili la viwanda, viwanda vyetu vingi vinategemea sana malighafi na malighafi zetu zote ni za kilimo. Inasikitisha leo kwamba tuna tani milioni 6 za uzalishaji wa nafaka mbalimbali. Mahindi, badala ya kuuza unga, tunauza mahindi yenyewe. Nasema huu ni udhaifu mkubwa sana kwamba hatuvezi hata ku-process mahindi tukapata unga, let alone ku-process mahindi tukapata mafuta. Haya nasema ni matatizo ya msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama agriculture produce tunazotoa haziwezi zikaingia kwenye viwanda, hatuvezi

4 FEBRUARI, 2015

tuka-create ajira, hatuwezi tuka-add value kwa wakulima wetu na wakapata bei nzuri ya mazao yao. Haya ni mambo ambayo yamesemwa kila wakati, tunayarudia, lakini hatujaona vitendo vya kufanyika pamoja na kwamba iko kwenye 2025 Vision lakini bado utekelezaji umekuwa ni dhaifu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningeomba kusema ni kwamba, tunashukuru sana vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama, wamefanya kazi kubwa sana. Nchi yetu imebarikiwa kwa amani, tunaendelea na amani vizuri sana. Lakini, ningependa tujitahidi sana kujenga mahusiano na wananchi. Mahusiano na maelewano ni jambo ambalo litasaidia sana kudumisha amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo katika Afrika kuna vikundi vya kigaidi visivyopungua 13. Tuna bahati Tanzania tumebak katika amani. Lakini ni vizuri amani hii tutailinda tu kama tutakuwa na mahusiano na maingiliano vizuri na pale watu wanapovunja heria basi wanaelezwa vizuri. Ziko taratibu za kufuata bila ya kutumia excess force. Hili ni jambo la msingi sana lazima tujitahidi kulitumia sana, kwa sababu kila unapotumia nguvu zaidi ndivyo hivyo hivyo mnavyoshawishi watu kufanya uhalifu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini liko tatizo la msingi ambalo nafikiri lazima tuliangalie kwamba, sasa hivi tumefika mahala raia wengi wanachukua sheria mikoni mwao, lakini hata vyombo vya dola navyo vingine vinachukua sheria mikononi mwake. Sasa hii siyo hali nzuri sana. Ningeomba both sides tukae tuone ni vipi tunaweza kuzuia raia wasichukue sheria mikononi mwao, lakini na vyombo navyo vile vile visichukue sheria mikononi mwao, hapo ndiyo tutapata uwiano mzuri, tutafanya kazi vizuri na nchi yetu itaweza kubaki katika amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tano ni suala zima la Afrika Mashariki. Nashukuru sana nimesoma taarifa, naona kazi inafanyika vizuri. Lakini inasikitisha kuona mgogoro wa Wabunge wetu ndani ya Bunge la Afrika Mashariki. Inasikitisha

4 FEBRUARI, 2015

sana, kwamba mwaka mmoja na nusu hakuna kinachoendelea katika Bunge lile. Watu wanakwenda na kurudi na kulumbana, hakuna kitu chochote kinachoendelea.

Mheshimia Mwenyekiti, sisi kama Watanzania tunafaidika nini na Wabunge wetu tuliowapeleka katika Bunge la Afrika Mashariki wakati wanajiingiza katika mgogoro ambaeo hauleti matunda kwa Taifa letu?

Kwa hiyo, ningeomba kwamba kwanza sasa hivi tu-harmonize zile taratibu za kupatikana kwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Hamuwezi kuwa na Wabunge Bunge la Kenya linachagua kwa utaratibu wake, Tanzania utaratibu wake. Tu-harmonize kwanza ile *election process*. Lakini pia tufike mahalatusiangalie watu katika vyama katika hili jambo. Hizi Jumuia hizi unapopeleka watu dhaifu, mnaumia sana katika nchi. Watu hawa-take *interest* kufanya kazi katika taasisi kubwa kubwa kama hizi. Nchi inaumia sana, watu wanaenda kulumbana badala ya kuangalia maslahi ya nchi. Kuna mitakaba, kuna ajira katika Afrika Mashariki, kuna vitu vingi tu ambavyo tunataka kuvijadili. Lakini watu wanapoteza muda mwaka mmoja na nusu hawafanyi kazi. Fedha ya umma inatembea, hawatembeleri katika jimbo lao la uchaguzi, yaani wananchi wa Tanzania hajajui wana matatizo gani. Watu wanajiendea tu na sisi tunakaa tunachekelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba sana hili suala tuli-address, tunayempeleka kutuwakilisha afanye kazi ya kutuwakilisha.

Nashukuru sana kuna vijana akina Mheshimiwa Kafulila na Wajumbe wale tulionao kwenye IPU, tunafanya kazi mpaka saa tano za usiku, hatuna msaada wowote, wenyewe tu. Watu wana sekretarieti, wana kila kitu, lakini watu hawafanyi kazi. Mimi nasema inasikitisha sana, inasikitisha sana kabisa kabisa. Hebu let us be serious, tunapokwenda kuwawakilisha wenzetu katika taasisi mbalimbali kama hizi zinatumia fedha nyingi, lazima tuwe

4 FEBRUARI, 2015

serious, kama watu hawapo serious wapumzike majumbani, tuwape wengine ambao watafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho katika hili, tutafute watu ambao dunia ya leo ni dunia ya kibashara, ni dunia ya kiuchumi, usimpeleke mtu kisasa. Kuna mambo kule mengine yakizungumzwa hayafahamu. Lazima tukubali. Ukienda ukikaa na mtu wa kama wa Kenya amezoea mambo ya biashara na kadhalika, wewe mwenzangu unapiga siasa tu kila siku, haiwezekani ukaleta maendeleo katika nchi. Tutafute watu ambao wataweza kutuwakilisha na wakafanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka nimalizie kulizungumza ni suala la kuwapongeza sana Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Kule jimboni Wawi wamejenga shule na napenda kutoa taarifa wanafunzi wa darasa saba, Zanzibar nzima ile shule ya Jeshi la Wananchi ya Wawi pale imekuwa ya kwanza. Wamefanya kazi nzuri sana. Namwomba sana Mkuu wa Jeshi awasaidie wamalize darasa la tisa waingie na form one pale, sorry na vichuma vyao vya label ili waweze kuendelea vizuri. Nawashukuru sana kwa hiyo nzuri.

Mheshimiwa Spika, lakini waendelee sana kujitahidi kuishi karibu na majirani. Taasisi za ulinzi zinafanya kazi nzuri sana, lakini zitadumu na zitafanya vizuri kama zitaweza kuishi karibu na majirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kengele ya pili, nakushukuru sana. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kamata dakika tano!

**MHE. VICK P. KAMATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika tano sintazielewa kwa sababu nipo namba 11 kwenye orodha na niliomba tangu jana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vick Kamata...

4 FEBRUARI, 2015

**MHE. VICK P. KAMATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika 10 za kwangu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vick Kamata, kaa chini kwanza. Sasa hivi muda wetu wa Wabunge kuchangia umekwisha, nafanya hivi kama kukusaidia. Kama unafuata haki yako, basi utasubiri Bunge lingine.

**MHE. VICK P. KAMATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana, Mheshimiwa aliyemaliza kuchangia hakuwa kwenye orodha. Mimi niko kwenye orodha na hukunipa nafasi. Yeye amepewa dakika 10, huo ni upendeleo na siyo fair. Kama aliyеongea hapa hakuwa kwenye orodha umemwita, mimi niko kwenye orodha unanipa dakika tano, *it is not fair.* (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Margareth Mkanga.

**MHE. VICK P. KAMATA:** Mheshimiwa Mkanga dakika ngapi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vick Kamata hili ni Bunge!

**MHE. VICK P. KAMATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lazima haki itendeke. Mimi ni Mbunge kama Wabunge wengine.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vick Kamata kaa chini! Kaa chini Mheshimiwa Vick Kamata!

**MHE. VICK P. KAMATA:** Siwezi kukubali kukaa chini kwa kuonewa, niambie kwa nini nipewe dakika tano wengine wapewe dakika 10! Ukiniambia sababu nitaelewa! Nimesikia umemtaja Mheshimiwa Mkanga, hujamwambia dakika tano!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vick Kamata hebu kaa chini. Mimi hapa siongozi Bunge kwa namna ninavyotaka mimi au kwa namna unavyotaka wewe. Kuna orodha ya majina nimepwa, kuna orodha ambayo nimeambiwa

4 FEBRUARI, 2015

watachangia jioni, kuna orodha ya majina wengine pia hawatachangia. Kwa hiyo ni *discretion* ya Kiti. Kama una malalamiko, Kanuni ya 5(4), peleka kwa Spika na sijakuruhusu useme sasa hivi. Mheshimiwa Mkanga, dakika tano!

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kidogo kwa haya niliyonayo.

Kwanza, niwapongeze Wenyeviti wapya wa jana, lakini sana sana nishukuru nadhani Bunge kama siyo Serikali kwa TBC kuweka wataalam wa lugha ya alama ambao wanatafsiri pale mbele. Hii inanipa moyo kwamba wenzangu viziwi wanaelewa kinachoendelea humu ndani. Nalishukuru hili na liwe siyo tu hivi leo tu, aah tuendelee katika program zote namna hii ili wote tuweze kufahamu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda mimi nitazungumzia sana mambo ya Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara. Nianzie na sehemu ya masuala ya ukosefu, nchi kukosa kuwa na mfumo au sheria inayoweza kuelekeza sekta ndogo ya fedha iende endeje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa inapendeza, tuna SACCOS, tuna VICOBA tena vinaendeshwa kweli kweli na akina mama. Wanadunduliza senti zao ili waweze kujikomboa na ku-sort out mambo madogo madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumbuke kwa kuwaacha tu hivi wakifanya jinsi wanavyoendelea na hizi kazi, kunaweza kukawa na matatizo kama yale ya DECI.

Mimi nashauri na Kamati kama ilivyopendekeza kwamba Serikali iliekezwa sana mambo haya kwamba angalau tuwe na mfumo huu, lakini kutokana na hali halisi bado haifanya chochote. Kamati hii kwa juhud zake inaandaa Muswada ambao huo tukiupitisha utasaidia kuelekeza SACCOS na VICOBA, michezo ile ya kupeana ile tuindeshe vipi kusudi hata hizo pesa ziweze kusaidia kuongeza hata kipato cha Taifa kuliko sasa hivi jinsi kazi inavyofanyika.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba Serikali, basi Muswada ule upangwe mapema hata kama chini ya masuala ya dharura Bunge lijalo tuweze kuupitisha ili wananchi hawa waweze kufaidika na kuwa na mfumo unaoweza kueleweka ambao tuta-monitor pesa zao na kuhakikisha kwamba ziko salama kuliko kama ilivyotokea kwenye mambo *DEC* pesa zilipotea wala hatujui mpaka sasa hivi ule mfumo umeishia ishia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nilikuwa nauliza, hizi hati za kimila ambazo mabenki mpaka sasa hivi hayawezi kukubali, hivi mpango wa MKURABITA umeishia wapi? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Chiza, dakika tano!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa dakika zangu hizi tano. Sijui hata niseme nini?

Naomba niseme makubwa mawili; Moja, naomba niseme nimesikia hoja za Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia. Ninachowea kuaahidi kuanzia hoja zilizotangulia ni kwamba tutajenga utaratibu wa kufuatilia hoja zote zinazotolewa ili kila mwaka tunapokuja basi tuwe tuna maelezo ya kwamba nini na jinsi gani tumetekeleza yale yaliyokwishatangulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, kwa sasa kwa sababu mimi ndiyo nimefika Wizara hii ya Uwekezaji na Uwezeshaji, naomba niwaahidi mambo yafuatayo:- Nataka nianze na mambo kama matatu hivi: Jambo la kwanza ni kushirikiana na Serikali ili kutambua hati miliki za kimila za mashamba ya wakulima. Tutajitahidi kushirikiana na Hal mashauri na mamlaka zote na kushawishi benki hususan *TIB* na benki zote za Biashara ili angalau waweze kutambua hati miliki hizi za kimila ambazo ndiyo rasilimali walijonayo wakulima iwaweze kukopo.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka nilifanyie kazi ni kukaa na Halmashauri za Wilaya ili wahakikishe kwamba wanakubali kutenga asilimia 10, ile asilimia 5 kwa ajili ya wanawake na asilimia 5 kwa ajili ya vijana. Kazi yangu ni kuweka sera na kushawishi Wizara na taasisi zingine za kisekta kutekeleza mambo yote haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulifanya *immediately*, tarehe 9 mwezi huu, mimi na Naibu Waziri wa Kazi na Ajira, Mheshimiwa Makongoro Mahanga, tumekubaliana kwamba tutaanzia katika Jiji la Dar es Salaam, tutazungumza na viongozi wa wajasiriamali wote (maarufu kwa jina la machinga). Tuone mazingira gani wanayofanya kazi, na tutaongea pia na viongozi wa Serikali ili tuhakikishe kwamba hawa nao wanawekewa mazingira mazuri ya kufanya kazi badala ya hali waliyonayo sasa ya kutanga tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba nimalizie dakika tano hizi kwa kuelezea Kituo chetu cha Uwekezaji kimefanya nini hadi sasa. Naomba nianze kwa kushukuru Bunge kwamba tarehe 11 Novemba, lilipitisha Sheria ya Ubua Bainu ya Sekta ya Umma na Sekta ya Binafsi. Mimi naahidi kwamba kufika mwezi Machi, 2015, Kanuni za sheria hii zitakuwa zimekuwa tayari. Sasa kazi ambazo hadi sasa Kituo kimekwishafanya naomba mnisikilize:-

Kati ya 2005 mpaka 2014 jumla ya miradi 7,159 yenye thamani ya shilingi milioni 74,274 ambayo imetoa ajira 8,635 ilikuwa tayari imesajiliwa na TIC. Katika mwaka 2014 peke yake Kituo chetu cha TIC kimesajili miradi 698 yenye thamani milioni 11,871. Kati ya hiyo, miradi ya kilimo ilikuwa ni 33 yenye thamani ya milioni 211.11 ambayo imetoa ajira 13,373. Sekta ya Utalii imesajili miradi 109 yenye thamani ya dola milioni 294.7 ambayo imetoa ajira 5,436 na kati ya yote hiyo wawekezaji wa ndani walikuwa na miradi 328, miradi ya ubia baina ya sekta binafsi na umma ilikuwa 159 na miradi ya wawekezaji wa nje ilikuwa 211.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nataka kusisitiza tu kwamba, bila kuwekeza hatuwezi kufikia malengo haya ya kuweza kutoa ajira na kuongeza uchumi kwa Watanzania wetu. Nataka niwaahidi kwamba, tutajitahidi kuweka mazingira mazuri na hasa hasa mazingira mazuri ya uwezeshaji kwa makundi ya wale wanyonge, tukianzia na wakulima vijjini ambaao hawana fursa za kupata mikopo kutokana na masharti makubwa yanayowekwa na hasa na benki za biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nikijibu swali hapa Bugeni nilisema; nilikuwa najibu swali la Mheshimiwa mmoja hapa nikasema, yeye alitaka kujua walemavu ni wangapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kuahidi kwamba, tutarejea yale masharti tuhakikishe kwamba masharti yanawa-favour wanyonge waweze kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Dakika tano ni chache, nilikuwa na mengi yakusema, lakini nakushukuru sana. (*Makofi*)

#### **WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA**

**KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutoa shukrani kwa Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa ushirikiano ambaao wametupatia kwa kipindi cha mwaka 2014/2015. Pia, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambaao kwa namna moja au nyingine walitusaidia katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu hoja ambazo zimeibuliwa na Kamati ya Mambo ya Nje na Waheshimiwa, naomba kwanza kwa faida ya Bunge lako tukufu nitoe taarifa zifuatazo kwa Waheshimiwa Wabunge:-

Kwanza, hivi karibuni tulipokea msiba mkubwa wa Mfalme wa Saudi Arabia, mlinzi wa maeneo muhimu ya dini ya kiislamu na viongozi wengi duniani walikwenda na Mheshimiwa Rais Kikwete pia alijumuika na viongozi wa dunia kwenda kutoa pole tarehe 25 Januari. Naomba Bunge lako

4 FEBRUARI, 2015  
tukufu liunge mkono hilo kwamba tumefanya kazi hiyo ya  
kutoa pole kwa Saudi Arabia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, siku ya tarehe 28 Januari,  
mwaka huu, Mheshimiwa Jakaya Kikwete kama olivyosema  
Mheshimiwa Masauni, alifungua Ubalozi Mpya Paris, Ufaransa.  
Hii ni hatua kubwa katika utekelezaji wa Sera yetu ya Mambo  
ya Nje na tunatoa shukrani kwa Bunge kwa kutupatia Euro  
milioni 22 katika kipindi cha miaka miwili, ili kupata jengo  
hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, tarehe 21 Januari  
mwaka huu, Chama chetu Cha Mapinduzi kilifanya kazi  
kubwa ya kuunganisha makundi matatu ya Chama Cha SPLM  
cha Sudan na kukiunganisha ili kunyamazisha mapigano  
yanayoendelea Sudan. Napenda kuchukua nafasi hii kumpa  
pongezi za dhati Mheshimiwa John Samuel Malecela,  
ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Usuluhishi pamoja na  
Katibu Mkuu, Kinana ambaye amemsaidia Mwenyekiti  
kuifanya kazi hiyo nzuri. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Mkutano wa 24 wa  
Wakuu wa Nchi za Serikali na Umoja wa Afrika ulifanyika Adis  
Ababa kati ya tarehe 30 na 31 mwaka huu. Mambo mawili  
makubwa kwa Tanzania yametokea; la kwanza, Ukumbi wa  
Amani na Usalama wa Umoja wa Afrika kuanzia sasa utaitwa  
*The Julius Nyerere Centre ya Peace and Security* katika Bara  
la Afrika. Hiyo ni heshima kubwa sana kwa Tanzania kupewa  
jengo la Umoja wa Afrika linaloshughulikia amani na usalama  
kwa jina la Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage  
Nyerere. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili lilitotokea,  
tumempata Mtanzania, Profesa Tolly Mbvette, kuwa Rais wa  
Baraza la Chuo Kikuu cha Umoja wa Afrika (*The President of  
Pan African University*). Ushindani ulikuwa mkubwa, lakini  
Profesa Mbvette aliweza kuwa wa kwanza. Nachukua nafasi  
hii kwa niaba ya Watanzania wote kumpongeza Profesa  
Mbvette. (Makofij)

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, naomba sasa kwa ufupi kabisa niishukuru Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuibua hoja mbalimbali. Serikali iongeze kasi ya kushughulikia tatizo la hali mbaya ya majengo ya Balozi zetu, tunalizingatia na hatua zimeanza kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu ikama ya utumishi ubalozini ya maslahi ya watumishi hao ikiwa ni pamoja na makazi, usafiri na mazingira ya kazi viboreshw; Wizara inakubaliana kabisa na ushauri huu na tunaanza kuutekeleza.

Serikali ihakikishe kuwa fursa muhimu kwa manufaa ya Taifa kwa kutumia dhana ya diplomasia ya uchumi zinatumika vema; tumeanza hivyo na Serikali siku zote imekuwa inazingatia fursa zinazojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za kidiplomasia katika kushughulikia mgogoro wa mpaka kati ya Tanzania na Malawi; naomba kuwaarifu kwamba, siku ya tarehe 30 ya mwezi Januari, Mheshimiwa Rais Kikwete alikutana na Rais Peter Mutharika wa Malawi na kuweka mambo sawa pamoja na wasuluhishi na hivi sasa tunasubiri mkutano wa kuendeleza majadilano kati yetu na Malawi kwa hali ya utulivu na kwa amani, bila ya kutishana katika maana ya kutumia silaha kali. Tuna uhakika kwamba mazungumzo kati ya Tanzania na Malawi yatafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi zetu za Ubaloz duniani kote ziboreshw; hilo ndilo tuliloanza baada ya kutupa pesa kuanzia mwaka 2007 hadi hivi ninavyozungumza. Tunashukuru Bunge kwamba, kila mwaka tunapata pesa za maendeleo na tunazitumia kwa ajili ya kuboresha Balozi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa na takwimu sahihi za kina kuhusu Watanzania wanaoishi nje; ni sahihi kabisa. Hadi sasa tunajua kwa takwimu za Umoja wa Mataifa...

(Hapa kengele ililia)

4 FEBRUARI, 2015  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
(*Makofii*)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Na mimi nashukuru kupata fursa hii kuchangia hoja ambazo zimewasilishwa na Kamati, mbele yetu. Kwanza, naishukuru sana Kamati yetu ya Uchumi, Viwanda na Biashara kwa Taarifa iliyoleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda mimi maeneo mawili tu; la kwanza ni kuhusiana na riba kubwa ambayo katika benki na taasisi za fedha, yaani *interest rates* zinazotolewa. Kamati imeonesha *concern* kuhusiana na issue hii, lakini labda tungeweza tu kutoa ufanuzi ufuataao kwamba, kwa sasa kama tunavyojua Tanzania inafuata mfumo wa uchumi wa soko huria kwa hiyo, bei zote zikiwemo riba za mikopo zinaamuliwa na soko kutokana na ule utashi pamoja na ugavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile sekta yetu ya fedha bado ni change, pamoja basi na upungufu huu uliopo katika muundo, bado soko letu halijafikia hatua ya juu kabisa ya ufanisi katika kutoa riba hizo zinazoendana na utashi wa ugavi halisi.

Kwa mfano, kiwango cha riba kinatolewa kutokana na historia ya uaminifu ya wanaohitaji mikopo vilevile. Historia ya uaminifu tukubali kwamba, bado iko ndogo hapa kwetu; hii inasababisha kama tukiona mtu mmoja mmoja anakosa uaminifu katika kurejesha ile mikopo, basi *effect* yake inakuja kuwaathiri hata wale wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kweli, kama ilivyosemwa kwenye Kamati kwamba, kukosekana kwa dhamana, wengi wetu hatuna dhamana ya *collateral* hasa kwa wale wakopaji wadogo wadogo, lakini vilevile hizo dhamana zenyewe haziwezi kutumika kama ni dhamana kwa hiyo mikopo ambayo inachukuliwa.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine na la umuhimu ni kwamba, kumekuwa kuna ucheleweshwaji mkubwa wa kesi za wateja wanaoshindwa kulipa mikopo kutoka benki. Wakichukua mikopo inachukua muda mrefu sana kuweza kuirejesha mikopo hii, kwa hiyo, benki zenyewe zinaona vilevile ni risk katika kukopesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili si tu linatokea nje, lakini hatia, yaani kwa mfano kama mimi Waziri ambaye nina dhamana ya fedha, bado ninakuwa napata barua kutoka benki niwasaidie katika ku-collect mikopo yao ambayo sisi Waheshimiwa tumechukua! Yaani ni vitu ambavyo vinakuwa vinatokezea kwa hiyo, effect yake ni kubwa sana. Kwa hiyo, kwa sababu tu soko letu ni huria inakuwa ni vigumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa mfano sasa hivi bado kutokana na hatua tuliyoko ni nzuri, kuna baadhi ya watu wanapata *interest rate* ndogo mpaka 10%! Ni kwa sababu *information* zao zinajulikana, kwa sababu imeonekana hata wao wanapochukua mikopo speed yao ya kurejesha na kumekuwa hakuna vikwazo katika urejeshaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, on *individual agreement* au *negotiation*, hizi rates zinaweza zikaenda chini. Wakati tunaendelea hivyo, sisi kama Serikali tumeona tunaweza ku-intervene kwa kuweka mazingira mazuri ikiwa mojawapo ni kuweka database kwa ajili ya watu kujuliakana historia yao, vipi wanalipa bili zao na vitu vingine kama hivyo. Hii tumewapa Kampuni mbili ambazo zinafanya kazi kama hizo, yaani kuanzisha ile database na ikawa open kuwa accessed na benki. Once ukitaka kwenda kuchukua mkopo, basi unaweza kuwa accessed wewe mkopo huu umechukua wapi ama bili zako unalipaje!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi tayari taarifa za wateja 820,000 nchini zimeingizwa katika database na baadhi ya benki zinaweza ku-access hizo taarifa. Kwa hiyo, sio jambo la Serikali ku-intervene moja kwa moja kwamba,

4 FEBRUARI, 2015  
kuchukua hatua moja kwa moja, lakini kuweka mazingira mazuri ya kisera kutawezesha riba zetu kuteremka chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine lilikuwa ni kuhusiana na kuweka mazingira mazuri again na hizi *micro finance*. Ni kweli, bado sasa hivi kuna changamoto hiyo na kwa sababu tu Watanzania wengi hasa waishio vijiji ni hawana *access to finances*, ni vyema na muhimu na sisi kama Serikali tumeona kwamba tuweke sasa mazingira mazuri kwa ili *micro finance institutions* ziweze ku-perform so that Watanzania waweze nao badala ya kuona kwamba, hawapati huduma rasmi zile za kibenki, lakini wapo katika zile sehemu nyingine za fedha ikiwemo VICOBA, ROSCA, SACCOS na taasisi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wetu sisi Wizara ya Fedha karibu tunaanzisha Idara itakayoshughulika na...

*(Hapa, kengele ililiaj)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Najua una mengi ya kusema, lakini muda ndio hivyo! Kwenye bajeti utaendelea kuyaongeza hayo ambayo...

Waziri wa Ulinzi, Mheshimiwa Mwinyi?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie machache ambayo yametolewa na Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Kwanza, nianze kwa kuishukuru Kamati chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mama Anna Abdallah kwa ushirikiano wanaotupa katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imezungumzia changamoto zinazokikabili Chuo cha Maafisa wa Kijeshi Monduli; zikiwemo uchache wa mabweni hasa ya wanawake, ukarabati wa majengo hasa nyumba za Maafisa,

4 FEBRUARI, 2015

mabweni ya wanafunzi, ukumbi wa mikutano na uwanja wa kwata. Tunatambua tatizo hili na tunafanya juhudzi za kuweza kupata fedha za kuweza kufanya ukarabati unaotakiwa, lakini kama mnavyofahamu bado upatikanaji wa fedha ni changamoto, lakini hili liko katika priority za Makao Makuu ya Jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tatizo la uvamizi wa maeneo ya mafunzo ya medani kupatiwa ufumbuzi; hili linafanyiwa kazi, lakini na lenyewe linahitaji fedha, kwa sababu waliopo katika maeneo haya wanahitaji kulipwa fidia ili waweze kuondolewa, lakini juhudzi zinafanyika za kuweka mabango kuonesha maeneo ya Jeshi, lakini wakati huohuo tukipata hizo fedha za fidia tutawapatia, ili waweze kuondoka katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makazi kwa askari na Maafisa katika Makambi ya Jeshi; nafurahi kusema kwamba, tunao sasa mradi mkubwa wa nyumba 10,000 ambaao umeanza kwa kasi kubwa. Na tayari tumeishakabidhiwa nyumba zipatazo 282 zenye uwezo wa kuishi familia 2,256. Kazi inakwenda vizuri sana, ujenzi unaendelea katika Mikoa kadhaa kwa wakati mmoja kwa sasa. Hapa Dodoma kuna ujenzi unaendelea, Dar es Salaam tumeishakabidhiwa, Pwani umeanza ujenzi na Pemba vilevile kuna ujenzi unaoendelea.

Kwa hiyo, tunashukuru kwamba, kampuni iliyopewa kazi hii wanafanya kazi, yaani utekelezaji kwa mujibu wa mkataba unakwenda vizuri sana. Ni mategemeo yetu kwamba, tutaweza kupata nyumba hizo kwa wakati kama ilivyopangwa katika mkataba. Lakini kuna changamoto ya kuweza kupata nyumba za ziada baada ya hii awamu ya kwanza, ili tuweze kukidhi mahitaji yote katika Jeshi letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Chuo cha Unadhimu (*Commanding and Staff College*); ni kweli, kwamba, kwa sasa wanafunzi wanapata mafunzo haya ya *Command and Staff College* pale Monduli – TMA kwa sababu chuo hiki hakijakamilika. Lakini, nafurahi kulieleza Bunge lako kwamba,

4 FEBRUARI, 2015

fedha sasa zimepatikana, Makao Makuu ya Jeshi yameweza kutenga fedha, shilingi biloni 9 zimepekwu pale wamekabidhiwa SUMA JKT kuweza kukikamilisha kile chuo na ni mategemeo yetu kwamba mwaka huu au tuseme mwezi Julai mwaka huu wanafunzi wataanza kupata masomo yao palepale Duluti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Jeshi la Kujenga Taifa, kulikuwa kuna hoja ya Kambi ya Oljoro isaidiwe kuongezewa nyumba za askari, vifaa na mafunzo. Napenda kusema kwamba, huu mradi wa nyumba 10,000 sio kwa Jeshi la Wananchi pekeyao, kuna mgawo kwa Jeshi la Kujenga Taifa. Pamoja na kwamba hautamaliza tatizo, lakini kwa kiwango kikubwa utaweza kupunguza uhaba wa nyumba za askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria kwamba, miezi mitatu ni michache haitoshi; Tunatambua kwamba miezi mitatu ni michache, tungependa iwe miezi 6. Lakini kama mnavyotambua kwamba, wanaohitimu kidato cha VI ni wengi mno kuweza kuwachukua kwa mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo letu lilikuwa ni kwamba, tuchukue kwa awamu, ili tuweze kuwamalizia wote kabla hawajajiunga na vyuo vikuu, kwa sababu, wakishajiunga na vyuo vikuu inakuwa ni shida tena kuwapata kuwarudisha katika mafunzo ya JKT. Kwa hiyo, tunachosema ni kwamba, hili linafanyiwa kazi, tutakaa na Wizara ya Elimu...

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kigoda, Waziri wa Viwanda na Biashara?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuishukuru Kamati ya Fedha na Uchumi.

Kabla sijaendelea kutoa maelezo yoyote, napenda nianze na lile suala ambalo limeleta mkanganyiko. Napenda

4 FEBRUARI, 2015

kuchukua fursa hii kuwapa taarifa wakulima wote wa Mkoa wa Tanga kwamba, machungwa yanayozalishwa katika Mkoa wa Tanga yanafaa kwa kutengenezea juice na ndio maana sasa hivi kila Halmashauri ya Wilaya ya Mkoa wa Tanga inaendelea na utaratibu wa kufanya uwekezaji katika machungwa ambayo yanaweza kutoa maji mengi zaidi kuliko yale ambayo tunayapata katika kipindi hiki tulichonacho. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni kuhakikisha kwamba, usindikaji huu wa machungwa haya unaondoka kwenye viwango vya viwanda vidogo vidogo, tunataka kwenda kwenye viwanda vya kati na viwanda vikubwa na ndio maana utafiti unaofanyika pale Ari Mlingano umeishateua vijiji karibu 9 vya Mkoa wa Tanga kuingia katika programu ya kuzalisha machungwa ambayo yatatoa maji mengi na kutengeneza juice. Vijiji hivi ni pamoja na Kijiji cha Maduma, Kwamhos, Kwabota, Semngano, Bwitini, Korogwe, Hale, Magila na Mnyuzi. Kwa hiyo, programu hizi zinatekelezwa, ili kuendeleza suala zima la kuboresha usindikaji wa machungwa kwa maana ya kupata juice kutoka machungwa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililojitokeza ni kwamba, maelezo yetu tuliyotoa kwamba machungwa yenye mbegu ambayo hayatoi maji mengi hayatoshelezi mahitaji ya viwanda hivi vya kati na vikubwa na ndio maana tukasisitiza kuingia kwenye programu hii inayofanywa hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa maelezo haya Wizara inapenda kuwatoa wasiwasi wakulima wa Mkoa wa Tanga na kuwahakikisha kuwa habari iliyoandikwa kwenye gazeti moja hapa nchini kwamba machungwa ya Tanga hayana sifa kwa juice, itakuwa imeandikwa kimakosa na kwa tafsiri potofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka kutoa msimamo huo. (Makof)

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala pia limeongelewa hapa suala la kuhusu urafiki hasa katika matumizi ya fedha ambazo zilitolewa kwa ajili ya kuendeleza Kiwanda cha Urafiki. Kiwanda cha Urafiki kilipata mkopo wa fedha za RMD milioni 217 kutoka China na kwa takwimu tulizonazo hapa fedha hizi zilitumika kwa kadri zilivyopangwa kutokana na mpango wa uwekezaji wa mwaka 1996. Mkopo wa kwanza wa RMD milioni 100 ulitumika asilimia 84 kugharamia uendeshaji na uwekezaji, asilimia 16 kugharimia uwekezaji katika ukarabati, ununuzi wa mitambo na usindikaji na takwimu ninazo hapa na bajeti ninayo hapa tutaiwakilisha kwenye Kamati ili waone matumizi hayo yamekwendaje kwa sababu ya muda ni mfupi.

Kuhusu suala la mgogoro kati ya *Tanga Fresh* na *Fair Competition Commission*. *Tanga Fresh* wameshakata rufaa na kulipeleka suala hili kwenye *Fair Commission Tribunal* na mpaka sasa kutokana na maeleo tuliyopata ni kwamba suala hili *judgment* yake karibu itatolewa lakini tunalifuatilia kwa karibu sana kama Wizara kuhakikisha kwamba halitaathiri shughuli za wale wajasiriamali wadogo wadogo ambao wanafanya kazi ya kuzalisha maziwa katika eneo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili napenda kulihakikishia Bunge Iako Tukufu kwamba tunalifanyia kazi kwa nguvu sana.

Suala la mwisho ni lile ambalo limezungumzwa kati ya *TBS* na *Intertek* tayari tumeshapeleka malalamiko yetu *Interpol* tarehe 10 Desemba, 2014 lakini vilevile tumepeleka malalamiko yetu kwa *Adjudicator* kuhusu *Intertek* katika suala zima la uingizaji bidhaa ambazo viwango vyake havikukidhi vigezo. Na nina hakika kwamba tukishapata majibu haya na kwa sababu tayari tumekwisha kupata fundisho itabidi tupime vizuri sana kwa zabuni zinazokuja kuona kwamba tunawekeza mawakala wa aina gani katika maeneo haya. (Makof)

Suala lingine....

4 FEBRUARI, 2015

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa najua muda huu ni mdogo lakini sasa lazima tu-manage time hapa. Sasa namuita Mwenyekiti, Kamati ya Ulinzi na Usalama, sorry, Mheshimiwa Chikawe.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie taarifa ilioletwa mbele yetu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwashukuru Wanakamati wote na uongozi wao chini ya Mama Anna Abdallah, kwa ushauri ambao wamekuwa wakiipa Wizara yangu na sekta nzima ya usalama ndani ya nchi hii na ushauri wao umekuwa unakuja *timely* na ni wa umuhimu sana katika utekelezaji wa kazi zetu.

Naomba pia nichukue nafasi kuwashukuru wote waliochangia na hasa kwa kutushauri mambo mengi ambayo yanatokea katika sehemu zao akiwemo Mheshimiwa Opulukwa ambaye naweza nikamwambia tu kwamba tumekusikia na tutachukua hatua stahiki kupambana na hali iliyopo katika jimbo lako. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na moja tu la jumla, niseme tu watu wengi wamekuwa wakizungumza kuwaalani askari polisi kwamba askari polisi ni binadamu, ni *flesh and blood* kama wewe na mimi, na wana familia na wanapotoka nyumbani kwenda kazini wanategemea kurudi nyumbani kwa waume na wake zao na watoto wao. Kwa hiyo, kama wanafanya makosa basi wanafanya makosa kibinadamu, lakini kazi yao kubwa wanafanya kazi kubwa kutulinda na ni kazi hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda hufahamu lakini leo nimepoteza askari polisi mmoja hapa hapa Dodoma sehemu ya Chang'ombe akijaribu kuokoa maisha ya mtoto ambaye alikuwa anauwawa na mzazi wake katika heka heka ya kumuokoa yule mtoto yule askari polisi ameuwawa, lakini yule mtoto ameokolewa. Kwa hiyo, tunao askari ambao wanafanya kazi nzuri sana nadhani we should have some

4 FEBRUARI, 2015

*kind words for them. Tuzungumze maneno mazuri pia kwao, tusiwe tunawalaani tu kama vile hawa ni wanyama, hawa si mashine, hawa ni watu. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba niseme tu kwamba labda nizungumze hoja za Kamati *thematically walizingumza* kuhusu mauaji ya vikongwe na wetu wenye ulemavu wa ngozi, kweli lile ni tatizo lakini Jeshi la Polisi limechukua hatua kadhaa kupambana na hali hii mpaka sasa unaweza ukasema mauaji ya vikongwe yamepungua hata haya mauaji ya walemovu wa ngozi lakini hata hivyo tumechukua hatua za kupambana na wapiga ramli chonganishi, waganga wa kienyeji hatuna matatizo nao lakini wapo wapiga ramli chonganishi ambao ndiyo hao wanaoelekeza watu kwenda kuua watu wenye ulemavu wa ngozi kwa sababu kadha wa kadhaa. Hawa tunapambana na tumeunda task force ya Jeshi la Polisi wakishirikiana na Chama cha Watu Wenye Ulemavu wa Ngozi pamoja kwenda kufanya kazi hii katika mikoa mitano ya Kaskazini na tunategemea basi kazi itakuwa nzuri huko. Nia ni kupambana nao na kumaliza kabisa tatizo hili la wauaji wanaoua walemovu wa ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio ya kuvamiwa vituo vya polisi na kuuwawa askari hayo ni matukio yamekuwa yakinkeo hivi karibuni na matukio haya na sisi tunayaunganisha na ugaidi kwa sababu kila yalipotokea na tukafuutilia tumefanikiwa kupata taarifa za kiintelijensia na tumefanikiwa kuwapata wengine na tunawashitaki sasa na tunaona mwelekeo ni huo, kwa hiyo, tutaongeza nguvu sana katika mapambano haya kwa sababu hatutaki turuhusu ugaidi uingie katika nchi yetu, ingawa tunajua jambo gumu, maana tunazungukwa na nchi ambazo shughuli hizo zinafanyika. Lakini tunategemea basi ushirikiano wetu na raia katika jambo hili utatufikisha mahali ambapo tutaweza kupambana na ugaidi effectively.

Lingine ni Jeshi la Polisi litafute njia mbadala na za kisasa kupambana na kudhibiti uingizaji nchini wa dawa za kulevyo ukiwemo usafirishaji wa bangi kwenda Kenya na

4 FEBRUARI, 2015

mirungi toka Kenya kuingia Tanzania. Mapambano dhidi ya dawa za kulevyta ni makubwa, ni mpambano ambao sisi tumeamua tunapambana nao kwa dhati kabisa. Kwa hiyo, tutafuta kila njia ya kupambana na watu hawa lakini tunategemea pia kupata ushirikiano wa wananchi ili tuweze kufanikisha lengo hili.

Jukumu la mapambana haya ni la kila mtu, kila mwananchi anahusika, unapoliona lazima upambane nalo. Lakini Serikali imeendelea kulijengea uwezo Jeshi la Polisi na uwezo wa kitaalam ili kukabiliana na mbinu mbalimbali ambazo inatumia katika kusafirisha dawa za kulevyta kwenda ama kuingia nchini.

Jeshi la Polisi kushirikiana na jamii kuongeza jitihada na mbinu za kuwadhibiti wale wote wanaoendesha uhalifu maeneo mbalimbali. Falsafa ya Jeshi la Polisi, jamii...

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mwenyekiti nitamuita sasa wa Kamati ya Ulinzi na Usalama au mwakilishi wake.

**MHE. JOHN Z. CHILIGATI – K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii nihitimishe kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati hoja ambayo tulitoa leo asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii imechangiwa na Wabunge 15; kuna waliochangia kwa maandishi, wako sita na waliochangia kwa kusema wako tisa. Sasa nina muda kiasi gani hujasema...

**MWENYEKITI:** Nusu saa.

**MHE. JOHN Z. CHILIGATI – K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jumla ya watu 15 wamechangia hoja hii na niwashukuru vilevile Waheshimiwa Mawaziri wamesaidia kufafanua baadhi ya mambo ambayo yamo katika taarifa yetu ya Kamati na baadhi ya mambo

4 FEBRUARI, 2015  
ambayo baadhi ya Wajumbe wameyasema wakati  
wakichangia hoja.

Sasa waliochangia hoja nikianza na Mheshimiwa Sabreena Sungura alisema mengi, mengi tu ya ushauri, mengine tumeyapokea tutayapeleka katika Wizara zinazohusika. Kwa mfano walikuwa na ushauri kuhusu vijana wanaojiunga na vyuo baadhi wanakataliwa kwa sababu hawajapita JKT, wakienda JKT wanaambiwa umri hautoshi. Sasa litafanyiwa uchunguzi tuone tatizo lipoje hilo tumelipokea na tutalipeleka katika Wizara zinazohusika ili hao vijana wanaotanga tanga huku wanakataliwa wakienda vyuoni wanakataliwa, wakienda JKT wanakataliwa litafanyiwa uchunguzi ili jawabu liweze kupatikana.

Vilevile Mheshimiwa Sungura alikuwa na ushauri kuhusu ujenzi wa mabweni ya wanawake katika magereza jambo ambalo hata kwenye Kamati yetu vilevile tumelisema na kwenye maazimio ambayo tutayapitisha vilevile limo kwamba Serikali ijithidi katika magereza yetu sehemu zile za mabweni ya akina mama yawepo na siyo yawepo tu vilevile wakinamama wengine wanalazimika kwenda na watoto wadogo, kwa hiyo, ile huduma ya mabweni katika magereza yetu ni muhimu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Sungura hili limo katika maazimio ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Vincent Nyerere naye amekuwa na mengi sana, lakini mengi kwa kweli yalikuwa ni ushauri na ameshauri kwamba tunapsema tuwe na amani endelevu basi tutazame suala la utoaji haki kwa sababu kama hatutendi haki hiki ni kichocheo cha chuki na vurugu nadhani ushauri mzuri.

Vilevile Mheshimiwa Nyerere amesema ili tudumishe amani na utulivu tulionao tutazame suala la pengo kati ya walionacho na wasionacho kati ya matajiri na maskini kwamba pengo hili likiachiwa likakua mno nalo vilevile linajenga chuki, linajenga vurugu, nafikiri ni mawazo mazuri na Serikali itayachukua ili kutazama jinsi gani ya kuwainua

4 FEBRUARI, 2015

hao ambao wako chini wanyonge hawa. Japo siku hizi hawapendi sana kusikia habari za neno ujamaa lakini ili mradi bado kuna maskini, bado kuna dhuluma, basi ujamaa kama silaha ya wanyonge kujiihua itakuwepo tu tutake tusitake.

Kwa hiyo, baadhi ya sera kama hivi kufanya elimu kuwa bure, kufanya matibabu kuwa kwa bei nafuu, maji vijiji ni sera ambazo zinainua hawa wanyonge ili na wenyewe waweze wakakua kiuchumi na kupunguza pengo kati ya walionacho na wasionacho. Kwa hiyo, mimi nakuunga mkono kabisa Mheshimiwa Vincent Nyerere katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ametukumbusha vilevile katika mchango wake kuhusu kutazama maslahi ya askari katika majeshi yetu yote na sisi Kamati jambo hili kila tunapokutana na Wizara zinazohusika tunalisisitiza sana habari za nyumba za askari katika majeshi yetu yote kwa sababu ni huduma muhimu kwa askari, sare za askari, mishahara ya askari, madai mbalimbali ambayo askari wanadai, huku uraiani wafanyakazi wanapodai wanadai mpaka wanagoma lakini maadili ya majeshi hawa hawawezi wakagoma. Kwa hiyo, Serikali lazima hawa ambao hawawezi wakagoma lazima iwatazame kwa karibu zaidi kwa sababu wao kwa mila na desturi na maadili ya kijeshi hawawezi wakagoma. Kwa hiyo, kila mara sisi Kamati tunapokutana na Serikali katika baadhi ya mambo ambayo tunaikumbusha Serikali tena na tena kutazama maslahi ya askari.

Vilevile Mheshimiwa Nyerere amekumbusha kwamba sasa hivi miji inapanuka kwa hiyo, hatari za moto zinakuwa nyingi, ile *risk* ya moto inakuwa nyingi, lakini jeshi letu vikosi vyetu vya zimamoto havipewi uwezo wa kukabiliana na hii *risk* ya miji kukua. Jambo hili sisi tumelizungumza sana katika Kamati, ni kweli jinsi miji inavyokua, majengo ya ghorofa yanakwenda sasa gorofa 30, ghorofa 40, huyu zimamoto yeye gari alilonalo lina uwezo wa kuzima mpaka moto wa ghorofa ya 18 au ghorofa ya 20, lakini sasa moto ghorofa ya 30 haya

4 FEBRUARI, 2015

ni mambo ambayo hata sisi Kamati tumeiambia Serikali tena na tena kwamba lazima iende sambamba na ukuaji wa uchumi, ukuaji wa miji na ndiyo maana katika moja ya mapendeleko ambayo tunaomba myakubali, tunasema kwamba Serikali iache utaratibu wa kutokutenga fedha yoyote kwa vikosi vya zimamoto ili viweze kupata pesa hizi kuweza kununua vifaa vya kuzima moto, kununua vifaa hata vya uokozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi inapotokea jengo limeporomoka, zimamoto wanapokwenda hawana vifaa, wanakuwa watazamaji hatuwatendei haki haya ni mambo ambayo ndiyo maana tunasema kwamba Serikali ione jinsi ya kuongeza uwezo Jeshi la Zimamoja kukabiliana na majanga ambayo jinsi jamii inavyopanuka, idadi ya watu imeongezeka, miji inapanuka na hatari ya majanga nayo vilevile inapanuka.

Mheshimiwa Ritta Kabati naye alikuwa na mambo mengi ya ushauri amezungumzia habari za uchache wa vituo vya polisi kule Iringa, nimeshampelekea Waziri anayehusika amezungumzia habari za Zimamoto, magari machache ya Zimamoto hili limo katika maazimio ambayo tunaishauri Serikali kuimarisha Vikosi vya Zimamoto, siyo Iringa tu ni kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia amezungumzia msongamano katika magereza na hasa Iringa na kwenye Kamati tumesema tatizo hili ni kwa magereza yote kwa hiyo, tumeishauri Serikali jinsi ya kupunguza msongamano katika magereza limo katika maazimio yetu. Amezungumzia habari ya uhamiaji haramu na katika maazimio hilo limo tumeishauri Serikali kupambana na hawa wahamiaji haramu na kubwa ni lile kwamba wakishakamatwa sasa hivi wanarundikwa tena kwenye magereza yetu ambayo tayari yameshajaa, tunalazimika kuwashudumia kwa chakula, kwa malazi, kwa matibabu, ndiyo maana katika azimio letu tumesema hawa sasa wakishakamatwa wakapelekwa mahakamani warudishwe makwao kama kwa ndege ni gharama basi hata kwa mabasi, basi la Ethiopia linafika, Kenya mabasi

4 FEBRUARI, 2015

yanafika, Uganda, Burundi hakuna ambako mabasi hayafiki wasiendelee kukaa ndani ya nchi yetu hawa wahamiaji haramu na ndiyo azimio ambalo tunalo katika waraka wetu.

Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac yeye amezungumzia habari za ulinzi mipakani na sisi katika Kamati hili tumelisema na kuna maazimio na mapendekezo kuhusu jinsi gani ya kuimarisha ulinzi mipakani pamoja na kudhibiti njia za panya ambazo ni kweli ziko nyingi na zinapitisha wahamiaji haramu wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwanamirisho Abama amezungumzia suala la mauaji ya vikongwe na albino na bahati nzuri Waziri sasa hivi amelitolea maelezo jinsi ambavyo Jeshi la Polisi linavyojipanga kupambana na haya matatizo ya mauaji ya vikongwe na albino ambayo ni kweli kwanza yanachafua kabisa taswira ya nchi yetu.

Vilevile amezungumzia suala la uhamiaji haramu ambalo limeshatolewa maelezo. Amezungumzia suala la mrundikano magerezani ambalo vilevile tumeshatolea maelezo. Ameshauri adhabu mbadala na sisi kwenye ripoti yetu tumeishauri Serikali hivyo hivyo kwamba ziko sheria kwa mfano ile Sheria ya Community Service ambao inasema watu wenyе makosa madogo madogo, wizi mdogo mdogo, mtu kaiba embe, kuku, kaiba nini ambao sasa hivi bado wanapelekwa magerezani, tunayo sheria nzuri tu kwamba hawa watumikie vifungo vya nje na wapewe kazi na akiwa nje anapewa kazi saa mbili mpaka saa sita kama ni kusafisha mji, kama ni kufyatua matofali ya maabara ya sekondari ya kata, shule yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mpaka sasa sheria hii haijatumika kwa ukamilifu, ukienda magerezani unakuta watu wenyе makosa madogo madogo wamejaa na sisi tumewashauri Serikali kwamba hii sheria itumike.

Tunayo Sheria ya Parole, nzuri tu kwamba mfungwa akionyesha tabia njema, mwenendo mwema, sheria inaruhusu nusu ya kifungo chake aitumie jela na nusu ya

4 FEBRUARI, 2015

kifungo chake atumie akiwa nje ya jela. Sheria nzuri lakini haijatumika kwa ukamilifu, hizi zote ni adhabu mbadala ambazo tumeishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwanamrisho Abama vilevile amezungumza suala la *NIDA*, vitambulisho vya Taifa kwamba wapewe fedha ambazo zinawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi, hili limo katika mapendekezo ambayo tutawaombeni myapitishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jitu Soni, amezungumzia habari ya tozo ya Zimamoto katika sekta ya kilimo, hili tumelipelea tunalipeleka kwa watu wa Zimamoto watazame maana yake yeye anasema kwamba huduma za Zimamoto kule kwenye kilimo bado hawazioni sawa sawa. Kwa hiyo, wao kutozwa wanaona kwamba si haki tumelipeleka kwenyewe walitazame watu wa Zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumzia mafunzo ya ufunzi kwa wafungwa, hili jambo lipo katika magereza yetu mengi, ukienda Karanga pale unajifunza kushona viatu, ukienda Gereza la Mbeya kuna chuo kabisa na unapata na vyeti, kwa hiyo na sisi tumewaambia magereza programu kama hizi waziendeleze kwa sababu mfungwa akitoka pale anaujuzi wake ambaa utamsaidia kuanza maisha mapya.

Vilevile Mheshimiwa Jitu Soni ameshauri kuhusu *traffic* kutumia kamera kwenye barabara kuwanasa wale wanaovunja sheria za barabarani kwa kutumia kamera ni jambo ambalo sisi Kamati tumeshazungumza na Serikali na wanatafuta uwezo tu wakipata uwezo ni utaratibu mzuri unatumika duniani kote na sisi muda si mrefu nina imani tutaingia katika ulinzi wa dijitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Iddi Azzan alikuwa na mengi lakini kubwa ambalo alisema ni kwamba ana wasiwasi Kamati inaposema hali ya ulinzi na usalama ni shwari anaona kana kwamba siyo shwari. Lakini Mheshimiwa Iddi Azzan tunaposema hali ya nchi kwa ujumla Tanzania ni

4 FEBRUARI, 2015

nchi kubwa sana hatusemi kwamba kila mahali hakuna tukio lolote la uvunjifu wa amani bali matukio hapa na pale yapo sisi tunazama sasa kwa ujumla wake. Kwa hiyo katika nchi yetu, katika mikoa yote na Wilaya zote kwa ujumla wake katika kipindi hiki hali imekuwa shwari, changamoto zipo na zinafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Azzan akasema kwamba hali ni mbaya sana kiasi ambacho sasa Serikali itumie Jeshi la Wananchi kulinda usalama wa raia na mali zao. Sasa Mheshimiwa Iddi Azzan Jeshi linaweza likatumika mahali ambapo kama kweli hali imekuwa mbaya sana, ni dharura kubwa sana ndiyo Jeshi la Wananchi linaweza likatumika na likitumika sasa zile taratibu za kawaida na kanuni za kawaida haziwezi zikafuatwa kwa sababu Jeshi lenyewe halikufundishwa kupiga risasi kwenye miguu ili kupunguza nguvu zako, Jeshi unafundishwa kupiga target ya Jeshi ni kupiga pale kifuani kwenye moyo au kwenye ubongo unamaliza ndiyo maana kuna tahadhari kubwa sana kutumia Jeshi, ila linaweza likatumika pale ambapo kweli kuna dharura kubwa sana hatujafika hatua hiyo Mheshimiwa Iddi Azzan na tunaomba Mwenyezi Mungu tusifike katika hatua hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotakiwa kufanya sasa hivi na ndiyo lengo la Kamati yetu kwamba Jeshi la Polisi tuliwezeshe, lifanye kazi ya ulinzi na usalama kwa ufanisi zaidi. Wanafanya kazi hiyo ya kutulinda sisi katika mazingira magumu sana mara nyingi gari hawana, mafuta hawana, zana za kufanya kazi hawana, nyumba za kuishi ni mazingira ambayo sisi kama Kamati tunaisukuma Serikali iboreshe mazingira, tunaamini kabisa kama Jeshi la Polisi tukiliwezesha kivifaa na maslahi yao mengine linaweza kabisa likatulinda vizuri bila ya kuita Jeshi la Wananchi kuingilia katika ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Khatibu naye alikuwa na mengi katika mapendekezo yetu na moja alizungumza habari ya Jeshi la Polisi kutumia nguvu kupita kiasi na hili Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani juzi wakati anatoa maelezo kuhusu tukio lililotokea Dar es Salaam

4 FEBRUARI, 2015

alilisema hili kwamba Sheria ya Jeshi la Polisi inaeleza kwamba lazima watumie nguvu kulingana na hali halisi ilivyo na akatoa ahadi kwamba katika lile tukio ambalo Mheshimiwa Khatibu alikuwa analisema kama kuna askari ambaye alikiuka utaratibu, akatumia nguvu kupita kiasi ambavyo haikutakiwa alisema kwamba uchunguzi unafanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani maelezo ya Mheshimiwa Waziri yalijitosheleza lakini Mheshimiwa Khatibu aliona tena aliibue upya na akaendelea kutoa laana tu kwamba ninyi mnaowaonea watu, siku yenu inakuja.

Sasa Mheshimiwa Khatibu hilo dua la kuku halimpati mwewe, kwa sababu hakuna mtu/Serikali inamtuma mtu amuonee mtu mwingine na huyo mtu akimwonea mtu mwingine akivunja sheria ni ye ye mwenyewe hajatumwa na Serikali wala hajatumwa na chama chochote cha siasa na sheria inamshughulikia na wala katika kukamata anasema funakamatwa sisi wapinzani tunapelekwa Mahakamani, lakini kiukweli ni kwamba hata chama tawala ukivunja sheria utakamatwa tu na Wabunge wa chama tawala rafiki yangu Mheshimiwa Aden alikwenda kwenye mkutano wa hadhara na pistol na nini alikamatwa akaendwa kuhojiwa huko mahabusu akaenda kutolewa kwa dhamana. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, rafiki yangu Mheshimiwa Kilufi kule Mbarali alikamatwa akapelekwa mpaka Mahakamani kwa kuvunja sheria, hivyo hivyo rafiki yangu Dkt. Kigwangalla aliendesha naye maandamano bila utaratibu naye alikamatwa akapelekwa.

Kwa hiyo hapa si suala la chama fulani, ni suala la sheria imefuatwa ama haikuatwa. Naliomba Jeshi la Polisi waendelee hivyo hivyo wasitazame mtu chama chake, wasitazame dini yake, wasitazame ukubwa wake, sheria ikivunjwa wachukue hatua, wafanye hivyo hivyo kama wanavyofanya hivi sasa.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Opulukwa nadhani alikuwa na mambo mengi ambayo Waziri wa Mambo ya Ndani ameyasemea na atayaafatilia.

Mheshimiwa Hamad Rashid yeye alitoa tu pongezi kwa Jeshi la Wananchi kuhusu huduma ya Kituo kule Wawi na akatoa angalizo kwamba anaomba wawe karibu na wananchi na ndiyo maana linaitwa Jeshi la Wananchi wakati wote lazima liwe karibu na wananchi, lihudumie wananchi na litafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimalizie tu kwa kutoa msisitizo kwa niaba ya Kamati mambo machache yafuatayo:-

La kwanza ni la bajeti katika vyombo vyatia ulinzi na usalama. Kila mwaka tunaishauri Serikali kwamba baadhi ya Watanzania wanafikiri usalama ni kama hewa ipo tu, usalama si kama hewa kwamba ipo tu, lazima inagharamiwa ziko gherama na ulinzi na usalama na amani ndiyo jambo la msingi katika maisha yetu bila utulivu bila amani hakuna kinachofanyika, Bunge hatuwezi kukaa, shule hauwezi, mkulima hawezo, viwanda haviwezi.

Kwa hiyo, Serikali inapofika katika bajeti ya vyombo vyatia ulinzi na usalama bado tunaishauri kwamba lazima tuwekeze kwa sababu ndiyo msingi wa maisha. Tumepita katika nchi za wenzetu ambako amani imevurugika kila kitu kimesimama. Kwa hiyo bado sisi amani tuliyonayo lazima tuwekeze, tuwape bajeti ya kutosha katika vyombo vyote vyatia ulinzi na usalama ili tudumishe ulinzi wetu na usalama, mbaya zaidi ni pale ambapo kile ambacho Bunge limepitisha bado hakifiki katika vyombo vyatia ulinzi na usalama tunavidhoofisha. Sasa unapodhoofisha ulinzi wako utaishije sasa unapodhoofisha ulinzi wako utaishiishije hili ndiyo jambo tunapenda Serikali ijue na Wabunge vilevile tunaoomba watusaidie hili Bunge zima tunapokuja kwenye bajeti ya vyombo vyatia ulinzi na usalama haya ndiyo maisha yetu, bila ulinzi na usalama maisha hayapo, maisha ni dhiki ni taabu.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba tushirikiane tuwape nyenzo za kutosha vyombo vyetu ili tudumishe amani na utulivu ambao ni moja ya tunu kubwa sana ambazo Mwenyezi Mungu ametupa lakini lazima tuzigharamie na hilo ni pamoja vilevile na maslahi ya askari kama nilivyosema askari wana madai yao, sisi uraiani tunadai kwa maandamano na kadhalika hawa hawawezi wakaandamana, hawawezi wakagoma.

Kwa hiyo tunaishauri Serikali kwamba haya madai ya askari kwa sababu hawawezi wakagoma wala kuandama basi tuwaenzi tunapozungumza sasa hivi kuna madeni mengi tu ambayo askari wanatudai, bado hatujalipa lakini bado tunataka watulinde usiku na mchana, nyumba zao tunashukuru Jeshi la Wananchi wana mradi wa nyumba 10,000 tunasukumana na Serikali ili zikamilike haraka wapate, lakini vilevile Polisi wangehitaji nyumba, Magereza wanahitaji nyumba, Uhamiaji wanahitaji nyumba, Zimamoto wanahitaji nyumba na ni haki yao ili waweze wakatulinda vizuri wapate morali ili motisha yao watulinde vizuri. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka kusisitiza tena na tena ni hili la kudumisha amani na utulivu. Hili ni letu wote wala si majeshi, wala siyo vyombo vya ulinzi na usalama ni wote. Sasa hivi wananchi wanaanza kuwa na viashiria vingi tu vya uvunjifu wa amani na vidole sasa tunaanza kunyooshewa sisi wanasiasa kwamba jinsi tunavyoendesha siasa za kiharakti harakati, za kutokutii sheria, za vurugu na fujo tunapeleka nchi kubaya. (Makof)

Kwa hiyo, naomba hili kwa vyama vyote vya siasa, wanasiasa wa vyama vyote tujue tunabeba dhamana ya kulinda amani na utulivu katika nchi yetu, tujiepusha na vitendo, lugha na kauli ambazo inaweza ikapeleka nci yetu katika machafuko. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni vitambulisho vya uraia kupitia NIDA. Suala la vitambulisho ni jambo kubwa sana kuliko ambavyo watu wengi tunavyofahamu. Unapokuwa katika nchi ambayo hujui nani yuko wapi,

4 FEBRUARI, 2015

anafanya nini ni taabu, taabu kiulinzi na usalama, taabu kiuchumi sasa hivi Waziri wa Fedha hata walipa kodi wake hawajui. Inakadiriwa walipa kodi tunatakiwa tuwe milioni 12 lakini tunaolipa kodi ni milioni mbili tu, kuna watu wengine milioni 10 wapo humu humu hajulikani anashughuli gani, anakaa wapi anaweza kulipa kodi kiasi gani lakini vitambulisho vya taifa vitakuwa na database, nani Chiligati, yupo wapi, anafanya biashara gani, anashughuli gani, anaghorofa mahali gani, analipa kodi kiasi gani, wala hatuna haja hata ya kungojea wafadhili waje watulipie katika bajeti yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *informal sector* kuna trilioni 46 kwenye *informal sector* ambako hazijulikani. Kwa hiyo, hili zoezi ni muhimu sana la vitambulisho vya taifa kwa hiyo naomba Serikali tunaomba toeni fedha za kutosha, tuplicate vitambulisho, tujuane nani, yuko wapi, anafanya shughuli gani, analipa kodi, halipi kodi, ni raia mwema ama ni mhalifu, vitambulisho hivi vitatupa mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa hili la magereza msongamano magerezani nalo linatutia aibu kama Taifa. Haki za binadamu zinavunjwa kwa sababu ya huduma ambazo msongamano mkubwa sana, tunaomba Serikali itazame hilo.

Katika Katiba inayopendekezo kama itapita kipo kifungu kabisa sasa kinachoainisha haki za mfungwa akiwa gerezani, haki za msingi, kwa hiyo, asipotekelezewa yale anaweza kama ile Katiba itapita anaweza kupeleka Serikali mahakamani kwamba imevunja Katiba ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa naomba Bunge lako Tukufu lipokee mapendekezo haya, iyajadili na baadaye kuyakubali kama yalivyoorodheshwa katika taarifa ya mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama ya mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.  
(Makofij)

4 FEBRUARI, 2015

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chiligati, toa hoja.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ULINZI NA USALAMA):**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (Makofij)

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na wameleta mapendekezo yao kuhusu Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, NIDA, Uhamiajji, Jeshi la Zimamoto na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa hiyo, nikihoji nitawahoji kwa pamoja kwa namna ambayo mapendekezo yao wameleta ambayo ni mazuri tu.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja lliamuliwa na Kuafikiwa)

(Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama katika Kipindi cha Januari 2014 hadi Januari 2015 liipitishwa na Bunge)

**MWENYEKITI:** Nawapongeza sana Kamati mmeefanya kazi nzuri sana Mama Anna wewe ni veteran kwenye Kamati hii ukisaidiana na Jenerali Ngwilizi ambao tunajua umuhimu wenu kwenye Kamati hii. Lakini nampongeza na Waziri vilevile kwa kazi nzuri alitoa ushirikiano mzuri tu pamoja na Kamati, Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi pamoja na Jeshi zima na Polisi, nampongeza Waziri wa Mambo ya Ndani na wote wanaohusika na Wizara hizi mbili.

Sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

**MHE. SELEMAN S. JAFO - K.n.y. MWENYEKITI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza awali ya yote napenda sana kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ye ye ametupa uzima na jioni hii tukiwa sote sisi Wabunge, wa Bunge hili la Jamhuri ya

4 FEBRUARI, 2015  
Muungano wa Tanzania kuweza kupitia taarifa za Kamati tatu kwa ajili ya maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyekiti wangu wa Kamati Mheshimiwa Edward Lowassa kwa kutuamini vijana wake kufanya kazi ya Kamati na pia nipende kukushukuru wewe Mwenyekiti wangu kama ukiwa Mwenyekiti wangu ukiwa ni kiongozi wangu katika Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa msaada mkubwa mnaotupa sisi ili mradi kwamba tunafanya kazi kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya katika kuishauri Serikali lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba mambo yote yanayohusiana na Wizara ya Mambo ya Nje hali kadhalika na Wizara ya Afrika Mashariki yaende sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kabla sijaingia katika wachangiaji ningependa kuwashukuru sana wananchi wangu wa Kisarawe kwa imani kubwa wanayonipa Mbunge wao katika kutekeleza majukumu waliyonipa katika kipindi hiki cha miaka mitano. Lakini mwisho siyo kwa umuhimu nilipenda kuwashukuru sana familia yangu na wazazi wangu kwa malezi mazuri waliyonipa kwa kipindi chote toka utoto wangu mpaka hivi sasa.

Katika Kamati yetu tumepesta wachangiaji watatu ambao wamechangia kwa maneno, lakini tumepesta mchangiaji mmoja amechangia kwa maandishi. Idadi hii ndogo inanipa jibu kwamba Kamati imefanya kazi kubwa sana kwamba hoja mbalimbali zinazohusu Wizara hizi mbili kwamba Wanakamati wameweza kuzichambua kwa kina na kutoa ushauri lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba Serikali inashauriwa kwa ajili ya mafanikio ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji wa kwanza alikuwa Engineer Hamad Yusuph Masauni yeye aligusa sana

4 FEBRUARI, 2015

katika kipengele cha diplomasia ya uchumi, lakini kama tujuavyo kwamba hata katika mapendeleko ya Kamati jambo hili tulijadili sana na hili naomba tuwekane wazi kwamba kuwa na Balozi ni jambo moja, lakini Balozi zile tuwe tunahakikisha kwamba jinsi gani zinanufaisha nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipitia katika Kamati yetu tulivyosema sehemu mbalimbali utakuta Balozi nyingine kuna fursa nyingi sana lakini kwa bahati mbaya sana utakuta kiwango cha watendaji waliokuwepo katika Ofisi za Balozi hizo ina changamoto kubwa sana.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Masauni alishauri kwamba ikiwezekana tuwe na vijana ambao watu hawa watasaidia kuweka diplomasia ya uchumi. Kuwa na Balozi ni jambo moja, lakini jinsi gani Balozi zile zinasaidia kuitangaza nchi yetu na jambo hili hata ndugu yangu Jitu Soni alizungumza katika mchango wake wa maandishi kwamba katika Ofisi zetu za Mabalozi hivi sasa ni vyema ikiwezekana tuwe na watafiti ambao wataona jinsi gani kuna kazi mbalimbali tunaweza tukanufaika nazo kama nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika tuna mtandao mkubwa sana wa kibashara, lakini ukiachana hivyo nchi yetu ina vivutio vingi sana vya utalii kama katika Ofisi za Mabalozi endapo tunakuwa hatuna watu ambao wenye weledi waa kutosha katika suala zima la mambo mbalimbali ya kiuchumi tutakuwa tumepata hasara kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimpongeze ndugu yangu sana Masauni na ndugu yangu Jitu Soni lakini na Wajumbe wa Kamati ambao jambo hili walilijadili sana kwa kina na kutoa mapendeleko ya kutosha kama yalivyoainishwa katika mapendeleko ya kamati yote 17 mionganoni mwao kwamba jinsi gani Tanzania tuhakikishe kwamba Ofisi za Balozi zote kwamba tunapata vijana mahiri wa kufanya kazi, lakini pendekezo lingine amependekeza Bwana Masauni kwamba upelekaji wa fedha imekuwa ni changamoto kubwa ni kweli.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine ukienda katika Ofisi za Mabalozi mpaka unaona huruma, utawakuta wafanyakazi wa Ofisi za Mabalozi hali zao ziko tete sana, lakini kama mtumishi wa Ofisi ya Balozi hapati maslahi yale yanayokusudiwa ina maana kwamba tunapata aibu kama Tanzania.

Kwa hiyo, changamoto kubwa ni kwamba upelekaji wa pesa umekuwa ni tatizo kubwa sana na hili namshukuru Mheshimiwa Waziri alipokuwa anachangia pale alisema kwamba tutahakikisha kwamba maoni yote ya Kamati yanafanyiwa kazi kama ilivyokusudiwa na hili ndugu zangu kama nilivyosema kwamba endapo kama Ofisi za Mabalozi tusipoweka nguvu za kutosha tutawaibisha Mabalozi wetu na tutaaibisha nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine lilikuwa suala ambalo ndugu yangu Masauni amependekeza suala zima la matumizi ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na kama unakumbuka mwaka jana hili jambo tumelijadili sana kuna Ofisi sasa hivi za Mabalozi kule nje ya nchi nyininge zinatia aibu. Hata Wabunge au wageni mbalimbali wakitembelea Ofisi zile kwa kweli hali inatia aibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe unakumbuka mwaka jana tulienda Maputo pale, tulipofika Maputo pale tukakuta mazingira changamoto lile jengo la Maputo hali ilikuwa siyo ya kuridhisha na mapendekezo haya tumeleta katika Kamati ya Bajeti na nashukuru kwamba leo hii kupata taarifa sasa rasmi kwamba Ofisi yetu ya Ubalozi ule wa Maputo unaendelea, lakini na Ubalozi wa Ufaransa umefunguliwa rasmi. Hii tupende kuishukuru sana Kamati lakini hali kadhalika tuishukuru Serikali kwa kutimiza yale ambayo Kamati iliagiza kwamba mambo haya Ofisi ya Ubalozi wa Ufaransa inunuliwe, ukarabati ufanyike kule Maputo ili mradi kwamba Mabalozi wetu wafanye kazi sehemu salama. Niishukuru sana Serikali kwa kutii utaratibu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Kamati ilipendekeza mara kadhaa na hili Mheshimiwa Masauni amelisema

4 FEBRUARI, 2015

kwamba Tanzania tuna Mifuko ya Hifadhi ya Jamii mingi inawezekana tukitumia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kujenga Ofisi za Balozi zetu katika nchi mbalimbali tutakuwa tumeweka kitega uchumi kikubwa sana. Hivi sasa katika bajeti zetu kila mwaka tunatenga pesa kwa ajili ya kupeleka katika Ofisi za Mabalozi, lakini ukiangalia Ofisi hizi za Mabalozi zingine zingeweza kuijendesha zenyewe na hili tulishauri mwaka jana na tulipeleka Kamati ya Bajeti na ninaamini kwamba Wizara itachukua hili moja kwa moja kuhakikisha kwamba Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, licha ya kuwekeza ndani ya nchi, iweze ikatumike kuwekeza nje ya nchi, lengo kubwa ni kwamba kutengeneza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufike wakati sasa badala Bunge tunakaa tunatengeneza bajeti hapa, tupeleke nje katika Ofisi za Mabalozi, Balozi zinaweza kuijendesha. Kwa mfano, hiyo Ofisi ya Ubalozi peke yake pale ya Maputo ambayo *apartment* moja gharama yake pale wakati tunakwenda kuuliza ni dola 10,000 kwa mwezi, ni pesa nydingi sana. Kwa hiyo, Ofisi ya Maputo peke yake maana yake ingeweza kuijendesha Maputo na Balozi nyingine za nchi ya Kusini mwa Afrika.

Kwa hiyo, hili tunaomba Wizara hasa na kwa sababu mchakato huu umeshaanza sasa, naomba tusipoteze muda, maana wakati mwingine upotezaji wetu wa muda tunajikuta kwamba kama nchi tunapata hasara kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukipanga mambo lazima twende kwa wakati, kama hii Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na yenyeewe imeona kwamba itapata fursa katika kuwekeza sehemu ambayo inaleta tija kwa wanachama wao, kwamba wenyeewe watawenza kuwekeza na watapata *returns* kwa mujibu inavyokusudiwa, na vilevile tutalinda heshima ya nchi yetu kutopata aibu katika nchi za nje.

Naomba sana Wizara, kama alivyoahidi Mheshimiwa Waziri hapa, tuhakikishe kwamba jambo hili tunalifanyia kazi na mimi bahati nzuri Mheshimiwa Waziri ninakuamini sana

4 FEBRUARI, 2015

kwa kazi yako, naamini hili litaenda vizuri na lengo ni kwamba kuivisha nguo Tanzania iendelee kuwa na heshima yake kama inavyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Masauni vilevile alizungumzia suala zima la mikataba ya mtengamano, nadhani Mheshimiwa Waziri amelikubali hili jambo kwamba litakwenda kufanyiwa kazi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upande mwingine Mheshimiwa Hamadi Rashid, Mzee wangu Mbunge wa Wawi, yeye alizungumzia suala zima la mgogoro wa Wabunge wa *East Africa*. Hapa ni lazima tuzungumze ukweli, inawezekana kuna mahali tulikosea. Hapa inawezekana kuna mahali tulikosea, inawezekana umakini wetu lazima tujitathimini vizuri. Watu ambao tunawachukua kuwakilisha katika vyombo mbalimbali wanaleshima kiasi gani kwa nchi yetu na wamejipanga vipi kuitetea nchi yetu. Hili ni jambo lazima tuwekane wazi. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba watu wanavyochaguliwa wakienda katika vyombo mbalimbali wasipofanya vizuri siyo wanajabisha wao wenyewe, maana yake wanaiabisha nchi yetu ya Tanzania. Lakini ndugu zangu lazima katika hapa kuna jambo la kujitathimini, Wabunge wale wamechaguliwa na Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inabidi kama Wabunge tujitathimni katika siku zijazo tutafanya vipi kuhakikisha kwamba umakini unafanyika. Tusichukuane katika nafasi nyingine kwa ushabiki, hilo halifai, maana ushabiki inawezekana ukatupeleka mahali ambapo si sawa sawa, lakini kitu kingine kikubwa lazima tuhakikishe chaguzi zetu zisiendeshwe na rushwa, hilo ndilo jambo la msingi. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna watu saa nyingine huenda wanataka kupitia katika michakato na nani... hatuwezi kufika salama, mwisho tutawapata watu wasiokuwa bora kwa nchi yetu. (*Makofij*)

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama Wabunge, kama nchi lazima tujitathimini hapa, kama kuna sehemu tumejikwaa lazima tujitathimini. Na sisi kule kinyumbani kwangu Mzee Mnyaa kuna lugha moja wanasema kuleka kikuzile kwa kukunenguo yaani unaacha pale sehemu ambayo ilifanya tatizo tunakuja kulaumu mbele ya safari. Kuna mahali tulifanya makosa katika uchaguzi wa viongozi hawa inawezekana kuna mahali tulifanya makosa. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo jambo la msingi kama nchi, jambo la msingi kama Wabunge kwa siku zijazo lazima tujitathimini vizuri jinsi gani tutapata viongozi bora ambao siyo kwamba kumpa mtu apate nafasi fulani, hapana. Mtu apate nafasi lakini kwa ajili ya kuitumikia nchi yetu.

Kwa hiyo, Mzee wangu Hamad Rashid tunashukuru sana kwa ushauri wako na katika hili maana yake ni tathimini ya Wabunge wote. Lazima kama nchi tukae vizuri, tuangalia tutafanya vipi kuhakikisha kwamba nchi yetu inasonga mbele. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala zima la East Africa, hili ni jambo pana ambalo tunaona kwamba lina mambo mengi sana. Leo hii katika hotuba yetu tumezungumzia suala zima la wenzenzu ambao wanajiunga katika ule utatu tuliozungumza, je, sisi Watanzania tunajipanga vipi? Ina maana katika haya sasa na jinsi gani Wabunge wetu wanaenda kule wanaweza kujenga hoja vizuri kuhakikisha kwamba mambo mengine kutokana na uwezo wao wa kujenga hoja yanafanywa kwa ajili ya kuinufaisha Tanzania. Hili lazima tuseme, tusiwe Watanzania watu wa kulaumu kila siku, lazima tujipange kupambana kuangalia ni jinsi gani tutafanya kuibadilisha nchi yetu.

Mheshimiwa Waziri, ninamuombea kila la kheri Mzee wangu Sitta, Mzee wa viwango na speed, kwamba sasa amepata Wizara hii, mwanzo alikuwa Wizara hiyo Mzee Sitta na sasa hivi amekuwa ndugu yangu Mheshimiwa Mwakyembe ambao najua kwamba ana uzoefu mkubwa

4 FEBRUARI, 2015

sana wa eneo hilo. Yeye ametumikia eneo hilo kama Mbunge wa East Africa, sasa tuna imani kwamba katika Wizara yake hiyo aliyokuanayo hivi sasa Tanzania tutaenda kwa kasi zaidi, lengo kubwa ni kwamba sisi Tanzania tuko katika nafasi nzuri sana ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika nchi zote zinazotuzunguka sisi, tuna ukanda mzuri sana wa Bahari, tuna fursa ya kila kitu kuweza kuwasaidia wenzetu. Ina maana kwamba tukifanya vizuri na tukijipanga vizuri kama nchi yetu tutapata mafanikio makubwa sana, lakini vilevile tuna kila fursa ya wingi wetu, Tanzania ina idadi kubwa sana ya watu kulinganisha na nchi zingine, lakini hata kijiografia hata idadi ile square kilometers tulizokuwa nazo huwezi ukalinganisha na hao wenzetu. Kwa hiyo, tuna kila sababu kujipanga vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini Mheshimiwa Mwakyembe pia ataenda kuifanya vizuri, lakini kazi yake na uhodari wake katika nyanja ya kisheria atawasaidia hata Wabunge wetu pale ambapo saa nyngine wanaonekana kwamba wanateleza kuwaweka vizuri. Kazi kubwa aliyofanya Mzee Sitta sasa amemwachia Mheshimiwa Mwakyembe na imani kwamba sisi kama wana Kamati tuna imani na Mzee Sitta aliyetoka na vilevile hali kadhalika tuna imani na Mheshimiwa Mwakyembe ambaye hivi sasa ameingia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi ambalo kama Kamati tumelizingumza suala zima la kibajeti na hapa kama Kamati tunaiomba sana Wizara ya Fedha kama mtiririko unaokwenda Wizarani haupo sawa sawa tunaomba urekebishwe, kwa sababu Wizara hizi zisipopata fursa kubwa ya kufanya kazi yake, maana yake tumeyaharibu mahusiano yetu, tumeharibu nguvu yetu katika medali za kimataifa.

Kwa hiyo, nakuomba sana Waziri wa Fedha hasa wa Hazina kuhakikisha kwamba jinsi gani Wizara hizi tunaziwezesha. Lakini hata katika mchakato wa kibajeti, tumeona katika Wizara ya Afrika Mashariki jinsi gani kila mwaka ilikuwa na changamoto za kibajeti. Ndiyo maana

4 FEBRUARI, 2015

hata mwaka jana kama Kamati tulipendekeza kwamba ikiwezekana pesa Hazina zitoke moja kwa moja zilipe katika ile, kwa sababu ukiangalia fungu kubwa la bajeti ya Afrika Mashariki yote inaenda katika mchango wa Jumuiya, lakini bajeti ya uendeshaji wa Wizara imekuwa ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika ulimwengu wa mashindano, nchi mbalimbali zinatafuta fursa katika suala zima la kushindana na sisi watu wetu na wawakilishi wetu tunawapeleka lakini hawana resources za kufanya kazi vizuri, hapa tutakuwa hatujawatendea haki watumishi ambao tuliwaweka kule, lakini hatutaitendea haki Tanzania, kwa sababu tuna fursa hizi kubwa naomba tujipange vizuri. Nakuomba sana Waziri wa Fedha uziangalie sana Wizara hizi mbili ambazo zinatupa kioo halisi cha Utanzania wetu huko katika nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwamba Mheshimiwa Waziri Membe alizungumza na ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi yako kubwa unayoifanya na imani sifa ya Tanzania itaendelea kudumu kama ilivyo, kwa sababu tunaamini kwamba watu wote mliopo katika Wizara kazi zenu ni kubwa sana na tuna imani kwamba medali ya Tanzania kama inavyoonani na hapa taarifa uliyotupa Tanzania itaendelea kung'ara na hii niwambie Waheshimiwa Wabunge, kwamba Tanzania huko nje tuna heshima kubwa sana.

Kwa hiyo, changamoto kubwa ni kwamba, sisi wenyeWE Watanzania jinsi gani tunajivunia heshima yetu tuliyokuwa nayo, kwa sababu sisi ndiyo tunatembea sehemu mbalimbali. Inawezekana wewe Mtanzania mwenyeWE hu-recognize ile heshima yako watu wanayokupa nje ya nchi. Kwa kweli kama Watanzania tuna heshima kubwa sana, lazima tulinde heshima hii na kuhakikisha kwamba Tanzania yetu inang'ara katika medali za kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nilimzungumzia ndugu yangu Jitu Soni ambaye amechangia kwa maandishi na hoja yake nimezungumza kwamba imegusa katika

4 FEBRUARI, 2015  
diplomasia ya uchumi mambo ya utafiti nikushukuru sana  
Jitu Soni kwa mchango wako mkubwa uliochangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali kwamba wachangiaji katika Wizara yetu hii Kamati yetu walikuwa wachache kutokana na kwamba kamati iliweza kudadavua mambo mbalimbali ambayo Wajumbe au Wabunge kwa ujumla wake waliweza kudadafua mambo mbalimbali ambayo Wajumbe au Wabunge kwa ujumla wake walirizika na mchango mkubwa wa kamati ambao taarifa hii imewasilishwa leo asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo yote sasa naomba Bunge Iako Tukufu likubali na kupilisha mapendekezo yote yaliyowasilishwa na Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kipindi cha Januari 2014 hadi Januari 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
(Makofii)

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Jafo umeeleza vizuri sana, mimi na wewe tuko Kamati moja, lakini umeileleza kwa weredi mkubwa sana.

Kwanza nampongeza Mwenyekiti wa Kamati kwa kazi nzuri, Wajumbe lakini nampongeza na Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje yeye na timu yake kwa ushirikiano mzuri ambao wameipa Kamati mpaka kufikia muafaka wa kuweza kusaidiana kati ya Kamati na Wizara. Lakini kazi kubwa ilifanya Kamati na nashukuru Serikali chini ya

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Waziri kusaidia ujenzi wa Mabalozi yetu na kununua majengo ya Balozi zetu ili tusiwe tunalipa kodi. Nakupongeza sana na naipongeza Kamati na Mwenyekiti wa Kamati.

Sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa hiyo.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Taarifa ya Mwaka ya shughuli ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Njena Ushirikiano wa Kimataifa pamoja katika kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015 ilipitishwa na Bunge)

**MWENYEKITI:** Sasa namuita Mwenyekiti Kamati ya Uchumi!

**MHE. LUHAGA J. MPINA – MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji waliochangia kwenye Taarifa ya Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara kwa maandishi ni wanane kwa kuongea pia ni wanane, lakini hoja zao ni nyingi sana. Kwa hiyo, nitakuwa ninazitaja kadri ambavyo tutakavyokuwa tunaenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo bila kupoteza muda, Mheshimiwa Kasikila pamoja na Mheshimiwa Shakifu

4 FEBRUARI, 2015  
wote walitoa hoja ya kwamba Serikali ianze kazi ya kujenga viwanda na Mheshimiwa Kasikila alikuwa anasema kwamba Serikali ijenge viwanda bila kufanya *reallocation*.

Ninachotaka kumueleza tu ni kwamba Serikali hajengi viwanda na Serikali walishakwishajtoa katika suala zima la kujenga viwanda nchini.

Kwa hiyo sasa, katika bajeti yetu ya Serikali ambayo tunaipitisha kila mwaka, hakuna fedha yoyote ile inayotolewa kwa ajili ya kujenga viwanda, isipokuwa msisitizo wa Kamati ni kwamba nchi zote duniani huwezi kuwaacha wananchi wako mikononi mwa wafanyabisahara peke yake hasa kwenye viwanda vinavyoongeza thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, huwezi kuacha hao wakulima wa matunda wakakaa hivi hivi wakasubiri mwekezaji kutoka Ufaransa aje awekeze huwezi. Huwezi ukasubiri mpaka Mchina aje ajenge kiwanda cha nguo hapa nchini wakati pamba ya Tanzania anainunua kwa bei ya kutupa anaipeleka kule China anatengeneza nguo na bado Serikali inaomba zabuni za kwenda kununua hizo nguo kwa bei kubwa, huwezi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sasa, suala kubwa na msisitizo wa kamati imekuwa ikisisitiza mara kwa mara kwamba Serikali iamue na iachane na hayo mawazo ya kusema kwamba, eti hawafanyi biashara, halafu huku wananchi mazao yao yote ya biashara na ya chakula hayana soko.

Kwa hiyo, dawa ni moja ni Serikali kuamua kujenga kiwanda baada ya kingine. Jenga kiwanda, tunajua kweli Serikali isiweze kuendesha, lakini unajenga kiwanda unasema najenga kiwanda cha matunda hiki hapa Tanga, mnapata

4 FEBRUARI, 2015

kiwanda cha matunda, suala la kuendesha sasa nenda kwenye sekta binafsi wanaweza kuendesha kiwanda lakini already kiwanda unacho na wananchi wako wanaanza kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, msisitizo wa Kamati yangu ni kwamba tunakubaliana kabisa na hoja ya Mheshimiwa Shekifu kwa maana ya ujenzi wa viwanda vya matunda, lakini Mheshimiwa Kasikila kwamba ni lazima Serikali sasa ianze kuwekeza kwa kujenga viwanda badala ya kusubiri wawekezaji wale waje kuwekeza hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni viwanda vya nguo nchini ambavyo hoja imetolewa na Mheshimiwa Naomi mke wa Kaihula, Mjumbe wa Kamati, Mheshimiwa David Kafulila, Mjumbe wa Kamati na Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mwenyekiti wa PAC kuhusu viwanda vya nguo. Tunaendelea kusitiza kwamba, hoja zao wamezitoa nzuri sana katika maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa David Kafulila na Mheshimiwa Zitto Kabwe wao wamezungumzia juu ya marekebisho, tukifika kwenye marekebisho yao tutazungumza, lakini ninachotaka kuendelea kusitiza ni kwamba nchi yetu haifanyi vizuri katika viwanda na moja ya sekta ni hii ya viwanda nguo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi imejaaliwa, tunalima pamba kwa kiwango kikubwa sana katika nchi za Afrika, tunauza na kusafirisha, lakini tunasafirisha pamba ambayo haijaongezwa thamani. Pamba tunayouza nje ni asilimia 20 tu. Pamba tunayotumia na wananchi wetu katika tani 300,000 sisi tunatumia asilimia 20 yake ya hiyo pamba ambayo inazalishwa na asilimia 80 yote tunasafirisha kwenda nje ya nchi.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miaka nenda rudi si Wabunge wala si wananchi wakutoka sehemu mbalimbali ambazo zimelima pamba zikiomba Serikali kutatua tatizo la bei ya pamba. Bei ya pamba sasa inacheza kwenye shilingi 600/= na 700/= bei ambayo haitoshi kabisa hata kulipia gharama tu za hawa wananchi. Wameteseka kwa muda mrefu, Serikali imeshindwa kupata ufumbuzi wa kutatua tatizo la bei ya pamba kwa wananchi wake. Sasa nini kifanyike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukilinganisha Tanzania na nchi jirani hapa Kenya ambao sisi tunawazidi kwa kilimo cha pamba kwa mbali sana, katika soko la Marekani mwaka 2009 Wakenya waliuza kwenye soko hilo wakapata thamani ya milioni 195.4 USD; sisi tukauza milioni 1.2 USD. Watu ambao hawalimi pamba sana kama sisi, watu ambao hawana ardhi kama sisi, watu ambao hawana wasukuma wanaolima pamba kama sisi tunavyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ilikuwa na viwanda 22 sasa vimebaki nane tu, wote wanajitoa katika viwanda vya nguo kwa sababu viwanda hivi kwanza wanakabiliwa na ushindani huo mkubwa kama baadhi ya mapendelekezo yaliyotolewa kuingia kwa bidhaa holela hapa nchini wanashindwa kushindana, lakini vilevile hata Serikali yenewe hainunui kutoka kwao, wakitaka kununua sare za majeshi wanaagiza kutoka nje, wakitaka kununua nguo za hospitali, taulo, shuka na kadhalika wanaagiza kutoka China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hali ya namna hii maana yake ni kwamba hata nchi yenewe haijui namna gani ivilinde viwanda vyake, tatizo kubwa kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, enzi ya miaka ya 1990 Baba wa Taifa alikuwa very smart wakati anavanzisha viwanda hivi viwanda vyote tulivyonavyo hivi alikuwa very smart, hapakuwa na namna yoyote ile ambayo Serikali inaweza ikanunua manunuzi toka nje yanayozalishwa kwa pamba ya kutoka nje.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, *imagine Wachina wanakuja hapa nchini, wananunua marobota yetu ambayo hayajaongezwa thamani kwa bei ya kutupa kwa shilingi 600 kwa kilo, wanabebe hiyo pamba wanaipeleka, halafu Serikali hiyo hiyo inaacha kiviunga mkono viwanda vilivyoko nchini, inaenda kununua kwa wao kwa bei kubwa. Ni lini utaviwezesha viwanda vyako kukua? (Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili tumeweka azimio kubwa sana, Watanzania zaidi ya milioni 16 wananufaika na pamba, sasa Bunge hili leo liwabebe kwa kuiamuru Serikali kwamba hakuna namna yoyote ile ya kununua nguo inayotengenezwa kwa pamba kutoka nje ya nchi, zaidi ya hapo viwanda vyetu vya ndani viweze kutengeneza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninamtazama kaka yangu Cheyo pale anasikitika sana kwa sababu sisi kule bila pamba hakuna maisha. Kusomesha mwanafunzi ni pamba, kujenga nyumba ni pamba kila kitu. Kwa hiyo, ukiwawezesha hawa wakulima wa pamba anaongeza na unanufaisha sana maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze hili suala limezungumzwa na Mheshimiwa David Kafulila. Tulisema kabla sijahama hapa kwenye suala hili la nguo pamoja na maelekezo hayo tuliyoyatoa, lakini pia tumemuagiza PPRA kufanya ukaguzi wa manunuzi yote yaliyofanywa ya nguo na Serikali, kutoka mwaka 2011/2012, 2012/2013, 2013/2014 mpaka sasa ili aweze kutuletea ili aweze kuona hali halisi muone hiyo volume ya billions of money ambayo Serikali inaspend kwa ajili ya kuagiza bidhaa za nguo zilizotengenezwa kwa pamba kutoka nje kuileta hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze hili suala alizungumza Mheshimiwa Kafulila la mkataba tata wa ShivaCom na Vodacom Tanzania Ltd. Kama ambavyo nilitaja kwenye hotuba yangu wakati ninaongea lakini vilevile kama Mheshimiwa ambavyo alitaja, huu mkataba kama sisi tumemuagiza Waziri wa Fedha kwa maana ya TRA wafanye ukaguzi wa maddai haya.

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama zinavyodhibitika ni kwamba ni zaidi ya dola za marekani milioni 650 ambayo ukibadilisha ni shilingi bilioni 620 yaani ndiyo fedha ambayo inaonekana kwamba katika mauzo *Shivacom* amempunja *Vodacom Tanzania Limited*. Sasa kama hiyo ikithibitika ni kweli, shilingi bilioni 620, ukiacha ile hasara ya profit ambayo *Vodacom* amepoteza, hakuna kodi yoyote iliyolipwa katika hizo shilingi bilioni 620 kwa maana ya VAT pamoja na Ushuru wa Bidhaa. Ushuru wa Bidhaa tunao-charge katika airtime ni asilimia 17 vilevile VAT ni asilimia 18 maana yake ni kwamba pale ni asilimia 35 yote ya hiyo volume imepotea, itakuwa Serikali imepoteza mapato lakini na mlolongo mwingine mwingi tu wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile msiwaache wale wananchi ambao walinunua vocha yao, wakaondoka, hawakuweza kurudishiwa. Wakanunua vocha, baadaye ile vocha ikawa haina thamani, ikaandikiwa hiyo vocha ulioingiza ilishatumika maana yake ni kwamba na wao walipoteza fedha hizo, kwa hiyo, fedha hiyo ilipotea katika uchumi. Katika shilingi bilioni 620, unaweza kujikuta kwamba ambayo ni mali ya *Vodacom* labda shilingi bilioni 120, then shilingi bilioni 500 yote, uchumi wa Tanzania utakuwa umeibiwa. Kama nilivyosema, Waziri wa Fedha anafanya kazi hiyo, Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia anafanya hiyo kazi, tutakapopata ushahidi wa kutosha, tutakuja sasa mbele ya Bunge kulieleza kwamba Tanzania imepoteza fedha kiasi gani katika mkataba tata wa *Shivacom* na *Vodacom Tanzania Limited*. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee sasa usimamizi wa uchumi nchini. Kama nilivyosema kwamba kuna usimamizi dhaifu sana wa uchumi, kwa sababu *parameters* zote za uchumi zinaonesha kwamba hazisimamiwi kikamilifu. Ukianza na mfumuko wa bei, tuna-enjoy sasa hivi, ni kweli na mimi napongeza, kwamba mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 4.4 Juni, 2012 lakini kufikia Desemba, 2014 mfumuko wa bei ulikuwa umefikia asilimia 4.8. Utata uliopo ni kwamba, kushuka kwa mfumuko huu wa bei hapa nchini hauna mahusiano na bidhaa

4 FEBRUARI, 2015

zinavyouzwa sokoni. Huu mfumuko wa bei unakuwa ni mfumuko wa tarakimu tu lakini bidhaa zinavyouzwa viwandani ziko vilevile tena zinapanda na bei, bidhaa zinazouzwa sokoni ziko vilevile tena zinapanda na bei. Kamati yangu inatafsiri kwamba kushuka kwa mfumuko huu ni kitarakimu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine Kamati inashangaa, hivi inakuwaje, Serikali kwa kujivunia kabisa, inahutubia ndani ya Bunge kwamba tumefanikiwa vizuri, bei ya chakula imeshuka. Serikali inashangilia, BOT wako happy wanasema bei ya chakula imeshuka na hivyo mfumuko wa bei umeshuka. Unashangilia hilo, mkulima wa Sumbawanga, Kisesa, Bariadi, mazao yake aliyoyazalisha yanaoza bila soko, yananunuliwa kwa bei ya kugalaliza lakini wewe unasema uko happy, hujui kwamba huyu mkulima anapokuwa na *low purchasing power* hawezi ku-consume. Sasa kama huyu haweze ku-consume, then wewe katika uchumi wako kodi utapataje? Kama mkulima mazao yake yanaoza, utapataje VAT inayopatikana baada ya ku-consume, utapataje ushuru wa bidhaa kama hawawezi ku-consume? Mazao yao yanaoza, Serikali ina furaha kwamba bei ya chakula imeshuka, mkulima anauza gunia Sh.20, 000/=, mkulima anakopwa mwaka mzima halipwi lakini unakuwa happy kwamba bei ya chakula iko chini na mfumuko wa bei umeshuka, then uchumi umepanda. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, riba za mabenki. Tumezungumza hapa kuhusu riba za mabenki na kila mtu analalamika mpaka na Serikali yenye inalalamika kana kwamba hakuna chombo ambacho kinaweza kikadhibiti riba nchini. Watanzania wamefilisika! Ukikopa benki huwezi kupata faida, riba ni asilimia 21 ukiweka na gharama zingine za uzalishaji huwezi kupata faida. Wewe utakuwa ni kibarua tu wa hizo benki lakini Mtanzania hawezi kukopa akapata manufaa kwa riba zinavyokwenda hivi sasa za asilimia 21 na wengine wanakwenda mpaka asilimia 22. Mwaka 1992, benki zilikuwa tano tu nchini leo benki zetu zimefikia 57, toka tano mpaka 57. Hata hivyo, Watanzania wanaopata mikopo

4 FEBRUARI, 2015  
ni asilimia 14 tu ya Watanzania wote licha ya utitiri wote wa hizi benki tu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa kwenye hoja ambayo Waziri wangu wa Fedha, Mheshimiwa Saada Mkuya alivyo sema kuhusu taarifa ya uaminifu. Nilisema asubuhi, hizi *parameters* zote ambazo zinasababisha riba kuwa juu, hazisababishwi na mabenki asilimia kubwa zinasababishwa na Serikali. Kwa mfano unasema kwamba unataka taarifa ya uaminifu kwa wananchi waliokopa benki. Nilizungumza asubuhi sasa hivi ni shilingi triliioni 3.6 Serikali imekopa wananchi wake, haiwarudishii, unategemea watalipaje mikopo yao benki! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazabuni na wakandarasi ni shilingi triliioni 1.3, hawa ndiyo wadau wakubwa wa benki, wanlipaje sasa hizo fedha kama Serikali umezichukua kwao, wanlipaje hayo madeni ya benki? Sasa unakataaje wewe Serikali kwamba wewe ndiyo unaye-facilitate suala la Non-Performing Loan (NPL), ni wewe unaye-facilitate. Umekopa fedha shilingi triliioni 3.6 haziko kwenye uchumi, umezishikilia Serikali. Zile zote ndiyo zinachangia kwenye hii taarifa ya uaminifu. Hata ukifanya hiyo credit reference bureau yako unayofanya, utakuta tu kweli watu hawalipi fedha, kwa sababu wamekopa benki, Serikali imewakopa haiwalipi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni kwamba, *treasury bills*, nilisema asubuhi, Serikali ina *float* hizo *bonds* zake sokoni kwa asilimia 15, wanauzwa mabenki yananunua. Kama wewe unatoa riba ya asilimia 15, hayo mabenki yatatoa riba chini ya hiyo? Kwanza ukichukua mkopo wa benki, yale mabenki yana uhakika kwamba hizi fedha ni za uhakikia, tutarudishiwa, hawawezi kuhangaika na Mzee Buhondo, wa kule Mwabusulu, eti yule Mzee waanze kum-trace ili waweze kumkopeshwa, wakati fedha zote ambazo mabenki haya yanakopeshwa au asilimia kubwa ya fedha zote zinazokopeshwa kwenye mabenki zinakopwa na Serikali kwa nini wakahaingaike na huyu mwananchi. Kwa vyovyote vile lazima wamwekee riba kubwa na lazima wasimjali wala

4 FEBRUARI, 2015

wasimfuatilie na ndiyo maana mpaka sasa hivi tuna asilimia 14 tu ya Watanzania ambao wanashughulika na hizi benki. Hata hivyo, Serikali mnakopa mno kwenye mabenki haya ya kibiashara. Sasa ukikopa kwenye mabenki ya kibiashara ndiyo hilo, linakwenda pamoja hilo, unatoa *treasury bill* ya asilimia 15 halafu unakwenda kukopa kwenye mabenki wewe mwenyewe, hawawezi kumpa nafasi mwananchi mwengine wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza suala la SMR (*Statutory Minimum Reserve*), kwamba ni asilimia 10 zinakuwa reserved na Benki Kuu, fedha zote za *private sector* ambazo ziko *deposit*, asilimia 10 zinakuwa reserved. Hii asilimia ni kwamba sana, kwa nini unafanya hivyo, huna *deflation*, kwa nini unafanya hivyo? *Principles* hizo za kiuchumi zinakupeleka pale kwa sababu gani, huna *deflation* kwenye uchumi wako. Kwa nini uwe na asilimia kubwa hivyo ya SMR? Unaweza kupunguza kabisa kutoka asilimia 10, ukafanya hata asilimia tano. Vilevile *treasury bills* za Serikali bora zikauzwa hata kwa asilimia 10 kuliko hiyo asilimia 15, mkitoa asilimia 10 ninyi, wale wafanyabiashara sasa hawawezi kufika huko kwenye ishirini na zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubadilishanaji wa fedha za kigeni, tumekuwa tukizungumza kila siku. Kila ukizungumza, Benki Kuu wana-defend kwelikweli, wanasema hakuna tatizo lakini hakuna tatizo, uchumi tunauona unaharibika! (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha yetu ya Tanzania inaporomoka kila leo. Mheshimiwa Mnyaa hapo alisema sasa ni Sh.1800 na zaidi, wengine wamenunua Sh.1820, haina thamani. Hii ni kwa sababu ya usimamizi wa uchumi wetu ambao hauko imara na haijulikani tunasimamia wapi. Tulishawashauri Benki Kuu mpaka tumechoka, ni kwa nini ninyi mna-apply hii *unofficial dollarization*, kwa nini mna-apply hii, kwa nini nchi zingine wako *smart* sana na hii *unofficial dollarization*, wako very *smart*. Ukipika *South Africa, Tanzania shilling* unaiacha hapahaha Tanzania, kwanza huwezi hata ukaenda nayo, wala dola yenye kipika nayo ni palepale *airport*, lazima utafute fedha yao ndiyo uingie Afrika Kusini

4 FEBRUARI, 2015

Iakini sisi tuko happy tu tunasema tukileta mambo haya sijui yatakuwaje. Tunayasikiliza hayo mambo na tunaheshimu hiki chombo cha Benki Kuu kama chombo cha wataalam lakini sasa mbona mambo hayawi mazuri? (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda siyo rafiki kabisa na nikimbilie suala la Kiwanda cha Maziwa cha *Tanga Fresh*. Mheshimiwa Waziri hapa amezungumza, namshukuru sana Mheshimiwa Shekifu amechangia, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tanga, mzee mzito, namheshimu sana na Mheshimiwa Waziri Waziri mwenyewe na Wabunge wengine ambao wameandika kwa maandishi. Nachotaka kusema tu ni kwamba, hapa Waziri wa Viwanda na Biashara hajatenda haki kwenye Kiwanda hiki cha *Tanga Fresh* na ye ye ni Waziri ambaye anatoka Tanga, kiwanda hiki ni cha washirika. FCC iko chini yake, hii Bodi inayozungumzwa iko chini yake, sisi tuliwaita kwenye Kamati, tukazungumza nao FCC, tukazungumza na *Tanga Fresh*. Hawa waliwapa *fine* hiyo ya shilingi milioni 406 Iakini kwa kiwanda ambacho kilishafungwa, viwanda vyote viwili vile walinunua mitambo ile viwanda vile vilishafunga biashara! Sasa inakuwaje leo Waziri atoe ahadi kwamba eti wakienda kwenye FTC itakwendakwisha wakati alishindwa kusimamia ilipokuwa kwenye FCC? Waheshimiwa Wabunge hatuna viwanda vya maziwa sisi hapa nchini. Viwanda vyetu tunavyo 22 na vyote viko *under capacity*, vina produce asilimia 30 tu, tunanunua maziwa ya kutoka Kenya, Wakenya wametugeuza kuwa soko lao na viwanda vyetu tunavipiga faini kwa makusudi ili tuviondoe kwenye soko ili Wakenya waweze kuedelea kutuuza maziwa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha *Tanga Fresh* ndiyo kiwanda pekee ambacho tunaki-refer kwa utoaji mzuri wa maziwa, unaweza ukaenda Dar es Salaam ukayakuta. Viwanda vya Arusha vilivyo vingi vimekufa kwa sababu ya ushindani wa Kenya na Wakenya wamekuwa wakitumia viwanda vyetu na yawezekana kabisa hata taasisi yetu ya FCC inaweza ikawa inatumiwa na Wakenya kuua viwanda hivi. (Makofii)

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuua kiwanda ambacho kwanza ni cha washirika, kinanunua maziwa yote ya Tanga na Mikoa mingine jirani, kwa makusudi yako, tena cha washirika, cha wananchi wa Tanzania wala siyo mwekezaji wa kutoka Ufaransa wala wapi. Wewe unataka mkawatoze faini ya shilingi milioni 400 kwa ajili ya kuja kulipana posho na matokeo yake, Watanzania wale wote ambao wanapata fedha hizo, wanashindwa kunufaika na fedha hizo halafu Waziri ambaye leo sisi tumependekeza Waziri wa Viwanda na Biashara, upewe viwanda vyote. Sasa kama utakuwa na tabia hii ya kuhujumu viwanda hata vile unavyovisimamia, itakuwa ni *problem!* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya wazabuni, wakandarasi, watumishi wa Mifuko ya Jamii na wakulima. Nimesema deni hilo limefikia shilingi trilioni 3.6. Sasa nataka niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge, unapoziondoa shilingi trilioni 3.6 kwa wananchi wako, umezishikilia Serikali, Serikali hulipi kodi, Serikali huzalishi, umezishikilia zile fedha! Ungeziruhusu zile fedha zikaenda kwa umma, ile shilingi trilioni 3.6, umewapokonya wananchi wako wazalishaji, umewapokonya wananchi wako wanaolipa kodi, hawawezi kulipa tena, hawawezi kuzalisha. Umepokonya ajira walizozizalisha, wanawafukuza watu sasa kwa sababu huna fedha unadaiwa na benki huwezi kuendelea kuajiri. Sasa kwenye ajira huko, ulikuwa unakusanya PAYE kila mwezi, wananchi wale wamefukuzwa, hawana kipato tena, hawawezi kufanya shughuli zozote za kiuchumi, hawawezi ku-consume, kama hawawezi ku-consume kama nilivyosema, huwezi kukusanya ushuru wa bidhaa na huwezi kukusanya VAT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa nchi mnausimamiae kwa upungufu mkubwa wa namna hiyo? Unakubali kuwanyang'anya wananchi wako purchasing power, unategemea sasa ufanye nini? Mbaya zaidi, unakwenda kunyang'anya mpaka wakulima maskini wale, unawanyang'anya kabisa fedha zao kwa sababu ambazo hata hazieleweki. Mpaka sasa hivi shilingi bilioni 74 wakulima wale wanadai. Hawawezi kupeleka watoto shule, hawawezi

4 FEBRUARI, 2015

kuchangia shughuli za maendeleo, tunataka wajenge zahanati, tunataka wajenge maabara, fedha Serikali umeishikilia. Wao waki-consume, wakinunua cement, wakinunua nondo, wakandarasi wakilipa madeni yao, sisi tunakusanya fedha! Sasa kwa nini tunafanya mzaha wa namna hii? Serikali tunaitaka, madeni haya...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti ahsante sana na kuna kiwanda sasa cha AZAM, kiwanda cha Dar Fresh na Watanzania tuwe na utaratibu wa ku-buy Tanzania.

Mheshimiwa Mpina hukutoa hoja.

**MHE. LUHAGA J. MPINA – MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maeleo niliyoyatoa, niliombe sasa Bunge lako Tukufu likubali mapendekezo ya Kamati na kuyapitisha kama ambavyo Kamati yangu ya Uchumi, Viwanda na Biashara imeyaleta hapa mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**WABUNGE FULANI:** Toa hoja.

**MHE. LUHAGA J. MPINA – MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutoa hoja.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, hoja imeungwa mkono, Mheshimiwa Zitto. (Makofii)

4 FEBRUARI, 2015

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda moja kwa moja au yote kwa pamoja?

**MWENYEKITI:** Hapana, soma moja moja, tutahoji moja moja.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Sawa!

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, mapendekezo yangu tuongeze ibara ya 4.6 mara baada ya ibara ya 4.5 na isomeke kama ifuatavyo:-

"Kwa kuwa sekta ya viwanda vya nguo ni muhimu sana kwa ajili ya kuongeza ajira na mapato ya fedha za kigeni;

Na kwa kuwa viwanda vya nguo nchini vimegubikwa na changamoto nyingi ikiwemo ukosefu wa umeme wa uhakika, kukosekana kwa vivutio na uingizaji holela wa nguo nchini;

Hivyo basi, Serikali ilete Bungeni mkakati maalum wa kuendeleza viwanda vya nguo kabla ya Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge na kuweka ratiba ya utekelezaji itakayojadiliwa na kupidishwa na Mkutano wa Bunge wa bajeti 2015/2016". (Makofii)

Waheshimiwa Wabunge, naomba mniunge mkono katika pendekezo hili, kwa sababu sekta ya nguo ni sekta ambayo bado hatujaifanyia kazi sawasawa na wakulima wa pamba, pamba yetu nyingi bado tunaipeleka nje, almost 80% kama alivyosema Mwenyekiti wa kamati. Kwa hiyo, naomba tuhakikishe kwamba tunaongeza thamani ya pamba yetu ndani kwa kuwa na mikakati maalum ya sekta ya nguo na viwanda vya nguo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pendekezo hili liweze kukubaliwa na Bunge lako Tukufu.

4 FEBRUARI, 2015

**MHE. LUHAGA J. MPINA – MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mwenyekiti mwenzangu, kijana mwenzangu Mheshimiwa Zitto Kabwe kwa hoja aliyoitoa na mimi pendeleko lake nalikubali kwa niaba ya Kamati kwa asilimia mia kwa mia. (Makof)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kujua tunafanyaje kuhusu utaratibu na utaratibu ni ule ambao unaweza ukatumia pia kwa kutumia Kanuni ya 5, kwa mujibu wa uzoefu wa uendeshaji shughuli za Bunge na ambao tumekuwa tukiutumia toka tumeanza kujadili ripoti hizi za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya hivyo, tumekuwa tukipokea mabadiliko ama marekebisho ya mapendekezoo yanayotolewa na Kamati kuititia kwa Wabunge ama Kamati zenyewe na sisi Serikali pia tulikuwa tukipewa nafasi ya kujaribu kuona, maana sisi ndiyo watekelezaji, kujaribu kuona uwezekano wa utekelezaji wa maagizo hayo kwa mujibu wa utaratibu utakavyokuwa umeelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo, nikirejea kwenye hili pendeleko lilitotolewa na Mheshimiwa Zitto ambalo ni pendeleko zuri sana na ni pendeleko ambalo linaini Serikali iangalie na iijitayarishie utaratibu hasa wa kuona ni namna gani inathamini uwepo wa viwanda vya nguo hapa nchini na kwa kweli Bunge, kwa mujibu wa Kanuni, taratibu na kwa mujibu wa Katiba, lina nafasi hiyo ya kuishauri Serikali na kuona Serikali inatekeleza ushauri na kuona Serikali inatekeleza ushauri huo. Hata hivyo, kwa ukweli kabisa, Mkutano huu ndiyo tunaumaliza wiki hii na baada ya hapo tuna wiki chache sana za kufanya maandalizi yote ambayo yanatakiwa pia kuingia kwenye Mkutano wa Kumi na Tisa. Jambo hili halitakiwi kuja likiwa halijakamilika na kufanyiwa kazi ya kutosha. (Makof)

4 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaondoka hapa tukiwa tumekubaliana Mkutano ujao Serikali ije na kitu hiki bila kufanya maandalizi hayo ya kutosha halafu matokeo yake Serikali itaonekana haitekelezi wajibu wake vizuri. Tunakubaliana na hoja hii lakini kwa hakika, kwa dhamira safi na kwa mapenzi yote ya maendeleo ya nchi yetu, Mkutano huo unaokuja ni muda wa karibu sana wa kufanya kazi hii. Tunaomba mtuachie sisi Serikali, Kamati inayohusika na hoja hii ipokee mapendekezo ya awali ya Serikali kushughulikia jambo hili wakati wa vikao vya Kamati na kama itaonekana hoja hiyo inawezekana ietwe na kama itakuwa bado basi Serikali iendelee kuifanyia kazi na taarifa zije kuletwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupendekeza hilo.  
(Makof)

**MHE. LUHAGA J. MPINA – MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dada yangu hapa mimi namheshimu sana lakini tatizo la umeme la nchi hii linajulikana na wenyewe viwanda ukisoma kwenye ripoti pale wamekuwa wakiilalamikia Serikali kila siku kwa jinsi wanavyopata hasara. Wenyewe viwanda wamelalamika uingizaji wa bidhaa holela nchini, vyombo vya kudhibiti bidhaa kuingia holela nchini viro na vinafanya kazi kila siku. Hili jambo linalozungumzwa hapa si jambo jipya kwa Serikali, ni suala tu la kuja na mkakati. Kama ambavyo Kamati yangu ilipendekeza pale kwamba inakuwaje kama tuna kilometa 1,424 ule ukanda wa Bahari ya Hindi lakini tuna Wanajeshi wetu, sheria zinasemaje, hao Wanajeshi wetu hawawezi kutulindia huu ukanda? Tuna tatizo la umeme, je, hatuwezi kuja na mkakati wa sasa badala ya kusubiri huo uwekezaji mkubwa tunaoufanya wa kutuletea umeme nchini walau tukawanusuru hawa wafanyabiashara, walau kupunguza maana hatuwezi kuzimaliza zile hasara ambazo wanazipata kwa sasa lakini walau tuka-minimize ile *risk* yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jambo ambalo Serikali inaomba hapa ipewe muda ni jambo lipi, kwa sababu vitu hivi vyote viko kwenye order. Uingizaji wa bidhaa holela iko

4 FEBRUARI, 2015

TBS, iko FCC wanafanya kazi gani? Polisi wapo wanafanya kazi gani? Tatizo la umeme wanawasilishiwa Viwanda na Biashara na Serikali kwa ujumla wanalijua. Sasa unataka muda gani mwengine wakati nchi hii ina matatizo makubwa? Yeye Mheshimiwa Waziri na mimi tunamaliza muda wetu wa Ubunge, tuache tatizo hili tumelitatu. (*Makofii*)

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Mpina alivyosema ananiheshimu na mimi ninamheshimu sana Mheshimiwa Mpina. Ninasema namheshimu Mheshimiwa Mpina kwa maana kubwa ifuatayo. Mheshimiwa Mpina mara zote amekuwa akihangaaika kuishauri Serikali kufikia katika malengo yenye nia njema kabisa kwa maendeleo ya Taifa la Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mpina amejumuisha vitu vingi katika kujenga hoja ya kurejea katika msimamo huu ambao ameuleta mbele ya Kamati. Yale mengine sina matatizo nayo na wala sikatai kwamba Serikali haitakwenda kuleta taarifa hiyo mbele ya Kamati kushughulikia suala hili na wala hatukatai kwamba Serikali ina wajibu wa kuhakikisha kwamba tatizo hili linakwisha moja kwa moja kama siyo kulipunguza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba sana Mheshimiwa Mpina, sisi kama Serikali tutaleta taarifa hiyo...

## **TAARIFA**

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hebu subiri kwanza.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Taarifa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Subiri Mheshimiwa.

4 FEBRUARI, 2015

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tunasema tutaleta taarifa hiyo katika vikao ambavyo vitaandalisti vya maandalizi katika Mkutano huo wa Kumi na Taisa. Kama itakuwa imekamilika, tutaitaarifu Kamati na kama itakuwa haijakamilika, Kamati itatuelekeza nini cha kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuendelea kutoa msisitizo kupelekea maagizo haya ya tuwe tumemaliza kuhitimisha mpango huo katika Mkutano unaokuja, naomba nieleweke hivyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri wa Biashara.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo hili nami naliunga mkono lakini kimantiki kwa maana ya logically kuleta taarifa hii katika kikao kijacho kwa vyovoyote vile itakuwa vigumu. Kwa sababu ziko taasisi nyangi zinahusika hapa, kuna mambo ya umeme, matatizo ya umeme sisi sote tunayafahamu hapa, kuna mambo ya bandari bubu, *involvement* ya hizo bandari bubu udhibiti wake tunaufahamu. Kwa hiyo, mimi napendekeza kwamba muda huu ni mfupi kufanya kazi suala hili labda Mkutano wa Ishirini ndio tunaweza kuleta taarifa nzuri zaidi kuliko Mkutano wa Kumi na Tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja hiyo.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali Mkutano wa Ishirini. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Zitto ana mapendekezo mawili, nitawahoji moja baada ya lingine. Moja ni hili la ongezeko la ibara ya 4.6 pamoja na kukubali pendekezo lake lifanyiwe kazi Mkutano wa Ishirini.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)

4 FEBRUARI, 2015

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu la pili, naomba kuongeza ibara ya 4.1.3 mara baada ya ibara ya 4.1.2 na isomeke kama ifuatavyo:-

*"Kwa kuwa uwekaji akiba nchini (savings) upo chini yaani asilimia 16 tu ya pato la Taifa kwa sababu ya Hifadhi ya Jamii nchini kutofikia wananchi wengi zaidi;*

*Hivyo basi, Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha mfumo wa matching ambapo mwananchi anayechangia kwa hiaru katika Hifadhi ya Jamii atachangiwa kiasi fulani na Serikali kama kivutio cha kuchochea uwekaji akiba na mfumo wa pensheni nchini".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la pendekezo hili na kwa sababu linahitaji kufanyiwa stadi na ndiyo maana nimesema Serikali iangalie uwezekano, ni kwa sababu tumesikia hapa mjadala wa financing, uwezo wa wananchi kufikia taasisi za kifedha ni mdogo sana. Hivi tunavyozungumza ni Watanzania milioni moja tu ambao wamo kwenye Mifuko ya Hifadhi ya jamii. Kwa hiyo, kuna Watanzania wengi sana ambao hawafaidiki na hawapati access ya Hifadhi ya Jamii, kwa hiyo hawako covered.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna juhudhi ambazo zinafanya hivi sasa za kuweza kuwafikia Watanzania wengi zaidi, wakulima...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto samahani, nimeongeza muda kwa mujibu wa Kanuni.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakulima, wafugaji na kadhalika ili waweze kuwa covered na Hifadhi ya Jamii na wapate bima ya afya na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwa kuwa Kamati hii ndiyo inahusika na Sera za Hifadhi ya Jamii

4 FEBRUARI, 2015

na Kamati imezungumzia namna gani ambavyo Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inavyofanya kazi. Kamati hii inasimamia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii mitatu, GEPF, PPF na PSPF, nikaona kwamba nilete kwa Waheshimiwa Wabunge pendekezo hili ili sasa Serikali iweze kuangalia hiyo possibility ya kufanya matching kwa wananchi ambaa wanachangia kwenye Hifadhi ya Jamii kwa hiari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Bunge lako Tukufu likubaliane na pendekezo hili.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mapendekezo haya ya Mheshimiwa Zitto kuna mambo mawili ambayo ndiyo key. Moja, anawazungumzia wale wanaochangia kwa hiari. Katika hilo maana yake anatafuta kujenga ukubwa na upana wa Hifadhi ya Jamii kwa hiyo Serikali iweke some matching fund. Pendekezo la pili, anaitaka Serikali ikaangalie uwezekano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi hili si wazo baya na katika mfumo wa pensheni ambaa tunataka kuujenga ili uwe na nguvu zaidi na wachangiaji wengi zaidi, ni sawa. Kwa hiyo, kimsingi kama tunakubaliana, kama tulivyosema juzi wakati tunajibu swali hapa, tulisema kabisa kwamba Serikali inaangalia uwezekano wa kupanua mfumo wa hifadhi ya jamii kwa lengo kwamba mfumo uwe mkubwa zaidi. Sasa hii ni moja katika mikakati hiyo, nadhani Serikali itakubaliana na pendekezo hilo kama tunaelewana katika misingi hii ya kwamba tunakwenda kuangalia uwezekano na kulifanyia kazi na tutalitolea taarifa mbele ya safari. (Makof)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane mkono na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Adam Malima kwa maelezo hayo ya Serikali, kwamba hakuna tatizo kwa Serikali kwenda kuangalia

4 FEBRUARI, 2015  
uwezekano wa kutengeneza huo mfumo mpya wa hifadhi ya jamii kwa kuangalia uwezekano huo kama upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitaomba tu katika kuchukua *Hansard* ya mapendekezo haya, lugha ya Kibunge sidhani kama hii inatupelekea kwenye mapendekezo ama maazimio. Unapoanza na kwa kuwa, hivyo basi, haya ni maazimio. Sasa *Hansard* itakapokuwa inachukua lugha hii ya Kibunge katika maeneo hayo, nadhani ni tatizo tu dogo hilo, ili tubaki katika *concept* yenye we iliyojengwa kama pendekezo ambalo sisi Serikali tunalichukua.

**MWENYEKITI:** Kitu kikubwa mmekubali, hicho ndicho kitu muhimu. Niwapongeze maana mngekataa tungewashangaa kwelikweli maana mmeambiwa muangalie halafu mlete. Hata hili la kwanza vilevile, Serikali msijivekee caveat, kila saa mnajivekea ugumu, open up to ideas nchi hii ndiyo itakwenda vizuri, nawashukuru mmekubaliana na yote. Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. LUHAGA J. MPINA – MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina tatizo na pendekezo hilo la Mheshimiwa Zitto Kabwe la kuongeza ibara ya 4.1.3. Kwa nyongeza ni kwamba maazimio yaliyoletwa ni kumi na moja, yako kumi na mbili na ndiyo maana Mheshimiwa Zitto Kabwe pale amesema yeye ni 4.1.3. Sasa azimio namba 4.1.2 halipo.

**MWENYEKITI:** Eeeh, sawa. Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji. Mheshimiwa Zitto una la kusema tena?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** (*Aliongea nje ya kipaza sauti*)

**MWENYEKITI:** Serikali haiwezi kusimama wakati mimi nimesimama. Haya, simama sasa. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Labda suala tu la utaratibu, tulikuwa tunataka kufahamu kwamba mapendekezo ya Mheshimiwa Zitto yanakwenda sambamba na mapendekezo haya ya Kamati? Kwa sababu

4 FEBRUARI, 2015

sisi kama Wizara vilevile tulikuwa kidogo tuna mchango wetu katika mapendekezo haya. Kama tukipata hiyo nafasi ya kwenda katika pendekezo moja baada ya lingine itakuwa vizuri, kwa ruhusa yako Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Eeh, soma.

**WAZIRI WA FEDHA:** Ahsante. Sisi kama Serikali tunaona hili pendekezo la kwanza la Kamati limetufunga sana kwamba tuje na huo mkakati mahsus wa kupunguza na kudhibiti viwango vya riba ambavyo vinatozwa na Benki kabla ya Mkutano wa bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016 na Mkutano nadhani katika Mkutano wa Kumi na Tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika notion ileile ya kuwa kwamba hii ni kazi kubwa na ina mambo mengi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hiyo ya kwanza iache kabisa, imeshapita, wewe nenda ya pili sasa. Kwa sababu hiyo ya kwanza walikubali Serikali wenyewe. Kwa hiyo, sasa tuko katika hoja ya pili ya Mheshimiwa Zitto. Hoja ya kwanza imeshapita na Bunge limeshahojiwa limesharidhia. *No retreat, no surrender. (Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri, with due respect, mngeyasema haya wakati bado sijalihoji Bunge lakini sidhani kama lina uzito wowote. Hii sasa ni changamoto kwa watendaji wa Serikali kuanza kufanya kazi hizi, kuja na mikakati, Bunge la Ishirini kama bado hamjajiandaa mnatoa ripoti Bungeni, mambo haya bado tunaendelea nayo na *Inshallah* Serikali ijayo ukiwepo wewe tutakwenda nayo. Government moves, Serikali haikai tu, kwa nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Zitto huna lolote, umeridhika?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Ndiyo!

4 FEBRUARI, 2015

**MWENYEKITI:** Sasa nitawahoji kuhusu pendekezo hili la Mheshimiwa Zitto ambalo limeungwa mkono na Serikali pamoja na Mwenyekiti.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kafulila.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu la kwanza ni kwenye 4.1, kwamba:-

“Serikali ipunguze riba kwa mauzo ya dhamana za Serikali kwa kiwango ambacho kinakaribiana na riba inayolipwa na benki ili benki zione tija ya kukopesha sekta binafsi badala ya Serikali kwani ndiyo msingi wa uanzishwaji wa benki za biashara na kuondoa hali ya sasa ambapo Serikali inashindana na sekta binafsi kukopa ndani”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uksoma kwenye pendekezo la Kamati utaona kwamba kuna tatizo la riba kubwa, kwamba benki za biashara zinatoa mikopo kwa riba kubwa. Sababu kubwa ya kwa nini benki za biashara zinatoa mikopo kwa riba kubwa ni kwa sababu Serikali inapouza dhamana zake inaziuba kwa riba ya juu. Kwa hiyo, benki ya biashara inakuwa ina njia mbili za kuamua. Njia ya kwanza ni kuikopesha sekta binafsi na njia ya pili ni kuikopesha Serikali kupitia dhamana zake ambazo inaziuba. Sasa kama Serikali inauza dhamana kwa riba ya juu inakuwa inatoa tija zaidi kwa benki ya biashara kwenda kununua zile dhamana za Serikali badala ya kukopesha sekta binafsi. Kwa maneno mengine ni kwamba Serikali na sekta binafsi zinashindana kukopa kwenye benki ya biashara. Sasa kwa sababu benki ya biashara inaona kwamba Serikali ina guarantee kubwa ya kulipa kuliko sekta binafsi inakuwa ni vyepesi kwa benki ya biashara kuikopesha Serikali kuliko kuikopesha sekta binafsi.

Mheshimiwa mwenyekiti, kwa hiyo, pendekezo hili lengo lake ni kuweka uwanja sawa au kupunguza nafasi ya Serikali kukopa ndani zaidi kiasi cha kuathiri nafasi ya sekta

4 FEBRUARI, 2015

binafsi kukopa ndani. Kwa hiyo, naomba Bunge lako Tukufu lione mantiki hiyo ya kupunguza ushindani kati ya Serikali na sekta binafsi kwenye kukopa na tuongeze nafasi ya sekta binafsi kukopa zaidi kwenye benki za biashara kuliko hali ya sasa kutokana na muundo wa dhamana hizi.

**MWENYEKITI:** Mmemuelewa lakini hoja yake? Ukitaka kukataa unasema. Mmeielewa hoja yake kwa sababu Serikali sasa inaingia ushindani na watu. Wao wanaweka riba kubwa, mabenki sasa hawana *interest* ya kukopesha watu ambao hawana uhakika wa kurudisha. Kwa hiyo, *they are running to the government, treasury bonds za Serikali, wanapata uhakika wa kulipwa pesa zao.* (Makof)

Hoja ya huyu Bwana anasema, Serikali sasa ifikirie vilevile wananchi wake ambao na wao wanataka kukopa. Saa ninyi jibu lenu 'yes' or 'no', Bunge tutalihoji hapa, ndiyo kazi ya Bunge, Mheshimiwa Waziri wa Fedha!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, narejea tena, kwa ushauri wako pendekezo si pendekezo bayo lakini ile *balance ya factor ya kwa nini benki hizi zinaweka riba hii, siyo function ya government securities na treasury bonds peke yake, kuna elements nyingi.* Sasa ukiniambia kama hizi *interests rates zina elements ya syndication* hapo nitakubali kwamba labda watu wanakaa wanasema ziwe na element hiyo, hapo nitakubali na kwamba hazina *any competitive structure ama market structure,* hiyo nitakubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nasema hivi, kwa kuwa Benki Kuu ndiyo ina *banking supervision function,* tutakwenda tutakaa nao, pamoja na Serikali, sisi watu wa Hazina na Benki Kuu na kuangalia hii *function ya financial management,* kwa maana ya Serikali na *level ya interest rates* na kuangalia kama *zina effect* kubwa. Namuomba tu Mheshimiwa Mbunge aelewewe kwamba siyo *function* tu peke yake ya *treasury bills,* kuna *element ya risk inategemeana* na sekta gani na *economic activity* lakini *kwamba inaondoa motivation* ya watu kushiriki, labda kweli, wacha twende

4 FEBRUARI, 2015  
tukazifanyie kazi. Ni wazo zuri sana, tunaenda kulifanyia kazi pamoja na Benki Kuu na tutarejea kutoa maelezo.

**MWENYEKTI:** *No, no, yeye imependekeza Serikali sasa ni mawili, mnaichukua inabakia kama pendekoz, you are going to work on it, kama haifai mnakuja kusema, no, hiki kitu hakiwezekani kuna factors nyingi kwenye kukopa, siyo tu suala la riba na mambo mengine. Kwa hiyo, mimi nataka nijue je, mnalikubali ombi lake, mnakwenda kulifanyia kazi, if it is workable mnasema yes, sawa lakini haifanyi kazi kwa sababu component siyo hiyo tu anayoizungumzia Mheshimiwa Mbunge kuna mengi kadha wa kadha ambayo yata impair function ya Serikali na mabenki na private sector.*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K.A. MALIMA):**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uelewa huo tunakubali kwamba Serikali inaenda kufanyia kazi uwezekano wa kupunguza riba ili pawe na structure inayofanana baina ya riba hizi za government bonds na zile nyingine. Ni wazo zuri kwenda kulifanyia kazi halafu turudi kutoa taarifa lakini siyo hivi ilivyoandikwa hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. LUHAGA J. MPINA – MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ile hoja mama ya pendekoz hili liliopendekezwa, hoja ya Mheshimiwa Kafulila imo humo ndani. Nimshukuru pia Naibu Waziri alivyojibu, ndiyo maana tumeiweka hivi tukijua kwamba item za kupunguza riba ni nyingi sana. *Treasury bills* tumezungumza, kuna suala la mikopo ya wazabuni na wakandarasi, nalo tumeagiza. Vilevile tuna kile chombo cha Benki Kuu ambacho nao katika ripoti hiyo, kwa sababu hii ripoti lazima itaeleza, lazima waseme *treasury bills* kwa nini ni 15, kwa nini isiwe 8 au 5, watatueleza. Bahati nzuri Mheshimiwa Kafulila yeye ni Mjumbe wa Kamati hii ya Uchumi, Viwanda na Biashara, kwa hiyo, tutapata hayo manufaa ya kuipokea hii taarifa yenyewe kwa sababu katika hiyo taarifa hili azimio namba 1, hiyo *TBs* itakuwemo na watatueleza kwamba kwa nini siyo asilimia 10, ni kwa nini asilimia 15, tut-

4 FEBRUARI, 2015

debate nao na tutafikia muafaka. Kwa hiyo mimi nimshauri Mjumbe wangu wa Kamati akubaliane kwa sababu hili pendekezo alilolitoa liko-covered katika hili pendekezo namba 1.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, mmeridhika. Kwa kweli hapa tunabadilisha maneno tu, Serikali itakaa na BOT kutizama *the way forward...*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):**  
Basi.

**MWENYEKITI:** Pamoja...

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali hiyo tumeridhia kwamba Serikali itaangalia uwezekano wa kufanya kazi. Hiyo kauli inaondoa hii kauli ya kwamba Serikali ikapunguze riba, hiyo haiwezikani lakini Serikali ikafanyie kazi uwezekano wa kupunguza riba ili hizi zifanane, inawezekana hili tunalipokea. (Makofij)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kafulila.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na mawazo ya Mheshimiwa Malima kwamba Serikali ikaangalie uwezekano huo wa kupunguza riba za TBs ili kupunguza ushindani wa Serikali na sekta binafsi katika kukopa kwenye benki za biashara.

**MWENYEKITI:** Sasa nitawahoji hoja hii ya Mheshimiwa Kafulila katika marekebisho yake, hii ya (a), tunatoa maneno ipunguze tunaweka maneno Serikali itakaa na vyombo vyake ili kutizama uwezo wa kufikia muafaka wa kuweza kupunguza riba hizi.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

4 FEBRUARI, 2015

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kafulila, endelea na hoja yako ya pili.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ya pili ni kuongeza maneno mapya katika azimio la 4.3 na isomeke kama hivi ifuatavyo:-

“Serikali ikamilishe Kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Madini ya mwaka 2010 ili migodi yote iorodheshwe kwenye Soko la Mitaji la ndani DSE, ili mapato na matumizi yawe wazi na hivyo Serikali ipate kodi sahihi tofauti na hali ilivyo sasa ambapo hakuna uwazi na hivyo kuziba mwanya wa utoroshaji wa madini na ukwepaji wa kodi”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa pendekezo hili ni kukumbusha tu Bunge Tukufu kwamba mwaka 2010 lilipitisha Sheria ya Madini ambapo moja ya pendekezo muhimu kabisa kwenye kuhakikisha migodi inalipa kodi sahihi au Serikali inapata mapato sahihi kutoka kwenye migodi, ili kuwa migodi iorodheshe hisa zake kwenye Soko la Mitaji. Kuna faida mbili za kuoroshesha. Faida ya kwanza na muhimu kabisa ni kwamba hesabu za mgodi au kampuni zinakuwa wazi. Zikiwa wazi maana yake inakuwa ni rahisi Serikali kujua kwa usahihi mapato na matumizi na kwa hiyo inatoa nafasi kwa Serikali kujua faida sahihi ya mgodi au kampuni. Kwa kujua faida sahihi ya mgodi au kampuni inaiweka Serikali kwenye mazingira ya kujua kodi sahihi ambayo mgodi unapaswa kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sheria ilipitishwa mwaka 2010 lakini mpaka leo Kanuni za kuifanya Sheria hii itekelezwe hazijaandaliwa. Kwa hiyo, kwa takriban miaka mitano Serikali imeshindwa kuandika Kanuni za kufanya sheria hii iliyopitishwa na Bunge hili lenye heshima itekelezwe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kafulila umeeleweka.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Kwa hiyo, ndiyo msingi wa pendekezo hili. (Makof)

4 FEBRUARI, 2015

**MWENYEKITI:** Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES**

**M. KITWANGA):** Mheshimiwa MwenyeKITI, kwanza nianze kumfahamisha Mheshimiwa Kafulila kwamba hii migodi iko mingi sana, kuna migodi midogo, kuna migodi ya kati na kuna migodi mikubwa. Hizi multinationals nydingi zimekuwa listed katika Stock Exchange za nje na hivyo zina publish very transparently. Kwa hiyo, suala la Kanuni tunalifanyia kazi na tutaendelea kulifanyia kazi na siyo tu katika eneo la kuli-list kwenye Stock Exchange. Ku-list kwenye Stock Exchange, kuna mambo mengi ambayo anapitia. Ni lazima kwanza kampuni yenyewe ikubalike na Capital Market Authority, mahesabu yake yaye yamekaguliwa na kukubalika angalau kwa miaka mitatu. Kwa hiyo, hapa tukubaliane tu kwamba Serikali inaendelea kuboresha Kanuni zake kuhakikisha kwamba kile ambacho anadhani kitasaidia zaidi katika transparency, hata sasa hivi baadhi yake kipo. Vilevile tumeongeza uwazi zaidi kwa kuhakikisha kwamba TMAA inakagua na inaweka wataalam kwenye migodi ambayo tunaiona ni mikubwa ili kuhakikisha kwamba Serikali inapata mapato yake kulingana na sheria iliyopo ya mwaka 2010.

**MWENYEKITI:** MwenyeKITI wa Kamati.

**MHE. LUHAGA J. MPINA – MWENYEKITI WA KAMATI YA**

**UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa MwenyeKITI, Mheshimiwa Naibu Waziri hawezi kutueleza hadi leo mwaka 2015 bado anatengeneza Kanuni. Sheria hii ni ya mwaka 2010 tulipitisha hapa na tulishauriwa sana. Lengo letu kubwa tulitaka tuone ushiriki kwa sababu hawa waki-list share zao pale DSE, itawezesha pia licha ya suala la uwazi wa hesabu zao lakini utawazeshaa Watanzania kushiriki katika uwekezaji wa miradi hiyo mikubwa ya madini. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri hawezi kutueleza leo toka mwaka 2010 mpaka 2015 bado wanatunga Kanuni, ni Kanuni gani hizo? (Makofij)

Mheshimiwa MwenyeKITI, nalishauri Bunge lako kwamba hii hoja ya Mheshimiwa Kafulila imekuja muda muafaka na tumeishauri Serikali mara nydingi, wamekuwa

4 FEBRUARI, 2015

wakitoa ahadi ya kwamba Kanuni zitatumwa leo hii imepita miaka minne uneleza kuhusu Kanuni. Nadhani sasa ni muda muafaka tuweke azimio ambalo ni sheria ili tuilazimishe Serikali kutekeleza suala hili. (Makof)

**MWENYEKTI:** Serikali!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaangalia maelezo ya Mheshimiwa Kafulila na ya Mwenyekiti wa Kamati lakini hayatofautiani sana pia na maelezo ya Naibu Waziri mwenye dhamana ya shughuli hizo za madini katika Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili kwa kweli ni jambo la kimsingi na ni muhimu sana. Sisi kama Serikali tunafikiri, kwa kuwa sasa tunaenda katika kufanya marekebisho na kuboresha Kanuni hizo mbalimbali, tunalichukua pendeleko hili ili kusudi liweze kufanyiwa kazi. Tutaona ni namna gani linaweza kuendana na matakwa ya kisheria kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyosema lakini na mapendekezo haya tunafikiri ni mapendekezo muafaka. Kwa hiyo, nadhani halitakuwa na matatizo lakini litafanyiwa kazi kwa kiasi cha kutosha kulingana na zile taratibu na hali halisi iliyopo kwa wakati tuliona sasa. (Makof)

**MWENYEKTI:** Mheshimiwa Zitto, kuna lingine, Serikali wameshakubali.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo wamekubali lakini kuna vitu ambavyo inabidi ku-clarify ambavyo Mheshimwia Naibu Waziri amezungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, ni kweli kwamba makampuni mengi *multinationals* yame-list katika Stock Exchange za nje na siyo za ndani. Ni vigumu sana kwa Watanzania kuweza kushiriki kwenye umiliki kwenye Stock Exchange za nje kwa sababu hata *capital market* na *capital accounts* Tanzania haijafunguliwa. Kwa hiyo, ni lazima upate kibali cha Gavana wa Benki Kuu ili uweze kwenda kununua

4 FEBRUARI, 2015  
hisa katika London Stock Exchange au huko nje. Within East Africa ndiyo imefunguliwa mwezi Julai, 2014, hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili na natilia nguvu hoja ambayo Mheshimiwa Kafulila ameizunguza, hizi multinationals zina subsidiaries hapa Tanzania. Kwa mfano, Barricks Gold ambayo sasa hivi sijui inaitwaje, maana kazi yao kubadilisha majina tu, ina migodi mitatu. Tunachokisema, huu mgodi mmoja mmoja, Bulyankhulu, Buzwagi, North Mara, ziwe listed kwa sababu kila mgodi una MDA yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili Sheria ya Madini ilieleza clearly, ya mwaka 2010 kwamba migodi mipya yote itakayoanzishwa kuanzia hivi sasa itafuata utaratibu huo na Serikali kuwa na hisa. Hivi sasa kuna migodi kadha mipya ambayo Serikali imeshatoa special mining licence.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nafikiri na nakubaliana na Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba tukubaliane na hoja ya Mheshimiwa Kafulila ili kuwezesha migodi hii iweze kuwa listed katika Soko la ndani la Hisa ili Watanzania wawezé kumiliki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge).

**WABUNGE FULANI:** Kakubali.

**MWENYEKITI:** Kuhusu muda jamani, mimi ndiyo naongoza Bunge sasa ninyi mnasema kakubali, kakubali nini, kakubali kuongeza muda. (Kicheko)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERÀ, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshasema jambo hili...

**MWENYEKITI:** Nachokuomba utoe hoja ya kuongeza muda mpaka tutakapomaliza shughuli yetu.

4 FEBRUARI, 2015

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni, naomba Bunge lako litumie nafasi hii kuongeza muda wa shughuli hizi mpaka pale tutakapokuwa tumezimaliza, kwa umuhimu wa shughuli yenyewe na ratiba ya Bunge fuliyonao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
(Makofi)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Haja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na kazi. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuliona hilo lakini vilevile hoja ya Wabunge, najua Serikali ina nia njema, namshukuru sana Mheshimwia Naibu Waziri wa Nishati na Madini, ni mtu ambaye anajali mastahili. Vilevile pitieni kuna Dodd-Frank Act ya Marekani ya 2010 ambapo Marekani wenyewe wametunga sheria kuzisaidia nchi maskini, makampuni *multinationals* za nje ya disclose mapato yao kwenye Serikali ya kule ili sisi tujue, sasa wakati mwingine sisi wenyewe tunajiwekea *caveat*, hatutaki. (Makofi)

Someni *Financial Times* ya jana, Marekani wanataka kuweka sheria kutoza asilimia 11 ya faida ya makampuni yaliyoko nje ya Marekani yajenga miundombinu Marekani. Kwa nini wasijenge kwetu wakati madini yako kwetu? (Makofi)

Sasa nitawahoji...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

4 FEBRUARI, 2015

**MWENYEKITI:** Sasa nitawahoji kuhusu pendekezo la Mheshimiwa Kafulila ambalo Serikali imeridhia kulifanya kazi na imeona umuhimu wake.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kafulila.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili la (c), kwa sababu tayari Serikali imekubali pendekezo la Mheshimiwa Kabwe la kuja na mkakati wa jumla kuhusiana na sekta hii, nadhani katika mkakati huo hili pendekezo la tatu litakuwa ndani yake, kwa hiyo, nina-withdraw. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Serikali!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaridhia kwa sababu tayari tulishatoa maelezo na tulisema tutakuwa tayari katika Mkutano wa Ishirini. Kwa hiyo, basi katika Mkutano huo tutayatizama yote kwa upana wake.

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti wa Kamati!

**MHE. LUHAGA J. MPINA – MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nilitaka kumshauri hivyo Mheshimiwa Kafulila kwa sababu limekuwa covered katika lile pendekezo la Mheshimiwa Zitto ambalo tumekwishalipitisha kwa hiyo sina tatizo. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali, yale mambo muhimu mmeyakubali lakini nichukue nafasi hii kuipongeza Kamati na nampongeza Mheshimiwa Kafulila na Mheshimiwa Zitto kwa hoja zenu ambazo zilitaka kuboresha hoja ili kuleta mafanikio katika nchi yetu.

4 FEBRUARI, 2015

Nilikuwa niyaseme haya baada ya kuwahoji kama mnakubali taarifa ya Kamati pamoja na mapendekezo na marekebisho yaliyofanyika, maana mnaweza mkakataa lakini nimeona bora niliseme hili kwanza ili muone umuhimu wa kukubali, sasa nitawahoji.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Bunge liliridhia Taarifa ya Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara pamoja na maoni, mapendekezo na marekebisho yaliyofanywa kwenye Taarifa hiyo)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, leo asubuhi kulikuwa na Mwongozo wa Mheshimiwa James Mbatia kuhusu Hoja ya Dharura ambapo alitaka Bunge liijadili lakini Kiti kiliona umuhimu wa kulijadili jambo hilo kwenye Kamati ya Uongozi ambapo ndipo tunapokaa na kuweza ku-digest mazungumzo yote na kuyapatia muafaka.

Leo asubuhi tulikaa, walikuja Mheshimiwa Mbatia ambaye ndiye mtoa hoja pamoja na Wajumbe ambao yeye aliomba waje na Kiti kilikubali kwa maana ya kutafuta muafaka ili nchi yetu tusiingie kwenye migogoro, wala tusiingie kwenye matatizo, tuwe na uchaguzi wa amani, atakayeshinda awe ameshinda kutokana na mikakati yake ya haki na uchaguzi uwe *fair and free*. Kwa hiyo, sasa natoa Mwongozo wa hoja ya ombi lake.

Maelezo mafupi ya Mwenyekiti wa Bunge kuhusu maamuzi ya Kamati ya Uongozi juu ya Hoja ya Dharura iliyotewa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka leo asubuhi nililazimika kuitisha kikao cha dharura cha Kamati ya Uongozi, kufuatia Hoja ya Dharura iliyotolewa Bungeni na Mheshimiwa James Mbatia. Mheshimiwa Mbatia pamoja na mambo mengine alitoa hoja yake kwa kueleza kuwa jana tarehe 3 Februari, 2015, Tume ya Uchaguzi imeanza kutoa elimu kwa wananchi juu ya zoezi la uandikishaji katika Daftari la Kudumu

4 FEBRUARI, 2015

Ia Wapiga Kura katika baadhi ya maeneo nchi kama Mikoa ya Lindi, Mtwara na kadhalika bila kuwashirikisha kwanza wadau muhimu katika jambo hilo ikiwa ni pamoja na Kituo cha Demokrasia nchini TCD jambo ambalo ni kinyume na makubaliano ya kikao cha pamoja cha Tume ya Uchaguzi na TCD kilichofanyika mwaka jana. Alieleza kuwa hali hii ni hatari katika kutekeleza jambo husika kwa kuwa wadau muhimu wanakosa uelewa wa pamoja juu ya jambo hilo.

Vilevile alieleza, kwa kuwa fedha zilizokuwa zimetolewa awali kwa ajili ya utekelezaji wa kazi ya uandikishaji wa wananchi katika Daftari ya Wapiga Kura zilikuwa chache kulingana na uzito wa kazi yenye we na kwamba kwa kuwa Tume yenye we imewahi kukiri kuwa inakabiliwa na changamoto nyingi katika kazi hiyo ikiwa ni pamoja na changamoto ya fedha na rasilimali watu; na kwa kuwa muda uliobakia kukamilisha kazi hiyo muhimu ni miezi miwili tu kabla ya mwezi wa nne ambapo inategemewa kuwa kutakuwa na upigaji wa kura ya maoni juu ya Katiba Inayopendekezwa ambapo Daftari hilo ndilo litatumika, kulikuwa na haja kubwa ya wadau muhimu kuwa na uelewa wa pamoja juu ya jambo hilo kabla ya kuanza kutoa elimu kwa wananchi ili kuzuia migongano na kutofautiani wakati wa utekelezaji wa wa kazi hiyo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa changamoto zilizokuwa zinaikibili Tume katika zoezi hili zinapatiwa ufumbuzi wa kutosha.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupokea hoja hii niliamua kukutana na Wajumbe wa Kamati ya Uongozi pamoja na baadhi ya Wabunge ambao ni Wajumbe wa TCD pamoja na wawakilishi wa Serikali, ili tujadiliane kwa kina juu ya jambo hili na baadaye tupate namna bora ya kulishughulikia.

Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Uongozi baada ya kupokea taarifa ya Serikali na majadiliano ya kina, imeridhia maelezo yaliyotolewa na Serikali kwamba Tume ya Uchaguzi itakutana na TCD na wadau wengine wiki ijayo

4 FEBRUARI, 2015  
na kwamba fedha zitatolewa kulingana na mahitaji halisi ya Tume ya Uchaguzi. Kamati ya Uongozi imeielekeza Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ifuatilie utekelezaji wa maelezo hayo na kuleta taarifa siku ya Ijumaa kwenye kikao cha Kamati ya Uongozi. Ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana, kazi tulioifanya leo ni kubwa. Nachukua nafasi hii kuwapongeza wote Serikali, Kamati pamoja na Wabunge wote. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.15 Usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,  
Tarehe 5 Februari, 2015, Saa Tatu Asubuhi)*